ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 17 April, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Hotuba ya Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani juu ya Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa bajeti kwa taasisi za serikali kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 92

Huduma Bora za Afya kwa Walemavu

Mhe. Raya Suleiman Hamad – Aliuliza:-

Sheria Nam. 9 ya 2006 ya Watu wenye ulemavu kifungu Nam. 11 kinaeleza kwamba mtu mwenye ulemavu ana haki ya kupatiwa huduma ya afya na kuchukuliwa hatua za kumkinga na jambo linaloweza kumpa ulemavu.

(a) Je, ziko *Clinic*, Zahanati na Hospitali ngapi zinatoa huduma na marekebisho kwa watu wenye ulemavu?

(b) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba sasa ipo haja ya kuwepo sehemu zinazotoa huduma za viungo (*physiotherapy*) kwa kila Hospitali ya Wilaya kwa watu wenye ulemavu, ili kuwapunguzia usumbufu wa kusafiri kwenda Tanzania bara kufuata matibabu na marekebisho?

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye Mhe. Mwakilishi kwamba kifungu cha sheria hiyo kipo na ndio maana majengo yetu yote hivi sasa tunayojenga tunaweka ngazi ambazo zinaweza kupandisha kiti cha magurudumu, ambacho kinatumiwa na watu wenye ulemavu (*RAMP*) kwa ajili yao.

(a) Tunazo *Clinic* zifuatazo zinazoshughulikia wagonjwa wa aina hiyo.

Unguja

Hospitali ya Mnazimmoja
(i) Kitengo cha Uchuwaji (*Physiotherapy*).
(ii) Kitengo cha Mafunzo ya Kazi kwa Vitendo (*Occupational Therapy*).
(iii) Kitengo cha Marekebisho ya Viungo na Mifupa (*Orthopedic Therapy*).

Vile vile kwa upande wa Pemba tunavyo vitengo kama hivi.

(c) Mhe. Spika, kuna mpango wa kupeleka huduma karibu na jamii (*Out Rich Program)*, ambapo wataalamu kutoka Hospitali ya Mnazimmoja huweka siku maalum kwenda kutoa huduma nje ya

hospitali hiyo na kuwepo katika hospitali nyengine na baadaye watu kutangaziwa wafike, kwa ajili ya kupata huduma katika kituo kilichochaguliwa. Vile vile huduma kama hizo hutolewa katika kituo cha Kitogani na Kivunge kila baada ya wiki mbili.

Sambamba na hilo pia kwa kushirikiana na Umoja wa Watu wenye Ulemavu kuna siku maalum iliyoandaliwa kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye ulemavu.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, hivi haoni kwamba tunao upungufu mkubwa wa watu hawa pamoja na wataalamu wa kuweza kutushughulikia. Kwa mfano, Pemba Hospitali ya Chakechake ndiyo inayobeba mzigo mkubwa wa watu wenye ulemavu na pale nafasi hapana, yaani wanacho kijumba kidogo cha kukodi nje ya hospitali na watu wale ukienda wanafanyiwa huduma zile nje barazani pamoja uwanjani.

Je, Mhe. Waziri ni lini utaweza kuwafikiria watu wenye ulemavu katika hospitali mbali mbali kuweza kuwatengea nafasi nzuri ya kufanyiwa shughuli hizo?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakubaliana naye pia kwamba kuna nafasi finyu ambayo haitoshi kwa ajili ya shughuli hizo, lakini angalau nafasi hiyo ipo. Sasa katika mipango yetu ya utanuzi wa hospitali hizo kutokana na kampeni kubwa sasa kwamba na walemavu nao wanahitaji kuhudumiwa kama watu wengine, basi kutakua na Kitengo Maalum kwa ajili hiyo, hasa hapa kwenye Hospitali Kuu ya Mnazimmoja suala hilo limezingatiwa katika marekebisho makubwa tutakayofanya kwenye kile Kiwanda cha Madawa.

Kwa kweli tatizo hilo lipo na pia tunalo tatizo kubwa la wafanyakazi wa utaalamu huo. Kutokana na upungufu huo wizara imeamua sasa kuanzisha masomo hayo maalum katika Chuo chetu cha Mbweni, ili kupata watu wengi wa kutosha kwa ajili ya huduma hizo. Kwa kweli wale waliopo sasa wengi wamezeeka.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kua walemavu katika kada mbali mbali wanapata matatizo makubwa ya kimaisha ikiwa ni pamoja na mawasiliano hususan pale wanapotaka kwenda kupata tiba katika mahospitali ya serikali na hata zile binafsi.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia walemavu hawa hususan walemavu wa kusikia kwenye vituo vya huduma zao kuwawekea wataalamu wa Lugha za Ishara kwa mfano hospitali.

(b) Kwa kua Wagonjwa wa UKIMWI wanapata msaada mkubwa kutoka katika Taasisi za Kimataifa na hata serikali, kwa ajili ya kupata lishe ya kuwaongezea maisha.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia walemavu wa mifupa, kwa sababu ulemavu wa mifupa mara nyingi unasababishwa na upungufu wa *calcium* mwilini. Hivi serikali ina mpango wa muda mfupi au wa baadaye kwa ajili ya kuwasaidia hawa kwa kuwapatia lishe yenye virutubisho vya *calcium*.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nimepata tabu sana kumuelewa Mhe. Mjumbe maswali yake aliyoniuliza. Kwanza naomba nilirudie nadhani ni suala la mawasiliano ya usafiri. Pili kuhusu kuwapatia kazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, serikali inasaidia katika Vitengo mbali mbali katika wagonjwa wa UKIMWI, hilo na (b). Je, hawa wagonjwa wa mifupa ambao tatizo lao kubwa ni lishe iliyokosa *calcium*. Hivi serikali ina mpango gani wa kuwasaidia lishe nyenye *calcium* kama vile wanavyowasaidia wagonjwa wa UKIMWI.

(a) Kuhusu Walemavu wasiosikia wanapata shida ya mawasiliano kwa sababu hakuna waatalamu wa Lugha za Ishara katika maeneo wanayokwenda kwa ajili ya kutaka huduma za matibabu na zile za kimaisha. Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia hawa walemavu wasiosikia katika kuwasiliana pale wanapotaka huduma za matibabu au za kimaisha katika maeneo mbali mbali? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama nitashindwa kujibu basi naomba nisamehewe, lakini nimepata tabu kidogo kuelewa. Kwa kweli nilichotaka kusema ni kwamba masuala ya tiba ni Wizara ya Afya na masuala ya huduma kuna Idara Maalum katika Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, nadhani hivyo ndivyo ilivyo.

Sasa kwenye matibabu tunao wajibu wa kuwasaidia na pale tutakapokua na matatizo ni suala la msingi kulishughulikia serikali. Lakini suala la kuwapatia kazi pamoja na vile vifaa vya kusikia, basi tutajitahidi kufanya hivyo. Kwa kweli kuna Idara Maalum katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya shughuli zinazohusu walemavu tu kwa mambo mengine nje ya yale yanayohusu matibabu.

Mhe. Spika, kama nakumbuka vizuri jana au juzi nimeona kuna mafunzo maalum yanayotolewa kuhusu Elimu ya Alama, tayari ipo hapa na inaendelea kwa kasi sana katika kuwasaidia watu hawa ambao hawasikii.

Nam. 106

Wachukuzi Kubeba Nyama Begani Sokoni Darajani

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Wizara ya Afya ina mpango gani wa kudhibiti vitendo vya wachukuzi katika Soko la Darajani kubeba nyama begani bila kuzingatia Kanuni za Afya.

(a) Je, kwa kua soko hilo ndio sura ya nchi, wachukuzi wangapi wameshachukuliwa hatua kutokana na makosa ya kubeba nyama begani huku wakiwa vifua wazi au wakiwa na nguo zilizokaukia damu zisizokuwa safi?
(b) Kwa kuzingatia Kanuni za Afya kuendelea kuachia wachukuzi hao sio kuvunja Kanuni za Afya na kuhatarisha maisha ya wananchi wake?

(c) Mhe. Waziri, je wachukuzi na wauzaji wa nyama wamekua wakipimwa afya zao mara ngapi kwa mwaka na kwa nini wanafanyakazi hiyo bila ya kuwa na sare?

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Soko la Darajani liko chini ya Baraza la Manispaa, masuala ya usafi na kufuata Kanuni za Afya Sokoni hapo zinasimamiwa na Maafisa wa Afya wa Baraza la Manispaa.

(a) Hatua kwa ajili ya wachukuzi wanaobeba nyama bila ya kufuata utaratibu zitaendelea mpaka Kanuni za kusimamia mambo hayo ya nyama na usafi wake kwa ujumla zitakapotoka kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(b) Mhe. Spika, pamoja na kua Kanuni za Nyama bado hazijatoka katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, lakini Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi inaendelea kuwapatia elimu ya usafi wachukuzi hao juu ya masuala ya ubora na usalama wa chakula ikiwemo na ile ya nyama. *(Makofi)*

(c) Jumla ya watu 187 wakiwemo wachukuaji na wauzaji wa nyama wamepima afya zao katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja. Aidha, wauzaji nyama wanatakiwa kupima afya zao mara moja kila mwaka. Kuhusu masuala ya wafanyakazi kuvaa sare yataanza kuchukuliwa hatua wakati kanuni inayohusika itakapotangazwa rasmi kama nilivyoeleza hapo awali. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kwa kua watu mbali mbali katika nchi yetu wanapenda kula nyama, pia kwa vile nyama ni sehemu ya lishe muhimu kwa ajili ya afya zetu.

(a) Je, kuendelea kuacha kutunga Kanuni zinazodhibiti uuzaji pamoja na ubebaji wa nyama si kuidhalilisha nchi yetu?

Vile vile kitu kinachotakiwa kiwe katika mazingira mazuri katika uchukuaji na usafirishaji wa nyama, kwa sababu tunawaona wenzetu kwa mfano nyama zinazotoka Saudi Arabia zinakua kwenye *packing* nzuri, yaani katika mazingira ambayo hayawi *contaminated*

(b) Je, Mhe. Spika kuendelea kuibeba nyama moja kwa moja kutoka katika *butcher* na kuiweka kwenye mgongo ambao hauna hata shati, huku si kuhatarisha afya zetu pamoja na kulidhalilisha taifa letu hili?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba radhi sana kwa sababu napata tabu kumsikia Mhe. Mjumbe wakati anapouliza maswali ya nyongeza. Kwa hivyo, naomba taja moja kwa moja yale maswali baada ya kua maelezo yameshasemwa.

Swali moja ni kwamba kama nimeelewa nyama kuendelea kuchukuliwa kwenye mabega inakua haiko kwenye mazingira mazuri ni kudhalilisha nchi yetu ndivyo nilivyosikia.

Kwa upande wa swali la pili sikulifahamu ni kitu gani. Mhe. Spika, kwa idhini yako, kwani alisema (a) na (b) sasa lile la (b) na halafu jamaa walivyokua wakishangiria wakati sisi tunazungumza nyama ya ng'ombe na kuku. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kimsingi swali langu la mwanzo kwa sababu wenzetu wanamudu kusafirisha nyama katika *packing* maalum kutoka Saudi Arabia mpaka nchi hizi zilizoko katika Jangwa la Sahara kwa mfano Tanzania, yaani zikiwa *well packed non contaminated*. Je, sisi kuendelea kuibeba moja kwa moja kutoka kwenye *butcher* na mgongo ambao hauna hata shati huko si kudhalilisha ustaarabu wa nchi yetu?

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, sauti yako ina nguvu sana sasa wakati unaposema taratibu kwa sauti kidogo ya chini, basi ndio tunasikia vizuri, lakini ukiweka ile *volume* ya juu wengi inakua hatusikii. Kwa hivyo, unapozungumza nadhani ujaribu kusema kwa sauti ndogo kidogo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli kwamba si vizuri na kwa kweli haielekei kua wenzetu wanatuletea nyama katika hali nzuri iliyofungwa kwenye vifaa na maboski uzuri na halafu sisi hapa tukaendelea kuibeba kwenye mabega au nyama tukaziacha wazi huria kwenye masusu. *(Makofi)*

Lakini katika juhudi ya Bodi yetu ya Chakula, Dawa na Vipodozi moja katika kitu ambacho inakipiga vita ni hiyo tabia ya kuuza nyama ya ng'ombe na kuku hasa siku hizi kwenye magari. Kwa kweli tumewalazimisha, kwamba yule ambaye anafanyabiashara hiyo aidha yule anayeleta au wale *agents* lazima wawe na vituo maalum wanavyouza nyama hizo kama vile zilivyo *butcher* iliyokua imetengenezwa kwa vioo tena yenye hali zote za usafi pamoja na sare.

Mhe. Spika, tumejitahidi kwa wale waliokua wakifanya hivyo tumewakamata na kuwapa miongozo na wale waliokua wakifanya kazi hizo tumewaambia wafungue maduka. Lakini mpaka wakati huo tutakapokua na nguvu za kisheria, hivyo itabidi tushirikiane na Baraza la Mji katika kulitekeleza hilo ambalo halipendezi.

Kwa kweli haipendezi na ni hatari kwa afya. Vile vile nilikua nikinong'ona na Mhe. Waziri hapa, Mhe. Spika kuna tabia ya muhali, yaani tumeacha mambo yamekwenda mbali kidogo, sasa tunapotaka kuyarejesha kwenye utaratibu watu wanakua na malalamiko mengi, badala ya kuona tunalinda usalama inakua ni kulaumiana.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi kwa kupitia chombo hiki tunaomba mashirikiano, wakati tunapojaribu kuwazuia watu wasifanye yale yasiokua ya kawaida ni kwa sababu ya kulinda afya za watu wetu na wala si kwa nia mbaya. Hata hivyo, utaratibu wa kisheria inabidi ufuatwe badala ya kutumia nguvu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wataalamu wa afya mara nyingi hutuelekeza wakati tunapoamua kuchinja nyama zetu za ng'ombe tuwapate wataalamu wa afya kwa ajili ya kuzipitia na kuziangalia usalama wake kiafya. Lakini mara nyingi vijijini wanapokuja baada ya ng'ombe kuchinjwa wao ndio huchukua nyama za ndani yakiwemo maini na mafigo.

(a) Je, huu ndio utaratibu wa Wizara ya Afya kwamba madaktari wachukue nyama za ndani?

(b) Mara nyingi tukitembelea kwenye *butcheries* huziona nyama za ng'ombe zimegandwa na damu kavu kiafya nini madhara yake?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, si agizo la Wizara ya Afya kwamba daktari akeshakagua kua nyama safi maini na moyo apewe yeye, nadhani pengine ni makubaliano ya mwenye kuchinja nyama na huyo daktari. Mhe.

Spika, kumekua na tabia hii hata kwenye karamu zetu za Kiswahili yule mwenye kusimamia karamu hupewa kichwa na maini na hayo ni mazoea na wala sio kawaida au taratibu ya Wizara ya Afya. *(Kicheko/Makofi)*

Kuhusu suala la *butcher* bado tunaendelea kuwasimamia kwa kasi sana na kuna baadhi ya *butcheries* tayari tumeshawahi hata kuzifunga, kwa sababu ya kutokulinda usafi. Kwa hivyo, tutaendelea kulisimamia hilo katika haja ya kulinda afya za wananchi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kua Wizara ya Afya ndiyo yenye jukumu la kusimamia afya za binadamu. Vile vile Mhe. Waziri alisema kwamba *butcheries* zijengwe na ziwe na vioo, ili kufuata utaratibu.

Je, kwa sababu kuna *butcheries* hazikujengwa kwa vioo na nzi wanakuwa wengi wanang'ang'ania ile nyama na wakati nzi wanahatarisha afya ya wanadamu. Hivi kuna kitengo maalum ambacho kimewekwa kwa ajili ya kupita kwenye *butcheries* na kuangalia huo usafi na kama hakipo, basi ni lini kitaandaliwa, ili kuweze kupita kwa ajili kuangalia usafi na wananchi wetu wawe salama?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Bodi yetu ya Chakula, Dawa na Vipodozi ina watu tunaowaita *inspectors*, ambao kazi yao maalum kila kukicha ni kupita na kuhakikisha kwamba biashara zile za vyakula wenye kuuza dawa, wenye maduka pamoja na shughuli zote zinazohusiana na chakula kua zinafanyakazi kwa utaratibu uliokuwepo.

Kwa hivyo, sheria ipo ya Bodi ya Chakula na wapo watu tayari wameshawahi kukamatwa na *butcheries* zimeshawahi kufungwa, maduka yameshawahi kufungwa, dawa pia zimeshawahi kuzuiliwa. Kwa kweli shughuli hiyo inaendelea na tunastahiki kushirikiana na wale watendaji wa Baraza la Mji, ambao wao kwa Manispaa za Mjini ndio wanaostahiki kusimamia na kila kwenye mji yupo Afisa wa Afya wa Baraza la Mji ambaye anastahiki kufanya hivyo.

Mhe. Spika, vyombo hivyo vipo, lakini narudia kusema Mhe. Mjumbe muhali kidogo unatusumbua na tunahitaji sasa kushikilia sheria zichukue mkondo wake. Kwa kweli mimi siko pamoja na kutumia nguvu. Lakini kama kuna sheria, basi sheria zifuatwe kwa sababu hasara ya maradhi wakati mwengine ni kubwa kuliko ule muhali tunaouchukua.

Vitu hivyo viko Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wako watu wa biashara, kwa mfano kuna Sheria moja ya Kumlinda Mlaji ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na zote hizo zinatakiwa zishughulikie usalama wa afya za wananchi katika kutumia nyama ya kuku, ng'ombe pamoja na vitoweo vyengine. *(Makofi)*

Nam. 138

Visiwa Vidogo Vidogo, Mali ya Zanzibar

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba na Visiwa Vidogo Vidogo vilivyoizunguka na bahari yake, ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

(a) Ukiacha visiwa viwili vikubwa vya Unguja na Pemba, je kuna visiwa vingapi mali ya Zanzibar?

(b) Je, visiwa hivyo vinatumiwa kwa shughuli gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 138 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba na Visiwa Vidogo Vidogo vilivyozunguka na bahari yake, ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, ukiacha Visiwa viwili vya Unguja na Pemba pia viko visiwa 62, ambavyo ni mali ya Zanzibar. Visiwa 28 vinazunguka katika Kisiwa cha Unguja na visiwa 34 vinazunguka katika Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, visiwa hivyo vidogo vidogo vinatumika kwa shughuli mbali mbali ikiwemo makaazi kwa vile visiwa vikubwa kama vile Tumbatu, Uzi kwa Unguja, kwa upande wa Pemba ni Kojani na Panza. Vile vile visiwa vyengine vinatumika kwa mambo ya uwekezaji wa utalii na vyengine vinatumika kwa shughuli za kilimo, hifadhi ya wanyama, ndege na kadhalika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwa kua kwenye majibu ya Mhe. Naibu Waziri amesema vipo visiwa vinatumika kwa makaazi, vyengine vinakaa ndege na vyengine vinashughulika na masuala ya utalii.

(a) Kwa kweli nataka kujua hivi vinavyoshughulika na mambo ya utalii viko vingapi na kama vimekodishwa, basi nataka kujua vimekodishwa kwa kiasi gani na muda gani?

(b) Vile vile nataka kujua serikali fedha inazopata kutokana na ukodishaji huo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, visiwa ambavyo vimekodishwa na vinafanyiwa shughuli za utalii nitavitaja kimuhtasari ikiwemo Kisiwa cha Mnemba, Changuu, Bawe, Misali pamoja na Chumbe.

Mhe. Spika, fedha zilizokodishiwa visiwa hivi kighafla siwezi kumjibu, isipokuwa nitampa majibu haya kiasi gani cha fedha hizo kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, fedha hizo zinazokodishwa visiwa hivyo zinatumika katika shughuli mbali mbali za serikali kwa mujibu na mustakbali wa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweza siku hii ya leo kuamka katika hali ya uzima. Naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kua kuna ripoti kwamba visiwa haviuzwi, je ni visiwa vingapi kwa Unguja na Pemba vilivyouzwa na vingapi ambavyo vimo mikononi mwa serikali?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni sahihi kauli ya Mhe. Mjumbe kwamba visiwa vya Zanzibar haviuzwi. Kwa hivyo, hakuna kisiwa chochote Zanzibar kilichouzwa. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu waziri alipokuwa akitaja visiwa ametaja visiwa vingi lakini bahati mbaya sikumsikia akitaja kisiwa cha Fungumbaraka ambacho kipo kwenye utata, naomba kujua kisiwa hiki cha fungubaraka ni mali ya Zanzibari au mali ya Tanzania Bara. Na kama ni mali ya Zanzibar kwa nini wavuvi wetu wanaopokwenda kwenye kisiwa hichi husumbuliwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Fungumbaraka ni kisiwa cha Zanzibar, hii ni tokea zamani kwenye historia inaonyesha kwamba Fungumbaraka ni mali ya Zanzibar na hata katika mwaka 1962 serikali ya Zanzibar ilikwenda kuweka bendera kule hakuna aliyesema kwa nini umeweka bendera hapa na mpaka leo tunajua kwamba ni kisiwa cha Zanzibar, kwa bahati tu kidogo kiko mbali kidogo na Kizimkazi kwa hivyo wanaweza wakatokezea watu kwa madhumuni ya kuchochoe wakasame ni mali ya upande mwengine. Ahsante sana.

Nam. 129

Upanuzi wa Kiwanja cha Banyamulenge

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Itakumbukwa kwamba Wizara ilipotaka kuongeza barabara iendayo Nungwi katika eneo linalopakana na uwanja wa mpira wa Banyamulenge katika Kijiji cha Potoa, ilikubaliana na wenye kiwanja kwamba waipishe barabara hiyo huku eneo la uwanja huo lipanuliwe kwa kusafishwa eneo la upande wa pili katika uwanja huo.

a) Je, ni lini Wizara itafanya kazi ya upanuzi wa eneo hilo la uwanja ili uwanja huo uweze kutumika ipasavyo.

b) Je, kuna sababu zipi za msingi zilizochelewesha upanuzi wa kiwanja hicho

c) Je, Wizara haioni kwamba ucheleweshaji wa kazi ya upanuzi wa kiwanja hicho ni kwenda kinyume na Sera za Michezo

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Swali lake Nam. 129 lenye vifungu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo. Nakubaliana na hoja ya Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali ilipojenga barabara ya Mkwajuni – Nungwi ilihitaji sehemu ya eneo la uwanja wa Banyamulenge katika Kijiji cha Potoa kwa kuwa uwanja huo ulikuwa karibu sana na barabara tukumbuke kuwa barabara hiyo ilijengwa na Mkandarasi na fidia ya uwanja inapaswa kutolewa na serikali kwa maana ya Wizara yangu.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, eneo linalotaka kuongezwa uwanja huo ni eneo lenye mawe magumu, hivyo kunatakiwa zana nzito yenye nguvu na uwezo wa kufanya shughuli hiyo. Kwa muda mrefu zana ambayo tulitegemea kuwa ifanye kazi hiyo ilikuwa imeharibika na matengenezo yetu ni kuwa baada ya muda si mrefu tunaweza kufanikiwa kurejesha katika hali yake ya kawaida. Matarajio yetu suala hili litakamilika ndani ya mwaka huu 2012. Naomba Mhe. Mwakilishi, tuwasiliane kwa karibu ili tuweze kufanikisha upanuzi wa uwanja uo ili tuweze kwenda sambamba na sera yetu ya michezo.

b) Sababu kubwa za ucheleweshaji wa suala hili kushindwa kufanyika kwa wakati ni pamoja na suala la gharama kutokana na ukweli kwamba gharama hizi ziliambatanishwa na gharama nyengine za fidia za vipando na miti ya kilimo. Aidha suala la kuharibika kwa vifaa vya zana nzito pia limechangia.

c) Ni kweli kutokamilisha uwanja huu ni kwenda kinyume na azma ya serikali ya kuendeleza masuala ya michezo, matarajio yetu tutalifanikisha suala hilo ili sio tu kutimiza ile azma ya serikali katika michezo, lakini pia kukuza vipaji vya wanamichezo hao waliopo katika jimbo la Mkwajuni.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Pamoja na majibu aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri ambayo sikubaliani nayo majibu haya kwa sababu majibu haya nilishayapata katika kipindi kilichopita na nikaambiwa muda si mrefu, tutakwenda kulifanyia ufumbuzi suala lako hili tukakutana tena kwenye kikao cha bajeti hapa kama utaangalia Hansard nilitishia kuizuia bajeti ya Wizara hapa kwa sababu ya suala hili hili na nikaambiwa muda si mrefu baada ya bajeti tu tutakwenda kulitatua suala hili. Lao Mhe. Waziri ananambia ndani ya mwaka huu wa 2012 litakuwa tayari, hivyo Mhe. Waziri haoni kama analidanga baraza hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Ninacho kumthibitishia Mhe. Muwakilishi na baraza lako tukufu kwamba adhma ya serikali ni kutimiza ahadi zake, changamoto kubwa inayoonekana ni upungufu wa fedha lakini namuomba sana Mhe. Muwakilishi ajenge imani na serikali yake na ahadi yetu ataona, tutajitahidi kadiri hali inavyokuwa tuweze kuifanikisha ahadi hii, tunajua sisi ni waungwana na watu wa Mkwajui ni waungwana hatuna budi kutimiza uungwana wetu kwao.

Nam. 131

Fidia kwa Wananchi Waliovunjiwa Nyumba zao Kiashange

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Katika zoezi la upasuaji wa miamba kijiji cha Kibuyuni na Kiashange, kuna baadhi ya wananchi waliahtika kwa kuvunjiwa nyumba zao bila ya kulipwa fidia.

a) Mhe. Waziri, kwa nini Wizara imechelewesha ulipaji wa fidia kwa wananchi hawa

b) Serikali haioni kwamba kuchelewa kwa fidia hizo kunawafanya wananchi hawa kuamini kwamba hawawezi kutendewa haki na serikali yao

c) Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba inwalipa fidia hiyo wahusika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhsa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 131 lenye vifungu a,b na c kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano haihusiki moja kwa moja na maeneo ya ulipaji wa fidia ya nyumba zilizoathirika katika maeneo ya upasuaji wa miamba huko Kibuyuni.

b=c) Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu inawaomba na kuwaelekeza wananchi walioathirika na zoezi hilo, kwenda kufikisha malalamiko yao hayo kwa Kampuni husika ya MECCO ili kupata wajibu ya ufafanuzi unaostahiki hata hivyo, Wizara yangu kwa kutambua uzito wa suala hili, tutaliratibu na kulifuatilia kwa karibu ili kuona haki inatendeka kwa kuhakikisha yale maliop yanayostahiki kwa wananchi hao wanafanyika. Aidha Kampuni ya MECCO tayari imeshatembelea eneo hilo na kufanya tathmini ya nyumba silizoathirika. Wizara itafuatilia na kuona kwamba wananchi wanalipwa fidia zao stahiki.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba Wizara yake haihusiki moja kwa moja, lakini wananchi wa Mkwajuni wanaifahamu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwamba ndio inayohusika, kwa sababu huyo mkandarasi itakuwa wao ndio waliompa kwenda kupasua miamba pale, sisi kama wananchi tunaifahamu serikali ndio wajibu huo na ndio maana tukafanya wajibu wetu tulikuja serikalini na tukapeleka malalamiko haya kama ambavyo yeye anasema tupeleke sehemu husika tulishakwenda kwenye Wizara ya Miundombinu na tulikwenda pale na Naibu Katibu Mkuu na watu wa Kampuni tukafanya tathmini pale tukapitia nyumba zote zilizoathirika pale. Mkatoa ahadi kwamba ndani ya miezi miwili itakuwa imekamilika, lakini ninachoshanga Mhe. Spika, mpaka hii leo hakujafanywa malipo yale ndio maana nikawa na suala la msingi linalosema.

Ni lini watahakikisha kwamba wananchi wale wanapata malipo yao?.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Nakubaliana mia kwa mia na maelezo aliyotoa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kuhusiana na tasmini kweli maafisa wangu walishiriki katika kwenda kukagua nyumba hizo, lakini tunaposema kwamba Wizara yetu haihusiki moja kwa moja kwamba zile fedha stahiki za kulipwa fidia hazitoki serikalini, kwa maana ya kwamba hazitoki kwenye wizara yetu.

Sisi kama wizara tunatakiwa kuratibu na kusimamia kuona kwamba ile kampuni husika waliosababisha ile athari ndio wanaopaswa kulipa fidia hiyo, tulichokiahidi kwamba tutahakikisha kwa mkandarasi anatimiza ahadi yake ya kulipa fidia kama tulivyofanya tathmini na ukaguzi tuliokwisha kuufanya kwa kushirikiana pamoja nay eye.

Sasa namuomba Mhe. Muwakilishi tuendelee kuhimizana kwamba sisi kama Wizara tumbane vizuri mkandarasi ili kuona kwamba ile ahadi aliyoitoa kwa kupitia Wizara yetu ya kuwalipa fidia basi inatimia, lakini sisi kama Wizara hatuna fedha moja kwa moja za kuwalipa isipokuwa mkandarasi ndie mwenye fedha sasa hivi na yumo ndani ya mkataba.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

a) Mhe. Spika, lazima tukiri kwamba Wizara hii ya Miundombinu imejitahidi sana katika kujenga barabara Unguja na Pemba, lakini mara zote kila penye ujenzi wa barabara wanashindwa kutoa fidia pale wananchi wanapoathirika, hebu Mhe. Waziri leo atupe siri kwa nini wanakuwa mahodari wa kujenga hoja na kupata miradi mikubwa mikubwa lakini wanakuwa wavivu au wanyonge wa kumiliki fedha za fidia.

b) Wataalam wanatwambia kwamba kila mradi wa barabara una asilimia 10 ya athari za kimazingira. Kwa nini wananchi wa Zanzibar hawapati asilimia hii pale wanapoharibiwa kimazingira.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Utaratibu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano sio kwamba kuwachelewesha wananchi kuwalipa fidia zao wala sio kama mabingwa wa kujibu hoja, utaratibu tulioupanga katika Wizara yetu ni kwamba tunapoendelea na miradi yetu ya kujenga barabara panapostahiki kulipwa fidia, fidia ya nyumba ndio kipaumbele chetu na fidia hii ya nyumba kuna zile nyumba ambazo tutazivunja ili kupitisha barabara hizi zinapewa kipaumbele namba moja.

Kuna fidia za nyumba ambazo zinaathirika baada ya kupita ujenzi wa barabara hizi zinapewa kipaumbele nambari mbili. Lakini Mhe. Spika, napenda nikiri kwamba tumekuwa tunachelewa kulipa fidia hata za miti na vipando kwa kutambua tu kwamba madai haya yanakuwa ni makubwa na serikali baadhi ya wakati inakuwa fedha hizi hazijatengwa.

Lakini jibu (b) ni kweli kwamba kunakuwa na asilimia kumi kati ya mradi ambazo zinapaswa kulipwa kwa ajili ya mazingira, fedha hizi zinastahiki kutolewa na serikali lakini kwa kutegemea ule mzigo wa serikali tuliokuwa nao katika miradi hii likiwemo suala la fidia, pamoja na mchango wa serikali katika miradi ile tunajikuta kwamba asilimia kumi hii tunashindwa kuitoa kama serikali ili kuwapatia maeneo husika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa suala la ulipaji wa fidia kwa hivi sasa hasa kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo ndio inayotujengea miundo mbinu katika maeneo yetu mbali mbali limekuwa kila siku linaongezeka.

a) Je, Mhe. Waziri huoni sasa iko haja wizara yako katika bajeti inayokuja kuangalia uwezekano na kuomba rasmi fedha za wananchi ambao waliokwisha kuathirika aidha kwa miti au nyumba zao au mali zao kwa jumla, ili kupeleka maombi maalum Wizara ya fedha kwa ajili ya kuweza kulipwa fidia hizi.

b) Mhe. Spika, kuendelea kuchelewa kulipa fidia hivi je hatuoni wale wananchi baada ya serikali yetu kuwa na program ya kuondoa umasikini moja wapo ni kuweka miundombinu, lakini sasa hivi programu hii hatuoni kwamba wengine inawaongezea huo umasikini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakubaliana na rai ya Mhe. Mwakilishi kwamba ipo haja Wizara yetu kuingiza katika bajeti malalamiko au kiasi hichi cha fedha ili kupata fedha kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi wetu, lakini Mhe. Spika, lazima tukumbuke kwamba serikalini katika utaratibu wa bajeti nako kuna keki ambayo mnapaswa kugawana wizara zote. Lakini kwa bahagti mbaya keki hiyo inasemekana imekuwa ndogo na imekuwa kisheti, sasa kisheti hichi hicho kidogo ndicho watu wanachogawana ili kuweza kupata huduma kwa jamii na sehemu husika. Mategemeo yangu kwamba serikali itaona uzito na umuhimu wa kutenga fedha ili kunusuru miradi yetu kuwasaidia wananchi wetu kujikwamua kadika dimbwi la umasikini, kama vile Mheshimiwa Muwakilishi maelezo aliyoyatoa.

Lakini suala la pili Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna fidia zinachelewa lakini fidia zinazochelewa sio zote tumeeleza kwamba tunapokwenda na mradi wowote hatutovunja nyumba ya mwananchi yoyote kabla ya kulipa fidia, fidia zinazochelewa ni fidia za miti na vipando na hii inatokana na kipaumbele na uzito wa ule mradi husika. KIama mradi utakuwa ni muhimu kwetu na nyumba ndio kikwazo hatutoivunja nyumba mpaka tumlipe fidia, lakini tunachokiamini kwamba fidia ya miti ni kweli kwamba inachelewa na itaendelea kuchelewa kwa sababu ya kutokana na upungufu wa fedha ambazo zimetengwa katika maeneo haya husika.

HOJA ZA KAMATI

Kamati ya Katiba Sheria na Utawala

(Majadiliano yanaendelela)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe tunaendelea na kujadili ripoti na leo tunaanza mjadala wa ripoti ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, naendelea kusisitiza tu kwamba tutumie muda mfupi ili tuhakikishe kwamba shughuli zetu tulizojipangia zinamalizika hadi pale tarehe 20/4/2012 bado tuna shughuli nyingi tena nyengine ni refu kidogo kwa hivyo tujibane sana ili tuweze kujadili ripoti hizi tukamilishe, pamoja na shughuli nyengine.

Kwa hivyo kwa muda mchache vile vile kama kawaida nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi leo hii asubuhi kunipa nitie barka katika ripoti hii ya Katiba, Sheria na Utawala, kwanza niwasifu sana Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wake kwa kuwasilisha ripoti iliyokuwa nzuri yenye upeo na ufafanuzi mzuri.

Mhe. Spika, kama ulivyosema kuwa mimi nitatumia muda mdogo tu na nitakuwa na mambo machache tu yanayohusiana na masuala mengi, kanza nianze na Mahakama tunaelewa kama ni mihimili mitatu kwa mujibu wa utaratibu, lakini vile vile Mahakama ina tume yake ya utumishi, sasa mimi hapa nilikuwa nataka nipate ufafanuzi mzuri sana ambao utaweza kunisaidia katika shughuli za utendaji pamoja na watu wengine.

Mhe. Spika, katika Mahakama kuna sehemu nyingi tu mle kuna mrajis, kuna majaji wakuu, lakini kuna mambo ambayo Mrajis anaapishwa na Jaji Mkuu, lakini majaji hawa wanaapishwa na mwenyewe rais lakini sijui inakuwaje hii mishahara hii inakuwa kima kimoja katia ya hawa majaji na wakati mrajis yuko chini ya hawa majaji, kama nitakosea naomba mtanirekebisha. Inakuwaje mishahara yao inakuwa kima kimoja.

Lakini vile vile Mahakama kwa mujibu wa katiba yetu ina tume ya utumishi ukurasa wa 127 Tume ya Utumishi ya Mahakama sasa hapa kidogo mimi huwa nachanganyikiwa kuwa tume ipo ya utumishi ambayo itakuwa na kazi zake kwa mujibu wa sheria kama ilivyotungwa na Baraza la Wawakilishi, lakini nashangaa kuwa kuna tume nyengine ambayo tayari inawafanyia kazi wao Mahakama, sasa mimi wasi wasi wangu hapa na unaambiwa kuwa ukikiuka katiba hii basi unakuwa unatizamwa katika hatua nyengine, kwa sababu katiba ndio roho ya nchi. Sasa hapa kidogo naomba Mhe. Waziri muhusika hebu tueleze umepataje viwango hivi vya fedha vya hawa watu wa Mahakama.

Kwa sababu huko nyumba kulikuwa na masuala mengi tu katika kuulizwa hapa na Mheshimiwa ulijaribu kujibu jibu, lakini najua ukijibu pale kila mtu ana majibu yake na staili yake ya kujibu kiufundi lakini akisha ndio imekuwa basi, unajua mara nyingi sana tulijaribu kutafuta hii mishahara ya Mahakama ya mwanzo lakini utakua mtu wa mahakama ya mwanzo tayri ana Diploma, sasa hapa ndio kitu ambacho kinachotuchanganya sisi kuwa humu kwenye katiba wana tume yao utumishi, mimi nafikiri hii tume ya utumishi tungeiwachia hii kwa mujibu wa utaratibu wa katiba yetu basi wale wangejua levule za kuweka mishahara kuliko kutoka Tume nyengine ya serikali kuingia pale. Ndio maana kukawa na mchafuko wa aina kama hii.

Mhe. Spika, vile vile tunasema kuwa huu ni muhimili nao katika watatu, lakini naomba hizi *protocol* hebu naomba kuwa Jaji Kiongozi na Jaji Mkuu hebu tuangalie, lakini ukiangalia kwa upande mwengine utakuta Jaji Kiongozi anakuwa ni sawa na Jaji Mkuu ni kitu ambacho mimi kinanihangaisha sana katika akilini mwangu hebu naomba na hili suala tuliangalie jamani, sheria hii hatu tuiangalieni ndio mara nyingi sana mimi nakwambieni kuwa tunapotunga sheria tuangalie sheria nyengine haitoipinga mwenzake. Sasa hatari zake zinakuwa mambo kama haya ya kukanganyana.

Lakini vile vile hebu twende kwenye Majaji na Kadhi Mkuu hebu tuangalieni nao vile vile utaangalia kuwa utaona kama levule ni sawa, lakini ni kitu tofauti kabisa Jaji Mkuu haingii katika muhimuli mwengine wowote Kadhi Mkuu, lakini utakuta kilevule au ki-*protocol* tunakwenda kupangua kitu ambacho hakina maana.

Lakini hebu twende katika maposho yao hivi kweli Maposho yao wanakatwa kodi hawa Majaji, sasa hebu tuangalie ndio maana nikasema kuwa mimi ningeomba sana kuwa tuipe heshima tume ile ambayo ipo kwa mujibu wa katiba ili iweze kufanya kazi zake vizuri kwa utelekezaji wa ufanisi kabisa.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kada nyengine ambayo ya hospitali kule kuna kada kuanzia madokta, Maspeshelisti, Manesi, Maodali mpaka mafundi kwa kweli bado hatujawatendea haki na hasa wepi sasa, inavyosemakana labda manesi wamepata lakini vile vile na wao wanapiga kelele. Sijui wana riski wana masuala mengine hawapati sasa hii kama itakuwa inaingia kwenye wizara ya afya watu wanariski basi kama inaingia kwenye tume ya utumishi au wanaingia kwa mwenyewe waziri, lakini aelewe hivyo kwamba hawapati mafao ya aina hiyo.

Mhe. Waziri juzi alisema kwamba ana hakika kwamba wizara zote zimeshapata katika zile asilimia ambazo zilizoongezeka 25% mimi nakwambia bado na hawa ninaokutajia sasa hivi sehemu za odali na wao hawajanufaika kabisa mpaka leo hivi wanahangaishwa tu, hawajapewa haki yao na ukiangalia sasa hivi wanafanya kazi kubwa sana sawa na watu wa mesi, kwa sababu utakuta chumba kimoja kina wagonjwa wasipungua sitini anawekwa mesi mmoja na odali mmoja inabidi yule odali nae awe nesi, hakuna njia inabidi lazima ifanyike hivyo. Kwa sababu kutokana na hali ilivyo kuwa mtu mmoja hawezi kuhudumia wagonjwa wa chumba kimoja wanaofika sitini, sasa na wao leo haki yao tuwape hebu tuangalieni kabisa niwashukuru sana ndugu zanguni Madokta, Manesi, Mwenyezi Mungu awape imani.

Mhe. Spika, hebu twende kwenye ripoti ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala ile ya ustawi wa jamii ilimalizika jana ambayo ndiyo hiyo ya madaktari.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Aa kumbe *(Makofi).*

Mhe, Spika, kwa sababu najua mambo ya utumishi wizara yake imo kwenye utumishi, mishahara yao nayo inapangwa kule mheshimiwa ndio kdigo nikaona nidokolee, sasa mimi naondoka huko ili twende kule unakotwambia.

Mhe. Spika: Tena kwa muda mchache sana uliobaki.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Kwa kumalizia jana Mheshimiwa wangu huyo huyo waziri wa afya jana alinipeleka kule kwa Waziri wa utumishi kuhusu habari ya yule mtu ambae mpaka leo mafao yake hajalipwa, sasa naomba sana Mhe. Waziri na hili unipe jibu lililokuwa rasmi na mwenyewe yupo amesharudi kutoka pemba yupo hapa anataka kukusika wewe kauli yako sasa na wewe unasema vipi kutokana na uwezo wa kumsaidia.

La mwisho Mhe. Spika, mimi niseme kuwa jana nashukuru sana chombo chetu hichi cha Televisheni kwa kutuonyesha mimi na wewe katika mahojiano yale na ishaalla Mwenyezi Mungu awabariki, lakini na pale ninapochangia kuwatetea wananchi nao wanitie katika taarifa ya habari kama walivyotutia mimi na wewe. Mhe. Spika, naunga mkono ripoti asilimia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kwanza namshukuru alla kutupa uhai, uzima na toufiki ya kuzungumza, mimi masuala yangu ni matati makubwa kwa leo tukijaaliwa.

Mwanzo kabisa lipo katika ukurasa wa 153 ya ripoti hii ya kamati kinadharia nimefarijika kuona kwenye kamati kwamba Idara ya Taasisi ya Utumishi na Maslahi ya wafanyakazi imepitia miundo ya utumishi na kufanya marekebisho ili kuwawezesha watumishi kuzijua daraja zao, mishahara na kila kitu.

Mhe. Spika, katika jambo ambalo linakosekana katika utumishi wetu ni huu utaratibu wa kuwa nyanyua au kuwaweka hapali pao wakiishi, wenyewe wataalam wanaita *aprisal* ya watumishi wetu mimi mara nyingi Mhe. Spika, unanisikia katika baraza lako napiga kelele, nazungumzia kuhusu utaratibu mzima wa namna gani tunavyowapandisha vyeo, namna gani wanavyonyanyuliwa mishahara yao wafanyakazi. Utaratibu huu Mhe. Spika, kwa sababu ya kukosekana kwake mota katika chanzo cha kuwaondoa wafanyakazi wakenda katika sehemu nyengine au nchi nyengine, kwa sababu inawezekana kwa mfanya kazi anafanya kazi pale kwa muda mrefu lakini ikija nafasi ya kunyanyuliwa cheo yule ambae anafanya kazi kwa muda mrefu huwa haonekani, anatafutwa mtu mwengine ambae pengine hana uzoefu wa kazi ile na anapewa.

Mhe. Spika, tulifanya kazi katika kamati ya Fedha na Uchumi katika Baraza lilopita , kuna mfanyakazi alikaimu nafasi kwa muda wa miaka miwili lakini ilipokuja kuthibitishwa sio yeye akawekwa mwengine kabisa. Sasa suala la kujiuliza mtu anawezaji kukaimu miaka miwili na akawa hafai ikawa bado anakaimu. Kwa ufupi ikiwa wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora imefikia hapa na kutayarisha hizo fomu za upimaji, kinachotakiwa sasa hivi Mhe. Waziri aje atuthibitishie ni lini utaratibu huu utaanza kufanya kazi. Kwa sababu kutayarisha ni jambo moja lakini kufanya kazi ni jambo jengine.

Mhe. Spika, mimi kwa ufupi kabisa namuomba Mhe. Waziri leo atakapokuja atueleze kinaga ubaga ni lini utaratibu huu wa kwamba wafanyakazi wa utumishi wa umma wanajijua daraja zao, wakifanya nini watapanda cheo, wakifanya nini watapanda mshahara, hili ni jambo muhimu sana. Itakumbukwa hata juzi tulipofanya marekebisho, bado nilimshukuru Mwanasheria Mkuu kwa kuwa yeye ndiyo chanzo cha kuanzishwa huu Mswada kulikuwa na semina na alisema kwamba hakuna utaratibu wa utumishi kwa hivyo tuipitishe hii. Ile sheria ikiwa ishapitishwa na ishafanyiwa marekebisho lakini hakuna mabadiliko ya ule utendaji wenyewe itakuwa kama kitu chenyewe hakipo, tumekiwepo kitu lakini hakipo.

Mhe. Spika, mimi binafsi sitaridhika kwamba maneno haya ni ya kweli mpaka nione utaratibu huu unafanya kazi. Wenzetu wanaheshimu sana *seniority* ya kazini mtu amefanya kazi miaka mingapi na jitihada yake. Ukiacha kuchukua ile *seniority* na ukachua utaratibu mwengine sio tu unamfanya huyu anayejitahidi kwamba asiendelee lakini unasababisha mizozo ya wafanyakazi wenyewe kwa wenyewe. Kwa sababu wapo watakaojihisi kwamba hawa ndio wanao pendelewa na sisi ndio tunaoonewa. Mimi kana nilivyosema nimefarijika kuona mambo haya yametajwa katika kamati lakini sasa je, utendaji wake wa kazi utaanza lini.

Mhe. Spika, la pili ni hapo hapo ukurasa wa 153 katika Kamati kifungu cha tatu. Kamati iliona kwamba kuna tofauti ya mishahara baina ya watendaji wanaofanya kazi Unguja hasa sehemu ya uhasibu na wale wanaofanya kazi Pemba. Inawezekana imetizamwa sehemu moja tu, lakini sehemu nyengine za wafanyakazi wengine hazijatizamwa. Kwa hivyo hili linafaa lichunguzwe kwa sababu hapa mara nyingi kunapotokezea upungufu wa wafanyakazi ikiwa ni madaktari Pemba kunakuwa zaidi. Pengine sababu yenyewe ni hizi zimejificha. Tunamuomba Mhe. Waziri aje na jibu lakini ajibu kwamba atafanya uchunguzi wa kina ili tulijue kwamba hili lipo na linaendelea au laaa.

Mhe. Spika, la tatu ni suala la Idara hii ya Nyaraka ambayo iko kwenye Wizara ya Utumishi wa Umma, kwenye shughuli za nyaraka tunahitaji kufanya marekebisho makubwa kama kamati ambavyo imependekeza. Nikija kwenye suala la mwisho nilonalo ni suala la upatikanaji wa vyeti vya wale waliozaliwa na wale ambao walikosa vyeti.

Mhe. Spika, kama kitu ni haki basi haki haiyombwi, haki hupewa mtu haki yake. Serikali nzima inazungumza kwenye kwenye *E- government* lakini tunashindwa kutoa cheti kwa wakati. Sasa kweli tutafika hukokwenye *E-government* ikiwa hivi sasa hata cheti tu cha kuzaliwa inakuwa matatizo.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu leo ulikuwa ni mambo matatu kama ulivyotaka mwenyewe tuwe *brief* nakushukuru sana na naomba Wizara hizi mbili ziweze kuyatizama mapungufu yake na nakubaliana na ripoti ya Kamati kwa asilimia 100. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nitajitahidi nitumie muda mchache zaidi kuliko hata huo niliokuahidi.

Mhe. Spika, mimi nataka kwanza niipongeze Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ambayo waliyoifanya tukijaribu kuangalia ripoti yao kwa kweli imejitosheleza.

Mimi nianze kwenye ukurasa wa 157 ambapo wamezungumzia suala zima la Mahakama. Mimi nataka kutoa ushauri kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, tujaribu kuangalia zaidi kuipa nguvu hii Mahakama ili iweze kufanya kazi zile zilizoweza kukusudiwa. Tunafahamu kwamba Katiba yetu ya Zanzibar kwenye kifungu cha 5 kimeeleza ile mihimili mitatu ya dola . Mihimili hii kwa kweli kila mmoja unatakiwa uwe na nguvu kubwa na kila muhimili mmoja aidha kwa lugha kama itakuwa ni sahihi kumuheshimu mwenzake au kuuogopa muhimili mwenzake.

Mhe. Spika, bado lakini tukiangalia ndani ya Katiba yetu ya Zanzibar kwenye kifungu cha 93 kimetaja eneo la Mahakama. Lakini ukija kwenye kifungu cha 116 tunahisi kwamba katiba yetu inahitaji ifanyiwe marekebisho kidogo, nitaomba nikinukuu kwa faida ya wajumbe pale kifungu kinaposema:

> “kutakuwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambacho kitakuwa ni chombo cha juu kabisa katika Tume zote za Utumishi chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya Utumishi wa Umma kwa Zanzibar”

Mhe. Spika, unaposema kutakuwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa na nguvu kubwa kuliko Tume zote, ina maana hizi nyengine kwa mfano kuna Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, kuna

Tume ya Utumishi ya Vikosi vya SMZ, kuna Tume ya Utumishi ya Mahakama, hapa kidogo nadhani ipo haja ya kuangalia kuweza kufanya marekebisho ili kila chombo kiwe na nguvu yake kisheria.

Mhe. Spika, mimi nataka niwapongeze Mahakama kwa kazi nzuri wanazofanya, lakini tunaomba sana Mheshimiwa wajitahidi sana kuharakisha kesi au kufanya maamuzi ya hizi hukumu. Vile vile Mhe. Spika, kuna kesi ambazo zinazorundikana rumande na kuna rumande ambao wanafika zaidi ya mwaka mmoja kesi zao zinakuwa hazijapata hukumu. Kwa kweli hili jambo ambalo halifurahishi, kwa sababu mtu yule akija akiachiwa ina maana atakuwa sawa sawa alifungwa bila ya sababu yoyote. Tulikuwa tunaomba kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka basi wajitahidi kuweza kuhakikisha kwamba hizi kesi zinaendeshwa kwa haraka ili ile dhana ya Mahakama iweze kupatina haki.

Mhe. Spika, vile vile nilikuwa naomba sana hizi tume za Utumishi kila tume ipewe mamlaka yake. Kwa sababu tunasema kwamba hapa serikali wakati mwengine inaonekana ina nguvu kubwa sana kuzidi hata Mahakama na chombo chetu cha Baraza la Wawakilishi. Nilikuwa naomba sana tujaribu kutumia hii Katiba tuitafsiri vizuri kwa vitendo.

Mhe. Spika, kuna nchi za wenzetu mfano kama sikosei nadhani ilikuwa Pakistani hizi nchi za Asia. Hivi karibuni tayari Mahakama ilitoa hati ya kukamatwa kwa Waziri Mkuu. Inapokuwa Mahakama inatoa hati ya kukamatwa kwa Waziri Mkuu hii inaonesha kwamba zile Mahakama zinavyokuwa na nguvu. Lakini lazima na maamuzi yao katika uwezeshaji ni lazima yaonekane vile vile kuwa yana nguvu kisheria.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 167 unazingumzia Afisi ya Usajili wa Haki Miliki. Afisi ya Msajili wa Haki Miliki, tunashukuru tumeiyunda hapa Barazani, tuleta sheria tumeiyunda. Lakini bado kuna malalamiko mengi ya uibwaji wa haki za wasanii mbali mbali lakini vile vile kutokusimiwa vizuri kwa hawa ambao wanaendesha hii biashara ambayo inaonekana kwamba sasa hivi wale ambao wanatumia vipaji vyao, wakaumiza vichwa vyao wakatunga vitu mbali mbali au wakabuni vitu mbali mbali matokeo yake wao wanakuwa hawafaidiki lakini wanaofaidika wale wengine.

Mhe. Spika, ukiangalia kwa Zanzibar hapa ukifanya ziara ndani ya wiki moja maduka yote tayari umeshayafahamu nani anafanya nini na nani anafanya nini. Kama hivi karibuni tulisikia kulikuwa kuna semina moja ya wenzetu Jeshi la Polisi wanazungumzia suala zima la uhalifu wa Hakimiliki za wasanii mbali mbali. Hivi juzi tu wenzetu Tanzania Bara baada ya kifo cha yule msanii mashuhuri ndugu yetu Kanumba basi waziri anayeshughulikia masuala ya Utamaduni kule ndio alitoa tamko kwamba watahakikisha kwamba wanapeleka sheria ambayo itakayokuwa ihakikisha kwamba Hakimiliki za wasanii zinakuwa hazipotei.

Mimi nadhani na hapa kwetu tusisubiri msanii maarufu akafa baadaye ndiyo serikali iweze kufanya hiyo kazi. Mimi nadhani hawa watu tunatakiwa tuwalinde bado wapo haki ili waweze kutumia rasilimali zao na ule ujuzi ambao walioutoa kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, kwama nilivyosema kwa kuwa leo nitakuwa na ripoti ndefu ya Kamati naomba niishie hapo. Lakini kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura tunaiyunga mkono ripo hii ya Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria. Nakushukuru sana Mheshimiwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii kutujaalia tena kukutana hapa tukiwa hai na wazima. Nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wetu wa Kamati Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kutusimamia vizuri katika Kamati yetu na kutuongoza vizuri hadi kufanikisha kutayarisha ripoti hii na kuiwasilisha hapa mimi nikiwa mjumbe wake mmoja.

Mhe. Spika, nataka nikuhakikishie katika Kamati ambayo haijawahi wajumbe wake hata kukwaruzana kwa sababu ya uongozi makini na mahiri wa kijitukizima wa Shekhe Ali Abdalla basi moja wapo ni Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, naomba nianze moja la jumla kabla sijaingia katika yale ambayo nataka niyazungumzie. Madhumuni ya kuletwa hizi ripoti za Kamati hapa ni kuisaidia serikali kuona wapi kuna mafanikio yaendelezwe na wapi kuna kasoro na mapungufu ili parekebishwe kusudi wananchi wetu waweze kupata huduma nzuri zinazostahiki kutoka kwa chombo hichi walichokiweka ambacho ni serikali.

Mhe. Spika, kwa ufupi kabisa nataka niseme mimi ningeomba kutoa ushauri hizi ripoti za Kamati kila Wizara kwa sehemu yake ingezichukua na kwa kila Idara au Kamisheni au kitengo kilichotajwa pale wakawa wanapitia ili kuona Baraza lako ambalo ndio kama kiyoo cha wananchi katika kuimurika serikali. Ili kuweza kuona mapungufu gani na kama mafanikio ni mafanikio gani yaendelezwe ili kila Idara ijitizame na ichukue hatua ya kuyatekeleza.
Mhe. Spika, isiwe tunafanya kitu *routine* kila mwaka kuja kutoa ripoti halafu tukaondoka. Hasa kwa vile tayari tumerekebisha kanuni zetu kuweka kifungu ambacho waziri kila mwaka zinatakiwa kuja kutoa ripoti za utekelezaji wa maagizo ya kamati nadhani hilo litasaidia sana katika kuimarisha misingi ya utendaji na kuachana na ule mfumo ambao Mhe. Rais anausema kufanya kazi kwa mazoea.

Mhe. Spika, na mimi nende moja kwa moja na mimi nitakuwa kama wenzangu *brief* ili kuwapa nafasi wengine naomba nigusie mambo matatu katika ripoti hii.

Kwanza kabisa nende katika Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ukurasa 153 wa ripoti yetu ambapo panazungumziwa Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Wafanyakazi.
Mhe. Spika, kwenye maoni ya Kamati kuna mambo mawili naomba niyasome haraka haraka.

1) " Kamati inaipongeza serikali kwa kuwaongezea maslahi watumishi wa umma na kuwafanya na wao wajisikie ni moja kati ya wanaonufaika na kodi za serikali pamoja na nguvu zao wanazozitoa kwa kujenga nchi. Hata hivyo inashauri kuzidi kufanyiwa kazi zoezi hili ili kuepusha malalamiko yasiyo ya msingi.

2) Kamati inasisitiza kuwepo kwa mawasiliano *(Net work)* ndani na nje ya Wizara ili wananchi wapate kuelewa mabadiliko na mwenendo mzima wa serikali"

Mhe. Spika, hapa ndio penye hoja yangu. Tunaipongeza serikali kwa marekebisho ambayo imeyafanya na bila shaka wengi wamenufaika. Lakini bado katika kufatilia kazi yetu kamati yetu imegundua kuna malalamiko mengi sana na tumeyataja katika ripoti hii.

Mhe. Spika, lakini pia mara nyingi katika kikao chako wewe na sisi sote ni mashahidi wajumbe mbali mbali wameuliza maswali kuhusiana na nyongeza ambayo imetoka mwaka jana mwezi wa Oktoba. Bado kuna kutokuelewa, bado wananchi wana wasi wasi, bado wafanyakazi wengi wanahisi wamepunjwa. Mimi nilikuwa nadhani dawa ya hili ni serikali kuwa wazi.

Misingi ya Utawala Bora ni pamoja na uwazi katika utendaji wake. Mara mbili tatu hapa tumeuliza maswali na tumemtaka Waziri atutajie kima cha juu kabisa cha mtumishi wa Serikali ya Zanzibar ni kipi, ili kilinganishwe na kile cha kima cha chini. Lakini zile figa hazitoki. Mimi nadhani kilichosiri ni mshahara, ukiuliza mshahara wa Mhe. Haji Omar Kheri ni kiasi gani kuutaja hapa ni siri lakini vile viwango kwa mujibu wa *scheme of service* kwa kada mbali mbali si siri.

Mhe. Spika, hili nafikiri tujifunze kwa wenzetu. Uingereza ni nchi ambayo *norm* yake ya kuendesha serikali, Mhe. Abubakar, Mhe. Mwanasheria Mkuu watakubaliana na mimi yaani ile kuweka siri ndio *norm* uwazi ndio *especial* lakini *still* mshahara wa Waziri Mkuu wa Uingereza unajulikana. Sasa mimi nadhani kwa watumishi wa umma ni vizuri ingewekwa ikaeleweka hasa kwamba hivi viwango vilivyoongezwa ni kiasi gani na fomular gani imetumika kwa uwazi kabisa. Humu tumependekeza hata kutumika vyombo vya habari kulifafanua hili ili kuondosha malalamiko.

Mhe. Spika, inapokuwa kitu hakieleweki kila mtu akajenga kitu rohoni kwamba labda kuna mambo fulani fulani yamefanyika inaondosha wasi wasi. Nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri ajitahidi na wizara yake hebu ile fomula iwekwe wazi kila mtu alielewe. Hilo ni moja wa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwenye Wizara ya Katiba Mhe. Spika, naomba niende katika suala moja lakini nitaligawa sehemu mbili, hili linahusu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Katika ripoti hii ipo kwenye ukurasa wa 165 hadi 166. Kuna mambo mawili yametajwa katika ripoti hii, kwenye ukurasa wa 166 namba 3 inasema kama hivi:

> "Kwa kuwa mali za Wakfu zinahusiana na masuala ya dini ya kiislamu ni vyema utekelezwaji wake ukafanywa kwa misingi ya dini hiyo. Kwa mnasaba huo tunashauri zifanyiwe marekebisho sheria zote zinazopingana na sheria ya waktu kwani imebainika kuwa mafanikio ni madogo tangu ilivyoanzishwa sheria hii".

Mhe. Spika, maoni yangu katika hili yanafanana na yale ambayo Mhe. Rashid Seif ameyazungumzwa kuhusiana na kupitishwa kwa sheria mpya ya Utumishi wa Umma mwaka jana. Kama tunatunga sheria lakini halafu utekelezaji wake na mafanikio yake yanakuwa hayaonekani wananchi wanakuwa hawaoni faida ya kufanya marekebisho ya sheria au kutunga sheria mpya.

Sheria hii mpya iliyotungwa ya wakfu ilirejesha mamlaka kwa Kamisheni kurudisha mali zote ambazo zilichukuliwa mali za wakfu katika mikono ya Kamisheni hii. Kuhakikisha kwamba zinafanya lile lengo lilokusudiwa.

Mhe. Spika, kama tulivyosema katika ripoti yetu, mali za Wakfu ni mali ambazo tunazishikilia kwa amana ni mali za Mwenyezi Mungu waliozitoa wamezitoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kwa utaratibu huu tuliouweka kwamba serikali imepitisha sheria na mara nyingi utakuta kule kwenye kikwazo katika kurejesha mali za Wakfu ni zile mali ambazo za Wakfu lakini zilichukuliwa zinashikiliwa na Serikali kupitia Wizara, Idara au Afisi nyengine. Kuna malalamiko makubwa kutoka Kamisheni ya Wakfu kwamba hizi serikali kupitia Idara, Wizara na Afisi nyengine kwamba hawatoi ushirikiano wa kutosha katika kusimamia utekelezwaji wa sheria ile kwa kuzirejesha mali zile za Wakfu.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba hili Waziri alitizame kwa karibu sana kupitia kwa Kamisheni na serikali kwa ujumla wake kwa sababu inawajibika kwa pamoja, kila wakati nalisema hilo itoe mashirikiano ili utekelezwaji wa sheria hii uweze kufikiwa.

La pili ambalo ni la mwisho kwa mchango wangu nipo katika ukurasa huo huo juu pale katika ukurasa wa 166 kifungu (d) kinasema:

> "Kitengo cha Wakfu chini ya Kamisheni kimefanya ukaguzi wa nyumba za Wakfu na kuangalia upya kodi za nyumba zinazolipwa sasa na kupendekeza kodi mpya".

Mhe. Spika, jimbo ninaloliwakilisha hapa jimbo la Mji Mkongwe ni eneo moja ambalo nyingi nyumba za Wakfu kwa kisiwa cha Unguja zipo pale kama ilivyokuwa kwa jimbo Chakechake katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, kuna malalamiko makubwa sana kutokana na ongezeko la kodi kwa nyumba na milango ya biashara ambayo ipo katika nyumba hizi za Wakfu. Na mimi kama mwakilishi wao, wapiga kura wa Mji-Mkongwe walinita, wakanipa malalamiko yao haya tumekuwa tukiya *rays* katika vikao vyetu vya Kamati lakini bado Mhe. Spika, majibu yake hayaridhishi.

Kimsingi mimi sipingi suala la kwamba kila wakati kama serikali kama tu mwengine anayemiliki mali na hasa Kamisheni ya Wakfu kwa sababu mali si zake ni za wenyewe Wakfu, italazimika kufanya utaratibu wa kupitia kodi na pengine kuongeza lakini kinacholalamikiwa na wananchi ni kile kiwango cha uongezekaji wa kodi. Utakuta kodi imeongezeka kwa asilimia 200 au asilimia 300 na juwa wizara inatwambia kwamba ilikuwa muda mrefu hazijaongezwa na wameangalia bei ya soko ilivyo. Lakini katika taratibu za kawaida kabisa kuongeza kwa mkupuo mmoja asilimia 100 au 200 au 300 ya kodi iliyokuwepo mwanzo kwa wapangaji ambao wanaishi katika nyumba hizo ambao wengi hali zao ni za chini inakuwa kama vile tunawashtua kwa mpigo mmoja na inakuwa kazi kubwa kuweza kwenda sambamba na ongezeko lile kubwa la kodi.

Pili hapo hapo aina zenyewe za uongezekaji, kumekuwa kama vile hakuna fomula, kuna baadhi ya nyumba utakuta katika nyumba moja kuna sehemu tatu ambazo zimegaiwa na zote zipo sawa sawa lakini utakuta kila mtu kapewa kiwango chake cha ulipaji. Lakini kama hiyo haitoshi ile barua ya kuongezeka kodi unaambiwa umeongezewa kwa mfano kuanzia sasa utalipa shilingi laki mbili na ishirini elfu kutoka shilingi thamanini elfu uliyokuwa ukilipa awali. Wakati ile iliyokuwa ikilipwa awali haikuwa dhilingi thamanini elfu pengine mtu alikuwa akilipa shilingi arubaini elfu au shilingi thalathini na tano elfu lakini kaandikiwa hapo awali ilikuwa thamanini elfu.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi sana katika utekelezaji wa suala hili. Ningemuomba Mhe. Waziri alifuatilie hili na pia atupe ufafanuzi wake. Lakini nimuombe kwamba akae na watendaji wa Kamisheni ya Wakfu kuangalia isijekuwa watu wanaingiza maslahi yao katika suala hili katika kupanga hizi bei.
Baada ya kusema hayo kwa niaba ya wapiga kura wa Mji-Mkongwe niseme naiyunga mkono ripoti ya Kamati yetu hii na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai asubuhi hii tukaweza kukutana katika Baraza lako hili tukufu.

Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii niweze kuchangia machache katika Kamati yetu hii. Tatu nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa hotuba yake nzuri na kama alivyosema mwenzangu Mhe. Ismail Jussa ni mtu mwenye busara kwa hivyo Kamati yetu tunaweza kuiyendesha vizuri bila ya migogoro.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu katika Afisi ya Mrajisi na hili nichangie kuhusu usajili wa vizazi na vifo. Hili ni tatizo kubwa ambalo jamii yetu bado haina uweleo wa kutosha juu ya jambo hili. Nimuombe Mhe. Waziri jamii bado inahitaji kuelimishwa kwa kina juu ya umuhimu wa kusajili vizazi na vifo. Na nimuombe Mhe. Waziri elimu hii ni vizuri ikaweza kupelekwa katika shehia zetu kama vile tunavyowatumia masheha wetu katika kazi mbali mbali, basi na elimu hii tungeweza kuwapelekea Masheha. Kwa sababu Sheha utakuta ana wajumbe wake kumi na katika wajumbe wale kila mjumbe ana kanda yake. Hivyo kinapopatikana kizazi au kifo basi mjumbe yule katika mahala pale alipo akaweza kwenda kufatilia maelezo ya pale na hatimaye akayapeleka kwa sheha wake tungeweza kuzipata takwimu nzuri tu za vizazi na vifo.

Mhe. Spika, pia niende katika upungufu wa magamba ya vyeti vya kuzaliwa. Hili ni tatizo sugu na nimuombe Mhe. Waziri kujitahidi kutatua tatizo hili ili kuweza kuwapa moyo wazazi ambao wanapopata watoto wao huenda kutafuta vyeti hivi kwa ajili ya watoto wao. Usumbufu ambao unakuwepo mpaka mzazi akakata tamaa na kumuacha mtoto hana cheti na hatimaye anapokuwa mkubwa gharama zinakuwa zimeongezeka zaidi. Nimuombe Mhe. Waziri kulifatilia kwa kina tatizo hili ili tuweze kuwapa moyo wananchi wetu juu ya jambo hili.

Mhe. Spika, pia niende upande wa Mahakama pia nimuombe Mhe. Waziri tujitahidi sana katika upande wa Mahakama zetu hasa ukizingatia majengo mengi ya Mahakama ni mabovu. Na kile chombo Mhe. Spika, ni chombo muhimu sana na chombo kikubwa sana na pale ndipo zinapotolewa haki za watu, kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwanza yale mazingira yanayofanyiwa kazi yawezekua mazuri ili hata yule anakwenda kudai haki yake pale aamini kama anaweza akaipata katika mazingira yanayostahiki. Lakini ikiwa majengo hayana hadhi nzuri pia kunaweza kukatisha tamaa kama kweli haki yako unaweza ukaipata kama inavyostahiki.

Mhe. Spika, tuchukue mfano mdogo tu kama wewe una shida ya fedha unakwenda kumkopa mtu pengine fedha zile ni nyingi, lakini umetoka nyumbani kwa miguu unamwendea tajiri kwenda kumkopa mamilioni ya pesa hivyo sio rahisi kukupa. Lakini ukenda na gari japo ya kuazima basi anaweza akakuamini kama fedha akikupa utazirejesha. Kwa hivyo, na sisi lazima tuboreshe majengo yetu ili tuone kama kweli haki pale inaweza kupatikana. Mhe. Spika, pia majaji wetu na wao wako katika mazingira magumu, hawana nyumba wala hawana usafiri. Mhe. Spika, mambo hayo kwa Majaji ni mazingira magumu kulingana na kazi zao.

Mhe. Spika, pia niende katika Mahakama ya Kadhi. Kwanza nichukue fursa hii kuishukuru serikali na kuipongeza kuweza kutupatia makadhi wetu hawa ambao wanaweza kututatulia migogoro yetu ya ndoa. Lakini pia niwaombe makadhi wetu wawe makini sana wanapopelekewa madai ya talaka, hivyo kabla ya kutoa maamuzi yao basi ni vizuri wakaweza kuwashirikisha wazazi wa pande zote mbili ili hukumu itakayotolewa pale iweze kuwa sahihi na kupunguza talaka zile la kiholela. Mhe. Spika, pia niwaombe makadhi wetu waweze kutupatia elimu ya ndoa kabla ya wana ndoa wenyewe kufunga ndoa ili pia ndoa zetu ziweze kudumu.

Mhe. Spika, niende katika Ofisi ya Mufti na hiki nacho ni chombo muhimu kwa Waislamu kwani kinashiriki sana katika kutatua migogoro ya Waislamu ukizingatia wanakwenda katika Misikiti na Madrasa, lakini chombo hiki nacho kimekosa usafiri hivyo migogoro hua inachukua muda mrefu kutatuliwa kwa sababu hawapati kufuatilia. Mhe. Spika, kwa heshima nimuombe Mhe. Waziri na hili aliangalie sana ili viongozi wetu hawa waweze kutatua migogoro kwa wakati muafaka.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache mimi kwa niaba ya kamati yangu naunga mkono ripoti hii Kamati ya Katiba na Sheria kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi asubuhi hii kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na kamati yake nzima.

Mhe. Spika, kwanza niishukuru wizara pamoja na waziri wake kwa uwajibikaji mzuri katika wizara yao, kwa kweli mimi niende kwenye upatikanaji wa fedha ni kwamba upatikanaji wao ni kua wamepata pesa za maendeleo pamoja na matumizi ya kawaida kwa asilimia 94. Kwa hivyo, pia niwapongeze Wizara ya Fedha kwa uwajibikaji wao mzuri.

Mhe. Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye Idara hii ya Nyaraka ambayo ni idara muhimu nayo pia inahitaji bajeti ya kutosha kwa sababu idara hii ni muhimu sana na inahifadhi nyaraka hizi ambazo kama sikosei kwamba huko nyuma Zanzibar ilibahatika kuwa ni kituo kikuu cha kukusanya nyaraka hizi. Kwa hivyo, nina hakika kwamba nchi mbali mbali wanakuja kutafuta nyaraka zao, na kwa kweli nyaraka zenyewe zinakua katika hali ngumu na hali mbaya hivyo inahitaji kuwe na pesa za kutosha. Mhe. Spika, vile vile niwashukuru kile kitengo cha *conservation* ambacho kiko pale kwa kazi ngumu na nzito ambayo saa nyengine hata bajeti inakua haikidhi, lakini wanajitahidi na nishukuru kwamba sasa hivi tunakwenda kwenye hii *system* mpya ya *digital*. Kwa hivyo, nashukuru sana kwamba nyaraka zile zitahifadhika vizuri na huoni raha kama hukutembelea idara ile, pale pana mambo mengi na ningeomba na wewe Mhe. Spika, siku moja ufanye ziara ya makusudi na hata Rais wetu mpate kuona raha na utamu wa sehemu ile ya nyaraka ambayo kuna nyaraka mbali mbali za taifa ambazo zinahitaji kutunzwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, niseme kwamba pale panahitaji nguvu za ziada ili tuweze kuzihifadhi nyaraka zile kwa vizuri zaidi.

Mhe. Spika, vile vile Ofisi ya Mufti kama alivyosema mwenzangu sina haja ya kurejea lakini hizi ni taasisi muhimu na ambazo ni za kidini. Kwa hivyo, ni lazima tuzipe nguvu zote ili na wao waweze kutekeleza zile kazi zao za kila siku. Vile vile Ofisi ya Mwanasheria nayo ina majukumu mengi niseme kwamba Mwanasheria ni mtu ambaye muadilifu na muaminifu na ni mtu mzuri sana, kwani amewahi kuwa Katibu wangu Mkuu nilipokua Wizara ya Katiba na Utawala Bora maana yake nimeshaogelea kwingi. Kwa hivyo, nashukuru kwa kumpata mtu huyu ambaye alitokea mbali alikuwa ni Mkurugenzi wa Mashtaka ameondoka pale amewacha mambo mazuri, nina hakika na hapa atafanya vizuri.

Mhe. Spika, niende kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa uwajibikaji wake pamoja na watendaji wake kwa kweli ni mtu hodari na ni mtu ambaye anajituma sana. Lakini leo nipitie kwako wewe Mhe. Spika, kwamba bado Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu bado hajapata ile haki yake hasa kwa sababu kama sisi Baraza la Wawakilishi tumo katika katiba na vile vile Bunge limo ndani ya katiba, lakini bado Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haipati ile haki na hasa kwa kupitia Tanzania. Lakini lakusikitisha zaidi ni pale inapotokea nafasi mara nyengine hua hata hana habari, hajuilishwi na wenzetu au tuseme kuna tatizo gani liliopo, lakini kulikua na haja ya kua ashirikishwe kikamilifu na zikitokea safari za nje ikiwa *CAG* wa Bara haendi basi kuna ulazima apewe *CAG* wa hapa ili aende. Lakini kwa udhaifu uliokuwepo sasa hivi anakwenda mtu pengine ni ofisa lakini *CAG* wa hapa anakua bado hajapewa ile nafasi ni jambo la kusikitisha. Mhe. Spika, ni kazi yako uzungumze na Spika mwenzako wa Bara ili hizi nafasi zikija basi na sisi huku tupewe.

Mhe. Spika, vile vile na sisi ili tufanye *shearing idea* na wenzetu na nilazima na sisi tuwe katika mfumo kama huo. Kwa hivyo, hapa tunakosa mambo mengi ikiwa yeye *CAG* hatambulikani bila shaka na sisi kama *PAC* tutakua hatutambulikani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa haya machache ili nisitumie muda wako mwingi naunga mkono ripoti hii pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Amani.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi kidogo yakuweza kuchangia katika kamati ya kudumu, kamati hii yetu ambayo ni muhimu sana tunastahiki na sisi kutoa mchango wetu kwa sababu na mimi Mjumbe katika Kamati hii ninayo kidogo mawili matatu yakuweza kuzungumzia.

Mhe. Spika, mimi kwanza katika suala zima nataka nitoe ushauri kwa Baraza hili tukufu kwamba jambo muhimu kwa ajili ya mambo mengi mara nyingi hua tunazungumzia habari ya afya zetu. Kwa hivyo, kuna lile suala la mfumo wa bima wa afya ambao mara nyingi tunashauriwa tujiunge katika bima hii kwa sababu yakuweza kupata manusura katika afya zetu. Kwa hivyo, tujue kwamba tukijiunga na bima hii ya afya itakua ndio kama mkombozi wetu kwa ajili ya kupata huduma bora. Mhe. Spika, ningewashauri wenzetu wote waweze kujiunga katika bima hii ya afya bora ambayo wachachagizi wa bima hii itakua ni hii Wizara ya Utumishi wa Umma ikishirikiana na Wizara ya Afya na vile vile inashirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kwa hivyo, hizi sehemu tatu ndio wao watakaotuwezesha sisi kuweza kujiunga na kusukuma mbele suala zima la bima. Mhe. Spika, huo ni ushauri natoa kwa wenzangu kwamba tuweze kujiunga na bima hii.

Mhe. Spika, suala la pili nikitaka nizungumzie juu ya vyuo vya mafunzo. Mhe. Spika, vyuo vya mafunzo ni binadamu walioko kule kama sisi lakini wale ambao wameingia katika hatia mbali mbali. Lakini ukitizama hali wakati tunapotembelea katika maeneo haya kuna hali ambayo kidogo inakwenda kinyume na haki za binadamu kwamba wenzetu wamepelekwa katika vyuo hivi kwa dhamira ya kupewa mafunzo ili watakapotoka wawe raia wema. Mhe. Spika, lakini hali ya kimaisha ambayo wanaishi watu hawa kama binadamu wengine inakua kidogo sio ya kuridhisha. Kwa mfano, ukitizama katika masuala yale ambayo tulitaka tupate mabadiliko ya vyoo watu hao waweze kwenda haja kama binadamu wengine, lakini hali ni ile ile ya mtondoo mpaka hivi sasa. Kwa hivyo, ningelishauri kwamba waziri anayehusika na masuala haya aweze kuangalia kwamba tutapata vyoo vya kisasa kama binadamu wengine ili hali ile inayojitokeza sio ya kiafya. Pia jambo jengine ni kwamba chakula

wanachopata sio cha kutosha, wapewe chakula kizuri na kuwashibisha kwa sababu ni watu wanaofanya kazi ngumu sana na chakula wanachopata sio kingi sana na hakina afya bora.

Mhe. Spika, malalamiko mara nyingi hua inatokezea kua hawapati vitoe vya kutosha kwa mfano samaki hawapati, mboga mboga na matunda pia hawapati. Mhe. Spika, kwa kua mtu tunamuweka ndani kwa muda mrefu basi ni lazima matunda apate, samaki apate na mboga mboga apate au vyenginevyo mtu kama huyu ambaye unataka kumtumilia kwa kazi za nje basi atashindwa kufanya kazi kwa sababu hajatimiza chakula bora katika mwili wake. Mhe. Spika, hali nyengine ambayo imejitokeza ni kua mara nyengine magodoro ni mabovu ya muda mrefu mwili wao hua unagongana na sakafu ya chini. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba magodoro yanapatikana yakutosha.

Mhe. Spika, hali ya kesi za vijana ambao mara nyingi wanawekwa rumande hua wanakaa muda mrefu kabla hukumu hazijatolewa. Kwa hivyo, hili suala naliomba vijana hao wasikae muda mrefu kwa kesi ndogo ndogo au za wizi mdogo mdogo kukaa wiki tatu au wiki nne kabla ya kesi zao hazijenda.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nimeligundua ni kwamba watoto bado hawajapata stara nzuri katika magereza haya na mwisho Mhe. Spika, katika hili ni suala zima la rufaa ya kesi. Rufaa zinachelewa muda mrefu sana hazishugulikiwi inakua walioko kule hawapati lolote kujua masuala ya rufaa zao za kesi ambazo wameziomba.

Mhe. Spika, suala jengine nataka nilizungumze ni suala la vyeti vya kuzaliwa, na mimi napenda suala hili nilizungumze kidogo kwa sababu hili suala limetugusa sote. Mhe. Spika, suala hili limekua ni zito na ni gumu sana, tuangalie historia ya wazee wetu. Mhe. Spika, wazee wetu hapo zamani walikua hawashughuliki kutayarisha mambo ya vyeti vya kuzaliwa hili ni jambo lilokua ni zito kwa wazee wetu na gharama zake katika kutengeneza hivi vyeti ni kubwa sana. Mhe. Spika, sasa tuangalie ule ubinadamu kweli sheria ipo lakini sheria tunaweza tukabadilisha kwa sababu watungaji ni sisi na wabadilishaji ni sisi, kweli sheria zipo lakini gharama zake ni kubwa sana na wao wanahitaji kupata vyeti. Mhe. Spika, vyeti hivi haviwezi kupatikana kwa mara moja na wazee wanashindwa kuwatengenezea vyeti watoto wao. Kwa hivyo, mimi ningeliomba kwamba hili suala Mrajis Mkuu wa Serikali atusaidie kidogo katika kuliboresha hili suala likawa jepesi zaidi kwa watu kuweza kupata vyeti bila ya matatizo. Mhe. Spika, tunataka tuingie katika haki za binadamu kila mmoja ana haki ya kupata cheti cha kuzaliwa kama watu wengine wanapozaliwa wanapata paspoti zao pale pale, kwa nini kuwe na ugumu wakuweza kupata vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Spika, hivi vyeti vya kuzaliwa vinafaida yake nyingi sana, anapopata hicho anaweza kutengeneza kitambulisho chake cha uraia ambacho kinaweza kumsaidia katika kupata haki zake nyengine, kupata ajira, kupata kufanya biashara na shughuli nyengine ndogo ndogo. Kwa hivyo, hivyo vyeti vya kuzaliwa ni muhimu sana ningeomba Ofisi hii ya Mrajis Mkuu wa Serikali atusaidie pamoja na waziri.

Mhe. Spika, jambo jengine katika suala hili ni kwamba tunasema hivi visiwa ni viwili, kuna Unguja na Pemba kwa nini Pemba mpaka leo hili suala sasa hivi tumezidi kuendelea *computer* tunazo Unguja na Pemba kwa nini haya mambo hayawi *computerised* na kule badala ya mtu kutoka Pemba akaja Unguja kwa kuja kutafuta cheti cha kuzaliwa au kumbukumbu za vyeti vya kuzaliwa. Kwa hivyo, ili kuondosha usumbufu ningemuomba Mhe. Waziri katika suala hili auondoshe usumbufu kwa wananchi wale waliokua tayari kutaka kujua vyeti vyao vya kuzaliwa viweko katika sehemu zao mbali mbali za kule Pemba kwa hiyo ni moja katika haki yao. Mhe. Spika, tufikiri kwamba muda umekua mrefu watu hawajapata vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumza na kwa sababu na mimi ni mmoja katika Kamati hii ya Katiba na Sheria ambalo nimehisi ni muhimu nilizungumze ni suala la Ofisi ya Mufti. Mhe. Spika, suala hili katika Ofisi hii ya Mufti kuna kitu muhimu ambacho nataka nikizungumzie.

Mhe. Spika, unajua hapa inapofika mwezi wa Ramadhani kunatokezea mgongano wa wananchi au jamii wote kwa jumla, kwamba kunakuja wakati kila mtu anafunga kwa wakati wake na anafungua kwa wakati wake, na anaswali kwa wakati wake hivi ndivyo inavyokua. Mhe. Spika, ili hili suala tuachane na tabia hii hebu hawa Mufti na Mashekhe wakae kitako pamoja watutolee uamuzi katika masuala haya.

Mhe. Spika, jopo la Mashekhe likae kitako lizingatie suala hili, kwamba hili suala kila mmoja afunge kwa siku zake na afungue kwa siku zake sasa hii imekua Ramadhani na Sikukuu imekua sikukuu ya Kibohora, maana Bohora yeye anaanza 28 mpaka 28 sisi hatujui tunakwenda wapi kwani sisi sote ni Waislamu tuangalie nini uislamu unataka katika suala hili. Mhe. Spika, mimi ningelimuomba Mufti akae na Mashekhe wenzake watupe uamuzi rasmi katika masuala haya, hii haipendezi kwa Zanzibar kwa sababu haijapata kutokezea kwamba leo

hawa imefika siku, leo hawa wanakula sikukuu wengine bado. Hili jambo halipendezi Mhe. Spika, mimi ningeliomba hili suala ni muhimu likaliwe kitako na lijadiliwe na tupewe maamuzi katika haya.

Mhe. Spika, naheshimu wakati wako kwa sababu kuna mambo ya kuzungumza kwa hivyo mimi naunga mkono ripoti hii ya Kamati ya Katiba na Sheria. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi napenda kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaaliwa kuwa wazima na kuweza kuhudhuria hapa ili kuendelea na shughuli zetu za kawaida. Lakini pili naomba kwa dhati kabisa niishukuru Kamati ya Katiba na Sheria kwa maelekezo yake na ushirikiano wake katika wizara yangu wakati wote wanapokua na masuala yoyote wanakuja wizarani na tunajadili kwa pamoja. Kwa hivyo, ushirikiano wao Mhe. Spika, napenda niwapongeze sana na kuwashukuru sana. Mhe. Spika, lakini shukurani za pekee zimuendee Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa muongozo wake mzuri katika kufanikisha masuala haya.

Mhe. Spika, napenda niwashukuru wachangiaji wote ambao wamechangia katika ripoti hii, wachangiaji wote waliochangia ni waheshimiwa 8 akiwemo:

1. Mhe. Ali Abdalla Ali - Mwenyekiti wa Kamati.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbaraouk
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Fatma Mbarouk Said
7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis

Mhe. Spika, kwa ufupi ni mambo matatu ambayo yamezungumzwa muhimu. Kwanza ni suala la Mahakama, la pili ni suala la Wakfu na la tatu ni suala la Mrajis Mkuu wa Serikali. Hayo ndio mambo muhimu matatu ambayo yamezungumzwa ingawa yapo mengine pia yameguswa guswa lakini haya ndio yaliyochomoza sana.

Mhe. Spika, nikianza na suala la Mahakama ni kweli Mahakama zetu zina matatizo kidogo kesi zinarundikana na Mahakama nyengine sio nzuri kama walivyosema. Mhe. Spika, hiyo ni kawaida hatuwezi kwa wakati mmoja tukazitengeneza Mahakama zote, lakini pia tujue kwamba kuna upungufu wa Mahakimu na Majaji ingawa tumejaribu kuajiri upungufu huu kidogo umepungua, lakini bado tunao upungufu huo, na inashaallah kila penye uwezo tutajaribu kuongeza idadi ya wafanyakazi hawa ili tuweze kupunguza *load* kesi ambazo zipo.

Mhe. Spika, pia ningelisema kwamba ucheleweshaji wa kesi hauwendani na Mahakama peke yake au na Majaji peke yake kuna *factors* nyingi ambazo nazo zinahusisha ucheleweshaji wa kesi. Kwa mfano, uchunguzi, mashahidi na mambo kama hayo, lakini hayo yote kwa pamoja tumeyasikia na *inshaallah* tutajitahidi.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma alisema Mahakama zetu hazina nguvu. Mimi napenda nitofautiane nae kidogo kwa kusema kwamba Mahakama zetu nazo zina nguvu kama Mahakama nyengine alizozisema. Mahakama yetu inaweza hata ikasema waziri au mtu yeyote akamatwe na achukuliwe kupelekwa Mahakamani. Ni kwamba nguvu hizo zipo lakini nafikiri haijafika tu lakini ikifika kama waziri au mtu mwengine yeyote mkubwa atakwenda kinyume na utaratibu uliowekwa na Mahakama basi Mahakama hiyo itatoa amri hiyo. Kwa hivyo, hakuna matatizo kwamba Mahakama zetu hazina nguvu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa katika suala la Mahakama ni suala lile la Tume ya Utumishi. Ni kweli kuna Tume ya Utumishi ya Mahakama na kuna Tume ya Utumishi ile kubwa ya Serikalini. Lakini hii tume ya utumishi ya Mahakama ni tume ambayo inahusiana na Mahakimu pamoja na Majaji kama ilivyosema katiba. Lakini alisema kwamba je huyu Mrajis kwa nini yeye ana *facilities* zaidi kuliko Mahakimu au Majaji katika Mahakama.

Mhe. Spika, napenda niseme kwamba Mrajis siku zote lazima masharti yake moja awe naye ni Hakimu wa Mahakama. Kwa hivyo, nae huyu Mrajis ingawa amepewa kazi nyengine lakini moja ni kwamba lazima awe ni Hakimu. Kwa hivyo, hakuna *facilities* ambazo anapata *extra* isipokua kwa sababu ya ule urajis wake ndio kidogo anaweza akawa na mambo mengine ambayo kidogo ni tofauti na Mahakimu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la vyeti vya kuzaliwa. Nakubali kwamba tuna matatizo ya vyeti vya kuzaliwa, lakini kama Waheshimiwa Wajumbe watakumbuka katika suala langu ambalo nimelijibu hivi karibuni katika Baraza lako hili tukufu, nilisema kwamba tunakubali kuna matatizo ya vyeti,

vyeti vingi vipo havijatolewa na hata nilitoa idadi ya vyeti ambavyo tulifanya utafiti na tukaona kwamba bado havijatolewa. Mhe. Spika, kwa Mjini Magharibi tulisema kwamba ni vyeti kiasi ya 3,000 kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja ni vyeti 1,500, kwa Chake Chake ni 1,500, Mkoani ni 1,300, Wete ni 500 na Micheweni ni 500. Mhe. Spika, pia nilisema katika Baraza lako tukufu kwamba tumejitahidi kuwalipa watu *over time* ili vyeti hivi vimalizike.

Mhe. Spika, nina furaha kusema kwamba kwa Mjini Magharibi vyeti vyote 3,000 vimeshamalizika, tatizo dogo lililopo ambalo hili naamini baada ya siku mbili litamalizika. Ni kwamba vile vyeti kama mnavyojua kiutaratibu ni lazima viwe *compare* kwa hiyo vyeti karibu 2,000 vimeshamalizika na vimeshatiwa saini na watu wameshaanza kuchukua. Mhe. Spika, vyeti 1,000 vimeshamalizika katika hivyo 3,000 vimeshatiwa saini lakini bado havijawa *compare* lazima tu-*compare* ili tuhakikishe kwamba vyeti vile ni feki au sio feki. Baada ya hapo nafikiri baada ya siku mbili tatu tatizo hili la Mjini naamini litakua halipo na hivi sasa tuna *focus* tuvichukue vyeti vyote vya Kaskazini 1,500 navyo tutoe *over time* ili watu wavipige. Mhe. Spika, kama nilivyosema katika kikao chako cha Baraza katika suala ambalo nimelijibu ni kwamba naamini katika mtindo huo ambao tunafanya basi *inshaallah* inapofika kwenye Juni vyeti vyote hivi ambavyo bado vilikua havijatoka basi tutakua tumeshavimaliza. Kwa hivyo, tatizo hili ni kweli, lakini naomba tushirikiane, kwa sababu kwanza ilikuwa fedha hakuna za kununulia vyeti, tukafanya mpango tukapata fedha na tukanunua vyeti vyote ambavyo vinahitajia kupigiwa. Kwa hivyo, vyeti hivyo tunavyo, na vyeti vyengine vitabakia ambavyo hivyo vitatumika kwa wale ambao wanazaliwa katika kipindi hichi.

Kwa hivyo suala la kuwa na vile vyetu itakuwa suala hilo halipo tena, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujalia baada ya muda mfupi, vyeti vile ambavyo watu wengi wanalalamika hawajavipata basi watakuwa wameshavipata. Isipokuwa ombi langu ni kwa wale watu wa Mjini Magharibi, hivi sasa wanaweza kwenda kuchukua vyeti vyao kwa sababu vyeti vyao hivyo sasa vimeshaanza kuwa tayari.

Mhe. Spika, suala jengine muhimu ambalo lilizungumzwa, ni suala la nyumba za wakfu. Mhe. Spika, nyumba za wakfu napenda niseme mambo matatu. Kwanza, nyumba za wakfu si nyumba za serikali, nyumba za wakfu ni nyumba zilizowekwa na watu ambao wameshafariki au pengine wameweka wakfu tu, lakini kwa madhumuni ya kitu fulani au kuwasaidia watu fulani. Kwa hivyo, ni tofauti kuzifanya nyumba za wakfu kama ni nyumba za serikali.

Sasa la pili lililotokea ni kwamba, katika hizi nyumba za wakfu bei za zamani Mhe. Spika, zilikuwa ni ndogo sana, kwa mfano hapa nina mifano mingi, nyumba ambayo ni ya ghorofa mbili ipo Shangani nambari 92 mtu anaweza kwenda kuitizama, nyumba hii ina ghorofa mbili mtu anakodishwa kwa shilingi 22,000. Sasa hii kwa kweli ni ndogo sana ukilinganisha na hali ilivyo. Nyumba hii Mhe. Spika, hivi sasa ni mbovu tumetakiwa sisi wenye dhamana tunaokamata hiyo wakfu itengenezwe, na amekwenda ***valuer*** amesema ili kuitengeneza nyumba ile zinatakiwa shilingi 60 milioni. Sasa kama mtu huyo atalipa shilingi 22,000 kwa mwezi hizi shilingi milioni sitini tutazipata lini? Lazima tutizame hiyo, hiyo ni moja Mhe. Spika.

Lakini pia tuna ripoti hii Mhe. Spika, ripoti hii tumepitia nyumba zote za wakfu matatizo yake na namna gani tunaweza tukazihuisha kidogo. Ripoti inasema kwamba zile nyumba zimegawika mafungu matatu, kuna A, B na C. Inaweza ikawa nyumba moja ina milango mitatu, sasa nyumba ile kila mlango unaweza ukawa *graded* katika *grade A*, mwengine B na mwengine C, kutokana na hadhi ya ule mlango ulivyo na kutokana na usafi na uzima wa ile sehemu. Kwa hivyo, mlango mmoja unaweza ukawa ni shilingi 30,000 kwa mfano, mlango wa pili ukawa shilingi 70,000 na mlango wa tatu ukawa shilingi 150,000 kulingana au kutokana na uzima wa zile nyumba zilivyokuwa *graded*. Kwa hivyo, watu wanaokaa pale wanaweza kuona milango imefanana au nyumba moja imefanana lakini moja inalipa zaidi na moja inalipa kidogo.

Kwa mfano, kuna nyumba nambari 92 hizi ni nyumba mbili sawasawa, mjengo sawasawa na kila kitu, lakini moja inalipa kodi shilingi 20,000, mmoja analipa kodi shilingi laki moja, kwa sababu ile grade ya ile nyumba ni nzuri zaidi kuliko ile nyengine. Lakini sisemi kama hakuna matatizo, kwa hivyo pale ambapo yapo matatizo naomba wale wanaopanga waweze kuja ofisini ili tuweze kuyatizama na kuweza kuyatatua matatizo hayo.

Lakini moja kubwa ambalo Mhe. Spika naomba nilisema hapa ni kwamba, wapangaji wetu nao wana matatizo makubwa. Matatizo ni kwamba wajue kuwa zile nyumba ni za wakfu na zile nyumba zimelengwa kwa mambo fulani. Kwa mfano, kuwalipia watoto waliopo au kulipia msikiti mfano kufanyia matengenezo au kitu kama hicho. Sasa kinachofanyikana ni kwamba unamkodisha mtu kwa ndogo shilingi 30 elfu, kuna kesi humu Mhe. Spika, nyumba nambari 1,590 iliyoko Mchambawima.

Kuna mtu alikodishwa kwa shilingi 20 elfu, sasa alipokodishwa kwa bei hiyo yeye akakodisha kwa shilingi 140,000; shilingi 20,000 anachukua anazileta kwetu na shilingi 120,000 anazitia ndani ya mfuko, ndio hao hao wapangaji. Tulipogundua sisi tukamwambia tutakunyang'anya tukatia mnada katika nyumba ile kukatokea watu wakafika mpaka shilingi 180,000 kwamba watakodi kwa mwezi wakati yeye alikuwa anakodi kwa shilingi 20,000. Huyu huyu aliyekuwa anakodi kwa shilingi 20,000 akasema mimi nitalipa kwa shilingi laki mbili. Kwa hivyo, nasema haya Mhe. Spika, ili mtu aone anakodishwa kwa shilingi 20,000 hivi sasa yuko tayari kwa kulipa shilingi laki mbili kwa sababu ya ile *value* na pale pahala palivyo.

Sasa ni kweli kutokana na hayo tumezidisha bei za nyumba ili kusaidia matengenezo, na ili kuwasaidia wale watu ambao wamewekewa wakfu huo, na bei hizo zimo katika ripoti. Kwa mfano, nyumba ilikuwa na shilingi 100,000 sasa hii ripoti inasema tuongeze asilimia mia moja. Kwa hivyo, ni kwamba ulipe shilingi laki mbili, lakini bado kuwaonea huruma wananchi wetu tukasema tusiongeze kwa pamoja kwanza tutaanza na asilimia hamsini kwa hivyo utalipa asilimia 50, halafu asilimia 75, baadae tena ndio utalipa asilimia 100. Kwa hivyo tulikuwa tunakwenda kwa hatua.

Lakini Mhe. Spika, hayo tunayoyafanya yote bado wananchi wao wanaleta matatizo katika sehemu hizi za ukodishaji wa nyumba. Kwa mfano Mhe. Spika, kuna mtu nyumba nambari 316 Gizenga, nyumba hii tumemkodisha mtu kwa dola 15 yaani 180 kwa mwaka, mtu huyu huyu kamkodisha mtu mwengine kila siku anapandisha mpaka akamwambia kwamba sasa mwaka huu 2012 atalipa dola 4000 kwa mwaka, yaani sisi tumemkodisha kwa dola 180 kwa mwaka, yeye anamkodisha mtu kwa dola 4000. Yule mtu akawa hawezi kulipa zile akaja ofisini kwetu kuja kulalamika kwamba anapandishiwa bei kubwa. Sasa watu namna hii Mhe. Spika, maana yake madhumuni yake ni kwamba au tafsiri yake ni kwamba, anakosesha wale waliowekewa wakfu mapato, anakosesha serikali mapato, na anazichukua fedha nyingi na kuzitia katika mfuko wake.

Sisi mtu kama huyu kwa mfano tulimfuta pale pale, baada ya kumfuta tukamwambia akodi huyu aliyekuwa anamkodisha kwa shilingi 4,000 tukamwambia akodi kwa shilingi 2000 kwa mwaka. Kwa hivyo, pato lote hilo alilokuwa analitia ndani ya mfuko tukalipata sisi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nikielezea masuala haya ya nyumba za Mji Mkongwe tutakwenda sana, lakini naamini kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa kuna matatizo sehemu zote mbili, kuna matatizo ya wapangaji kuna matatizo ya ofisini. Kwa hivyo, mimi nashukuru Mhe. Jussa ameyasema hayo nimemuomba kwamba aniletee hayo malalamiko hayo ya watu wanaofanya hivyo au walio na matatizo hayo tuyatizame *case by case*, hatuwezi kutoa hapa *general* lazima tutizame *case by case*, kwa sababu kuna wengine wametengeneza nyumba, nyumba zao ni nzuri, kuna wengine hawajatengeneza. Kwa hivyo, tukifanya hivyo tutapata *solution* ya kuwasaidia wananchi wetu, lengo ni kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni suala lile ambalo lilizungumzwa na Mhe. Suleiman Hemed kuhusu suala la Ofisi ya Mufti, kwamba huu mwezi utizamwe na tukubaliane kwamba mwezi uandame kwa siku moja. Sasa hili Mhe. Spika, ni suala la binafsi mtu na imani yake, lakini si suala baya, tumekaa na wenzetu hawa wa Mufti na utaratibu huo tunaujadili, tunaitizama kwa pamoja ili tuweze kupata kitu ambacho kitakuwa hakina matatizo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda sana niwashukuru kamati na wachangiaji kwa maoni yao mazuri, na yale mengine ambayo hatukuyasema humu nawahakikishieni kwamba tutayafanyia kazi kwa maslahi yetu sote. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi hii kupata fursa ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo yameelezwa hapa. Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa, lakini tatu nimshukuru Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na kamati yake, kwa mashirikiano mazuri ambayo wametupa wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi hii katika wizara yetu.

Mhe. Spika, na mimi nataka nimpongeze Mhe. Mwenyekiti na nikubaliane na taarifa hii isipokuwa mtaniwia radhi niweke sawa baadhi ya mambo ili ripoti hii niweze kuichukua kwa ukamilifu wake na kwenda kuifanyia kazi hasa kama vile Mhe. Ismail Jussa alivyoelezea. Maana madhumuni ya ripoti hii ni kuletwa hapa na hatimaye taasisi ya wizara inayohusika kwenda kuyafanyia kazi yale ambayo yameelezwa humu. Katika ukurasa wa 150 kwenye Idara ya Utawala Bora kwenye maoni ya kamati, kuna suala la malalamiko kuhusu Askari wa Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingilia kazi za polisi na kunyanyasa raia.

Nataka niwahakikishie wajumbe kwamba, haya yametokana na ripoti hii ya Tume za Haki za Binadamu ambayo ilikuwa ni ripoti ya mwaka 2007/2008. Nataka nilithibitishie Baraza kwamba hayo sasa hayapo, kwa sababu

kilichoripotiwa na kamati kilikuwa ni cha ripoti za nyuma, nilisema niseme hilo ili ionekane kwamba hilo jambo kwa sasa hivi ukilitafuta huwezi kulipata.

Lakini katika ukurasa wa 154 kuhusu Idara ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, kwenye mambo na majukumu kuhusu suala la *item* ya tatu, kazi za ukaguzi wa mwaka 2009/2010. Nataka niweke sawa tu kwamba, ripoti ambayo inaandaliwa sasa hivi ni ya mwaka 2010/2011, kwa sababu ya mwaka 2008/2009 hizo ripoti tayari nimeshaziwasilisha katika Baraza lako tukufu na ripoti ya 2009/2010 tayari nimeshaiwasilisha kwenye Baraza lako tukufu. Kwa hiyo ripoti ambayo inafanyiwa kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni ripoti ya mwaka 2010/2011.

Kwenye suala la upatikanaji wa fedha imeripotiwa hapa kwamba, ofisi ilipata karibu shilingi milioni 404,993,000 ambayo imeripotiwa ni sawa na asilimia 123. Napenda nilihakikishie Baraza kwamba ni asilimia 60 sio asilimia 123. Naomba niweke rikodi hizi sawa ili niichukue kwa ukamilifu kama ilivyo ripoti hii na wizara yangu niende nikaifanyie kazi. Baada ya maelezo hayo sasa Mhe. Spika, naomba kwa uchache kabisa niweze kujibu hoja kwa jumla ambazo zimeelezwa katika mkutano wetu huu, na nianze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Mshimba amezungumzia suala la mishahara ya wafanyakazi wa kada ya afya na kusema kwamba kuna malalamiko.Napenda nimwambie kwamba ni kweli malalamiko yatakuwepo kwa sababu mpaka leo hii nimetoka ofisini bado nashuhudia barua za watumishi ambazo zinafanya marekebisho ya mishahara yao. Na hii imetokana na nini, imetokana na wakati wa zoezi hili tunataka kulifanya nilisema kwenye bajeti, na nilisema kwenye masuala mbali mbali baadhi ya taasisi hazikufuata utaratibu ambao tulikuwa tumewaelekeza. Kwa maana hiyo malalamiko yatakuwepo, lakini napenda kumhakikishia kwamba kila linapotokea lalamiko wizara yangu iko tayari kulishughulikia na wafanyakazi wanapata haki zao.

Lakini nataka nimthibitishie kwamba, katika marekebisho ya mishahara ya wafanyakazi au watumishi wa umma Zanzibar, ni kada ya afya pekee ndiyo imeweza kupata maslahi mazuri zaidi kuliko kada nyengine yoyote. Kwa hivyo lile alilolisema Mhe. Mshimba nataka nimhakikishie kwamba hilo halipo, kuwa pengine kuna malalamiko, inawezekana pengine mtu alichopewa hakijamtosha, lakini amepewa kinachostahiki kwa mujibu wa *qualification* aliyonayo au ujuzi alionao. Hata hivyo, serikali kwa jumla inazingatia pia kuweza kuwafikiria na kuwapa marupurupu mengine wafanyakazi wa kada hii ya afya, ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa na huwa analizungumza Mheshimiwa na bado nataka niseme pale kwamba, kama bado kuna wafanyakazi katika kitengo kimoja wapo cha Wizara ya Afya bado hawajarekebishiwa mshahara wao wafuate utaratibu tu, na niliwahi kumwambia Mhe. Mshimba kama yupo amlete kwangu halafu mimi nifatilie niulize huko wizarani kwake kuna nini. Amlete ofisini kwangu asimlete nyumbani kwangu ili niweze kujua tatizo gani ambalo linasababisha huyo mfanyakazi asiweze kurekebishiwa. Kwa sababu wizara hiyo hiyo ya afya wako wafanyakazi mpaka leo wanarekebishiwa mishahara yao. Kwa hivyo nitamuomba sana Mhe. Mshimba ili hili asije akalizungumza kwenye bajeti, namuomba kama yupo huyo mfanyakazi saa 7 mchana leo amlete ofisini kwangu.

Mhe. Spika, lilizungumzwa suala la kukosekana kwa utaratibu wa kuwapima watumishi na kuwapandisha vyeo, na limeelezwa sheria imepitishwa na hakuna mabadiliko. Mimi nataka niseme sheria ya Utumishi wa Umma Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011 imetiwa saini mwezi wa Julai mwaka uliopita, baada ya pale wizara yangu imechukua hatua mbali mbali ya utekelezaji wa sheria ile. Sasa mimi sikubaliani na Mheshimiwa anaposema kwamba hakuna mabadiliko, mabadiliko yapo, hivi sasa hivi tu ukiangalia mandhari au mazingira ya watumishi wa umma baada ya kupitishwa sheria ile, utakuta kwamba mabadiliko yapo lakini lazima tukiri kwamba na matatizo kabla ya sheria ile yalikuwepo mengi mno, na mpaka sasa bado matatizo yapo mengi mno, na ndio maana tumechukua hatua hii ya kufanya *staff inspection* ya watumishi wa umma kutokana na hayo mambo ambayo yapo na tumegundua matatizo mengi. Muda wake ukifika tutakuja kuyatolea taarifa ndani ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Sasa ninachotaka kusema yeye ameuliza, kwa hivyo utaratibu huu kama ninavyosema tayari sisi tumeshaandaa muongozo na fomu za kuwapima wafanyakazi tayari tumeshazitengeneza si muda mrefu zitaanza kutumika. Na tunataka kufanya zoezi hili *pilot area* ninaifanya katika wizara yangu, wale wanaofanya kazi hii ndio wawe watu wa mwanzo wa kuweza kuwapima na kuwapa hii mikataba kati yao na wananchi, ili kujua kwamba wanawajibika sawasawa au namna gani. Kwa hivyo, nataka nimhakikishie Mhe. Rashid Seif kwamba jambo hili tutakapokuja kwenye bajeti tayari litakuwa limeshaanza kutumika na kuanza kufanyiwa kazi.

Kwa hivyo namuomba asione kuwa hakuna mabadiliko inawezekana pengine Waswahili wanasema, kasa anaweza akawa anacheza lakini yumo ndani ya gamba humuoni. Sasa mimi nadhani yale malengo ambayo tulijipangia ni pamoja na hili Mhe. Spika, kwenye bajeti yetu ya mwaka huu na katika utendaji ni moja kati ya mambo ambayo yanashughulikiwa na Idara hii ya Miundo ya Taasisi, na hivi karibuni hili jambo tunategemea kulianza ili tuweze kupiga hatua.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa Mhe. Spika, ni suala la Tume za Utumishi na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, tume ni *pillar* ambayo inafanya kazi kushughulikia watumishi wa muhimili au kada fulani. Kwa mfano, Tume ya Utumishi wa Mahkama, Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi Serikalini na Tume ya Idara Maalum.Hizi ni tume ambazo zinawajibika kufanya kazi kwa kupendekeza maslahi ya watumishi wao na kutengeneza *scheme of service* ya watumishi wao na baadae kupeleka Kamisheni ya Utumishi wa Umma kama mapendekezo.

Tume hizi na Kamisheni hazigongani katika utendaji wao wa kazi, kwa sababu kila mmoja amepangiwa majukumu kwa mujibu wa sheria, kilichotokea wakati wa marekebisho ya mishahara hizi tume bado zilikuwa hazijaundwa, kwa sababu wakati mimi nawasilisha bajeti hapa tume hizi nyingi zilikuwa hazijaundwa Mhe. Spika, wewe ni shahidi tume hizi zimeundwa baada ya sheria kutiwa saini na Mhe. Rais. Kwa hivyo mwaka huu na kipindi hiki ndio kipindi chake tume hizi sasa zinatakiwa zikae zipendekeze, ili pengine yale yanayoonekana yanafanywa kwa nini yasije yakatokea, kipindi hiki ndio kipindi chake, kipindi hiki ndio kipindi cha kutengeneza bajeti ya serikali kwa ajili ya matumizi ya serikali.

Kamisheni ni kama chombo cha juu ambacho kinapokea mapendekezo na maoni, au unaweza ukakiita kama ni chombo cha *appeal* kutoka kwenye hizi tume baada ya wao kuweza kufanya kazi zake. Kwa hiyo nataka niwahakikishie wajumbe kwamba, hakuna mgongano wowote kuhusu tume na Kamisheni ya Utumishi wa Umma, na hii ilizungumzwa na Mhe. Makame Mshimba vile vile ilizungumzwa na Mhe. Hamza Hassan nataka nitoe ufafanuzi kwa pamoja ili nisije nikarejea rejea.

Mhe. Spika, kuna jambo jengine ambalo limezungumzwa niliseme la mwisho, mengine yale yote nayachukua kwenda kuyafanyia kazi ambalo limezungumzwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu juu ya uwazi wa kujua hasa maslahi ya wafanyakazi.

Mimi nataka niseme kwamba, ofisi yangu kwa maana ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye suala hili la mishahara nataka niseme tena, tulitengeneza programu maalum inayoonesha kiwango cha mwanzo cha mishahara na cha mwisho cha mishahara na tukakipeleka kwenye wizara na taasisi zote za serikali na hicho kipo. Kwa hiyo, hata hayo malalamiko na marekebisho tunayoyafanya mfanyakazi anakwenda anaangalia baada ya kuona kwamba hakikutimizwa kile kiwango ambacho anastahiki kulipwa, ndio maana wanapata fursa za kusema mimi sijafanyiwa marekebisho haya.

Lakini nataka nimthibitishie kwamba kwa hatua ya awali tulisambaza programu hii kwa njia ya mtandao kwenye taasisi zote za umma, na kila mtumishi anayo fursa ya kuweza kuona maslahi yake yakoje. Lakini nataka nimthibitishie katika uwazi huo sasa hata katika *staff inspection* tunayoifanya sasa tumegundua baadhi ya watumishi wa serikali katika taasisi mbali mbali wanapata mshahara wasiostahiki, yaani wanapata mshahara mkubwa zaidi kuliko wanaostahiki kupata.

Na hiyo inatokana na nini? Walikuwa wanaweka *qualification* ambazo haziko, na hivi sasa hatua tunayoichukua kila tunayemgundua kwa hivyo malalamiko hayo pia yanaweza yakaja, kila tunaemgundua mshahara tunaukata. Kwa sababu haukuthibitishwa wala haukupitishwa kisheria, kwamba wewe unalipwa mshahara wa mtu mwenye *master degree*, lakini kumbe una *first degree*, tukigundua hivyo mshahara huo tunaukata.

Kwa hivyo, baada ya kuwepo uwazi ndio maana yote hayo tumeyagundua hata hivyo, tutajaribu kufuata ushauri wake na tutafanya hilo ambalo Baraza hili litatushauri. Na viwango vya mishahara kama nilivyosema kwenye masuala ambayo nilikuwa nayajibu ni kwamba, serikali huwa inatangaza kiwango cha mwanzo cha mshahara, lakini kiwango cha juu cha mshahara pia kipo na kiwango cha juu cha mshahara wanacholipwa watumishi kinalipwa katika kada ya afya, yaani wanalipwa madaktari na kipo. Wajumbe wote wakitaka *list* hii ya viwango vya mishahara kwa watumishi wa umma basi mimi niko tayari kuwapatia, hakuna kificho wala hakuna mizengwe katika hili, kuna uwazi na kuna suala la kutekeleza suala la kutekeleza utawala bora. Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Mhe. Spika, kwamba hili jambo lipo, na wizara yangu iko makini katika kulifanyia kazi jambo hili.

Mhe. Spika, kwa sababu ya kuokoa muda, yapo mengi lakini nitawaomba radhi kwa wale ambao wamezungumza na sikupata kutoa ufafanuzi, lakini mengi yao haya yalikuwa yanazungumzia juu ya ripoti, na ripoti hii kwa ujumla wake baada ya masahihisho ambayo nimeyasema naichukua mimi pamoja na watendaji wangu kule wizarani tutakwenda kuyafanyia kazi, na *Inshaallah* kwenye kitabu chetu cha bajeti mtaona tofauti kati ya haya yaliyoelezwa na yale ambayo tutakuja kuyaripoti katika Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, baada ya hayo nakubaliana na ripoti hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kwa mara ya pili kwa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili kufanya majumuisho ya michangio ya taarifa yangu niliyoiwasilisha jana.

Pili niwashukuru wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia ripoti yetu hii na naomba niwataje ili muwatambue.

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Fatma Mbarouk Said
7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
8. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria
9. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao mizuri ya taarifa yetu hii na pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kufanya baadhi ya marekebisho katika taarifa yetu hiyo. Nadhani mengi waliyoyasema waziri wote wawili wameyasikia na yale ambayo hawakuweza kuyasema wameahidi kwamba watayachukua wayafanyie kazi.

Mhe. Spika, mimi nilikua na mambo manne tu ya kusisitiza katika ripoti hii kwa Wizara zote mbili. Kwanza nije kwenye Ofisi ya Mufti juu ya suala zima la mali za wakfu. Tulipata taarifa kwamba taasisi hii ilifanya ziara ya kupita kukagua mashamba pamoja na nyumba zilizowekwa wakfu. Lakini ilibainika kwamba baadhi ya maeneo hayo kwenye mashamba kuna watu walikuwa wanayamiliki muda mrefu bila ya kutoa chochote kwa Ofisi ya Mufti ili kutekeleza lile ambalo lilikusudiwa na wenyewe walioweka hizo haki zao.

Sasa naishauri Wizara kama hiyo ni kweli basi wale wote ambao walikuwa wanachukua mali hizo bila ya kuzifikisha kunakohusika hivi sasa wawajibishwe waweze kuzirejesha mali hizo ili ile iliyokusudiwa na wenyewe walioweka wakfu iweze kupatikana. Nadhani hilo ni suala muhimu na lenye faida kwa wale ambao wameweka hizo haki zao katika sehemu hiyo.

Mhe. Spika, suala la pili tuje upande wa sheria. Pia kuna tatizo la Sheria ya Wakfu na Sheria ya Ardhi zinakua zinagongana. Sasa tunaomba Wizara zote mbili zikae zitayarishe hii sheria ili tuweze kuweka sawa hili suala la mgongano liondoke.

Kwa mfano, utakuta mashamba ya wakfu hayaruhusiwi kugaiwa kama maeka, lakini utakuta hivi sasa Sheria ile ya Ardhi inaruhusu hivyo na kwa hivyo basi hukata eka kuwapa watu wakati kitu kile kimewekwa katika hali hiyo. Sasa naomba na hili pia lifanyiwe kazi kwa Wizara zote mbili ili tuweze kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Spika, la tatu ni suala la vyeti vya kuzaliwa limezungumzwa sana hapa lakini kipande kimoja hakikuzungumzwa. Wako watu wanaozalia hospitali huwa wanapewa vipande maalumu moja kwa moja wanakwenda Makao Makuu wanapatiwa vyeti kwa urahisi. Lakini kuna watu wanazaa mitaani na vyeti wanakwenda kuchukua kwa sheha, sheha ikisha anapeleka wilayani. Sasa sheha akipata fedha wakati mwengine hali mbaya baadhi ya masheha hujikopesha pengine miezi mitatu ndio utakuta tatizo linakuwa kubwa. Kwa hivyo, ningeliomba Wizara zote mbili zikakaa tena kufuatilia suala hili ili na wale wanaozaa mitaani wakapatiwa vyeti vyao kwa wakati muafaka. Nadhani Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Waziri wa Katiba na Sheria wakutane walirekebishe suala hilo.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la hati miliki. Katika ofisi ya Pemba tumegundua kwamba kuna ofisa mmoja tu na akenda kusoma ofisi inafungwa. Sasa nadhani serikali imetoa nafasi ya kuajiri wawatafute wenye sifa waajiriwe ile ofisi ile isiwe inafungwa wakati ofisa huyu akenda kwenye mafunzo au akenda likizo.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nisipoteze muda naomba kuwashukuru wote kwa mara ya pili wachangiaji pamoja na Mhe. Waziri. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaopokea ripoti hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Ripoti ifanyiwe kazi pamoja na marekebisho madogo yaliyofanywa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Lakini kabla sijaanza kufanya hivyo Mhe. Spika, naomba niseme mambo yafuatayo.

Mhe. Spika, katika kitabu cha ripoti za kamati mbali mbali ambazo kila mjumbe amepata nakala, ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeanzia kutoka ukurasa wa kwanza wa kitabu hicho hadi ukurasa wa 25. Lakini Mhe. Spika, katika ripoti hiyo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeelezea mambo yafuatayo.

Kwanza malengo ya idara na taasisi mbali mbali zilizoko chini ya wizara hizo zinazosimamiwa na kamati yangu. Lakini kwa mwaka wa fedha, nyengine kwa mwaka wa fedha 2010/2011, lakini pia na ya mwaka 2011/2012. Pia imeelezea utekelezaji wa malengo hayo hadi kufikia Disemba, 2011 ikionesha pia maendeleo ya baadhi ya taasisi zinazosimamiwa na wizara hizo.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 23 hadi 25 wa ripoti hii ya kamati, kamati imetoa maoni au maagizo ya kamati kwa serikali kupitia wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hiyo ya Fedha, Biashara na Kilimo. Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imepewa maoni/maagizo 15 ambayo Mhe. Waziri tunamuomba ayafanyie kazi, ayapitie na maoni hayo kama yatatekelezwa tunaamini kwamba ufanisi mkubwa unaweza ukapatikana.

Lakini Wizara ya Kilimo na Maliasili imepewa maoni ya maagizo 7 ambayo nayo Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili kama atayazingatia na kuyafuatilia basi ufanisi utapatikana katika suala zima la masuala mazima ya kilimo.

Mhe. Spika, mwisho Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imepewa maoni na maagizo 13 ambayo nayo Mhe. Waziri kama atayatekeleza kama ilivyo basi itaweza kusaidia katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya wizara.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa Waheshimiwa waziri wawili sijawaona, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Waziri wa Kilimo na Maliasili, aliyekuwepo peke yake ni Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli hili sio jambo zuri na ni jambo ambalo sijui tuzungumzie lugha gani. Kwa sababu Mhe. Spika, chombo chako hichi moja kati ya jukumu lake kubwa au la msingi ni kuisimamia serikali kupitia kamati zako ulizounda ambapo kamati hupata nafasi ya kwenda moja kwa moja katika wizara, idara na taasisi mbali mbali ili kujionea namna ya utekelezaji wa maagizo yale ambayo wizara kupitia bajeti yake ya serikali imetoa. Lakini kwa bahati mbaya sana mawaziri wetu hawa wameingia mitini.

Mhe. Spika, unakumbuka juzi tu Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi alifanya kitendo kama hicho na Baraza lako tukufu likamtaka atoe maelezo na aombe radhi. Kwa hivyo, sijui kwa kitendo hichi ambacho kimefanywa na waziri wetu hawa utachukua hatua gani juu yao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kuwasilisha Muhtasari wa Hotuba ya Mwenyekiti inayohusiana na Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi la Zanzíbar.

Mhe. Spika, kabla ya yote naomba nichukue nafasi hii uliyonipa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake kwa kuendelea kutujaalia afya njema tukiwa hapa pamoja tukijumuika katika kuwatumikia wananchi wetu kwa ujumla.

Pili, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa niaba ya Wajumbe wenzangu.

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii niwapongeze sana Wajumbe wenzangu wa kamati kwa mashirikiano makubwa waliyonipa kwa kipindi chote ambacho tumekua tukifanya kazi mawazo yao, fikra michango na busara zao walizokua wakizitoa zimenisaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu. Ninafuraha sana kusema nimefarajika mno na msaada wao huo.

Mhe. Spika, naomba niwataje kwa majina wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Mohammed Ali - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe Mahmoud Muhammed Mussa- Mumbe
4. Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Mjumbe
5. Mhe Rufai Said Rufai - Mjumbe
6. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mjumbe
8. Ndg. Amour Mohammed Amour- Katibu
9. Ndg. Shemsa Maabad Mohammed- Katibu

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 108 ya Baraza la Wawakilishi ikiwa na majukumu yafuatayo:

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliopita.
b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.
c) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
d) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
e) Kuchunguza na kufuatilia mapato ya Serikali ya Wizara husika.
f) Kufikiria jambo lolote litakalopelekwa kwake na Spika.
g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokua zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
h) Kufikiria Miswada ya Sheria itakayopelekwa kwake na Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa vile muundo wa Kamati zetu ni wa Kisekta, basi Kamati yetu imepangiwa kutekeleza majukumu yake katika Wizara zifuatazo:

a) Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo

b) Wizara ya Kilimo na Maliasili

c) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizo, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Watendaji wao wote. Kwa pamoja wameipa kamati yetu mashirikiano makubwa na kuiwezesha kufanya kazi zake kwa mafanikio makubwa. Waliweza kutupa maelezo na maelekezo kwa kadri tulivyoyahitaji. Wamekua wasikivu wa kupokea maagizo na maelekezo ya Kamati na tunatarajia kwamba maagizo yetu yatatekelezwa kwa kadri ya uwezo uliopo.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilifanya kazi kwa muda wa wiki nane. Kazi ambayo ilifanyika Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Katika kutekeleza majukumu hayo Kamati ilifuatilia utekelezaji wa malengo kwa Wizara hizo tatu, pale ambapo malengo yamefikiwa ilipongeza na pale ambapo hayakufikiwa ilitaka kujua sababu na baada ya kuzijua ilitoa ushauri au wakati mwengine maagizo.

Mhe. Spika, kwa ujumla kumekua na changamoto nyingi katika utekelezaji wa kazi kwenye Wizara hizo, lakini la msingi ni suala zima la upatikanaji wa fedha. Wizara zimekua hazipati fedha za uendeshaji (Kasma ya

Matumizi mengineyo) kwa wakati na hivyo wizara kuwa na wakati mgumu wa kutekeleza na kuyafikia malengo yake kama ilivyokusudiwa. Hata kama fedha hizo za matumizi mengineyo *(OCs)* huingizwa kwa utaratibu uliopo kwa kila Wizara kuandika mahitaji yake *(Cash flow)* lakini kiwango kinachotolewa ni kidogo mno ambacho kimetokana na *ceiling* ambayo Wizara imepewa na hakiwezi kukidhi mahitaji yaliopo.

Mhe. Spika, tatizo la *ceiling* ambayo Wizara imepewa limeonekana kua ni changamoto kubwa. Yawezekana ni kwa sababu ya rasilimali tulizonazo lakini wakati mwengine ni tatizo la uteuzi bora wa vipaumbele ambavyo vingeweza kufanikisha ukamilishaji wa malengo.

Mhe. Spika, mahitaji ya matumizi ya rasilimali ni makubwa na yanaongezeka kila leo, wakati mapato halisi ni madogo yasiyoendana na mahitaji yenyewe. Ni kweli uchumi wetu unakua lakini kukua kwake hakufuatani kabisa na kasi ya mahitaji. Kwa mfano, mahitaji ni milioni kumi lakini mapato ni milioni tano. Wakati mwakani mahitaji ni milioni kumi na mbili, lakini mapato ni milioni saba. Kwa kutathmini mwenendo huu wa uchumi inakupa sura halisi kwamba ni lazima tufunge mkanda kikweli kweli katika suala zima la kuziba mianya ya mapato ili tuweze kuziba pengo hilo.

Mhe. Spika, ukusanyaji wa kodi katika maeneo ya Sekta za Utalii, uekezaji na kodi nyengine za mauzo pamoja na misamaha mingi ya kodi kwa Taasisi mbali mbali za kijamii na watu binafsi imekua ni kikwazo kikubwa. Bado hatujawa na takwimu halisi za pato linalotokana na Utalii, hatuna mazingira mazuri ya miundombinu yenye kuwavutia waekezaji, na bado wafanyabiashara hawana utamaduni wa kutoa risiti. Mhe. Spika, suala la kukusanya mapato ya Serikali kwa makadirio tu limepitwa na wakati, ni lazima Serikali iandae utaratibu wa kileo wa kukusanya mapato halisi na sio kwa makadirio kama ilivyo sasa.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inatoa wito kwa Serikali kuachana kabisa na utaratibu uliopo sasa, kwani utaratibu huo hupoteza mapato mengi ya Serikali, mapato ambayo yangeweza kusaidia sana katika kutatua matatizo mbali mbali yanayowakabili wananchi.

Mhe. Spika, tunaendelea kulitegemea zao letu la karafuu kama muokozi wa uchumi wetu. Kwa bahati ile changamoto ya magendo sasa imepungua kwa kiasi kikubwa ijapokuwa imegeukia kwenye magendo ya mafuta. Bado juhudi zichukuliwe kuendeleza mkarafuu na wakulima wake huku tukitafuta mbinu ya kuondoa kabisa magendo ya mafuta.

Mhe. Spika, huo ulikua ni mtazamo wa jumla tu unaohusu athari za utekelezaji wa malengo katika Wizara zetu. Sasa niruhusu nitoe tathmini ya utekelezaji wa malengo kwa Wizara ambazo Kamati yetu ilipangiwa.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kilimo bado kitaendelea kuwa ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Lakini bado kinakabiliwa na changamoto nyingi, ukosefu wa matrekta ya kutosha ya kuwezesha kulima kwa wakati, uhaba wa mbolea na ukosefu wa dawa za kuulia wadudu ni changamoto kubwa zilizopo.

Mhe. Spika, pamoja na changamoto zilizopo, kilimo bado kina mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi yetu na kutuwezesha kutufikisha pale tunapokusudia. Tunafahamu kua juhudi zimekua zikichukuliwa na Serikali na hata na wakulima wenyewe, lakini juhudi zaidi zinahitajika, hii ikiwa ni pamoja na kuwajibika kwa kila mmoja wetu katika eneo alilopangiwa na kuachana kabisa na tabia ya kuoneana muhali kwa wale wanaohusika.

Mhe. Spika, ni kweli ardhi yetu inayofaa kwa kilimo ni ndogo, lakini tuaamini kwamba endapo juhudi za dhati zitachukuliwa kwa kuongeza bajeti ya Kilimo, kulima kwa utaalamu, basi ardhi ndogo tuliyonayo inaweza kabisa kututosheleza kwa kiwango kikubwa kwa mazao ya chakula.

Mhe. Spika, chakula kikuu kinacholiwa hapa kwetu ni wali (mchele) ambapo wananchi wengi wa mijini na vijijini hutumia mlo huu kwa maisha yao ya kila siku. Ukulima wa mpunga ambao tunadhani utatupatia tija ni ule wa umwagiliaji maji. Kilimo hiki kwa kweli kina gharama kubwa, utayarishaji wa miundombinu yake kama vile ujenzi wa misingi, uchimbaji wa visima, upelekaji wa umeme katika maeneo husika ni changamoto kubwa.

Mhe. Spika, wakulima wengi wameshajihishika mno na kilimo hiki cha umwagiliaji maji kiasi kwamba hata yale maeneo yaliyotengwa kwa ajili hii yamekuwa hayatoshi. Pamoja na juhudi za Serikali na wafadhili katika kuinua kilimo hiki, bado changamoto kubwa ni suala la umeme kufikishwa katika maeneo ambayo miundo mbinu mingine kama vile misingi ya maji na visima vinakua tayari lakini tatizo linabaki kua ni umeme.

Mhe. Spika, suala la uhifadhi wa misitu ya maliasili nyengine nazo ni muhimu sana. Bado sheria na kanuni hazijaweza kuwazuia waharibifu wa misitu na wale wanaochimba mchanga. Serikali iliangalie suala hili ili uhifadhi wa maliasili zetu ulenge kwenye dhamira kuu ya kuzihifadhi na kuziendeleza rasilimali hizo.

Mhe. Spika, utafiti wa mbegu na ardhi ni muhimu sana katika kukiendeleza kilimo chetu. Maelezo mengi yametolewa wakati tulipokua tukijadili Mswada wa Kuanzisha Taasisi ya Utafiti Zanzibar. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaamini kwamba kuanzishwa kwa taasisi hii pamoja na Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa pamoja vitaweza kusaidia sana wakulima katika upatikanaji wa mbegu bora na pia uteuzi bora wa ardhi.

Mhe. Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Wizara hii ina jukumu kubwa la kuratibu hali ya mwenendo wa Biashara hapa nchini lakini vile vile kuangalia uwezekano wa kua na viwanda vidogo na vya kati pamoja na kuratibu upatikanaji wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwa ni kwa kuitangaza kibiashara Zanzibar, kupitia mtu mmoja mmoja, kikundi au jumuia za biashara kwa lengo la kuinua vipato vyao.

Mhe. Spika, kazi hiyo ni kubwa na inahitaji usimamizi wa karibu ikiwa ni pamoja na kuondosha urasimu usio wa lazima, bado tunao wafanyabiashara wengi wadogo wadogo wanaohitaji kuendelezwa, aidha uwezo wetu wa kusafirisha bidhaa nje ya nchi ni mdogo kuliko uingizaji nchini. Kwa mfano, bidhaa zilizoingizwa nchini kutoka Tanzania Bara pekee hadi mwezi Septemba, 2011 ni Tshs. 94,149 millioni wakati Zanzibar iliweza kusafirisha nje ya nchi bidhaa zenye thamani ya Tshs. 25,185 millioni kwenda Tanzania Bara. Taswira hiyo itoshe tu kuonesha namna ya pengo la nakisi katika biashara lilivyo kubwa.

Mhe. Spika, nchi yetu haiwezi kuendelea bila ya kua na viwanda. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ina wajibu wa kuhakikisha kwamba suala la kua na uwezekano wa kua na viwanda vidogo vidogo na vile vya kati linafanikiwa. Utafiti unaonesha kua wapo wafanyabiashara wanaotaka kuanzisha viwanda hapa nchini lakini wanashindwa kusaidiwa kufanya hivyo.

Mhe. Spika, suala la udhibiti wa bei nalo limekua ni mgogoro mkubwa. Ni kweli tumeachia biashara huru tukitarajia kwamba kutakua na ushindani wa bei ambapo soko lenyewe ndilo litakalopanga bei hiyo. Tukiwa na matumaini ya kushuka kwa bei au angalau kuwa na bei inayokidhi matakwa ya wateja lakini hali sivyo ilivyo, bei za bidhaa hasa za chakula zinapanda siku hadi siku.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba Wizara imejaribu kukaa na wafanyabiashara katika kuona kwamba kunapangwa bei muafaka, bado bei zinapanda na zikiwa na tofauti kati ya duka moja na jengine. Kwa mfano, bei ya mchele ya reja reja ni Tshs. 1,300/- hadi Tshs. 1,600/- kwa kilo ule unaojulikana kama mapembe wakati ule unaotoka Mbeya ni kati ya Tshs. 2,400/- hadi Tshs. 2,700/- kwa kilo. Sukari ni Tshs. 1,500/- hadi Tshs. 2,000/- kwa kilo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linasikitisha katika utekelezaji wa majukumu na malengo ni suala la viwango vya bidhaa. Bado bidhaa zinazoingizwa nchini haziko katika viwango bora vya matumizi. Lengo la Wizara la kuondoa au kupunguza kadhia hii ni kuanzisha Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Bidhaa Zinazotumiwa na Wananchi *(Zanzibar Bureau of Standard).*

Mhe. Spika, hebu tujiulize ni kwa kiasi gani Serikali imejiandaa katika kuanzisha taasisi hii ya viwango vya bidhaa nchini? Jibu hatujui. Kamati yetu inaipongeza sana Serikali kwa azma hiyo, lakini bado tuna mashaka juu ya uwezekano wa kuanzishwa kwa taasisi hii.

Suala la miundombinu yenye kuaminika kama vile eneo kubwa la ardhi, majengo ya maabara za kisasa na afisi pamoja na wataalamu wenye sifa mbali mbali za kielimu ni mambo ya msingi yanayohitajika.

Mhe. Spika, eneo jengine linahusu vipimo hasa vya uzito na ujazo ambavyo inahusu vifaa kama vile mizani. Ukaguzi wa mizani nyingi lakini bado zoezi hili haliendi vizuri hasa maeneo ya vijijini, Unguja na maeneo mengi ya Pemba. Hii inatokana na ukosefu wa nyenzo za kufuatilia kama vile vyombo vya usafiri. Je, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inachukua juhudi gani katika kundoa tatizo hilo?

Mhe. Spika, jambo ambalo linalalamikiwa mno katika siku za karibuni ni nishati ya mafuta ya petroli yasiyo na ubora. Vyombo vingi vya moto vimeharibika na kuwatia hasara watumiaji wa vyombo hivyo. Suala hili ni lazima liangaliwe kwani linaonekana halina msimamizi yaani halina mwenyewe linaelea tu.

Mhe. Spika, kwenye eneo la Utendaji wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) Kamati imeridhika kabisa hasa kwa kuzingatia bei ambayo Shirika inanunua kwa wakulima. Utekelezaji huo tumeueleza kwenye ripoti yetu na tunaliomba Shirika hilo kwenye muundo wake mpya uwe ni wenye tija kama ilivyokusudiwa.

Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango ya Maendeleo

Mhe. Spika, Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango ya Maendeleo ina jukumu la kuitunza hazina yetu, kubuni na kuratibu mipango ya maendeleo, kutafuta mbinu za mapato, kuratibu matumizi na ugawaji wa raslimali fedha pamoja na kutunza na dhamana za mali na raslimali zote za Serikali.

Mhe. Spika, jukumu hilo ni kubwa ambalo linaratibiwa kupitia idara mbalimbali na taasisi nyengine za kukusanya kodi na zinazohusiana na fedha. Idara kama vile Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma, Idara ya Uratibu wa SMZ – DSM na kwa upande wa mamlaka za kukusanya kodi ni Bodi ya Mapato, Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar; Taasisi nyengine ni Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Shirika la Bima, Zanzibar pamoja na Taasisi nyenginezo.

Mhe. Spika, kamati bado inasisitiza juu ya ugawaji wa fedha kwa Mawizara, kwa kuangalia zaidi vipaumbele vyao kwa mujibu wa malengo ambayo wameyainisha kwenye maombi ya makadirio ya bajeti ya mwaka unaofuata. Idara inayohusika itoe maelekezo yenye msisitizo huo.

Katika suala la udhibiti wa Mali za Serikali, kwa mara nyengine tena Kamati inahisi kwamba uanzishwaji wa daftari la mali za Serikali unachelewa mno. Hofu yetu ni kwamba ule msemo wa ‘mali bila daftari hughibu bila ya habari’ usije ukatufika na sisi. Tuna mali nyingi lakini habari yake haitambuliki.

Mhe. Spika, ukushanyaji kodi ni jambo muhimu sana; ili tuweze kutumia basi ni lazima tukusanye fedha. Mamlaka ya Mapato Tanzania (T.R.A), Bodi ya Mapato Zanzibar (Z.R.B) mnayodhima kubwa kwa Wazanzibari. Pamoja na dhima kubwa waliyonayo kwa Wazanzibari, Mashirikiano ya dhati yanahitajika katika kufanya kazi hizi ngumu za ukusanyaji wa kodi kati ya taasisi hizi na wananchi.

Mhe. Spika, Wazanzibari ni lazima tuwe na utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari na bila ya kulazimishwa. Lakini pia tuwe na tabia ya kudai risiti pale tunaponunua bidhaa yoyote dukani. Tunapodai risiti madukani tutaisaidia sana Serikali kupata mapato yake kwa uhakika.
Mhe. Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika nyanja mbali mbali za kimapato, bado Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inazo changamoto nyingi na kama zitashughulikiwa ipasavyo basi mapato zaidi yataweza kupatikana. Changamoto zenyewe ni kama hizi zifuatazo:-

1. Ukusanyaji wa mapato yanayotokana na Visa za wageni katika Viwanja vya Ndege na Bandarini
2. Utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Tume ya pamoja ya Fedha (J.F.C) kwa Serikali zetu zote mbili (S.M.Z na S.M.T) ufanyiwe kazi.
3. Kusimamia utaratibu wa malipo ya Kodi ya Mapato (*In-come Tax*) kwa wafanyakazi wa (SMT) wanaoishi Zanzibar kulipwa moja kwa moja Zanzibar.
4. Kuangalia upya suala la misamaha ya kodi, ambapo inaonekana viwango vya misamaha ya kodi bado ni vikubwa.

Mhe. Spika, kwa hiari yetu tumeamua kuitangaza nchi yetu kama eneo bora la uekezaji. Pengine kwa maumbile ya Visiwa vyetu, mvuto mkubwa zaidi umekua kwa waekezeji wa sekta ya Utalii kuliko sekta nyengine kama vile za viwanda, kilimo na nyenginezo. Hii inasababishwa zaidi na hali ya miundombinu yenyewe. Unalitangaza eneo huru la uchumi, lakini halina miundombinu ya uhakika kama vile umeme, maji na barabara. Hilo linawarudisha nyuma wenye nia ya kuekeza.

Mhe. Spika, jengine ni urasimu tulionao, bado hatujawa na *One Stop Centre* ya kweli katika hili. Inachukua muda mrefu kutoa jibu la kuukubali au kuukataa mradi. Hili kwa Dunia ya leo ni tatizo. Kamati ya kupitia maombi ya miradi, wajumbe wanaowakilisha sekta zao hawawi na maamuzi ya haraka, kwani hua hawana kauli ya mwisho ya taasisi wanayoiwakilisha.

Mhe. Spika, maeneo ni mengi yanayosimamiwa na wizara hii, pamoja na wizara nyengine zinazosimamiwa na kamati yetu, tumeyaeleza kwenye ripoti yetu ambapo tumeelezea kiwango cha utekelezaji kwa kila wizara na kwenye hitimisho tukaweka maagizo na ushauri wetu kama nilivyotangulia kusema.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe waichangie ripoti hii kwa makini, ni ripoti muhimu na tutakapoichangia itawasaidia Waheshimiwa Mawaziri waliopo kusaidia katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku za serikali na nchi yetu itaweza kupata manufaa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja, ahsante.

(Hoja litolewa ijadiliwe)

Mhe. Spika: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Bishara na Kilimo ametoa hoja na baada ya kuungwa mkono inabidi sasa mjadala uanze. Lakini alinikumbusha kwamba hivi tunakwendaje, wakati jambo hili linaambiwa hasa serikali na serikali yenyewe haikukamilika.

Niichukue nafsi kwanza kumshukuru Mhe. Waziri amekuja mbio sana. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili alipokua anapita pale kama angekuwepo mtu pale angemtoa meno wakati wa kufungua mlango. Kwa sababu ya haraka ya kufuatilia shughuli hii kwa kuelewa umuhimu wa kazi hii. Nakushukuru Mhe. Waziri, lakini ilikua kidogo.

Pamoja na hayo yote nafikiri viti wazi namna hii havituletei sifa nzuri kwa wananchi. Wapo baadhi ya mawaziri ambao taarifa ninazo, lakini wapo baadhi ya mawaziri ambao sina taarifa ya kutokuwepo kwao. Kwa maneno yale yale hii sio nidhamu nzuri kwa shughuli zetu. Kwa bahati mbaya sana nadhani tunatoa ushauri sio mzuri vile vile kwa Mhe. Rais, kwa sababu wapo baadhi ambao wamechukua likizo kwa kipindi hiki ambacho Baraza linaendelea, na hii nayo haielekei. *(Makofi)*

Mimi ningeishauri serikali kwamba kama kuna kipindi kizuri cha kuchukua likizo, basi iwe ni kipindi kile ambacho hakuna shughuli za Baraza, kwa sababu ni mazoea yetu makubwa kwamba shughuli nyingi za Baraza ni shughuli za serikali na nyingine za maswali, lakini maswali yako kwa serikali, sasa bila ya kuwepo serikali nadhani mambo hayatokwenda vizuri. Mtazamo na mwelekeo wa chombo hiki kikatiba haitakwenda sawa sawa bila ya kuwepo wajumbe wa *back benchers*, lakini pia na mawaziri wa serikali. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nitahitaji maelezo vile vile kwa wale ambao sina taarifa zao na wala sio tu wale ambao kwa shughuli hii wanahitajika hivi sasa, kwa kweli ni kwa wote. Taarifa watendaji wangu hua natoa kwa wajumbe wote, kwamba wawepo katika Baraza hili ili kuendesha shughuli zetu. *(Makofi)*

Hivi tuangalie katika historia ya tangu Baraza hili kuanza, ni lini waendeshaji wa kikao hiki kwa maana Spika, na wale wasaidizi wake wanachelewa angalau dakika moja kikao hiki. Haijawahi kutokea, anapokua mmoja hayupo basi mwengine yupo kitini, lakini shughuli zinaendelea kama kawaida. Hivi kwa nini isiwezekane hivyo kwa upande wa Waheshimiwa Wajumbe na mawaziri. Wakati sote wajibu wetu ndio huo mmoja, kuendesha shughuli za Baraza kwa mujibu wa katiba chini ya ibara 88 ya katiba ya Zanzibar. Huu sio utaratibu mzuri, ni lazima tuone kwamba shughuli zetu zinakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wewe ndio dhamana kwa hivi sasa. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipoondoka aliniandikia, akaniambia Kaimu wa Shughuli za Serikali ndani ya Baraza atakua Mhe. Mohammed Aboud. Sasa itabidi pia ni kazi yako ujue mawaziri wamekwenda wapi, unipe hiyo taarifa. Pia ni kazi yako kujua yule aliyekua hayupo anakaimiwa na nani, ndio kazi zenyewe hizo. Tena sio hayo tu, wewe ndio *Government Chief* katika chombo hiki. Tuone shughuli hizi zinakwenda vizuri za serikali au shughuli za Baraza kwa jumla.

Mimi nadhani tungekua tunatimiza wajibu wetu ili tuone kua tunakwenda na shughuli zetu vizuri na wananchi waridhike kwamba tunafanyakazi kwa niaba yao. Basi mjadala huu uendelee, lakini tuelewe nani sasa anachukua zile taarifa na michango ya Waheshimiwa Wajumbe. Waziri wa Kilimo na Maliasili mwenyewe yupo, Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo yupo. Lakini Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko sijui ni nani kazi hiyo unaifanya wewe na tujuwe nani anachukua hizo taarifa.

Nashukuru baada ya maelezo hayo mjadala unaendelea, nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa muda mfupi vile vile baadae Mhe. Hamza Hassan Juma.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza tunakushukuru kwa muongozo wako na busara zako, kwa kweli Baraza letu unalirejeshea ile hadhi yake ambayo hasa inatakiwa.

Mhe. Spika, mimi nilikua naomba ushauri. Mhe. Spika, tunakubaliana kwamba ripoti zote za kamati ni muhimu, lakini Mhe. Spika ripoti ya kamati hii ya uchumi na fedha ni muhimu sana. Tunajua kwamba tumebanwa na muda, lakini kwa ripoti hii tungekuomba ukatupa muda mzuri, kwa sababu mambo mengi ya uchumi wa nchi, makusanyo ya nchi, serikali ifanye nini ili iweze kukusanya fedha, tunashauri katika ripoti hii, ili Mhe. Waziri katika bajeti atakapokuja apate nafasi ya kuchukua ushauri wa kamati, lakini vile vile na ushauri mzuri ambao wajumbe tutakaoweza kuishauri serikali hii. Mhe. Spika, tulikua tunaomba kwa wizara hii kidogo utustahamilie kidogo. Naamini kwa busara zako Mhe. Spika, unaweza ukatukubalia, ahsante.

Mhe. Spika: Ombi ni zuri, lakini liendane na muda tuliojipangia shughuli zetu, muda wetu ni tarehe 20/04/2012, tena mara hii ni historia kikao hiki kimekua ni kirefu sana. Kwa kawaida kikao hiki ni cha wiki mbili, lakini mara hii kimekwenda kiasi hicho. Kwa hivyo, ombi hilo linakubalika lakini liendane kwa mujibu wa shughuli zetu tulizojipangia kumalizika tarehe 20/04/2012. Kwa hivyo, nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa kifupi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nitakwenda kwa kifupi tu kama ulivyonieleza ili kuweza kuokoa wakati, yale uliyokusudia twende nayo vizuri.

Mhe. Spika, pamoja na hayo ni lazima kwanza nikusifu sana, umekua unatenda haki kabisa, huna mdogo wala mkubwa. Kwa hili nakushukuru sana. Vile vile naomba suala hili lingetiwa katika taarifa ya habari yetu kwenye televisheni ya Zanzibar, kutokana na ule utaalamu wako uliotuonesha hapa, huna mdogo wala mkubwa, ahsante sana.

Mhe. Spika, nakwenda kwenye mchango kwa haraka. Katika ukurasa wa 4 wa Idara ya Kilimo. Hapa kwanza niwapongeze sana watendaji kwa jitihada zao nzuri ambazo wanazifanya, japo tumepitwa na wakati baada ya matayarisho ya ukulima kwa kutumia matrekta. Lakini hata hivyo, naomba kwa mara nyengine tena ili serikali ione kabisa hapa kuekeza suala hili la matrekta kuletwa kwa wingi sana ili kuwaondolea umaskini wananchi wetu kupitia kilimo cha kutumia matrekta.

Mhe. Spika, masuala ya pembejeo na dawa yamekwenda kwa wakati, lakini kila siku kukicha wakulima wanazidi kua wengi. Kwa hivyo, naomba na asilimia nayo iongezeke ili wakulima wapate kunufaika kwa kupata vifaa hivi na kwa wakati wenyewe.

Mhe. Spika, nakwenda ukurasa wa 5 kuhusu idara ya misitu. Mhe. Spika, kwa kweli namuunga mkono Mhe. Mwenyekiti, wangu, pale mwanzo nilikua sijamuunga mkono, lakini sasa hivi namuunga mkono kabisa Mwenyekiti wa kamati hii kwa maelezo mazuri kwa kuniona mjumbe wake na kuweza kunisafisha leo na kunivisha nguo suti nzuri sana, namshukuru sana.

Mhe. Spika, ukurasa huu wa 5 idara ya misitu. Naunga mkono kua sheria bado ni nyepesi kutokana na hali halisi ilivyo ya misitu. Kwa kweli tukifanya mchezo msitu unakwenda, wanajitahidi Mkurugenzi na watendaji wake katika kulinda, lakini wanakwazwa hasa sisi viongozi, tuseme kweli Mhe. Spika, kwamba tunatia mkono, tunampa wakati mgumu kusema ukweli. Kwa sababu magari yetu yakishakamatwa tunampigia simu, hajui cha kufanya sheria anaitaka na kumsaidia kiongozi anataka, tunampa wakati mgumu. Wale watendaji wetu kule wa misitu walinzi wanapata shutuma mbaya sana kwa jamii.

Kwa hivyo, ningeomba sana kwa makusudi kua tuendelee na elimisho zuri ili wananchi wajue nini faida ya msitu ule. Isitoshe sheria sasa hivi ikazwe, mheshimiwa watu wanaharibu msitu, mali asili iliyobakia ni hiyo tu kwa Pemba na Unguja, vyengine vyovyote tutakua hatuna kitu kama hicho.

Mhe. Spika, kwende katika umwagiliaji maji kwenye huo huo ukurasa wa 5. Mhe. Spika, umwagiliaji wa maji tumeona faida zake, hivi karibuni vimeletwa vile *power tiller*. Lakini mpaka sasa hivi sijaona sehemu gani ambazo wanaweza kugaiwa vile wakanufaika. Naomba wapewe wananchi kwa njia ya mikopo ili waweze kuondoa umaskini kwa kupitia umwagiliaji maji wa mpunga.

Mhe. Spika, kilimo hiki ni kizuri sana kwa sababu kinaondoa umaskini haraka, kwa sababu hungoji mvua. Sasa hivi wataalamu tunao wazuri tu tena wa kutosha. Kwa hivyo, mimi naomba kwamba natilia makazo hili suala la kua haraka sana liweze kufanikishwa kwa kupewa zile *power tiller* kwa njia ya mikopo, ili liweze kufanikisha.

Mhe. Spika, nakuja katika sehemu ya biashara, uwanja wa kimataifa wa maonesho ukurasa wa 8. Mhe. Spika, kwa kweli hili suala naliunga mkono na nalikubali, kwa sababu Zanzibar tumekua duni kutokana na masuala kama haya. Imekua tunasafiri kwenda Dar es Salaam kupeleka biashara zetu wakati wa saba saba. Mara hii

kama tunaanzisha basi tuwe *serious*, kwa sababu tumeshaanzisha sehemu nyingi, hatimaye serikali inakuja kuchukua kwa kuekeza kwenye masuala ya vyuo vikuu. Tunavitaka vyuo vikuu, lakini na hili nalo ni moja katika kuonesha bidhaa zetu bora za Wazanzibari jinsi gani ambavyo tunaweza kujigomboa katika umaskini. Naomba sana Mhe. Spika, uwanja huu ufanyiwe haraka sana, mzee wa fedha tia fedha watu wafanyekazi ili kuweza kusaidia kuondoa umaskini.

Mhe. Spika, nakwenda kwenye huo huo ukurasa wa 8. Kuhusu masuala ya *deport.* Mhe. Spika, hivi karibuni tulikua na matatizo mengi sana, watu wa *petrol* wanatabia ya kuficha mafuta, sasa hili wanawapa matatizo hawa waendeshaji wa vyombo. Wanakua na matatizo kila siku, msongamano hauishi, mafuta tunauziwa ya rushwa, mafuta yanatiwa na maji. Kwa kweli suala hili tunaomba sheria haraka sana iletwe ya nishati hii, ili kuweza kusaidia kujua nani sasa ni mmiliki wa masuala kama haya. Kwa sababu watu wanavutana hapa. Ukenda idara ya nishati wanakwambia ni mimi lakini sina sheria. Ukenda ZRB anakwambia mimi ni muhusika mpanga bei, lakini sina sheria.

Sasa Mhe. Spika, tunaomba sana iwekwe sheria haraka sana, ili muhusika aweze kufanyakazi kwa vizuri na kuweza kuleta mafanikio, tusiwe kila siku kukicha tunasongamana. Mhe. Spika, tusiwaogope hawa tufanyekazi kwa bidii sana.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 12 mfuko wa hifadhi ya jamii. Mhe. Spika, naomba sana ZSSF sasa hivi ijaribu kutafuta miradi mikubwa, isitafute miradi midogo midogo tukajipumbaza. Juzi tumekwenda kutembea kule Dodoma, tumewakuta wenzetu wameekeza katika vyuo, vile vyuo vyao ni vizuri sana. Kwa kweli wakilipwa zile fedha zinakwenda serikalini moja kwa moja, inakua hawapotezi zile fedha. Kwa hivyo, na hawa ZSSF na wao waige ili kuonesha jinsi miradi mikubwa inavyoekezwa. Wako wasomi kibao wanataka kusoma, kwa hivyo na wao nawaomba sana waekeze kwenye vyuo ili waweze kuzitumia vizuri fedha za hawa wavuja jasho kwa vizuri kabisa.

Mhe. Spika, nakwenda katika ukurasa wa 14 kuhusu majukumu ya tume. Hapa vile vile nakubaliana naye, lakini ile *account* ya pamoja sijui kwa nini mpaka leo haijaweza kusimamiwa na kuweza kupatikana, ili Wazanzibari wakajua haki yao iko wapi. Kila siku tunaambiwa kesho kuna marekebisho haya na yale, lakini hatuoni kitu kinachofanywa. Kwa hivyo, tunaomba tuweze kupatiwa maelezo na yenye umuhimu sana ili tuweze kufanikisha *account* yetu ya pamoja tuijue iko wapi, na kitu gani kimekwamisha mpaka leo hii.

Ukurasa wa 15 Mhe. Spika, kuhusu huduma za Benki ya Kiislamu. Nakubaliana nayo, lakini vile vile Waislamu wanapenda *formality* yao jinsi ya kukopeshana mikopo waelezwe nani na nani wahusika wanakuwemo pale wa kuweza kutoa mifuko hiyo, ili wananchi wanufaike.

Mhe. Spika, niwasifu sana bodi ya mapato. Katika ukurasa wa 17, bodi hii wanafanyakazi vizuri na wanajitahidi, lakini hapa tuweke msisitizo kua waendelee zaidi kujitahidi, kwa sababu hii ndio roho yetu ya Wazanzibari tunayoitumia katika ukusanyaji wa mapato yetu. Naomba sana Mhe. Spika, wamejitahidi na wamefikia malengo, tunaringia na hususani kumpa waziri wao kipaumbele kwenda kusema kua uchumi wangu umekua kutokana na chombo hiki ambacho kinafanyakazi kwa uwadilifu kabisa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tu niende katika sehemu ya *TRA*. Kwanza nimsifu Mhe. Waziri nisimnyime haki yake aliyoifanya hivi karibuni, sote tumemsikia katika vyombo vya habari na ameokoa mali nyingi sana, baada ya kugundua kua watu wanapitisha kinyemela mizigo kule kwa kupitia bandarini. Mhe. Waziri aliwaita na akawakemea na akaifanya kazi nzuri. Lakini Mhe. Spika, bado kazi ingali kubwa unayo mbele, usafishaji ule haujatosha, kutu bado zingalipo. Tunakuomba sana Mhe. Spika, safisha bandarini ili uokowe fedha ili wananchi waweze kupata mahitaji yao ambayo ndio yaliyokusudiwa ya muhimu katika serikali yako ya kimapinduzi ikiongozwa na serikali ya kitaifa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kama nilivyokwambia kwamba sitaki nichukue muda wako mwingi, maana yake Mhe. Spika, umenifurahisha sana leo na mimi nataka nikufurahishe nitumie muda wako vizuri sana katika kuchangia hii.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na ripoti hii iliyosomwa na mwenyewe pale Mnadhimu wetu, Mhe. Salmin Awadh Salmin, namuunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, na wewe Mhe. Spika, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akubariki kila jambo utuamulie kama hivi kwa kheri na fanaka na *Inshaallah* watu wa televisheni leo watatoa tena taarifa hiyo kupitia maelezo yako mazuri sana, ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi).*

Mhe. Hamza Hassa Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyengine kuweza na mimi kuchangia hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nipongeze ripoti hii ya kamati kwa kweli imejikita maeneo mengi na kimsingi imekuja na mambo mengi ambayo tulihitaji tupate maelezo yake, kwa kweli tumeridhika na ripoti hii.

Mhe. Spika, nataka niende moja kwa moja nianze na ukurasa wa 8 ambao unaelezea, kuna kidogo pale juu kinasema, uwanja wa kimataifa wa maonesho ya biashara. Mhe. Spika, katika kitu ambacho naiponageza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujaribu kuliona tena suala hili la kuwa na uwanja wa maonesho wa biashara. Mhe. Spika, tulikua tumeanza maonesho ya biashara hapa Zanzibar katika maeneo ya skuli ya Rahaleo pale, lakini baadae tukahamishia Mwanakwerekwe, na baadae tukapata eneo kubwa sana pale Tunguu, lakini ghafla likabadilishwa na kuwa Chuo Kikuu.

Mhe. Spika, nchi yetu ina asili ya biashara, kwa hivyo moja katika kivutio cha biashara katika nchi yetu ni kuwa na mabanda ya maonesho ya biashara. Tunajua tuna wafanyabiashara wetu mbali mbali wanahitaji kuonesha bidhaa zao. vile vile kuna wafanyabiashara wa nje ambao wanahitaji kuja kuonesha biashara zao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunaomba sana utaratibu huu, huku mwisho kabisa imeelezwa kua wamo katika utaratibu wa kutafuta tenda ya kuweza kujenga hilo eneo kwa ajili ya maonesho ya biashara. Mhe. Spika, suala hili serikali ikilifanya kwa kweli tutawashukuru sana, kwa sababu itazidi kuwahamasisha wafanyabiashara wetu wakubwa na wadogo kuweza kufanya biashara pamoja na wengine wa kimataifa.

Mhe. Spika, katika ukurasa huu huu wa 8. Kamati imeelezea vile walivyotembelea lile Shirika la Viwango. Mhe. Spika, hili ni suala muhimu sana na ukiangalia Zanzibar iko haja kua tuwe na chombo kama hiki. Kwa sababu Mhe. Spika, ukiangalia sasa hivi kuna bidhaa nyingi, sitaki kuitaja nchi tukawa kama tunaidhalilisha kibiashara. Lakini bidhaa nyingi ambazo zinazotoka maeneo ya China, wafanyabiashara wetu wanakwenda kununua vitu ambavyo viko katika *low quality*. Kwa hivyo, mara nyingi vikishatumika hapa Zanzibar vinakua havichukui muda mrefu vinakua vinachakaa. Sasa tulikua tunaomba sana hiki kitengo cha Shirika la Viwango, wenzetu wametembelea Tanzania Bara, yaani TBS wakaona. Kwa hivyo, ni vizuri na hapa Zanzibar tukawa tuna kitengo kama hicho ambacho kitakua kinafanyakazi kwa kuwasaidia zaidi wafanyabiashara wasilete bidhaa dhaifu, lakini vile vile na wananchi wetu wasinunuwe bidhaa ambazo ziko chini ya kiwango.

Mhe. Spika, hapo hapo kwenye ukurasa wa 8 imeendelea hapo, kwamba ziara ya kamati katika *deport* ya Mtoni. Mhe. Spika, tumeona maoni ya kamati na vile vile wakajaribu kushauri au kupiga vita ile biashara ya mafuta ambayo wanayoleta meli kwa meli. Kwa kweli ilikua kidogo inayapunguzia mapato serikali. Kwa hivyo, naamini Mhe. Waziri hili ataweza kulisimamia kwa karibu, atakaa na hawa waingizaji wa mafuta ili kuzungumza nao.

Hapo Mhe. Spika, mimi kuna jambo nilikua nataka kidogo nilizungumze, zaidi hapa katikati kulipotokezea uhaba wa mafuta. Mhe. Spika, sitaki niseme kwamba hao wenye biashara ya mafuta walikua wanachakachua mafuta, lakini kimsingi vyombo vyetu vingi vilikua vinatiwa mafuta na mafuta hayo yanaonesha yalikua yanachanganyika na maji.

Mhe. Spika, kuna gari nyingi zimepata matatizo vile vile na Vespa zimepata matatizo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunawaomba wafanyabiashara wetu hasa wanaoleta mafuta, kwamba Zanzibar ni nchi maskini uchumi wenyewe ndio huo huo, vespa mtu kakopa, gari kakopa, leo anapotia mafuta matokeo yake *engine* ikija ikiharibika mtu yule huku anadaiwa deni, hajamaliza kulipa lakini tayari *engine* yake ya gari umeshaiharibu. Kwa hivyo, tunawaomba sana wawe waungwana.

Vile vile kamati hapa ilijaribu kushauri na hapa Zanzibar kuwe kuna chombo ambacho kinadhibiti hasa hili suala zima la ukaguzi wa haya mafuta. Wenzetu kule Bara wana ile *EWURA* kama walivyosema, hua wanatembelea mpaka katika vituo wakati mwengine kwenda kuangalia. Katika ule uangalizi wao wanavamia tu, wanajaribu kwenda kupima yale mafuta, wakati mwengine wanayakuta katika yale ma-*tank* mafuta yanakua yamechanganyika na maji. Kwa hivyo, suala hili mimi nadhani Mhe. Spika, wakati sasa umefika ili taasisi zetu hapa Zanzibar zinazofanyakazi basi wafanyekazi kwa uadilifu uliokua mkubwa sana.

Mhe. Spika, nikiendelea niende katika ukurasa wa 14. Ukurasa huu ripoti ya kamati inaeleza tume ya fedha ya pamoja. Mhe. Spika, kama tunavyojua katiba ya Muungano kifungu 134, tume hii imetajwa ndani ya katiba. Lakini Mhe. Spika, kitu cha kusikitisha tume hii tokea imeundwa baadae ikaundwa na ile sheria, kama inavyoelezwa humu kamati. Lakini mpaka leo wamepeleka mapendekezo kwenye Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kimsingi hakuna lolote ambalo mpaka sasa hivi linalofanyika.

Sasa mimi ushauri wangu Mhe. Spika, nadhani sasa hivi wala tusimpe tabu Mhe. Waziri kwa kusema kwamba labda shughulikia hili na hili. Mimi nafikiria muda umebakia mchache, ni miaka miwili tu, mwaka 2014 ukifika, nadhani Zanzibar, sitaki kuwashawishi wananchi. Nadhani katika mambo yote ya uchumi kila nchi ishughulikie mambo yake. Hatuna haja tena kuishughulisha labda tume ya fedha ya pamoja, kwa sababu haya mambo yako katika msokoto mkubwa, msokoto na msokotano. Kuna masuala ambayo hayana jawabu wala hayawezi yakapatikana jawabu. *(Makofi)*

Kwa kweli tunawashughulisha wataalamu pamoja na wanasheria wetu wanakuja kutuambia maneno hapa wakati mwengine wanarejea yale kwa yale, kwa sababu maswali hayana jawabu, isipokuwa jawabu ni masuala ya kiuchumi yote kuyaondoka katika masuala ya Muungano. Kwa mfano, hii Tume ya Fedha ya Pamoja tokea ilipoundwa tayari imeshauri mambo mengi, lakini namna yalivyosokotwa au yalivyopindwa, basi hujui kipi cha Muungano na kipi si cha Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati umefika Wazanzibari tufanye maamuzi magumu kuhakikisha masuala yote ya uchumi kila mmoja akashughulikie la kwake, ili tusiendelee kuwashughulisha watu, kwa sababu tumeunda tume tunawalipa mafao au fedha, lakini ushauri wao hakuna mtu yeyote ambaye anayeushughulikia.

Nikiendelea na mchango wangu katika ripoti ya kamati sasa niende kwenye ukurasa wa 15 ambao unaelezea suala zima la *Islamic Bank*. Mhe. Spika, tunashukuru sana Benki yetu ya Watu wa Zanzibar kwa kuanzisha hii *Islamic Bank*. Kwa kweli *Islamic Bank* kama tutaitumia vizuri Mhe. Spika, basi itaweza kuwasaidia sana wananchi wetu.

Kwa mfano, hivi karibuni ilitoka kauli ingawa haikuwa rasmi, kwa sababu kama ingetangazwa hapa Barazani tungehisi ile kauli ni rasmi, lakini ilitoka kauli kwamba wananchi watafutiwa viwanja vyao wale ambao hawajajenga.

Mhe. Spika, sisi tulishtuka kidogo, kwa sababu ukiangalia mishahara ya wafanyakazi wetu wanayolipwa na viwanja vile vya *plan* mtu anapojenga hatakiwi kwanza ajenge chumba kimoja aweke polo, choo cha pipa, baadaye atoe. *(Makofi)*

Kwa kweli viwanja vya *plan* mtu anapopewa anatakiwa ajenge nyumba ya kisasa, sasa serikali ilipotishia kutaka kuvifuta viwanja vile basi sisi wengine tulitaka kuja kuzuia shilingi hapa, kwa nini wafutiwe viwanja na halafu tungewauliza je mshahara wa mwananchi anaoupata anaweza kulisha familia yake na halafu akajenga nyumba.

Sasa mimi nadhani kwa kuleta *Islamic Bank* Mhe. Spika, huu ni uokozi kwa wananchi. Kutokana na hali hiyo, naomba kutoa ushauri kwamba hivi sasa *Islamic Bank* wanaweza kufanya biashara kubwa Zanzibar, kwa sababu wapo wananchi wengi ambao wanavyo viwanja, lakini uwezo wa kujenga hawana.

Kwa hivyo, ni vyema wakafunga mikataba na zile nyumba wakajenga wao *Islamic Bank* na halafu wananchi wakapewa kwa mikataba maalum, ambapo wakaweza kuwalipa kidogo kidogo, yaani kila mwezi nadhani hii itaweza kuwasaidia sana kuweza kufanya kazi zao vizuri na hii *bank* ikaweza kuwasaidia wananchi pia.

Mhe. Spika, najua unaangalia saa, lakini nakwenda haraka haraka. Sasa niende kwenye ukurasa wa 19 imeelezwa hapa kuhusu *ZRB*, *TRA*. Mhe. Spika, nawapongeza sana ndugu zetu hawa *ZRB* pia nampongeza sana Mhe. Waziri Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa jitihada zake, kwamba hivi sasa kila wakati anakaa na vyombo vyake vya fedha na kutoa taarifa mbali mbali kuhusu ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Kwa kweli tunawashukuru sana ndugu zetu wa *ZRB* wanajitahidi kukusanya mapato na wanavuka mpaka malengo yao. Lakini bado tunamtaka Mhe. Waziri aendelee kujitahidi kwa sababu hatutaki fedha zikalipwe kwenye mkoba, isipokuwa tunataka fedha zilipwe kupitia malipo ya bank, kwani fedha zikilipwa kupitia *bank*, basi nadhani mapato haya ya *ZRB* yataongezeka kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Vile vile nataka niunganishe na *TRA* hapa hapa. Mhe. Spika, bado wafanyabiashara wa Zanzibar pamoja na vikao vyote vinavyokaa vya Kero za Muungano pamoja na mambo mengine, lakini bado malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kuendelea kulipa kodi katika taasisi mbili tofauti hili bado si suala sahihi. Kutokana na hali hiyo, tunahisi Mhe. Spika chombo chetu ambacho tumekipitisha hapa *ZRB* kipewe mamlaka ya kukusanya kodi zote kwa upande wa Zanzibar, Mhe. Spika hili tunalizungumza mara kwa mara. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni msikivu sana, hebu safari hii awe msikivu kabisa, ili atakapokuja kwenye bajeti yake atuambie ile Mamlaka ya Ukusanyaji wa Kodi Zanzibar yote tunaikabidhi Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*). Mhe. Spika, naamini tukiwapa kazi hii ufanisi utazidi pia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nizungumzie kuhusu suala zima la *BoT*, ambalo limeelezwa katika ukurasa wa 16 pamoja na jinsi inavyofanya kazi zake ku-*regulate* uchumi wa Zanzibar pamoja na wenzetu wa Tanzania Bara. lakini bado Mhe. Spika kwenye ripoti hii ya Kamati nasikitika sana kwamba pia wamegundua kuwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanaendelea kusikitika kwamba wanahitaji kufanyabiashara wakati mitaji yao midogo.

Kwa kweli suala hili napenda sana kulirejea, yaani bado *BoT* haitutendei haki. Mhe. Spika, Zanzibar wapo wafanyabiashara wengi ambao wanaoweza kupata mikopo kupitia hii mikopo ambayo *BoT* wanaita *Small Medium Enterprise* (*SME)*, ambapo kwa wenzetu kule Tanzania Bara kule Mhe. Spika wanapatiwa mikopo mpaka *billion* 4 na hizi sio fedha kidogo, sasa na hapa Zanzibar wapo wafanyabiashara. Kwa mfano, ukiangalia hao wafanyabiashara wa Bara wengi walikuja kujifunza hapa Zanzibar, sasa leo inakuwaje wafanyabiashara wa Zanzibar waweze kukosa hizi fedha kutoka *BoT*.

Mhe. Spika, tunaomba sana kwa sababu wenzetu *BoT* na suala hili tumeshalirejea mara nyingi na tunawajua watendaji wao wapo hapo juu, basi ni vyema wakae na wafanyabiashara wetu wa Zanzibar na waangalie fedha hizi hawazihitaji, kwa kweli wafanyabiashara wetu fedha hizi wanazihitaji. Kwa hivyo, tunaiomba sana *BoT* kupitia kwako Mhe. Spika, iweze kutoa mikopo hii kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Sasa niende kwenye ukurasa wa 20 kuhusu *ZIPA*. Mhe. Spika, bado hapa narejea tena ndugu zetu wa *ZIPA* wakati wanapotoa vibali hasa kwa wawekezaji, yaani katika Sekta ya Utalii, wanashindwa kuwashirikisha kikamilifu ndugu zetu au Idara inayoshughulikia mazingira.

Kwa mfano, juzi Mhe. Spika wakati tulipokuwa tunapitisha ile Sheria ya Kamisheni ya Utalii, nilikuwa mkaidi sana na wala sikukubali kwenye ile Kamisheni kwamba Mkurugenzi wa Mazingira asiwepo na nilizungumza vile kwa sababu naona uchungu kwamba miradi inapitishwa na *ZIPA*, lakini miradi ile ikienda kwenye *field* Mhe. Spika inakuwa moja miongoni mwa miradi inayoharibu mazingira kwa hapa Zanzibar. Sasa tunajiuliza hiki ni chombo chetu tumekipitisha ndani ya Baraza la Wawakilishi, yaani kipo kisheria, lakini bado miradi ambayo inapata kibali kwa *ZIPA* wakati unapokwenda *field* unaikuta imefanya uharibifu mkubwa wa mazingira. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika *ZIPA* wanapotoa vibali, basi lazima wawashirikishe ndugu zetu wa Idara ya Mazingira, ili kuhakikisha kwamba udhibiti wa mazingira unahifadhiwa.

Mhe. Spika, nataka nitoe mfano mdogo kuhusu haya Maeneo Huru ya Kiuchumi (*Special Economic Zone*). Mhe. Spika, sisi ulitupeleka China nashukuru katika Baraza lako tukufu mimi uliniteua katika kundi la mwanzo nilikwenda China. Kwa kweli wenzetu kule China na hii naizungumza zaidi katika masuala mazima pamoja na kwenye kodi hasa kwa upande wa Zanzibar na Bara.

Mhe. Spika, wenzetu kule China baada ya kuona kilimo kitachukua muda mrefu kuweza kuwaokoa katika uchumi, yaani kuinua uchumi wao, basi walihamisha sera yao katika kilimo na kuhamishia zaidi katika maeneo ya uwekezaji (*Special Economic Zone*). Mhe. Spika, ndani ya ile China yenyewe ulipaji wa kodi katika yale maeneo ambayo wanaanzisha ile *Special Economic Zone* wanaweka mpaka utaratibu maalum.

Kwa mfano, eneo la Micheweni ambalo lenye umasikini mkubwa, basi hata zile kodi za upande wa kule zinakuwa ziko chini, ili kuweza kuwavutia wafanyabiashara waweze kwenda kuwekeza katika maeneo ya kule. *(Makofi)*

Lakini bado kwa upande wetu wa hapa Tanzania, uwekezaji wa Zanzibar na Bara utakuta kodi ni moja, ndio maana tukasema kwamba hata katika malipo ya wafanyabiashara kodi za Zanzibar na Bara lazima ziwe tofauti, kwa sababu uchumi wetu ni tofauti.

Mhe. Spika, tunapopelekwa safari tunatakiwa tukajifunze. Kwa kweli China tumejifunza ndani ya ile China moja, yaani China Bara, basi kodi katika maeneo tofauti zinakuwa ziko tofauti na wala haziko sawa kama maeneo mengine.

Mhe. Spika, nataka nimalizie haraka najua unajaribu sana kuangalia saa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, malizia kwa dakika mbili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hee! Mhe. Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la kilimo ambapo juzi tumepitisha ile Sheria kuhusu Utafiti wa Kilimo. Mhe. Spika, katika eneo ambalo tunaweza kuwasaidia sana na kuwaondolea umasikini wananchi wetu ni eneo la kilimo, lakini bado tunahitaji tufanye utafiti wa kina. Kwa mfano, hivi sasa tukiangalia Mhe. Spika uwekezaji wa Zanzibar hasa katika maeneo ya hoteli tunaagizia mboga mboga nyingi sana tena zinatoka Tanzania Bara. Mhe. Spika, Zanzibar tunayo maeneo mazuri tena makubwa au mabonde mazuri ambayo baada ya kulima mpunga wakati mwengine basi tunaweza kulima hata mboga mboga, ambapo soko lipo kubwa sana katika maeneo ya utalii.

Mhe. Spika, kama utafiti wa kilimo unahitajika kufanyika, basi ufanye hasa katika yale maeneo ambayo tunayoweza kuzalisha mboga mboga. Lakini tunamuomba sana Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili kupitia kwako Mhe. Spika kwa kweli amepewa wizara ambayo ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu, lakini hayo maeneo ya kilimo Mhe. Spika hivi sasa yanavamiwa sana kwa ujenzi wa nyumba za makaazi.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili kupitia kwako Mhe. Spika asikae tu afisini na tunamtaka aende mabondeni akasimame kwenye mabonde ya mpunga pamoja na yale ya mboga mboga, ili ahakikishe wale wote wanaojenga kwenye maeneo yale nyumba zile zote anaziondoa na eneo libakie kwa ajili ya kilimo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa Shirika la Bima tunalipongeza kwa kazi zake nzuri. Lakini bado tunaomba Mhe. Spika, suala la bima kwanza katika mambo ya Muungano halimo. Kwa kweli bado kuna sheria ambayo inayodhibiti Mashirika haya ya Bima likiwemo la Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunasikitika sana Shirika la Bima bado linaendelea kukodi maeneo mengi hasa kule Tanzania Bara. Kwa mfano, katika lile eneo la Mtaa wa barabara ya Uhuru, eneo lile Shirika la Bima walitaka kununua, lakini kwa kuwa kuna ile *regulation* ya Msajili wa Bima Tanzania aliwazuia kwa sababu aliwaambia fedha nyingi watatumia kwa ajili ya kununua lile jengo, matokezeo yake wanaendelea kukodi jengo kwa fedha nyingi sana na tunajua wenzetu Bara hivi sasa kila siku thamani ya majengo inazidi kuongezeka.

Mhe. Spika, tunaomba Shirika la Bima wajaribu kuzungumza na Msajili wa Bima Tanzania, kwamba bima sio mambo ya Muungano na wawaachie pale wanapohitaji kununua zile *asset*, kwa sababu bado *liquidity* ni kubwa tunaijua ya Shirika la Bima, yaani wanao uwezo wa kulipa fidia kwa wale wateja wao pale inapotokezea matatizo.

Mhe. Spika, ili mara nyengine usijekuninyima fursa hii, basi naomba niishie hapo. Lakini kama nilivyosema mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaipongeza pamoja na kuishukuru Kamati hii, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa mara nyengine tena asubuhi hii kupata nafasi ya kutoa mchango wangu katika Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nimpongeze sana Mhe. Salmin Awadh Salmin ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii kwa uwasilishaji mzuri aliofanya kwa muhtasari wa ripoti yake, ambao umetusaidia sana kuweza kujikita katika yale maeneo, ambayo ni machache na kila mmoja anaweza kupata nafasi ya kuyachangia. *(Makofi)*

Vile vile niwapongeze na Waheshimiwa Wajumbe wengine wote wa kamati hii kwa kazi nzuri walioifanya na ripoti yao nzuri imejumuisha maeneo mengi sana muhimu katika kuzingatia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba katika mchango wangu kwanza nianze katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ukurasa wa nane wa ripoti kuhusiana na suala ambalo tayari wenzangu wawili waliochangia wameligusa hivi sasa.

Mhe. Spika, suala linalohusu biashara ya mafuta hapa Zanzibar. ni kweli kabisa hatua iliyojitokeza hivi karibuni kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya wananchi wengi, ambao wanaotumia vyombo vya moto kupiga kelele suala la kuharibikiwa na vyombo vyao, kutokana na uhafifu wa viwango vya mafuta vilivyopatikana hivi karibuni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati kwenye ripoti imeeleza hapa kwamba urasimu mkubwa katika Bandari ya Dar-es-Salaam kutokana na kubadilika kwa Sheria ya *EWURA*, ambayo inaruhusu muagizaji mmoja tu wa mafuta kutoka nje ya nchi na kuzizuia kampuni mbali mbali za mafuta.

Kutokana na hali hiyo, kumesababisha kuwepo kwa foleni kubwa, jambo ambalo linapelekea meli ndogo hasa zinazotoka Zanzibar kuchelewa kuyapata mafuta hayo kwa wakati, ambapo Kampuni ya *GAPCO* ndio inayochukua Dar-es-Salaam.

Mhe. Spika, hoja yangu hapa ni kwamba kwanza *EWURA* si chombo cha Muungano. Lakini ndio hayo yanayozungumzwa maswali yasiyo na majibu. Kwa mfano, ukitizama katika orodha ya mambo ya Muungano, mafuta limechambuliwa sana kwamba pengine ni pamoja na biashara ya mafuta, lakini uendeshaji kwa upande wa Zanzibar kwa miaka yote haujawahi kufanywa kimuungano. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, nadhani bila ya kurefusha mjadala, basi nafikiri Serikali ya Jamhuri ya Muungano umechukua hatua katika kudhibiti bei pamoja na mambo mengi kuwa na utaratibu huu wa kuwa muajizaji mmoja (*Balk Oil Importer* na halafu baadaye wakawasambazia wengine.

Mhe. Spika, nikasema kama ni hivyo, basi kwa nini Zanzibar na sisi tusianzishe utaratibu wetu wenyewe wa ku-*import* mafuta yetu sisi wenyewe hapa na kuyasambaza kwa watumiaji wa Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa kweli katika hili nawatetea sana wauzaji wa biashara ya mafuta kwa Zanzibar katika suala hili la uchakachuaji, kwa sababu suala hili kwa wenzetu Bara limekuwa ni tatizo la muda mrefu sana na wala hatukulisikia Zanzibar hata siku moja Mhe. Spika. Lakini limejitokeza hivi karibuni baada ya kuja utaratibu huu, kwa sababu sasa wanalazimika kuchukua mafuta kule ambako yanakoagizwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati fulani tulikuwa na utaratibu hapa hata bei yetu ilikuwa rahisi, kwa sababu wafanyabiashara ya mafuta walikuwa wanachukua mafuta kutoka Mombasa Kenya. Lakini tumekuja kuingiza vizingiti vingi katika yale maswali yasiyo na majibu kuhusu Muungano, basi na sisi tunalazimika hata hili tukachukue mafuta kutoka kwa ndugu zetu wa damu.

Sasa lile linalowasumbua wao limeingia na Zanzibar kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma hapa Zanzibar likiingia linaathiri sana, kwa sababu hali ya uchumi wetu ni mdogo, wananchi wetu wengi ni masikini, sasa unapomuharibia chombo chake kwa sababu ya mafuta ambayo ni hafifu katika ubora wa kiwango, unamuathiri sana Mhe. Spika.

Kwa hivyo, katika hili nataka kutoa pendekezo kwa serikali, kwamba kama ambavyo wenzetu wanavyoliangalia kuwa wamejinusuru wao kwa kutafuta *One Major Balk Oil Importer*, basi na sisi Zanzibar tuwe na utaratibu kwa kiwango hicho kidogo tuwe na uagiziaji wetu wa mafuta, kwa ajili ya kuhudumia soko la ndani la Zanzibar. Mhe. Spika, naomba sana suala hili serikali ilitizame katika kujibu hii hoja ambayo imetajwa katika ukurasa wa nane. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende katika Wizara ya Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambayo imeanza ukurasa wa 10 hadi 23 kama sikosei.

Mhe. Spika, katika hii naomba nianze pale ilipo *BOT* kwenye ukurasa wa 16. Kwa kweli Mhe. Hamza Hassan Juma amesema hapa kwamba *BOT* ni chombo cha Muungano na hichi ndicho kinachosimamia masuala mazima ya sarafu pengine na kuratibu uchumi wetu. Lakini kama tunavyosema mara nyingi katika Baraza hili, yaani wengi au sote tunaochangia humu, kwamba uchumi katika Jamhuri ya Muungano kuna chumi mbili na chumi hizi kwa vyovyote hazilingani.

Kwa maana hiyo, uchumi wa Bara siku zote utakuwa ni *resource based*, kwa sababu wenzetu ni nchi kubwa na yenye rasilimali nyingi za maumbile. Lakini sisi Zanzibar kama visiwa uchumi wetu ni *service based*. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile masuala ya uwekaji wa viwango vya kodi za aina mbali mbali, inataka vitizame kiasi gani vinahudumia chumi hizi mbili kwa njia tofauti na kila moja iweze kujenga uchumi wake kulingana na hali halisi ya maumbile ya eneo letu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyosema uchumi wetu ulipaswa kuwa uchumi wa huduma. Kwa maana hiyo, uchumi wa huduma ni lazima uvutie kwa kuwa na viwango vidogo vya kodi. Mhe. Spika, katika masuala ya uchumi Mhe. Waziri ni mtaalamu zaidi kuliko mimi, yaani ni mtaalamu sana na wala mimi si mtaalamu wa fani hii, lakini tunajua kwamba *Interest Rate* ndiyo inayotumika ku-*regulate economy* ya nchi. *(Makofi)*

Lakini leo sijui na mara nyingi katika kuzipitia *reports* za *BOT* sidhani kama zinaonesha hilo, kwamba katika ku-*set* hizi *Interest Rate* tunaangalia haja ya ku-*set Interest Rate* ambazo zita-*regulate* uchumi wa Zanzibar mbali kwa viwango vyake na haja ya kuzingatia *Interest Rate* kwa upande wa Bara mbali. Mhe. Spika, katika hili BoT bado haisaidii Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla ya kuja kwa Benki Kuu ya Tanzania mwaka 1966 tulikuwa tukitumia nchi zote Sarafu ya Afrika ya Mashariki na kulikuwa na Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki, ambapo huku nyuma wanachama wake walikuwa ni nchi 6, yaani ilikuwa Kenya, Uganda, Tanganyika, Zanzibar Aden na Somalia, baadaye wenzetu wa Aden na Somalia wakajiondoa na kubakia nchi 4. Lakini katika kufanya maamuzi katika uwakilishi kwenye vyombo vyake, yaani ile bodi yenyewe, basi kila nchi ilikuwa ikipewa haki sawa na hata katika kupata huduma zinazotolewa na Bodi ya Sarafu ilikuwa inafanyika sawa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ndio maana hata Bodi hii ilipokuwa inavunjwa Zanzibar ilipata mgao wake kutokana na kuvunjwa kwa bodi hii. Kwa kweli umeliwa katika *BoT* mpaka leo hatupati chochote katika *BOT* wakati tumeingiza hisa yetu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa mara nyengine tena wakati atakapokuja atueleze suala hili limefikia wapi? Katika kuundwa *BOT* Zanzibar iliingiza mtaji wa hisa asilimia 11.02. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ilipaswa kuanzia mwaka 1966 hadi hii leo katika faida inayotokana na *BoT* Zanzibar ipate mgao huo na hivi karibuni imefanya utaratibu inapata mgao, lakini siamini kama unalingana na asilimia hii 11.02.
Vile vile yale madeni ya nyuma kuanzia mwaka 1966 mpaka pale tulipoanzwa kulipwa na sijui ilikuwa mwaka gani katika miaka ya 1990 hatujaambiwa chochote. Je, deni lile la miaka yote ambapo Zanzibar ilipaswa kulipwa kutokana na mchango wake wa hisa na si kama mbia kama Muungano, isipokuwa ni kama mwenye hisa kwenye Benki Kuu litalipwa lini, naomba Mhe. Spika nipatiwe maelezo? *(Makofi)*

Lakini lengo kubwa la BoT ni ku-regulate uchumi bado Zanzibar hawajatusaidia. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Spika, aje na mapendekezo ili tuone vipi tutasaidiwa katika kupata utaratibu wetu wa ku-*regulate* uchumi wetu kulingana na mahitaji ya uchumi wa visiwa. Hilo naomba niliache hapo Mhe. Spika.

Sasa naomba niende katika suala la mapato nitachanganya pamoja kuhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania na *ZRB*. Mhe. Spika, ukurasa wa 19 wa ripoti katika kuzungumzia viwango vya ukusanyaji naomba nisome paragraph ya pili kutoka chini kwenye ukurasa wa 19, Mhe. Spika naomba kunukuu.

Ukurasa wa 19 *paragraph* ya pili kutoka chini inaeleza hivi:-

> "Idara ya Forodha imevuka lengo la kipindi hicho cha miezi saba kwa takriban kwa asilimia 109 baada ya kukusanya shilingi 31,485.9 milioni. Aidha Idara ya Kodi za Ndani haikufikia lengo la kipindi hicho baada ya kukusanya shilingi 18,294.6 milioni dhidi ya lengo la shilingi 28,897 milioni. Utendaji huu ni wa asilimia 63".

Kwa maana hiyo, Idara ya Kodi ya Ndani katika *TRA* kiwango kilichoekewa kimepatikana asilimia 63.

Mhe. Spika, maelezo yanapatikana hapa hapa, Ripoti ya Kamati inaeleza kwenye ukurasa huo wa 19 paragraph ya mwisho Mhe. Spika naomba kunukuu.

Ukurasa wa 19 paragraph ya mwisho inaeleza hivi:-

> "Sababu kubwa ya kutofikia lengo kwa Idara ya Kodi za Ndani Zanzibar kumechangiwa na kutohaulishwa kwa shilingi 10,500 milioni za *PAYE* kwa kipindi cha Julai hadi Januari, 2012 zinazotokana na watumishi wa Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar…"

Mhe. Spika, nakumbuka Mhe. Waziri mara nyingi ametujibu humu ndani, kwamba unafanywa utaratibu, ili payee kwa wafanyakazi wa Taasisi za Muungano wanaofanyakazi Zanzibar, kwa sababu wanatumia huduma ambazo zinatoka Zanzibar, yaani zinatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi kodi hii iwe inaingia katika Hazina ya Zanzibar. Sasa ninapata mashaka nikiambia kwamba lengo halikufikiwa kwa sababu fedha hizi hazikuingizwa. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri katika hili atusaidie tumefikia wapi au ndio muendelezo wa maswali yasiyo na majibu katika Muungano?*(Makofi)*

Mhe. Spika, hapo hapo niunganishe hoja yangu nyengine. Kwa mfano, ukiangalia utendaji wa *ZRB*, unaonekana katika kila sehemu takriban ama malengo yamezidiwa yamevuka kiwango au kama yamepungua basi ni kwa asilimia chache ambayo inafidiwa na kule ambako ifanya vizuri. Kwa hivyo, *ZRB* inafanyakazi nzuri zaidi kuliko *TRA* kwa Zanzibar na inaonekana wazi wazi. *(Makofi)*

Sasa kama ni hilo nakumbuka wakati Mhe. Rais wa Zanzibar alipokuwa akifungua jengo jipya zuri kabisa, pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika kulisimamia hili jengo la Makao Makuu ya *ZRB* hapo maeneo ya Mazizini. Kamishna wa ZRB ndugu Moh'd Hashim Ismail, yeye mwenyewe ambaye ndiye msimamizi wa ZRB aliiomba serikali pamoja na Mhe. Rais pale kwamba wakati umefika sasa Zanzibar kuwa na Mamlaka moja tu ya Kodi. *(Makofi)*

Vile vile alisema kwamba tunazungumzia Zanzibar uchumi wake unategemea zaidi biashara, lakini ikiwa biashara zenyewe kuna utitiri wa kodi, kwa sababu kila mamlaka wakati ipo itatafuta njia zake za kukusanya kodi na tunajua kwamba zote zinaongozwa na sheria. Lakini naamini kama ingekuwa Zanzibar ina mamlaka moja, basi ingeweka utaratibu mzuri zaidi wa pengine kutanua wigo wa walipa kodi badala ya kuwakamua wale walipakodi waliokuwepo, kwa ajili na wao waweze kuimarisha biashara na Zanzibar iweze kutononoka.

Mhe. Spika, katika hili kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma, basi Mhe. Waziri atakapokuja atatueleza hapa kwamba tunachukua taratibu gani, kwa sababu haya ndiyo matakwa ya watu wa Zanzibar, yaani kila wanapopata nafasi katika *Forum* Wazanzibari wanazungumza hili la suala la kuwa tunahitaji mamlaka moja ya kodi. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja atuambie lini tutafanya utaratibu, ili tubakie na *ZRB* kwa ajili ya kukusanya kodi na wala sidhani kama kutakuwa na ubaya kuwa na mamlaka moja ambayo itakuwa inakusanya kodi za Muungano ambazo zinazotambulikana na zile ambazo za Zanzibar zinapaswa zikusanywe.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala la Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, malizia kwa dakika mbili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, suala hili lipo kwenye ukurasa wa 14 katika ripoti hii. Kwa kweli katika ripoti hakuna maelezo kuhusiana na jambo hili zaidi ya kueleza kazi zake pamoja na mapendekezo ya ripoti. Mhe. Spika, inafahamika na wala simlaumu Mhe. Salmin Awadh Salmin ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja wajumbe wake, kwa sababu wataripoti nini kwetu na wizara itaripoti nini kwetu.

Mhe. Spika, tangu mwaka 2006 Mshauri Mwelekezi na siku hizi nadhani imekuwa katika kutafuta maswali yasiyo na majibu, basi imekuwa ni kutafuta Washauri Waelekezi Mhe. Spika, kwa sababu hili lilitafutiwa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuja kuzishauri serikali zetu, namna ya kutekeleza kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu cha 133 na 134 kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha na *Account* ya Pamoja ya Fedha. *(Makofi)*

Sasa alipokuja Mshauri Mwelekezi alifanyakazi nzuri na kuonesha kwamba vyanzo vya mapato vya Muungano vinatosheleza kuendesha Muungano bila ya haja ya Tanganyika na Zanzibar kuchangia chochote. Mhe. Spika, kinyume chake ilipaswa Serikali ya Muungano kutokana na vyanzo vya mapato itoe gawio kwa serikali hizi mbili kama kila moja ingekuwa na upande wake na serikali yake, kwa sababu kuna kuwa na bakaa ya matumizi na mimi Mhe. Spika nilipata kuiona nakala ya Ripoti ya Mshauri Mwelekezi huyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sisi tangu mwaka 2006 na katika hili nimpongeze sana Rais Mstaafu wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume. Kwa kweli alifanyakazi ya kushirikisha pande zote mbili kabla hata Mfumo wa Umoja wa Kitaifa bado haujaletwa wakashiriki katika Semina iliyoandaliwa kwenda Kupitia Ripoti ya Mshauri Mwelekezi. Zanzibar imefanya mapendekezo yake, yaani imemwita Mshauri wa Ziada wake kuja kushauri namna ya kuandaa mapendekezo yake na upande wa pili tangu mwaka 2006 mpaka leo bado umebana kimya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama ninavyosema mara nyingi hawa kweli hawajafanya maamuzi au hawana nia ya kufanya maamuzi na wala hawawezi kufanya maamuzi, kwa sababu utaratibu uliopo sasa unawanufaisha wao na kuinyonya Zanzibar. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, nadhani imefika wakati serikali ituambie, lakini kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma kama hakuna majibu basi ni muendelezo wa maswali yasiyo na majibu, basi nafikiri wananchi wa Zanzibar watakuwa na majibu.

Vile vile mimi kama mwananchi wa Zanzibar tukijaaliwa tutafika pahala nitakuja kusema ikifika wakati wake, kwamba nadhani kwa Muungano huu uliopo sasa wa Katiba, nadhani tutafika pahala tuseme tunahitaji tuweke upande na tuwe na Mkataba ambao utakuwa kila nchi na mamlaka yake na ifanye mambo yake na halafu yale ya ujirani mwema pamoja na ushirikiano ya udugu itakuwa tukishirikiana. Lakini maswali haya yasiyo na majibu yamalizike na tupate majibu ya ufumbuzi wa matatizo yetu katika Zanzibar. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema naiunga mkono Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Mji Mkongwe, ambayo katika haya ninayoyasema wao wanaouchungu sana kuliko hata mimi ninayezungumza hapa. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu, pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia machache katika Ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Kwanza nichukue fursa hii kwa kumpongeza Mhe. Salmin Awadh Salmin ambaye ndiye Mwenyekiti wa kamati hii pamoja na wajumbe wake, kwa kuitengeneza ripoti hii na kuiwasilisha katika Baraza hili kwa umakini na umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kuiunga mkono ripoti ya kamati mimi mwenyewe binafsi pamoja na wanawake wenzangu wa Wilaya ya Micheweni kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Kwanza nataka niseme kwamba kilimo ndio uti wa mgongo. Lakini tujue kilimo kinacholimwa hapa Zanzibar zaidi watu wanategemea kulima kilimo cha mpunga, ambacho kuwa kwa asilimia kubwa ya wakulima wa mpunga ni wanawake, ambao wengine ni wajane na nguvu zao ni ndogo. Kutokana na hali hiyo, wanahitaji mchango mkubwa kupitia serikali yao kwa kuwawezesha katika ufanisi huo wa kulima kilimo hicho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa niende kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili katika Idara ya Umwagiliaji Maji. Kwanza kabisa nachukua fursa kuipongeza idara hii kwa malengo yao ambayo wamejipangia pamoja na serikali kwa jumla jinsi wanavyoshughulikia malengo na kuyatekeleza kwa umakini. *(Makofi)*

Kwa mfano, malengo yao ni pamoja na kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji kwa kuongeza maeneo mengine ambayo hayako katika umwagiliaji maji. Vile vile kuendeleza uchimbaji wa visima katika mabonde mbali mbali na upelekaji wa umeme pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Mabwanashamba na Mabibishamba, ambao wataelimisha watu katika masuala mazima ya kilimo.

Mhe. Spika, naiomba Wizara hii ya Kilimo na Maliasili, kwa sababu hawa Mabwanashamba na Mabibishamba mara nyingi sehemu wanazokwenda ni zile za umwagiliaji maji, ambazo wengine huwa kama ni wafanyakazi walioajiriwa. Pia wanakwenda kwenye miradi mingine ambayo pengine ni Kilimo cha Mboga Mboga au kuna mradi wa upandaji wa migomba, basi humu utawakuta Mabwanashamba na Mabibishamba wanafanyakazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Lakini kuna hawa wakulima ambao wanategemea kilimo chao cha mvua, kwa kweli katika maeneo yale si aghalabu sana kuwakuta hawa Mabwanashamba na Mabibishamba katika kuwapa elimu wakulima wale, ili na wao waweze kulima katika mpango uliomzuri, kwa sababu wengine wanalima hata utaalamu hawana.

Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia kwako Mhe. Spika, Mabwanashamba pamoja na Mabibishamba wawawezeshe, kwa ajili ya kuwafuatilia wakulima wale wanaotegemea kilimo cha mvua, kwa sababu wizara haina uwezo wa kuyaweka mabonde yote katika mpango huo wa umwagiliaji maji. Lakini na wale wanaolima katika mfumo wa kutegemea mvua, basi na wao pia wanahitaji taaluma nzuri ili waweze kufanikiwa katika kilimo chao.

Mhe. Spika, bila ya kusahau kuwapelekea matrekta kwa wakati unaofaa. Kwa kweli kilimo cha mpunga kama hujakilima kwa wakati, basi siku zote utalima na matokeo yake huvuni. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa jumla kwa kutaka kuwa na lengo la kuanzisha Shirika la Viwango, kwa kweli naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika suala hili ni lazima tujipange, kwa sababu serikali yetu inaukosefu wa wataalamu katika sekta zote zilizopo hapa Zanzibar. Kwa hivyo, tukizingatia Shirika hili la Viwango ambalo linategemewa kuanzishwa, kwa sababu mimi ni Mjumbe ya Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo na tuliwahi kutembelea Shirika hili la Viwango *TBS* Dar-es-Salaam. Mhe. Spika, kwa taarifa hilo Shirika lenyewe liko kwenye kiwango, sasa ukiangalia sisi hata Mtaalamu wa Kung'oa Meno hatuna. Kwa maana hiyo, tunahitaji kujipanga vizuri sana na wala sio mas-hara katika kuanzisha hili shirika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naiomba serikali ijipange kwa hili na wala isijeikakurupuka na halafu kuja kushindwa njiani au kukafanywa mambo ambayo hayamo katika kiwango. Vile vile kuna suala zima la Maonesho ya Saba Saba. Mhe. Spika, ni kweli Maonesho hayo ni mazuri na yanawasaidia sana Wajasiriamali kupata kuona wenzao wanafanya nini, ili na wao wakirudi waweze kujipanga vizuri. Lakini katika suala hili nimegundua jambo, yaani kunatafutwa watu ambao si Wajasiriamali wakapelekwa kwenye Maonesho haya. Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri wakati tulipokuwa kwenye majumuisho alituambia kulikuwa na Maonesho na kuja Mhe. Rais kukagua maonesho hayo na kulikumutwa mikeka karibu Mhe. Rais kwenda chafya kutokana na vumbi iliyokuwa nayo.

Hali hii inasababishwa na wale wanaochukuliwa wakati mwengine hupewa fomu na kupelekwa kwenye Maonesho yale na wala si Mjasiriamali, yaani akeshakuambiwa kwamba tarehe fulani kuna Maonesho ya Saba Saba Dar-es-Salaam, basi mtu yule anajitayarisha kwa kutafuta mikoba, mikeka pamoja na vitu vyengine, yaani akifika kule aonekane kama ni Mjasiriamali. Mhe. Spika, Wajarisiamali sehemu nyengine wanaachwa na kutafutwa watu ambao si Wajarisiamali na kupelekwa kwenye Maonesho. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika Wajasiriamali hao watakaochukuliwa na kupelekwa, basi serikali ijipange kwa kujua hawa ni Wajasiriamali kweli au ni watu wameshaambiwa tu, kwa sababu kuna riziki fulani wapelekwe wao, kwa kweli wajarisiamali wengine wanaachwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hayo machache nashukuru sana, isipokuwa narudia tena kusema kwamba naunga mkono ripoti hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nakushukuru kwa mchango wako pamoja na kuunga mkono ripoti hiyo. Waheshimiwa Wajumbe, tumebakiwa na dakika chache tu, nadhani ni vyema tukapumzike, ili jioni tufike kwa wakati na tuendelee na shughuli yetu hii. Kwa hivyo, naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:55 mchana Baraza liliahirishwa
mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, kuna taarifa mbili kidogo nizitoe ili tupate kuendelea na shughuli zetu.

Taarifa ya kwanza ni tangazo maalum la wanamichezo wetu waheshimiwa wajumbe nimeombwa niwaarifu kwamba leo Timu ya Baraza la Wawakilishi ilikuwa kwenye mashindano leo tarehe 17/4/2012 mnamo Saa 8.00 mchana kwa mpira wa miguu kati ya Baraza la Wawakilishi na Timu ya Mahakama, mechi hiyo ni maalum kwa kombe la Mei day. Timu ya Mpira wa Miguu ya Baraza la Wawakilishi imeshinda mabao 2 na timu ya Mahakama haikupata kitu nunge *(Makofi)*

Nimeambiwa magoli hayo yamefungwa na wachezaji mahiri wafuatao, Mchezaji Mhe. Hamza Hassan Juma amefunga goli moja na Dereva wangu Ndugu Abeid Abdalla Khamis nae amepachika bao jengine la pili. Kwa taarifa hii naomba tuipongeze sana timu yetu ya Baraza la Wawakilishi kwa kuwa wachezaji mahiri na tuwaombee mungu kwamba michezo inayoendelea tuendelee kushinda, sitaki muniulize je tukishindwa mbona hutoi taarifa huwa siletewi hizo taarifa lakini pia kwa masikitiko ningekuwa nazitoa hapa.

Waheshimiwa wajumbe jambo la pili ni kuhusiana na shughuli zetu kwa mujibu wa ratiba ya leo tulitegemewa tumalize ripoti tatu na kwa sababu ya shughuli ambazo zimebakia, kuanzia kesho zote zinategemewa kuchukua muda mkubwa zaidi kufuatana na uzito wake.

Kwa hivyo nitangulie kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe niweke msisitizo kwamba tutumie muda mfupi lakini tuweke maelezo yetu sahihi na niwaombe radhi mapema wale ambao hawatapata nafasi basi wanisamehe kwa sababu ya ufinyu wa muda tuliokuwa nao, nategemea tutachukua muda wa michango mpaka saa 12 jioni na

baada ya hapo tuitumie nusu saa kwa kuwaita Mawaziri pamoja na Mwenyekiti ili kufanya majumuisho ya shughuli hii. Baada ya hapo tuendelee na kupokea ripoti ya Kamati ya Kusimamia viongozi wakuu wa kitaifa.

Basi baada ya hayo waheshimiwa wajumbe naomba sasa tuendelee na mjadala na nafasi ya kwanza jioni hii inachukuliwa na Mhe. Mohammed Haji Khalid na baadae Mhe. Rashid Seif Suleiman wote tutumie muda mfupi ili tupate wajumbe wengi zaidi kuchangia.

Mhe. Mohammed Haji Halid: Ahsante sana Mhe. Spika, jioni hii kuwa mtendaji wa mwanzo katika ripoti hii iliyo mbele yetu ya Kamati ya Fedha Bisahara na Kilimo, kabla ya yote nichukue nafasi kwanza ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia kukushukuru wewe kwa busara zako, hekima zako, umahiri wako katika kuliendesha baraza hili, kama ingelikuwa tuna viongozi zaidi ya kumi wenye busara kama zako, hekima kama zako basi tungepiga hatua za haraka haraka wala tusingelisema kuwa serikali iko mbioni.

Mhe. Spika, aidha nimpongeze na kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii kwa namna alivyowasilisha hotuba yake, mimi nianze kwa ufupi juu ya Idara ya Kilimo, Idara hii ni miongoni mwa Idara ya Kilimo idara iliyo na jukumu la kuwahudumia na kuwasimamia wakulima kwa kuwapatia pembejeo, mbegu na mahitaji mengine ya kilimo.

Mhe. Spika, wakulima katika mfumo tunaolima bado tunachelewa kufika ile adhma ya serikali ya kujitosheleza kwa chakula, kwa sababu wakulima wetu walio wengi bado tunalima katika mtindo tuliorithi kwa mababu zetu hadi hii leo. Kwa hivyo idara hii ya Kilimo iko haja ya kuwashajihisha, kuwaelimisha, kuwaelekeza wakulima katika ukulima wa kisasa ili kilio chao kilete tija na manufaa yale ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Spika, pia nigusie kidogo tu Idara ya Umwagiliaji kwa kuwa siku hizi tabia ya nchi imebadilika, misimu imebadilika, miongo imegeuka iko haja ya Idara hii kuimarisha kilimo cha umwagiliaji mali hususan mpunga ambao ndio chakula kikuu Wazanzibari wanachokipenda, kwa hivyo iko haja ya Wizara ya Fedha na uchumi kutizama kwa mtazamo maalum Idara hii ya Kilimo sehemu ya umwagiliaji na kuiwezesha ili iweze kutimiza majukumu yake katika kilimo ili tukwamuke hapa tulipo.

Mhe. Spika, sasa kidogo nigusie katika idara ya misitu pindipo Idara hii na Wizara ya Kilimo na serikali kwa jumla kama haitokuwa makini iko siku visiwa hivi vitakuwa nusu jangwa, kwa sababu misitu yetu tunaikata ovyo na kumeingia hii misumeno ya moto ambayo haina huruma na mti wowote inakoelekea ndio kwenda zake tu, kwa hivyo tumeelekewa na hatari siku moja nchi hii ikaitwa ni nusu jangwa. Mbali ya hivyo kukata misutu kama tunavyoikata pia tunaharibu na tunachafua mazingira, kwa hivyo mambo mawili haya yakifanyika kwa pamoja nusu jangwa na mazingira kuchafuka tutakuwa katika hali ngumu ambayo hatimae itakuja kushindwa kuirekebisha.

Kwa hivyo ili kunusuru hilo Idara ya Misitu ijiandae kuweka sheria na kanuni za ukataji wa misitu, kwa sababu misitu tunahitaji kwa matumizi yetu mbali mbali lakini pia tusiiangamize na kufika pahala ikawa hatuna msitu zaidi.

Mhe, Spika, sasa niguse kidogo katika Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko na hii nigusie sehemu ndogo tu ya huu usimamii wa bei za bidhaa za vyakula kama mchele sukari na mengineyo. Kama wizara hii haitokuwa makini kushughulikia bei za chakula tukichukua tu kwamba biashara huru biashara huru mtu kuagizia na kuleta nchini lakini na mipaka ya bei lazima watumiaji wetu ambao ndio sote kuwe na bei ambazo zinakidhi na wanazozimudu, tunasema kuwa kila mtu ana uwezo wa kula mchele kwa kima anachoweza kwa sababu bei zimekuwa tofauti. Lakini siku zote huyu mtu wa chini siku zote anakula huu mchele ambao keshokutwa una *expire* kwa sababu ndio uwezo wake, kuna Michele inakaa leo lakini kesho ina- *expire* sasa huu ndio anaoweza kula mtu wetu wa kawaida yeye kila siku ale huu, kwa sababu ule ambao ni mzuri kidogo yeye hana uwezo wa kumiliki na kununua. Kwa hivyo Wizara hii ishirikiane na wafanya biashara na wajue wanafanya biashara kwa ajili ya Wazanzibari ambao bado uwezo wao sio mkubwa, Wazanzibari ambao wanahitaji kula mchele mzuri na unga mzuri sio kila siku wawe wanakula ule ambao umepitwa na wakati.

Mhe. Spika, vile vile wizara hii katika mambo ya kilimo ya Wizara hii ya Biashara juu ya zao la karafuu, moja ni kununua na kusafirisha lakini pia liwajibike na kuotesha mikarafuu ili hizo karafuu zipatikane, nilisema mara moja kwamba mikarafuu ya Wizara ya Kilimo au hii iliyooteshwa mara nyingi wakulima wengi wanahisi kuwa sio bora kwa sababu inaishi kwa muda mfupi kulikoni ile ambayo wanang'oa mwituni moja kwa moja na kuiotesha. Kwa hivyo kuna haja ya kufanyika utafiti wa kina juu ya suala hili na ukweli wake.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nitamke kuwa naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, inshaalla na mimi nitajaribu kuiga nyayo za Mhe. Mohammed Haji Khalid kama inavyowezekana, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, uhai na kutupa toufiki ya kuzungumza. Pili nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache kuhusu ripoti ya kamati hii.

Kwanza bila ya wasi wasi wowote naipongeza kamati hii jinsi ilivyofanya shughuli zake na sisi tunaahidi kwamba tunaiunga mkono. Kwanza nianze na kilimo pamoja na mambo ambayo yametajwa katika kamati lakini suala la ukurasa wa 24 kifungu cha 7 kinasema kuhusiana na wakulima wapelekewa matrekta, suala la matrekta kwa kulimiwa wakulima ni suala la mtihani. Kwa sababu inafanya makisio ya malengo ni wizara na sio wananchi, sasa sijui kuna uhusiano gani baina ya yale malengo yanayofanywa na wizara na matakwa ya wananchi ili kuweza kujua hasa nguvu gani ipelekwe kwa wananchi kuhusiana na matrekta inawezekana takwimu zikagongana.

Mhe. Spika, mwaka 2009 ilibainika kuwa ekari zilizolimwa kwa mkoni ni kubwa zaidi kulikoni zilizolimwa kwa trekta katika kisiwa cha Pemba hususan, sasa hali hii bahati nzuri yakaletwa matrekta lakini waswahili wanasema nguo mpya harabu ya mbovu, kwamba yale matrekta mapya yaliyoletwa yalikuwa ndio yale yale yamekuja ku-*replace* yale makongwe sio yamekuja kuongezea, sasa idadi yake ikawa vile vile haitoshi sasa tukingojea tana miaka kumi ndio tulete matrekta itakuwa kila siku hayatoshi kwa sababu hakuna nyongeza, yanapokuja yale yale yamekwisha yana-*replace* yale ambayo idadi ndio ile ile. Sasa suala la matrekta na *replacement* yake nyongeza yake ilikuwa ifanywe kama inavyoongezwa bajeti, kila mwaka bajeti inaongezwa tunamshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha Mipango na Maendeleo kwamba anaongeza bajeti, lakini matrekta yanakuwa yale yale. Sasa hapa mapinduzi ya kilimo yako wapi hapa hilo la mwanzo.

Lakini la pili mimi nimeona labda wezangu wamenyanyua mikono kamati hii mara hii, kwa sababu katika kipindi cha baraza lililopita Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa katika kamati ya aina hii lakini ilikuwa na jina jengine tu ilikuwa ikiitwa fedha na uchumi, lakini ni hii hii ambayo tulikuwa tukenda kwenye karakana za matrekta na tukayatolea kauli wee nafikiri kwa sababu hawakuitia wamenyanyua mikono wanaona tena hakuna libadilikalo basi bora tumuachie mungu.

Kwa hivyo tukitaka kujua hasa hizi karakana za matrekta ziko wapi katika uso huu wa wizara, kwa sababu mwisho wa maneno ilikuwa zibadilishwe ziwe Idara ziingizwe katika idara lakini hatukujua kama yamekuwa yale au hayakuwa, kwa hivyo kwa kuwa hawakuitia na ni kidonda cha Wizara niliona labda wamenyanyua mikono.

Halafu Mhe. Spika, kuna jambo hapa ingawa lililetwa katika baraza kisheria na Wizara ya kilimo lakini kimantiki na Wizara ya biashara imeingia ni suala zima la ghala ya akiba ya chakula dunia nzima basi serikali zote moja katika jambo walilokuwa nalo ni ghala ya Akiiba ya chakula, kwa sababu mbili kubwa kwanza kutokezea hali ya hewa iliyokuwa haikutabiriwa kwa hivyo wakulima ambao wamejitayarisha kulima wakawa hawakunufaika na kilimo chao, kwa hivyo serikali inatoa *in put* kwa wakulima wale ili kuweza kuwasaidia katika shughuli zao za kila siku na maisha yao ya kila siku.

Sasa hapa ndio inapoingia Wizara ya Kilimo lakini shughuli nyengine au madhumuni mwengine ya ghala ya Akiba ya chakula ni uwekaji mudawa wa bei za vyakula hasa, inapotokezea duniani kuna mafuriko na mahali mwengine ndio ambamo mchele tunanunua unapanda bei na mambo mengineyo ghala ile ya akiba inatumika kupunguza makali ya upandaji wa bei. Sasa mpaka sasa hivi hakuna kauli iliyokuwa nzito iliyotolewa na kamati wameeleza kuwa maghala ya akiba ya kuhifadhia chakula yamo katika matengenezo, lakini maghala hayaingizi chakula namna gani chakula hichi kitapatikana cha akiba tunamuomba Mhe. Waziri kama analo la kueleza kabla ya bajeti basi atueleze.

Mhe. Spika, nikitoka hapo kwa sababu niligusia na wizara ya biashara naona niende kabisa, karibuni hivi nilikuwa nikisikia kwamba makampuni ya mafuta ya Tanzania bara yanayoleta mafuta yamechukua mtindo wa kuagizia mafuta kwa pamoja jambo ambalo linafanyiwa tathmini, je hapa petu makampuni haya kila mmoja anaagiza mafuta kwake au yanaagiza mafuta kwa pamoja na kuweza kupunguza yale makali ambayo yanatokana na gharama kubwa inayotokezea ikiwa makampuni yale kila mmoja ataagiza mafuta yake na hali ya kuwa mafuta yanayotumika hapa sio mengi sana. Sasa nilikuwa nauliza tu kwamba makampuni yetu yanayotuletea mafuta hapa yapo katika mtindo gani wa kuagiza mafuta, na vipi hutokezea mafuta yale sasa yakawa yameingia maji na kuharibu baadhi ya gari za watu.

Lakini Mhe. Spika, suala la mwisho ambalo nililokuwa nalo mimi liko katika Wizara ya Fedha na Uchumi, mimi pamoja na yote ambayo kamati imeyaona lakini tulipokuwa katika shughuli hizi za kamati mara ya mwisho tulitembelea *TRA* Dar es Salaam na mimi nikawauliza suala, kwamba *harmonization* ya *Tax* ilifanywa kwa sababu wafanya biashara wengi walikuwa wakikwepa ushuru. Kwa hivyo ili kuweka usawa ndio ikaja kwa sababu hapa kipindi cha nyuma viwango vya ushuru vilikuwa ni tofauti na Tanzania Bara, sasa mimi nikamuuliza kwamba kwasababu sasa hivi udhibiti wa ukwepaji ushuru umeshakuwepo. Sasa hamuoni kwamba mnaifanyia sivyo Zanzibar kwamba viwango vya ushuru ni vile vile vilioko Tanzania bara ambavyo biashara yake ni kubwa sana.

Mhe. Spika, kwa mfano mpe kreti za soda mfanya biashara Darajani na mwengine Kariakoo halafu jioni nenda kakukasanye mapato, tofauti kabisa sasa mfanya biashara wa Zanzibar ukimpa *tax* kubwa wale wakubwa watapata lakini wale wadogo wataendelea kudumaa na matokeo yake hayalipi. Sasa ikiwa ile ilikuwa ni *temporary* ya *harmonization* kwa ajili ya kuondoa wakwepaji kodi, sasa imekuwa ni mazoea kwa hivyo nahisi mimi moja katika suala ambalo hata halihitaji katiba hili kwasababu kamishna alinambia hili ni suala linalohitaji *formulation* ya *policy*. Kwa hivyo nawaomba waziri wa fedha je suala hili wameliona linafaida na Zanzibar na watu wake au wameliona vipi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu ya muda kama ulivyosema naunga mkono ripoti ya kamati na ishalla baada ya kujibiwa hayo mambo mengine tutakuja kukutana kwenye bajeti inshalla Mwenyeti Mungu akitupa uhai *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu tuliyotumwa na wananchi, lakini pia nachukua nafasi ya kukupongeza kunipatia nafasi hii na mimi kutoa mawili matatu juu ya kuchangia ripoti ya kamati ya fedha biashara na kilimo.

Lakini nitakuwa mchache wa fadhila kama sikumpongeza Mhe. Salmin Awadh Salmin mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wake wote, hususan Mhe. Salmin nampongeza kwa ule utangulizi wake wa awali ambao aliuripoti hapa alipokuwa akisoma ripiti hii kwamba alisikitishwa sana na watendaji wa taasisi ambazo kamati yake ilipitia ilikuwa bado hawajakuwepo barazani. Hili ni jambo zuri na kwakweli limetufanya wajumbe wengi tuone kweli Baraza la Wawakilishi la umoja wa kitaifa liko mahiri kwa fani zote.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mimi nakwenda moja kwa moja katika idara ya Kilimo ukurasa wa nne, idara hii kama ilivyoelezwa na kwamba ina majukumu makubwa miongoni mwa majukumu yake ni kusimamia maendeleo ya wakulima kutoa pembejeo za kilimo na upatikanaji wa mbegu na dawa. Nchi yetu ya Zanzibar asilimia kubwa ya watu wake ni wakulima na kutokana na taarifa ya Mhe. Waziri wa Kilimo alipowasilisha ripoti yake ya bajeti aliwajengea matumaini makubwa wakulima wa Zanzibar kwa kuwalimia kwa bei nafuu kwa kuwapa pembejeo pamoja na madawa kwa bei nafuu.

Kwa hivyo wananchi wengi wa Zanzibar wakulima walijenga matumaini hayo na wakaendelea kwa kusubiri matrekta pamoja na dawa kwa hali zote, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba ukulima ulichelewa baadhi ya maeneo na baadhi ya maeneo mpaka leo ikiwa ni msimu wa kupapalia baadhi ya maeneo mipungua haijalimwa. Kwa hivyo ningeiomba Idara ya Kilimo ifanye tathmini ya kutosha kabla ya msimu ujao wakulima wa Zanzibar wanalima ekari ngapi, katika msimu wa kilimo cha mpunga na wanahitaji matrekta wakati gani yapelekwe mabondeni ili kusije kukatokea usumbufu kama huu ambao umetokea mwaka huu.

Mhe. Spika, pamoja na kuchelewa kulimiwa wananchi hivi sasa tunapigiwa simu kila siku katika maeneo yale ambayo watu wengi wanalima, wanatuuliza dawa za kuulia majani (za kupalilia) na sisi tunafanya juhudi kubwa ya kuwauliza wenzetu dawa hizi zitapatikana wapi. Hili ni tatizo kwa hivyo tunaiyomba Idara ya Kilimo ijiweke makini juu ya kuwawezesha wakulima wetu katika pembejeo na madawa.

Mhe. Spika, inasikitisha kwamba mkulima ana zaidi ya hekari mbili anapewa dawa nusu lita, itasaidia nini. Kwa hivyo naiyomba Idara ya Kilimo ijipange vizuri katika msimu ujao wa kilimo ili tatizo hili lisije likatokea tena itakuwa ni kuwarejesha nyuma kabisa wakulima wetu ambao ukulima ndio uti wa mgongo wanchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiacha hapa nakwenda katika udhibiti wa nzi wa matunda. Hii ni kadhia kubwa, nzi wa matunda wanayashambulia sana matunda. Hivi sasa inaoneka kwamba kuna baadhi ya maeneo hata ukifika msimu wa matunda kama maembe basi yanashinda kuliwa kutokana na nchi wengi ambao wanayashambulia matunda

hayo. Nashukuru kwamba Idara hii imeeleza kwamba imefanya juhudi kubwa ya kununua mitego 65,000 kwa ajili ya kuwatega nzi hawa, lakini bado nzi hawa wanaendelea kuyashambulia matunda.

Kwa hivyo ningeiyomba Idara ijipange na ijikite kufanya utafiti wa kina na kutafuta ufumbuzi wa uhakika kabisa juu ya kadhia hii ambayo inayashambulia matunda yetu na yakishambuliwa matunda ina maana tutashambuliwa sisi. Kwa sababu matunda ni miongoni mwa virutubisho ambavyo vinajenga miili yetu.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo hayo niende kidogo katika suala zima la Idara ya Uhakiki Mali katika Wizara ya Fedha. Idara ya Uhakiki Mali ina jukumu kubwa mno. Inasikitisha sana kuona kwamba hivi sasa kuna mali nyingi za serikali hazijulikani thamani yake. Hili Mheshimiwa ni tatizo. Kwa mantiki hii mimi naiyomba Idara ya Uhakiki Mali chini ya Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba mali zote za Serikali zinafanyiwa thamani. Kwa sababu ni aibu kiasi fulani kwamba kuna maeneo mengi ya mali za serikali hazijulikani thamani yake. Kwa hivyo naiyomba Wizara ya Fedha iwezeshe Idara ya Uhakiki Mali ili izifanyie tathmini mali zake, serikali ijue kwamba ina mtaji kiasi gani katika mali zake zote.

Mhe. Spika, baada ya hapo kwa kuuchunga muda wako na kwamba kuna baadhi ya wajumbe wanataka kuchangia. Niende kidogo katika benki ya watu wa Zanzibar. Naipongeza Wizara ya Fedha na kupitia Shirika lake la Benki ya Watu wa Zanzibar kutandaza huduma zake hapa nchini Zanzibar pamoja na Tanzania Bara. Pia naipongeza Benki ya Watu wa Zanzibar kwa kuanzisha tawi la Benki ya Kiislamu. Kwa kweli hii niwape pongezi na niwape hongera sana. Kwa maana hiyo naiyomba hii benki ya watu wa Zanzibar tawi hili la Kiislamu lihakikishe kwamba linatekeleza majukumu yake kama lilivyo jina lake Benki ya Kiislamu. Lisije kulalamikiwa, kwa sababu kulalamikiwa kwao kutakuwa ni pengo kubwa kwa dhana na dhamira na malengo ya benki hii.

Mhe. Spika, kwa haya machache na kwa ajili yakuuokoa nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi pamoja na wananchi wa jimbo langu naiyunga mkono ripoti hii kwa asilimia zote. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Mengi niliyotaka nizungumze naona wachangiaji wa mwanzo waliochangia wamenifilisi kwa kiasi fulani, sasa nisipoteze muda wako sana. Kwanza niiyunge mkono ripoti hii mia kwa mia lakini nichangie mwahala mudogo sana kwa hiyo nitachukua muda mchache sana, Mhe. Spika.

Mimi nilikuwa nataka nizungumzie zaidi kwenye Wizara ya Biashara, viwanda na Masoko. Kuna tatizo kidogo kwenye wale wauzaji wa bidhaa kwa jumla hasa bidhaa za nafaka kama mchele, sukari na unga kwenye vipimo. Nilikuwa nina wazo kwamba hebu kuandaliwe utaratibu wale wauzaji wa jumla wawe na mizani pale za kupimia. Kwa sababu wanapouza kwa jumla kuwauzia wale wanaokwenda kuuza kwa reja reja mitaani mara nyingi bidhaa zile unazikuta zimepungua uzito. Kunakuwa ni tatizo kwa sababu hesabu aliyopigiwa ya kilo 50 lakini unaweza kukuta kilo moja unusu, mbili wakati nyengine mpaka tatu zinakuwa zimepungua. Kwa hivyo hawa wanakula hasara au wanaongeza bei ili waweze kufidia zile kilo ambazo zimepungua bei ile inakwenda kwa mwananchi wa kawaida.

Ushauri wangu ni kwamba kama itawezekana ni vyema wafanyabiashara wa jumla wakaweka mizani ili yule ambaye wanamuuzia zile kilo awe anapimiwa kwanza kupimwa kile kipolo kinahakikishwa kilo zake ndipo awe anachukua zile kilo. Hilo lilikuwa moja ambalo nilikuwa nalizungumzia katika Wazara ya Biashara.

Niingie kwenye Wizara ya Fedha kidogo kwenye ZRB pale. Kwanza mimi nitoe pongezi sana kwa ZRB kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutukushanyia fedha zetu. Kwa kweli hawa wenzetu wanajitahidi sana na wameonesha namna ya mapato yetu yanavyokuwa makusanyo. Hii ni kuonesha umahiri wa kazi wanayoifanya, mimi niwapongeze sana kwa kazii hii wanayoifanya.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka niishauri serikali, kwa nini na hii Income Tax wasipewe wao hawa. Hizi ni kodi za ndani tunazokusanya lakini zimepelekwa TRA na TRA ipo upande wa Muungano na kama tunavyojua tuna tatizo kwenye mambo hayo, tusema ukweli hakuna haja ya kufichana katika hilo. Mimi nilikuwa nashauri hii Income Tax ilikwa ianze hii, kwa sababu hawa ZRB ni ya Serikali ya Mapinduzi basi hii Income Tax ihamishiwe ZRB ili waweze kukusanya vizuri. Kwa sababu wameonekana wenzetu wa ZRB wana upeo mzuri wa kukusanya hizi kodi. Napata wasi wasi kwa wakusanyaji hawa wa TRA. Kama tunavyoona kwenye masuala haya wanatupiga vita wenzetu, tuseme ukweli. Na hili nina wasi wasi kwamba hata haya makusanyo yenyewe yanawezekana yakawa si mazuri kwamba watakuwa wanakusanya kiasi wanachoona sawa tu.

mfano mdogo uliokuwepo Mhe. Spika, hivi leo nimepokea masege ya kijana wangu alikuwa ameleta basi kubwa la abiria kalipeleka Dar-es-Salaam hapa alilipia shilingi milioni tatu na kidogo hivi. Kenda kule anaambiwa alipe tena nyengine milioni tano na laki juu yaani hata zile ambazo kalipa hapa imekuwa kama hakulipa kitu, imekuwa kama ile gari anapeleka kule Dar-es-Salaam inatoka nchi nyengine wakati hii TRA ni moja.

Hili ni tatizo ambalo tumeshalizungumza sana lakini linaonekana kupatiwa ufumbuzi wake umekuwa mgumu. Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hebu atwambie hasa hili tatizo la kulipa kodi mara mbili litakwisha lini hasa au ndio nalo tunasubiri mpaka tufike huko 2014. Kama ni hivyo basi tuache mambo yote tuisubiri hiyo 2014, lakini haya mambo mengine mimi sioni tatizo lake. *TRA* moja, wafanyakazi wale wa *TRA* wanapokea mshahara kutoka *TRA* ile ile moja, lakini hapa akitoza kodi anakuwa kama hakutoza kitu. Gari kalipia milioni 3 na zaidi, ushahidi ninao kule anaambiwa alipe milioni tano na hata zile tatu zimekuwa kama hazimo, akijumlisha na zile tatu milioni nane. Eeh! Gani gani hilo.

Mhe. Spika, hayo nilikuwa nataka kidogo Mhe. Waziri ayachukue mimi nisikupotezee mda wako. Mengi yamezungumzwa na wenzangu wamechangia vizuri zaidi sitaki nitoe ladha ya yale ambayo yamechangiwa. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi nitahakikisha nitaokoa muda wako, ambao kwa sababu mambo yametutinga.

Kwanza niipongeze sana Kamati hii Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa ambao wapo kwenye kama hii, kwa kweli wamefanya kazi nzuri na ya kina na wamefafanua kila kitu, tunalolingoja ni utekelezaji.

Mhe. Spika, na mimi niseme kwamba wenzangu kidogo wamenifilisi, Mhe. Ismail Jussa amenifilisi, Mhe. Hamza amenifilisi. Lakini si vibaya nikatilia nguvu baadhi ya mambo. Nitakwenda ukurusa wa 23 ambayo Kamati imetoa maoni na maagizo ambayo imetoa maoni na maagizo ambayo.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kwamba Kisiwa chetu cha Zanzibar sisi hatuna kitu cha kutusaidia hasa kuiendesha serikali yetu. Tunategemea zao lakarafuu pamoja na utalii. Ni vyema hawa wenzetu tunapozungumza baadhi ya mambo wenzetu wa Tanzania Bara wakatufahamu hakuna lengo jengine, lengo ni kuhakikisha na sisi wananchi wa Zanzibar na wao wanapata zile baadhi ya raha ambazo ni haki yao. Kwa hivyo na mimi niunge mkono tu kwamba hawa wafanyakazi ambao wanatoka Tanzania Bara wanakuja hapa yale malipo yao basi yachukuliwe na *ZRB* ili tuwe na kituo kimoja ambacho kitaweza kusaidia hasa na kitakuwa ni kituo ambacho hata wafanyabiashara hawa kuliko ule utitiri tulionao sasahivi, wataepuka na mambo mengi ili wafanyabiashara wetu hawa waweze na wao kujua ile raha ya biashara na kuwa na sisi pamoja.

Lakini pia nije katika suala la utaratibu wa *electronic receipt* hili tumelizungumza sana katika Baraza lako hili tukufu. Naiyomba sana serikali kwa sababu tunakosa mapato mengi sana kutokuwa na hii *electronic receipt* hii itasaidia na kwa kweli kutakuwa hakuna wizi. Yeyete anayekwenda pale katika duka ni kuwafahamisha tu wafanyabiashara. Lakini kama tukisema tunangoja matokeo yake kwa kweli tunakosa pesa nyingi.

Mhe. Spika, lakini pia nisiwe mwizi wa fadhila lazima niipongeze Benki ya Watu wa Zanzibar kwa kweli Benki yetu hii inajitihada kubwa na inajitahidi kuhakikisha kwamba inatoa huduma kwa wananchi wake ipasavyo. Niichukue nafasi hii kuipongeza kwa sababu hata sasa hivi imeshajishajihisha ingawa neno hilo halitakiwi kujishajihisha lakini kwa kweli imefungua branchi Dar-es-Salaam ambapo tulikuwa na matatizo sasa hivi mtu akenda Dar-es-Salaam hana matatizo.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la Uhakiki Mali, naiyomba sana serikali ina machakara mengi mno na mengine kwa kweli si mabovu ni mazima lakini gari ikiharibika klachi inawekwa hiyo ndiyo klachi itakaa mtu keshaipiga jicho. Kuna machine haya ya matrekta likiharibika kitu kidogo ambacho tunajisahau kwamba kitu kile tumekinunua kwa mamilioni lakini kwa elfu kumi tu tunashindwa kukitengeneza kitu kile.

Mhe. Spika, naomba sana Idara hii ya Uhakiki Mali na namuomba Mhe. Waziri ahakikishe vinahakikiwa kweli vifaa vyote vya serikali ambavyo ni vibovu na vizima ili kama vyengine kama havifai basi wauziwe wananchi watakwenda kutengeneza mbele ya safari. Lakini kwa kweli serikali ina vitu vingi sana vimeachwa saa nyengine ukipita katika Mawizara unasikitika. Namuomba sana ndugu yangu Mhe. Waziri suala hili alitupie jicho la huruma ili tuhakikishe kila Wizara inafanyiwa uchunguzi. Sisi tunakata yasiletwe *used* lakini sisi wenyewe tuna ma- *used* tumeyaweka hapa mabovu mengine mpaka yanatia maradhi.

Mimi namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kila Wizara inahakikiwa mali ambayo hazifai na mimi nilisema nisichukue wakati wako mwingi Mhe. Spika. Naunga mkono ripoti hii ambayo ni ripoti mwanana na inajieleza vizuri. Kwa hivyo naunga mkono ripoti 100 kwa 100. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi hii ya kuchangia machache katika ripoti hii ya Kamati ya Fedha. Kwanza kabisa na mimi nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hii ambayo ameweza kuwasilisha ripoti yake kwa umakini na vizuri kabisa.

Mhe. Spika, na mimi nianze mchango wangu katika Idara hii ya Kilimo. Kwanza niipongeza sana serikali kwa kuhudi kubwa ya kuwapatia wakulima wetu yale yote waliyoahidiwa wakati wizara ilivyopitisha Mswada wake ambao mswada huo ulikuwa na lengo la kuwakomboa wakulima.

Mhe. Spika, Wizara kwa upande wake imejitahidi lakini bado kuna kasoro ndogo ndogo zinazojitokeza kwa watendaji wetu wa chini zaidi. Kwa hiyo, niseme wakulima walijenga matumaini makubwa lakini baadaye hapo kati yamevurugika kwa taratibu za ugawaji wa vifaa ambavyo kwa kweli katika Idara ile ya Kilimo imeweza kutolewa kama ilivyopangwa katika Mswada huu, lakini ugawajii kule chini haukwenda vizuri. Vifaa vilitolewa, matrekta yalikuwepo lakini kwa bahati mbaya kama walivyosema wenzangu hayakuweza kufikia lengo la kulima kama ilivyopangwa lakini mpaka mda huu kuna mashamba hayajalimwa. Lakini mbegu, mbolea, dawa za kuulia magugu zililetwa lakini utaratibu wa kugawa ulikuwa mbaya hivyo wakulima wengi wamekosa na hata hivi jana imetolewa mbolewa lakini kwa idadi iliyotolewa watu wamekataa wameona itasababisha ugomvi mkubwa.

Mhe. Spika, niiyombe Serikali iweze kujipanga vizuri wakati ilikuwa na lengo zuri la kuweza kuwasaidia akulima ili wakulima hawa waweze kupata mafanikio makubwa kwa kutegemea kilimo kama ndio uti wa mgongo wao.

Mhe. Spika, niende katika Shirika la Taifa la Biashara, pia nichukue fursa kulipongeza sana Shirika letu hili kwa ununuzi mzuri wa karafuu na kuvuka lengo ambalo alilokuwa amejipangia lakini bado nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa shirika limeweza kupata fedha nzuri kwa msimu huu wa karafuu basi pia iweze kununua boti nzuri za kisasa ili kuweza kupambana na changamoto ya watu wanaovusha magendo ya karafuu kuweza kuzinusuru karafuu zetu kwa msimu ujao. Ili serikali iweze kupata mapato zaidi na kuweza kuondoa kero mbali mbali ambazo tunategemea kuziondosha kwa zao hili.

Mhe. Spika, pia niendelee niipongeze serikali kwa juhudi kubwa ambayo imechukua kwa kupita katika maduka mbali mbali na kuangalia bidhaa lakini bado mchele mbovu upo, bado vifaa vibovu vipo vilivyokwisha muda wake vinauzwa. Kwa hivyo serikali bado iendelee kuchukua juhudi za kuona inashughulikia na wananchi wa Zanzibar wanaweza kupata chakula kilichokizuri kwa kujenga afya zao.

Mhe. Spika, pia niende katika Wizara ya Fedha kwanza nichukue fursa hii kama walivyosema wenzangu walivyoipongeza Wizara hii na mimi naipongeza kuweza kupata huduma nzuri kabisa katika Benki yetu ya Zanzibar. Pia kuweza kuongeza huduma kule Dar-es-Salaam kwa kufungua benki nyengine. Pamoja na hayo na changamoto ipo. Kule Dar-es-Salaam tumepeleka wafanyakazi ambao wameondoka huku majumba hao yapo huku na kule wamelazimika kupanga hivyo basi wanakabiliwa na changamoto hasa ukiangalia hali ya uchumi ilivyo kwa hivyo wanapambana na ukali wa maisha kutokana na zile kodi ambazo wanakodi nyumba kule.

Mhe. Spika, ninde katika Idara ya Misitu kwa kuwa Idara hii inajukumu kubwa la kulinda na kuhifadhi basi na wao niwatake waweze kupambana sana na waharibifu wa mazingira ambao wanahatarisha na kutaka kuifanya nchi yetu kuwa jangwa kwa hivyo waweze kupambana nao ili nchi yetu ibaki katika usalama na kuendelea katika mazingira mazuri. Pia na wao niwaombe waweze kutuhamasisha wakulima kwa kutupatia miche ya miti bora tukiipanda ambayo tunaweza tukapata faida kubwa na ikaongeza pato kwetu na taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono ripoti hii kwa asilimia 100 kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hoja.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii fupi ya kuchangia ripoti hii tukufu ya Kamati. Kwa vile muda ni mfupi Mheshimiwa naomba nianze moja kwa moja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tumeona ripoti ya Idara ya Misitu lakini kidogo naomba kuongeza yafuatayo. Misitu ni yenye umuhimu mkubwa sana kwetu sisi. Misitu ina matunda ambayo ni chakula cha wanyama na pia binaadamu.

Misitu inaleta mvua katika nchi na misitu inaleta rutuba katika ardhi ni muhumu sana. Kwa bahati mbaya na kwa sababu ya umasikini misitu yetu inakatwa ovyo tena ovyo kabisa, kiasi ambacho hivi sasa ni cha kutisha na athari yake itakuja kujitokeza baadaye. Kwa hivyo naiyomba wizara hili ilitilie maanani sana kwa kuhakikisha kuwa kuna utamaduni wa kuatika miche mipya na kueneza ili kuchukua nafasi ya sehemu kubwa ya msitu ambao tayari hivi sasa umeshaangamizwa.

Mhe. Spika, pili ni kilimo nashukuru katika ripoti kuna hata mapendekezo ya kutengeneza matrekta ya kulimia yaliyokuwa yameharibika. Kama unavyojua katika kilichopita hapa tuliahidiwa kupatikana matrekta kwa wingi kulimiwa kwa bei rahisi na kupata mbolea iliyokuwa bei yake ni rahisi kabisa ili mkulima waweze kujitegemea kwa chakula na kuuza ikiwezekana.

Mhe. Spika, wizara imejitahidi lakini kuna sehemu kwa bahati mbaya matrekta haya yakufika na kwa sababu walikuwa wanasubiri na haya mambo yanakwenda kwa wakati kwa msimu huu wameharibikiwa sana.

Pili wale waliowahi kulima ambao nyengine kwa sababu wamepata msaada wa matrekta walilima sehemu kubwa sana utoaji wa mbolea kwa taarifa tulizozitaka ni mdogo kwa hivyo watu hawakupata mbolea kama walipohitaji kutokana na kilimo walicholima. Kwa hivyo naiomba Wizara ikiwa kuna sababu yoyote ya kutotoa mbolea kutokana na mtu alivyolima. Kwa hivyo tuelezwe vyenginevyo hili suala lifanyiwa zoezi upya kwa sababu watu wanalalamika sana.

Mhe. Spika, jengine ni kuwa tunao Waziri wetu wa Biashara tunashukuru sana kuwa imepandisha bei ya karafuu, imenunua karafuu zaidi katika ripoti imehimizwa kuatika mikarafuu kwa ajili ya wananchi. Lakini Mheshimiwa zaidi ya hapo hii wizara pia ni ya viwanda na masoko. Ushauri wangu Mheshimiwa kwa Wizara kama ilivyoelezwa katika ripoti ni kuwa wakati umefika kutafuta vile viwanda ambavyo vitakuwa endelevu ambavyo mali ghafi itapatikana hapa hapa vianzishwe kwa maslahi yetu na kwa maslahi ya nchi kwa kupeleka biashara yetu nje.

Kwa mfano kiwanda cha kusindikia minofu ya samaki, hakuna sababu kuwa mpaka leo hatuna hata kiwanda kimoja wakati tumezungukwa na bahari, wenzetu wanavua bahari kubwa huko na sisi hatuna faida yoyote tunayoipata. Halafu jengine naomba kwa vile tunayo Kamati ya Wataalamu wa Kilimo hawa watu wafanye kazi ya ziada. Tunajua mpaka hivi sasa tuna matatizo ya kupata maradhi katika matunda. Mfano embe zetu zimeharibika kwa wingi sana lakini utaalamu wetu wa mwisho tulionao hivi sasa ni wa kutumia mitego na mitego haiwezi ikaondoa nzi wote wanaosababisha maradhi.

Ushauri wangu kwa vile ishakuwa ni jambo la kawaida kupata maradhi ya matunda, tulikuwa na maradhi ya migomba ikiitwa *black sigatoka,* ilikuwa ni kukata majani na kupiga moto, lakini utaalamu hasa ni maradhi gani, yafanywe nini ili yaondoke hatukufikia huko. Tulikuwa na maradhi ya mihogo tukiita *mill burg* hatukufikia ifanywe nini ili maradhi yaondoke, isipokuwa kutafuta sisimizi kutoka nchi za nje, wakawala wale wadudu lakini tiba ya kuwatibu hasa haikupatikana. Kwa hivyo namuomba kwa sababu tunaingia katika utaalamu na dunia inabadilika na sisi tunaingia katika soko la Afrika Mashariki ni lazima tufike mahala tuaminike katika matunda yetu. Vyenginevyo itakuwa tunazalisha na tunatumia sisi wenyewe.

Vile vile kwa sababu ya uchumi wetu mdogo tulionao tuna mazoea ya kuagiza kila kitu kutoka nje pamoja na matunda ambayo shughuli zake ni tofauti na zamani. Zamani ilikuwa yakiingia matunda hapa yalikuwa yakiangaliwa na daktari kwa hali ya juu kabisa ndiyo tena yakatumiwa kwa binaadamu, siku hizi kila mtu anapita kwa mlango anaoutaka na sijui kama ndiyo sababu ni hiyo lakini utaona kuwa Wazanzibari hata juzi walipokuja madaktari ilikuwa waheshimiwa hali ya maradhi ndiyo hivyo, sasa siji kwa wananchi ni vipi. Tujitayarishe tuone kuwa yale matunda na chakula kinachoingia ndani ya nchi kinaangaliwa katika hali ya juu kabla ya kutumiwa.

Mhe. Spika, la mwisho ninaloomba kuchangia ni kua tunacho kiwanda cha makonyo pale Chake-Chake kimetajwa humu, lakini kiwanda kile mpaka sasa hivi kinatoa mafuta ya karafuu, kinatoa mafuta ya makonyo, kinatoa mafuta ya mkaratusi na kidogo mafuta ya mchai chai. Mhe. Spika, kiwanda uwezo wake ni mkubwa kimefanyiwa matengenezo lakini malighafi yakutosha hamna. Kwa maana hiyo ni hasara kwa upande mwengine, ushauri ni kua Wizara ya Kilimo ione kwamba kile kiwanda kinafanyakazi kwa kuzalisha kutokana na uwezo wake ili tuweze kuleta faida kwa shirika lenyewe na kwa taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, nashukuru naomba kuunga mkono ripoti hii.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nashukuru sana kunipa fursa na mimi nichangie ripoti hii ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Mhe. Spika, kwanza nataka nianze kwenye hii Wizara ya Fedha kidogo na mimi nizungumzie kuhusu suala la *TRA*.

Mhe. Spika, kwa kweli suala la *TRA* wafanyabiashara wetu kulipa mara mbili ni tatizo sugu, na tatizo hili Mhe. Spika, linasababishwa na utendaji wa viongozi kwa sababu wao watendaji wa *TRA* wanasema kama sisi hatuwezi tukabadilisha kitu chochote kwa kusema nyinyi Barazani au kwenda Bungeni watu wakipiga kelele tu ikisha wakarudi. Mhe. Spika, wanasema wakati hatujapewa sheria yoyote na maandishi yoyote basi tunafuata sheria ya nyuma iliyopo wala hatusikilizi chochote. Kwa hivyo, nawaomba viongozi wetu waone kama kuna haja ya hawa *TRA* wasiwape kwa makelele ya wana siasa tu, wapewe kwa maandishi utendaji wao.

Mhe. Spika, na wao wanasema hasa hawawezi wakabadilisha hata kidogo na hili limekua kama ni tatizo sugu la kuwakomoa Wazanzibari. Kwa sababu Wazanzibari wakishalipwa ushuru huku wakienda kule Bara inakua kama wanakomolewa. Mhe. Spika, haiwezekani mtu ameshalipa ushuru kamili halafu akifika kule anaambiwa alipe tena milioni 12, hilo ni tatizo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri suala hili alione kama ni tatizo na walitafutie ufumbuzi wa kudumu, si kwamba humu Barazani tukija tunaambiwa tatizo hili limeshamalizika halafu tukifika kule ngoma inaendelea kama kawaida. Kwa hivyo, imekaa kama danadana na chombo kama hiki haiwezekani kuja wakaambiwa kwamba tatizo limeshamalizika halafu baadae wakenda kupata usumbufu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ninalotaka kulizungumza ni Wizara ya Kilimo. Mhe. Spika, kwa kweli tulitangaza mapinduzi ya kilimo na watu wakaitikia lakini kwa kweli wananchi wetu wanapiga kelele kuhusu nyenzo za kilimo hawakupata watu hata kidogo. Mhe. Spika, wananchi wetu hawakupata dawa ya kuulia magugu, wala hawana mbolea. Kwa hivyo, serikali kama ilitangaza mapinduzi ya kilimo, basi kuna haja ya kujirekebisha kutafuta nyenzo ili wananchi wetu wasilalamike. Kwa kweli wananchi wetu wanalalamika sana na huko nyuma kulikua na kamati labda za vijiji sijui kama zimepanguliwa au vipi. Kwa hivyo, sasa hivi inakua kama ni mchezo wa kukomoana, kamati zinasema tunataka kuitazama serikali inasimamia wenyewe je, itatekeleza kweli suala hili? Kwa hivyo, naiomba serikali ione kama kuna haja ya kuwashughulikia hawa watu ili wapate hizi nyenzo za kilimo ili kilimo kiwe endelevu.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba sisi kama tumetangaza mapinduzi ya kilimo, basi tuwe na mapinduzi ya kilimo kwa sehemu zote isiwe kilimo cha mpunga tu, kwani kuna baadhi ya sehemu za maweni kama vile kwetu Micheweni, sehemu za Mwambe na sehemu nyengine za mawe.. Mhe. Spika, kama tukitangaza mapinduzi ya kilimo basi iwe ni mapinduzi ya kilimo ya sehemu zote, wananchi wetu wanahitaji kilimo na wao. Kwa hivyo, serikali kupitia Wizara ya Kilimo ijipange vizuri ili iwaelimisha wananchi wetu kwa ajili ya kilimo, na kama ni sehemu za maweni basi waelekezwe kupanda kilimo ambacho kinastahamili ukame wa maweni.

Mhe. Spika, isiwe kwa upande wa mpunga tu kwani mpunga peke yake haututoshi kuna mboga mboga, kuna viungo na sehemu za maweni ni sehemu moja ambazo zinakua vizuri sana mboga mboga. Lakini sasa wananchi wetu wanataka kupewa elimu ya kweli kuhusu mapinduzi ya kilimo. Mhe. Spika, hawa mabwana shamba na mabibi shamba wateremke chini kila siku tunasema ili kuwaelimisha watu, kama ni mapinduzi ya kilimo iwe baadhi ya mabonde na kule sehemu za maweni nako kuwe ni sehemu ya mapinduzi ya kilimo.

Mhe. Spika, sasa hivi nije kwenye maliasili na misitu. Mhe. Spika, kwa kweli Wazanzibari nawaomba tubadilike tuwe kama wenzetu sio vibaya binadamu kufuata yale mazuri, ukiona mwenzako anafanya jambo zuri kulifuata sio vibaya. Mhe. Spika, Mtume alisema anataka watu waliokuwa ni wezi, lakini sio wezi wa kuiba vitu vya watu. Wezi wa kuiba tabia zilizokuwa ni nzuri sio kwamba ukaibe vitu vya watu kwa sababu Mtume amesema anawapenda wezi na wewe ujifanye umo kwenye kupendwa na Mtume. Mhe. Spika, ni vizuri kuiba yale mazuri na mtu anasema lile analoliona mimi nitazungumza kwa sababu mlinipeleka China basi nitazungumza kwa niliyoyakuta China, keshokutwa mukinipeleka Marekani nitakuja kuzungumza la Marekani.

Mhe. Spika, kule China tulipokwenda kwenye maliasili hiyo sehemu tuliyopelekwa ni sehemu ya utalii, lakini tulikwenda kumkuta mnyama anaitwa Panda, huyu Panda ukimtizama sura yake paka si paka, ukenda kwenye mbwa sio mbwa, ukenda kwenye kondoo sio kondoo ilimradi ni mnyama yupo tu. Na huyu mnyama anapatikana sehemu moja kule China, lakini wenyewe wanavyofanya kwa sababu ya kuenzi maliasili zao, basi huyu panda anawatilia fedha nyingi sana za ajabu kwa sababu watalii wanaokwenda kumuona panda basi itabidi upange foleni ya kwenda kumuona mnyama huyo. Lakini ukitizama wale panda wachanga wanavyoenziwa hata binadamu haenziwi kuliko wanyama hao. Mhe. Spika, wanyama hao wanatibiwa kwa dawa, wanajengewa nyumba wanaenziwa huwezi kuamini hata kidogo. Kwa hivyo, wenzetu wanathamini mambo kama hayo kwa sababu fedha za serikali zinaingia kila upande, kwa hiyo huyu anawaingizia fedha nyingi sana.

Mhe. Spika, kwa hivyo, na sisi hapa Zanzibar tuna wanyama wengine kama huyu panda au na zaidi ya panda, lakini hatuwaenzi. Kwa hivyo, mimi nashauri hawa watu wa maliasili sasa hivi waone kama umefika wakati maliasili zetu kuingiza fedha kwa serikali. Kwa mfano, sisi tuna mnyama hapatikani sehemu yoyote ile hapa Zanzibar, tuna kimapunju mnyama huyu yupo hapa Zanzibar tu, lakini ukenda hao kimapunju hakuna sehemu hata moja anayoenziwa. Mhe. Spika, anaweza akaja mtalii akataka kumuona basi akamkosa kwa sababu hakuna sehemu waliyowekewa mazingira mazuri yakua akija mgeni apatikane. Lakini wenzetu wa China panda wamemuweka sehemu ambayo wakija watalii hawana tabu wanakwenda kumuona pale.

Mhe. Spika, pia kuna wanyama wengine kama popo tulionao hapa Zanzibar hakuna sehemu nyengine yoyote walionao popo hawa tunao sisi na tuna misitu mikubwa mizuri na wamo wengi, lakini hakuna hata sehemu moja wanaoenziwa wale popo wakajuulikana kama ni sehemu wakija watalii watakua wanakuja kuwaona na sisi tunapata fedha. Kwa hivyo, pia China kuna wanyama ukiwaona wamekaa kama komba lakini hivyo hivyo wamefanywa kama panda wanaenziwa watu wanakwenda kuwaona.

Mhe. Spika, katika misitu yetu kuna wanyama wa kila aina na watalii wanaweza wakaja wakatuingizia fedha nyingi, lakini sisi tunashindwa kupanga mambo ambayo yatatuingizia fedha katika nchi yetu. Kwa hivyo, nawaomba Wazanzibari tubadilike zile rasilimali zetu tulizonazo basi zitufae kwa faida ya Wazanzibari. Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono ripoti hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka niungane na wenzangu nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake. Kwa kweli ripoti yao ni nzuri na nataka niwahakikishie mbele yako Mhe. Spika, na Baraza lako tukufu kwamba mapendekezo yao yote ambayo waliyoyatoa katika ile ripoti ya kamati mimi na watendaji wangu tutayafanyia kazi kwa faida ya nchi yetu na kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, wajumbe wako wameeleza mambo mengi, wametaka ufafanuzi katika maeneo mengi. Kwa heshima na taadhima nataka niwambie kwamba yote ambayo wameyaelekezea kuhusiana na ofisi yangu basi nimeyachukua na nitayafanyia kazi. Mhe. Spika, nitakachokifanya hapa nikumsaidia mtoa hoja kutoa ufafanuzi kwa yale maeneo muhimu sana, nasema yote ni muhimu na ndio maana tutayafanyia kazi. Lakini yale yaliyojitokeza ambayo mimi nimeyaona haya ni muhimu sana kuyatolea ufafanuzi naomba kidogo kwa heshima na taadhima nimsaidie mtoa hoja kutoa ufafanuzi ili wajumbe watakapoondoka leo jioni waweze kupata kidogo nini kinachoendelea.

Mhe. Spika, la kwanza lilijitokeza na wajumbe wengi sana wamelichangia ni suala la uimarishaji wa mapato ya serikali. Nataka niseme kwamba hili kwa kweli tunalifanyia kazi kwa nguvu zetu zote, tunalifanyia kazi katika nyanja mbali mbali.

Mhe. Spika, lilijitokeza suala la mapato ya visa, tayari tumeunda kamati, tayari kamati ile kwa mashirikiano kabisa mimi na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano tumetembelea kituo cha *Air Port* tumeona hali ya ukusanyaji wa mapato ya visa, tukatembelea na wataalamu wetu pamoja na watu wetu wa benki tumemleta mshauri mwelekezi. Mhe. Spika, mshauri mwelekezi ametoa maelekezo ya awali kwamba ni vyema zile *visa* pale *air port* zikaunganishwa na mtandao wa *PBZ* ili kila mmoja akaweza kuona mlipaji wa visa na amelipa kwa kiwango gani. Tayari tunasubiri ripoti kamili tuipate kutoka kwa mshauri mwelekezi ili tuweze kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Ndani kwamba hili suala sasa tutalitekeleza kwa mujibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyoona inafaa.

Mhe. Spika, lilikuja suala la misamaha katika suala zima la kuimarisha mapato, nikawaeleza baadhi ya wajumbe kwamba bado misamaha yetu ni mikubwa. Nakubaliana nao wajumbe wote waliosema misamaha bado ni mikubwa, lakini hii inatokana na ile sheria yetu ya *ZIPA*, sasa hivi sheria ya *ZIPA* tunaifanyia marekebisho ili Mungu akitujaalia katika mkutano wetu wa mwezi wa 10 tulete marekebisho. Lakini kwa ile misamaha ambayo waziri ana mamlaka nayo, nimejitahidi sana safari hii kuipunguza. Mhe. Spika, nimejaribu kuangalia wawekezaji walichoomba na michoro yao na kutokana na misingi hiyo ndio misamaha yangu inamokwenda, sio kwamba kila mwekezaji analeta malighafi anapewa misamaha tu. Nimewaambia lazima nione na ninafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na kamati na nawashukuru sana wana kamati wananisaidia sana.

Mhe. Spika, lilikuja suala jengine kutoka kwa wafanyakazi wa SMT, tulikubaliana na sisi tukaiweka kwenye bajeti kwamba kuna 18 bilioni wenzetu wa Muungano watupatie. Lakini nataka niseme kwamba wenzetu wale katika mkutano ule unaoendeshwa chini ya Makamo wa Rais ilitokeza hoja kwamba wabadilishe sheria. Na katika ile ripoti iliyofanywa kiko kipengele kwamba walitakiwa wabadilishe sheria ili Zanzibar waweze ku-*access* hizi *payee* za wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar.

Mhe. Spika, mpaka tunakutana na wenzetu kumbe ile sheria walikua hawajaibadilisha, tumewaomba sana wabadilishe ile sheria ikiwezekana haraka iwezekanavyo ili hata Waziri Mkuu aliwaambia katika mkutano wetu tuliofanya chini ya Makamo wa Rais kwamba haiwezekani wenzetu waweke huko halafu msiwapelekee. Kwa hivyo, bado kuna utata wa kisheria kubadilisha sheria, lakini tunawaomba wenzetu wabadilishe sheria ili tuweze kuzi-*access* zile fedha za *payee* kwa wafanyakazi ambao wanaofanya kazi Muungano, lakini wapo Zanzibar. Hilo tutalisimamia nataka Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wametupa kazi hiyo basi watuamini tutaifanyia kazi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilojitokeza ni ugawaji wa mapato uendane na vipaumbele. Mhe. Spika, nataka niseme kwamba vipaumbele vinapangwa na sekta wenyewe, sisi hazina tunakuja na vipaumbele wakati wa bajeti, tukivileta hapa hivi ndio vipaumbele vya kitaifa Baraza lako tukufu linaidhinisha vipaumbele vya kitaifa. Mhe. Spika, tunapokuja kwenye sekta yenyewe sasa inasema kipi kianze mwanzo na kipi kitakuja mwisho. Nataka nikuhakikishie tu Mhe. Spika, kwamba hakuna wizara hata moja ambayo imekosa OC iko chini ya asilimia 70. Leo tunazungumzia miezi 9 hakuna wizara hata moja ambayo OC iko chini ya asilimia 70.

Mhe. Spika, kamati yangu walipotembelea Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo pamoja na wizara yangu nataka ninukuu tu wizara hizi mbili. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo OC yao jumla ilikua ni 1.8 bilioni mpaka miezi 9 inamalizika tumeshawapa 1.597 bilioni sawa na asilimia 86. Wizara ya Biashara OC yao ilikua ni 0.9 bilioni mpaka miezi 9 inamalizika tumeshawapa 0.778 bilioni sawa na asilimia 87.

Kwa hivyo, unapopata asilimia hizi za fedha za OC kama mwenyewe huzipangii vizuri mimi naomba sana na nitawaomba Waheshimiwa Mawaziri mbele ya Baraza lako tukufu kwa sababu mawaziri ndio tunaosulubiwa humu ndani, ningelikuombeni sana tukae karibu na Makatibu wakuu ili watwambie OC kila mwezi inapatikana kiasi gani na tunaigawa vipi. Ni wajibu wetu Waheshimiwa Mawaziri OC kuelewa tunaigawa vipi.

Mhe. Spika, jengine ambalo lilojitokeza ni suala la ukamilishaji wa daftari la mali za serikali. Nataka niliarifu Baraza lako tukufu kwamba daftari tumeshalikamilisha, mali za serikali tunajua sasa hivi serikali ina gari ngapi, serikali ina mashamba ya ukubwa gani na yapo wapi, serikali ina meza ngapi hilo tayari, serikali ina viti vingapi hilo nalo tayari. Tatizo ambalo hatujakamilisha ni tathmini ya ile mali, tumeshatia mtaalamu sasa hivi anafanya kazi kwa wizara tano. Wizara zenyewe ni Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Mawasiliano.

Mhe. Spika, zile mali ambazo wenzetu wa wizara hizi wameziorodhesha tunaanza sasa hivi kuzifanyia *quantification*, hii mali hii thamani yake ni kiasi gani. Tukimaliza wizara hizi tano tutakwenda wizara nyengine na hatimae mali yote ya serikali tutaijua kwa idadi na tutaijua kwa thamani na tutaijua ilipo. Mhe. Spika, hiyo kazi tunaifanya na *we are hopping by next year* tutakuwa tumeshaikamilisha kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, suala jengine liliibuka hapa ZSSF wajikite katika kuekeza katika miradi mikubwa mikubwa, mimi nakubaliana sana na Waheshimiwa Wawakilishi. Mhe. Spika, chombo hiki hakitakua kwa kuekeza katika miradi ya njugu, lazima kuekeza katika miradi mizito. Mhe. Spika, tatizo tunalo moja, kwanza taratibu za ZSSF katika kuekeza hawatakiwi kuekeza kwa kutumia zaidi ya asilimia 20 ya fedha zao. Lakini la pili tunasema tukipata dhamana ya serikali na sioni sababu za msingi kwa nini tusiwape dhamana ZSSF. Mhe. Spika, ZSSF chombo nakisimamia mimi na dhamana naitoa mimi, sioni sababu kwa nini tusiwape miradi mikubwa. Mhe. Spika, leo nimeonana nao nimewauliza Uwanja wa Ndege wa Pemba kuujenga mnaweza, wakipata dhamana wanaweza. Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutafanya kazi kwa karibu zaidi ili chombo hiki kiweze kuekeza sasa hivi katika miradi mikubwa ya kitaifa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo liloibuliwa ni suala la mafuta ya magari kuingia maji. Hili suala limeleta utata mkubwa sana, na nathubutu kusema kwamba meli ambayo imeleta mafuta ndio ambayo iliyokua na matatizo haya. Mhe. Spika, mafuta yale Tanzania Bara na hata nchi za jirani imeripotiwa kwamba yalikuwa na maji, hata hapa Zanzibar walipoya-*test* yale mafuta yalikuwa na maji. Mhe. Spika, tulichokifanya wiki iliyopita nimekaa na ZRB tukalitafakari hili suala, suala la mafuta wizara tatu tunahusika hivyo tunataka turejeshe majukumu ya kila wizara kusimamia haya mafuta. Wizara ya Biashara kwa maana yakua ni biashara ya kawaida kwa hivyo wanahusika kwa upande wa leseni na kwa upande wa biashara ya kawaida. Wizara ya Nishati inahusika kwa maana yakupima mafuta na Wizara ya Fedha inahusika kwa maana ya kodi zinazotokana na mafuta.

Mhe. Spika, imeonekana kwamba wizara zetu hizi kila wizara imeacha majukumu yake isipokua Wizara ya Fedha kwa sababu tu ya kutafuta kodi. Mhe. Spika, tunataka turudishe majukumu ya kila wizara ili hatimae hii hali iondoke. Mhe. Spika, tulichokifanya tumewataka wenzetu wanaoleta mafuta kabla ya mafuta yao

hatujayatoa Mtoni kuyapeleka katika vituo watie saini *document* pale ZRB kuhakikisha kwamba wanachukua dhamana mafuta yale hayataharibu magari ya watu. Mhe. Spika, kwa sababu wanaoleta mafuta ndio wenye vituo vya mafuta kila mmoja anapeleka katika sheli zake tutakua tunajua kwamba mafuta haya nimeyanunua sheli gani ili kutupa nafasi na sisi tuweze kuyafuatilia.

Mhe. Spika, limekuja wazo hapa kwanza kua na taasisi mbili zinasimamia kodi, mimi nakubaliana nao Waheshimiwa Wawakilishi kuwa na taasisi mbili ndani ya nchi moja zinazosimamia kodi ni tatizo. Mhe. Spika, nimetembea sana ndani ya dunia sijawahi kuiona nchi ambayo yenye kusimamia kodi, nataka niwaambie waheshimiwa tunalifanyia kazi. Tunalifanyia kazi tunataka kuangalia athari zake na faida zake, athari hizo ni kwa nani na faida hizo ni kwa nani. Mhe. Spika, tukifikia pahala basi tutakuja kutoa taarifa nini cha kufanya.

Mhe. Spika, lilikuja suala jengine lilikua suala la uidhinishwaji wa miradi inayofanywa na ZIPA ushirikishe Idara ya Mazingira katika utekelezaji wake. Mhe. Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba miradi yetu mingi ina athari za kimazingira na ndio maana tunatoa ile *envoromental impact assessment* na hata katika utekelezaji lazima ZIPA ishirikishe Idara ya Mazingira. Nimelipokea wazo hilo nitalifikisha kwa watendaji wangu na mimi mwenyewe nitahakikisha kwamba watendaji wangu wanalisimamia hili. Hii nchi ni yetu sote lazima tusimamie mazingira yetu tukifuja mazingira sisi ndio ambao tutakaoathirika na tutashindwa kukaa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, suala jengine limekuja suala la utumiaji wa *electronic machine* kwa kutoa risiti. Hili nimelipokea tutaangalia hali ilivyo kule Tanzania Bara walianza kutumia hizi *electronic machine* baadae ikaonekana kwamba wafanyabiashara baadhi yao wanazikimbia hizi *machine*. Kwa hivyo, sasa badala yakufanya kazi iliyokusudiwa sasa haifanyi kazi iliyokusudiwa kwa sababu wanazichokora halafu inaleta matokeo tofauti. Kwa hivyo, hili tutaliangalia na kuweza kuangalia ni machine za aina gani tuweze kuzi-*implement* kwa upande wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la kupanda kwa bei ya vyakula mara kwa mara. Hili kwa sababu nilikua nalifanyia kazi kwa karibu zaidi na mwenzangu Waziri wa Biashara kwa upande wetu sisi kama ni serikali tumetoa unafuu wa kodi mkubwa sana. Mhe. Spika, wiki iliyopita nilikua Pemba nimezungumza na wafanyabiashara wa Pemba baadae wao wenyewe wakaanza kujadili kwamba wanapandisha bei za vyakula kwa sababu tu baadhi ya wafanyabiashara wanataka kupata faida kwa wingi zaidi, jambo ambalo sio zuri kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, nitashauriana na mwenzangu Waziri wa Biashara tuendelee kukaa pamoja na kuunda timu yakufuatilia hizi bei ili tuweze kuwatanabahi wale ambao wanapandisha bei kinyume na taratibu zetu.

Mhe. Spika, la mwisho limeibuka wazo la Tume ya Pamoja ya Fedha kutaka nitoe maelezo, lakini nashukuru baadhi ya wajumbe walikiri kwamba sina maelezo. Kwa upande wetu Zanzibar kazi tumemaliza tunasubiri wenzetu, mara ya mwisho nimekutana na waziri mwenzangu Mhe. Mkulo alikua waraka hajaupeleka kwenye *cabinet* tukashauriana basi waupeleke kwenye *cabinet* kwa kusaidiana wataalamu wetu na wataalamu wao. Mhe. Spika, bado sijapata *feedback* kutoka kwake kama ule waraka umeshapelekwa au haujapelekwa.

Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar tayari mapendekezo yetu tunayo hivyo yatakapotakiwa tutayawasilisha katika kikao cha pamoja. Mhe. Spika, kama nilivyosema maoni na mapendekezo ni mengi lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba yote tumeyachukua na wataalamu wangu wamejaa wengi kule juu nawashukuru sana kwamba tumeyachukua yote kwa pamoja.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kama nilivyokwambia ilikua leo nisafiri niende Marekani kuhudhuria mkutano, lakini nimeghairisha kwa sababu ya kamati ya leo hii na Kamati ya PAC. Kwa sababu nimetoa uzito wa kamati hizi mbili, kwa hiyo Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii iliyotolewa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati mia kwa mia.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kufanya majumuisho kutokana na michango na mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuhusu Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayoshughulikia Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe kwa kuchangia uzuri ripoti yetu hii na napenda kuwahakikishia kua michango, mapendekezo, maelekezo na ushauri tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo kadri ya uwezo utakavyoruhusu kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya kazi na maendeleo ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa ripoti yao nzuri, ambayo imetoa mchango na maelekezo na tunaahidi kwamba wizara itayafanyia kazi maelekezo na ushauri walioutoa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kujibu hoja na kutoa ufafanuzi wa maelekezo na maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kama hivi ifuatavyo:-

Wengi wa wajumbe walichangia kwa kuipongeza ripoti hii na kuunga mkono hoja, maelekezo, na mapendekezo yaliyotolewa na kamati ya Baraza hili tukufu inayoshughulikia fedha, biashara na kilimo. Nachukua fursa hii kuwahakikishia wajumbe kuwa maoni, maelekezo, na mapendekezo yao tunayachukua na kuahidi kuyafanyia kazi. Miongoni mwa maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe walitoa maoni yao kwa msisitizo naomba niyasome moja baada ya moja kama ifuatavyo:

Kupitia sheria na kanuni zinazohusiana na makosa ya uharibifu wa misitu, na maliasili nyengine kwa lengo la kuongeza adhabu iliyowekwa. Adhabu zilizokuwepo hazimfanyi mtu ashituke akiambiwa anachukuliwa hatua, inakuwa kwake yeye ni kitu cha kawaida, anatia mkono mfukoni analipa anaendelea na shughuli zake.

Sehemu nyengine ni uongezwaji wa utoaji wa elimu juu ya matumizi bora ya gesi na majiko mengine. Tutumie gesi, hali ya ukataji wa kuni bado inaendelea ingawa katika kiwango kidogo kimepungua, lakini bado tupunguze mashoka yetu kwenda mwituni, ili tuweze kuwa na maliasili na kuilinda kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Spika, suala jengine linalohusiana na misitu kama ni maliasili, ni kuweka mkakati makusudi wa upandaji mikarafuu na usimamizi katika makuzi yake. Tunatazamia katika siku ya tarehe 21 mwezi huu nafikiri itakuwa moja katika siku ya upandaji wa miti, na ningewaomba ndugu wajumbe tushirikiane pamoja ili misitu iliyokuwa imepigwa mashoka tuirudishe katika kiwango cha juu sana.

Suala jengine ni kuendeleza Chuo cha Kilimo hadi kufikia kutoa mafunzo ya kiwango cha shahada. Suala hili tunakwenda nalo na kuwapatia matrekta na mbegu za mpunga wakulima kwa muda mfupi sana. Kama mnavyofahamu vijana wetu watatu walikwenda China kuhusiana na mashine za kilimo au kwenda na wakati wa kilimo badala ya kukaa na kile kijembe muda wote toka asubuhi mpaka jioni ukishamaliza umevuna gunia zako mbili, lakini kazi uliyoifanya ni kazi ya kuvuna milioni mbili badala ya magunia mawili. Kwa hivyo vijana wetu kama Katibu wa fedha, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili na Ndugu Said Hassan Said, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali walikwenda China na kuangalia mashine zipi ambazo zitafaa katika kuondosha ule utaratibu wa kizamani wa kulima kizamani zamani.

Kwa hivyo, kuwapatia matrekta na mbegu za mpunga wakulima na kwa muda muafaka, hayo ni masuala muhimu sana, wakati gani wakulima wanapewa mbegu, wakati gani matrekta yanakuwa yapo uwanjani yanafanya shughuli zake kwa sababu yanakwenda pamoja na suala la mvua na uwezo wa mvua kuwa nao kidogo inakuwa ni ngumu. Lakini tujitahidi ili wakati unapofika wa kuyatumia matrekta na kutumia mbegu zetu za mpunga, wakulima wawe wamepata muda mzuri wa kutosha na muda muafaka.

Jambo jengine Mhe. Spika, upatikanaji wa fedha. Napenda nimpongeze Waziri wa Fedha ambaye kwa juhudi zake kubwa, amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kila mtu anapata kile alichokiomba na anakitumia kwa vile alivyokiombea, hii nimpe shukurani sana. Kwa sababu bila ya hapo mambo mengi yangelikwama, lakini amekuwa hodari wa kuyakwamua.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na juhudi za kuifanyia marekebisho sheria na kanuni za misitu na maliasili zilizopitwa na wakati. Katika kutekeleza hayo, wizara hivi karibuni imezindua kanuni mpya juu ya udhibiti wa matumizi ya msumeno wa moto, ikiwa ni sehemu ya kusaidia kupunguza ukataji wa miti ovyo. Kwa sababu msumeno kwa dakika moja au mbili unaweza kukuta minazi kumi imeshakwenda zake, kwa hivyo kidogo tushirikiane katika eneo hilo na tuhakikishe kwamba kilimo tunachokipangia hakiendani na ongezeko la kukatwa miti katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe Wizara ya Kilimo inaendelea kushajihisha wananchi kutumia nishati ya gesi hususan kwa kupikia. Katika kufanya hivyo wizara inaendelea kutoa elimu kwa njia ya redio na vielelezo mbali mbali. Katika kufanikisha azma hii, wizara inazindua kampeni ya matumizi ya gesi huko Pemba, kwa lengo la kupunguza matumizi ya kuni na misitu kwa jumla, zaidi ya nyumba 2000 sasa zinatumia nishati hiyo kwa kupikia ambayo inatolewa bure kwa matangi mawili kwa kuanzia.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo inaendelea na mpango wake madhubuti na kuongeza idadi ya miche laki tano ya mikarafuu kwa mwaka kuanzia mwaka huu. Aidha, kuhusu mpango uliopendekezwa na kamati ya kuweka takwimu halisi za upandaji, ukuaji na maeneo yameonesha kiwango kizuri cha ukuaji. Wizara yangu inachukua ahadi na kuzifuatilia kwa karibu takwimu hizo na kuziripoti kunakohusika na kuzichukulia hatua kama ipasavyo.

Pia Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu suala la kukiendeleza Chuo cha Kilimo Kizimbani, na kukipa uwezo wa kutoa mafunzo kwa kiwango cha shahada. Wizara ya Kilimo imefanikiwa kukipatia usajili chuo hicho katika Baraza la Taifa la Vyuo yaani *NECTA*, ambapo kwa hatua mitaala ya chuo inabadilishwa na vyetu vitavyotolewa na chuo vitaweza kutambulika ndani ya Jamhuri ya Muungano na kwengineko duniani. Kutokana na mitaala hiyo, itakapofika mwaka 2013 chuo kitaanza kutoa wahitimu wa stashahada yaani diploma. Aidha, chuo kwa kushirikiana na Chuo cha Kilimo cha Sokoine pamoja na taasisi nyingi kama vile Obalozi wa Norway, kimeingia katika makubaliano ya pamoja na kukiendeleza kitaalamu kwa baadhi ya miundombinu. Wizara kupitia mradi huo wa *ASP* imekamilisha mchakato na mpango wa ujenzi wa Dakhalia ya Wanafunzi wa Kike.

Mhe. Spika, katika msimu huu wa kilimo, wizara imetoa mbegu ya muda wa kati na mfupi kiasi tani 353 na kuziuza kwa wakulima kwa bei ya shilingi 200 kwa kilo, ambayo ni ndogo zaidi ikilinganishwa na bei halisi ya shilingi 2000 kwa kilo.

Aidha, kuhusu suala la matrekta, wizara imejipanga kuhakikisha ifikapo mwezi wa Oktoba matrekta yatakuwa tayari kuingia mabondeni kwa kulima. Hata hivyo, kwa msimu wa mwaka huu matrekta hayatoweza kulima kwa wakati kutokana na mvua ya vuli kunyesha kwa kipindi cha miezi miwili baada ya uzinduzi wa kilimo cha mpunga. Wizara pia imenunua matrekta 10 mapya ya ziada kutoka Suma JKT, ili yaweze kuongeza nguvu sambamba na yale makongwe yaliyotengenezwa.

Mhe. Spika na ndugu Wajumbe kuhusu suala la utayarishaji wa maombi ya fedha serikalini mapema. Wizara kama ilivyo kawaida yake kwa taasisi nyengine inao utaratibu wa kuandaa mpango wa matumizi ya *cash flow* na kuiwasilisha Wizara ya Fedha kabla ya kuanza matumizi yake. Katika kufanya hivyo wizara imehakikisha kwamba inaainisha mambo muhimu ambayo yanahusiana na misimu mbalimbali ya kilimo kwa kuzingatia mwenendo wa msimu mmoja na matarajio ya hali ya hewa. Wizara kupitia Taasisi hiyo ya Utafiti wa Kilimo, na Idara ya Kilimo, inachukua ushauri uliotolewa wa kufanya utafiti juu ya ukulima wa mbogamboka katika baadhi ya maeneo ya wizara, na inaahidi kwamba itafanya kazi kwa ushauri uliotolewa.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, kuhusu ugawaji wa *power tiller*, wizara tayari imeshazigawa *power tiller* hizo katika baadhi ya taasisi na kwenye mabonde ya umwagiliaji Unguja na Pemba. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe nikushukuru tena Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimalizie hapo, na tujitayarishe na wajumbe wako kwa upandaji wa miti siku ya tarehe 21.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika, kupata nafasi hii ya ku-*respond* kwa baadhi ya masuala ya wajumbe. Kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na wajumbe wote wa kamati yake kutokana na michango mizuri na ripoti nzuri ambayo wameiandika na wakatoa mapendekezo yao 13 katika ripoti hii.

Mhe. Spika, katika ripoti hii kuna mambo 13 ambayo tumeyazingatia kwa kina na tutayafanyia kazi kwa haraka iwezekanavyo.Lakini nikiangalia katika mambo 13 haya, mambo mawili yalikuwa kwa kweli ni hapa katika wizara yetu.

Kwanza jambo la tisa ukarabati wa ghala za kuhifadhi chakula cha hakiba ya nchi pamoja na matatizo mengine yanayohusiana na uhifadhi huo kwa mujibu wa sheria ufanyike haraka, ili angalau mwakani ghala hizo ziweze kutumika kuhifadhia chakula cha hakiba.

Mhe. Spika, hii kama unavyojua tumepitisha sheria hapa ya *Grain Reserve* ambayo itakuwa chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kwa hivyo, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni mjumbe tu wa hii kamati.

Lakini la pili wizara isimamie suala la uhifadhi wa mafuta ya nchi kwa ajili ya mafuta ya dharura. Kwa bahati mbaya suala la mafuta haliko chini ya wizara yangu ya Biashara liko chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Baada ya kutoa taarifa hiyo sasa naomba niendelee na kutoa maelezo yafuatayo:-

Suala la elimu kwa wajasiriamali, hili naahidi kwamba tutalifanyia kazi na ni muhimu sana. Suala la kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi wa kutosha vile vile na hili tutalifanyia kazi kwa karibu sana. Suala la vituo vya kuuzia karafuu ni kweli vituo hali yake si nzuri, kwa sababu kwa muda mrefu vituo hivi ilikuwa havijafanya kazi, ni hivi karibuni tu vimeanza kufanya kazi, lakini kwa maelekezo ya mwenyewe Mhe. Rais na kwa maelekezo ya wanakamati, vyote vituo vyetu vitakarabatiwa sawasawa, vitachimbiwa vyoo na mule mwahala ambamo mna ukaribu wa kupatikana maji vitaungwa maji na umeme.

Kwa hivyo, nataka tuhakikishe kwamba vituo vyote 36 ambavyo vipo sasa hivi na vitakavyojengwa, vitakuwa vituo vya kisasa na vitakuwa vinakidhi haja ya kuwabembeleza wateja kuja kuuza bidhaa zao kwa kuwapatia mabenchi ya kukalia na vyoo na mengineyo. Vile vile pamezungumzwa hapa kuna masuala ya kupanda bei mara kwa mara. Kwa kushirikiana baina ya Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Fedha tunakaa pamoja kuangalia namna gani tutaweza serikali kusaidia wananchi, ili bei ziwe chini na kupitia kanuni zetu tulizozigawa mara ile tulipokuwa hapa za kukaa pamoja na wafanyabiashara, ili kuangalia bei za bidhaa za kuuziwa wananchi, mpaka sasa hivi tunafanya kazi kubwa ya kuweka bei za bidhaa ziwe chini.

Kama tunavyojua kwamba sasa hivi bei za bidhaa Zanzibar ziko chini kuliko bei za bidhaa hizo katika Afrika Mashariki nzima. Bado naahidi mbele yenu kwamba tutafanya kazi ya ziada kuona kwamba bei hizi haziongezwi kiholela na baadhi ya wafanyabiashara ambao hu-*create environment* ya uhaba wa chakula ili waongeze bei za bidhaa. Wafanyabiashara hao tutapambana nao kuona kwamba wanadhibitiwa.

Suala la mizani katika vile vipolo vya kilo 50, hili tumelifanyia kazi na kila mwenye kuuza bidhaa hizi kwa jumla anatakiwa aweke mizani za kupimia kipolo cha kilo 50, na mizani hizo tunazipitia na kuzifanyia ukaguzi mara kwa mara. Ninachowaomba wananchi wote pamoja na wawakilishi waliomo ndani humu, wanapokwenda kununua bidhaa zao katika maduka ya jumla wahakikishe kwamba kipolo hicho kinapimwa kabla ya kukichukua. Inawezekana kabisa kuwa ujanja huo upo lakini njia thabiti mwambie kipolo hicho nilichonunua cha kilo 50 naomba ukipime niangalie niridhike ndio nikichukue, hilo ni suala muhimu sana.

Suala jengine kuhusu suala la Ofisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS)*. Wizara iliomba shilingi milioni 201 kwa ajili ya kununulia vifaa vya maabara, na pia iliomba fedha nyengine kwa ajili ya ukarabati wa majengo kwa programu ya *BEST*. Katika Programu ya *BEST* fedha hizo bado hazijapatikana na hata hivyo, wizara imeanza kutafuta majengo na serikali imeshapata majengo katika yale maeneo ya Mtoni pale kwenye kiwanda cha sigireti. Kwa hivyo, Idara ya Majenzi imeanza kutoa ushauri juu ya ujenzi ambao utafanywa katika eneo hilo lililokuwa Kiwanda cha Sigara hivyo kazi imeshaanza.

Kuhusu ujenzi wa viwanja vya maonesho, katika bajeti yetu ya mwaka huu hatukuwa na kasma ya ujenzi wa viwanja vya maonesho. Lakini tuliomba msaada kupitia hiyo programu ya *BEST*, wizara ilikusudia kupata shilingi milioni 380 kutoka BEST, na *Windup* vile vile shilingi milioni 400. Kwa hivyo, tunatarajia kwa mwaka huu tutapata shilingi milioni 780 ambazo zitatusaidia kuweza kuanza kutengeneza angalau ma-*document* na ujenzi mdogo mdogo katika sehemu hiyo, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo msaada huu bado hatujaupata.

Hata hivyo, wizara yetu imetayarisha *document* za *tender* za michoro, ili tukipata fedha tu tuweze kutangaza *tender* na wakandarasi waweze kufuata *tender* hizo. Suala muhimu ninalotaka kusisitiza ni kwamba, hatutaki kujenga mabanda ya maonesho, tunataka kujenga nyumba za maonesho ya kisasa ambayo kwamba ni bora zaidi katika Afrika Mashariki nzima. Kwa hivyo, tutahitaji fedha nyingi sana, na hivyo tupewe muda zaidi wa kutafuta wafadhili, wa kutafuta wa kuwakopa, lakini tunataka kujenga jengo la maonesho la kimataifa ili liweze kuwa kivutio cha wote watakaokuja kuwekeza katika biashara katika eneo hilo. Naomba tuvumilie na naamini kwamba katika kipindi kifupi tutaweza kufanikiwa *Inshaallah*.

Mhe. Spika, suala la upelekaji wajasiriamali kwenye maonesho ya Saba Saba. Wizara yetu ina mpango mzuri kabisa wajasiriamali Zanzibar ni wengi, kuna wajasiriamali ambao wana uwezo mkubwa na kuna wengine wana uwezo mdogo. Wizara ina uwezo mdogo vile vile haina uwezo mkubwa, kwa hivyo tunachofanya sisi tunawatangazia wajasiriamali wote ambao wanataka kwenda kushiriki katika maonesho ya saba saba waje kujaza fomu katika Wizara yetu ya Biashara.

Wanakuja wajasiriamali wanajaza fomu zao za *questionaire* ya kwenda kuonesha bidhaa zao katika ukumbi wa Saba Saba. Na wakifanya hivyo basi, jopo la maofisa kutoka Wizara ya Biashara wanakwenda kutembelea sehemu ambayo mjasiriamali anafanya kazi hizo na anatembelea vile vile na kuangalia ubora wa zile bidhaa wanazozitoa na vile vile wingi wa bidhaa zenyewe. Baadae wanaangalia nani katika hao ni bora zaidi ambaye atakwenda kuonesha bidhaa hizo.

Huu ni kama mtihani Mhe. Spika, mnaweza kuwa watu mia lakini watu 50 wakapasi wakenda katika maonesho. Kwa sababu maonesho hayo nafasi zenyewe ni 50 tu, kwa hivyo wale ambao hawakubahatika mara iliyopita vigezo tumewapa vya kufanya kazi kwa jitihada zaidi za kuboresha bidhaa zao ziweze kuwa na vigezo vizuri ili viweze kuuzika.

Kwa hivyo, wakifanya hivyo naamini kwamba mara hii iko nafasi kubwa zaidi, tumetayarishiwa nafasi kubwa zaidi ya kupeleka watu zaidi ya 50. Kwa hiyo naomba wawakilishi wawasaidie wajasiriamali katika majimbo yao, ili waweze ku-*qualify* waweze kupata nafasi ya kushiriki katika maonesho ya Saba Saba yanayokuja. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kusema kwamba yote maelekezo tumeyapata na tutayafanyia kazi, na tuko tayari wakati wowote kushirikiana na kamati hii ili kuendeleza mbele taifa letu.

Mhe. Spika, naomba radhi kwamba leo asubuhi sikuwepo hapa kwa kweli nilikuwa na mambo mawili mazito, jambo la kwanza nilikuwa katika ziara ya Mhe. Rais ambayo leo alikuwa katika Wizara yangu kule Pemba, lakini la pili nilifiliwa na ami yangu mimi leo. Kwa hivyo nilikuwa na mambo mawili mazito ndio maana sikuja hapa kuja kushirikiana na nyinyi. Sikudharau mimi kamati hii ninaipenda sana, naithamini sana na nataka tushirikiane, lakini ilikuwa nina mambo mawili mazito sana ambayo yamenikabili lakini nikasema yote matatu nitayafanya. Nitakwenda katika ziara ya Mhe. Rais, nitakwenda katika maziko ya ami yangu na nitakuja katika Baraza la Wawakilishi na Mwenyezi Mungu kanijaalia nimefika. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe, sasa ni nafasi ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Jitahidi ufanye kwa kifupi ili twende na ripoti nyengine iliyobaki.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikaeleza majumuisho ya ripoti yangu kwa kifupi kabisa.

Mhe. Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia ripoti yetu hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Lakini pia tunaamini kwamba wajumbe wengi zaidi wangeweza kuchangia ripoti hii kutokana na umuhimu wake, lakini kutokana na uchache wa muda ndio hivyo wengine hawakupata nafasi ya kuchangia.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwataje basi Waheshimiwa Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia ripoti yetu hii.

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid
6. Mhe. Rashid Seif Suleiman
7. Mhe. Mohammed Mbwana
8. Mhe. Mbarouk Wadi Mtando
9. Mhe. Asha Bakari Makame
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Salim Abdalla Hamad
12. Mhe. Subeit Khamis Faki
13. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
14. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili
15. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wamepata nafasi ya kuchangia mambo mbali mbali ambayo mengi yameweza kupata ufafanuzi kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri husika. Lakini kuna jambo moja ambalo Mhe. Rashid Seif Suleiman alitaka kujua hatma ya Karakana ya Matrekta ambapo hapo awali ilikua haijulikani kama ni shirika au idara. Pia kaelezea kwamba Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo haikuweza kuzungumzia lolote juu ya jambo hili pengine labda kamati imeshakata tamaa. Lakini ukweli kwamba sasa hivi Karakana ya Matrekta iko chini ya Idara ya Kilimo na sio kama vile zamani kwamba ilikua haijulikani kama ni shirika au idara. Sasa hivi Karakana ya Matrekta iko chini ya Idara ya Kilimo ikisubiri maamuzi ya serikali kama ifanywe idara kamili au vyenginevyo. Tayari Wizara ya Kilimo na Maliasili imeshaiandikia serikali juu ya mapendekezo ya jambo hilo. Kwa hivyo, hatukuliacha lakini bahati nzuri ufafanuzi wake tunaujua.

Mhe. Spika, Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo inawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote. Kwanza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuakhirisha safari yake ya Marekani, ilikua leo asafiri alikua kishaniaga, nikamuuliza mbona hujaondoka, akanambia aaa kutokana na umuhimu wa shughuli hii basi naakhirisha safari yangu. Kwa hivyo, tunakushukuru kwa kuakhirisha safari na kwa kuona umuhimu wa jambo hili.

Lakini pia Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili bahati nzuri amewahi asubuhi amekuja amesikia masuala ya wajumbe, alikua na dharura kidogo lakini amewahi na bahati nzuri amepata nafasi ya kutoa ufafanuzi.

Lakini pia Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko nae tunamshukuru sana na tunampa pole kwa kufiliwa na ami yake Mwenyezi Mungu ampe subira. Lakini pia tunampongeza kwa kuweza kushirikiana nasi na kupata nafasi ya kutoa ufafanuzi juu ya masuala mbali mbali yanayohusu wizara yake.

Mhe. Spika, tunaamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe wameridhika na ufafanuzi uliotolewa na Waheshimiwa Waziri wetu na kwa kweli wameweza kuzungumza na kujibu vizuri na tumeipokea ahadi yao kwamba wataweza kuyachukulia hatua yale yote ambayo yameelezwa katika ripoti yetu ya kamati.

Mhe. Spika, mwisho Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo inawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliotupongeza kwa kazi nzuri tuliyoifanya katika kamati yetu na tunawashukuru sana. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa uwasilishaji na hoja hiyo. Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoipokea ripoti hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Ripoti sasa iko tayari kufanyiwa kazi na serikali.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea muda wenyewe sidhani kama utatosha kumaliza ripoti hiyo lakini kwa hali ilivyo tumalize. Nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu aombe wajumbe wakubali tumalize ripoti hiyo mpaka mwisho. Inategemea kwa kiasi tutakavyojibana kwa muda ndipo tutakapomaliza mapema.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa sababu muda uliobaki hautoshi kumaliza shughuli iliyoko mbele yetu, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likubali kutenga kando kanuni ya muda ili tuweze kumaliza shughuli ilioko mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa umuhimu huo naomba sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii nikasimama mbele ya kiriri chako kuweza kutoa Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, kutokana na muda nitaomba hii ripoti yangu nitaisoma kuna baadhi ya maeneo nitajaribu kuyaruka ili kuweza kukidhi muda vizuri.

Mhe. Spika, awali ya yote nakushukuru tena kwa mara nyengine kunipa nafasi hii na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na uzima kwa kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Taasisi za Serikali kwa Mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, napenda kuitumia fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa michango yao ya kina waliyoitoa katika kazi zetu za Kamati pamoja na mashiriano makubwa waliyonipa wakati wote wakati Kamati ilipokua ikitekeleza shughuli zake. Napenda niwataje Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	-	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mohammed Ali	-	Mjumbe
7.	Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mjumbe
8.	Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9.	Ndg. Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu

Mhe. Spika, Kamati yetu imepangiwa kutekeleza majukumu yake chini ya Ofisi zifuatazo:-

- Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar
- Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na
- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Zanzíbar

Mhe. Spika, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nane kwa utaratibu ufuatao:

i. Pemba kuanzia tarehe 19/09/2011 hadi 30/09/2011 kufuatilia utekelezaji wa kazi za April – Juni 2011.
ii. Tanzania Bara kuanzia tarehe 12/12.2011 hadi 16/12/2011 kufuatilia utekelezaji wa kazi za Julai – Septemba, 2011.
iii. Unguja kuanzia tarehe 19/12/2011 hadi tarehe 23/12/2011 kufuatilia utekelezajia wa kazi Julai – Septemba, 2011.
iv. Pemba kuanzia tarehe 20/02-02/03/2012 kufuatilia utekelezaji wa kazi Julai –Disemba, 2011.

Mhe. Spika, naomba sasa nichukue fursa hii kuelezea Utekelezaji wa Kazi kwa Taasisi husika kwa mwaka 2011/2012, changamoto zao pamoja na maoni na ushauri wa Kamati.

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Idara ya Sera, Mipango na Utafiti na miongoni mwa kazi zake ni kuratibu shughuli za Ofisi, kutathmini Utekelezaji wa Ilani, Malengo ya Bajeti, miradi ya Ofisi na kuweka Mpango Mkakati wa kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya *Diaspora*. Kwa kuwatumia wataalamu iliowaajiri iliendelea na mchakato wa kuanzizha tovuti na barua pepe rasmi za Ofisi pamoja na Kitengo cha Habari na Mawasiliano.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Idara hii kutoa elimu na taarifa kwa jamii na duniani kote ili Wazanzibari walioko nje waweze kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu fursa zilizopo na mahitaji mengine pamoja na wao kushiriki kikamilifu katika kuchangia uchumi wa nchi yetu. Kamati pia inaishauri Idara hii kuangalia uwezekano wa kuwasaidia Wazanzibari walioko nje ambao wamekwama kimaisha na wanataka kurudi kwao lakini wameshindwa kwa sababu tofauti. Kamati pia inaishauri Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa kupitia Bajeti kuwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya Maendeleo ya Uitikiaji Wito wa Serikali kwa Wazanzibari walioko nje kuja kushiriki katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, Kamati ilipokea taarifa za Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais kuhusu utekelezaji wa shughuli zao, pamoja na kuipongeza kwa kazi kubwa wanazofanya lakini bado kuna upungufu mkubwa ikiwemo uchakavu wa majengo ya Ikulu, hasa Bwefum, Mkokotoni, Kibweni, Mkoani na Dodoma.

Mhe. Spika, majengo ya Ikulu ya Bwefum yamechoka sana ni ya muda mrefu hayatumiki na hayana hadhi ya kuwa ni majengo ya Ikulu. Kunahitajika matengenezo na ujenzi mkubwa wa majengo pamoja na ukuta, ili kuimarisha usalama wa eneo hilo.

Pia kamati imeshauri Ofisi ya Rais kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira kutafuta mshauri ili kuangalia ni jinsi gani watafanya ili kuzuia kasi kubwa ya mawimbi ya Bahari

yanayotishia usalama wa eneo hilo kuliwa na bahari, kwani hapo kale kulikuwa na jengo ambalo limekwishachukuliwa na bahari na kilichobaki ni dalili za mawe makubwa. Hii inatupa sura kua hata na hiyo sehemu iliyobakia kama hakujachukuliwa hatua za dharura, basi nayo itasombwa na maji na kutoweka kabisa.

Mhe. Spika, Kamati yetu inashauri majengo yote ya Ikulu yalioko vijijini Unguja na Pemba yaboreshwe ili Mhe. Rais anapohitaji aidha kuzungumza na wananchi wa maeneo hayo au anapohitaji kubadilisha upepo aidha kwa mapumziko au haja nyengine yeyote ile aweze kuyatumia.

Mhe. Spika, Ikulu ya Mkokotoni kwa hivi sasa haina hadhi ya kuitwa Ikulu kwani majengo yake yamechakaa sana na ile nyumba haifai kumuweka Kiongozi wa Nchi kwani ujenzi wake haukuzingatia usalama wa kiongozi mkubwa. Kwa hiyo, Kamati yetu inashauri nyumba ile ivunjwe na ijengwe nyengine yenye hadhi na muundo ambao utazingatia usalama zaidi. Pia kunahitajika pawepo nyumba za walinzi na wahudumu. Aidha, Kamati yetu inashauri kwanza zichukuliwe hatua za dharura za kuzungusha ukuta eneo hilo ili kuzuia mifugo kama vile ng'ombe ambao huharibu mazingira ya eneo lile.

Mhe. Spika, katika Ikulu ya Kibweni, Kamati yangu imesikitishwa sana na taarifa iliyopewa na watendaji wa Ikulu kwamba imepakwa rangi nyeupe ya *ANTI FUNGUS* kumbe si kweli kwani baada ya mwezi mmoja tu kunyesha mvua rangi ile ilikua tayari imeshafanya mwani. Kwa hiyo Mhe. Spika, naomba kuwatahadharisha watendaji wa Ofisi pamoja na Mawaziri wao kwamba kuidanganya Kamati ya Baraza kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria Nam. 4 ya Mwaka 2007 ni kosa na adhabu kali itachukuliwa kwa mtu yeyote pale atakapoidanganya kamati. Kwa hiyo, kamati inamtaka Waziri muhusika kuipaka rangi ya *ANTI FUNGUS* kama ilivyoambiwa na kamati wakati wa ziara ili kuweza kuleta haiba nzuri katika jengo lile. Pia kamati inashauri kua nyumba hizi ziwe zinatumiwa mara kwa mara na viongozi wetu kwani hua kwa muda mrefu hazitumiki matokeo yake kuchakaa haraka lakini pia husababisha kuibiwa vifaa vilivyomo ndani.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiboresha Ikulu ya Migombani ambapo kwa hivi sasa imekua na hadhi ile inayotakiwa. Hata hivyo, Kamati yangu inaishauri Serikali kuu kutafuta eneo jengine lililo mbali na barabara kwa ajili kujenga makaazi ya Rais kwani eneo lile lipo pahala sio pazuri kiusalama na pia liko barabarani sana kwani linamkosesha utulivu kiongozi hasa kwa milio ya magari ya mara kwa mara (ndio maana wakati wa ukoloni kuna eneo lilibatizwa jina "Regeza mwendo" ili kuwafanya viongozi wanaokaa katika eneo lile wasipate bughudha ya milio ya magari).

Mhe. Spika, Ikulu ya Mkoani Pemba iko hali mbaya sana na inahitaji ujenzi mkubwa na sio ukarabati tu. Kamati inaishauri Serikali kuu iwe na mradi maalum wa majengo ya Serikali na usifanywe kama mradi wa kawaida kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia kuna umuhimu mkubwa kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha uhifadhi wa eneo hilo sehemu ya nyuma ili kuzuia mmong'onyoko wa ardhi katika eneo hilo.

Mhe. Spika, Kamati yetu imepata nafasi ya kutembelea Dodoma na kuona hali ya Ikulu ya Dodoma. Kwa kiasi fulani inaridhisha lakini bado kwa hadhi ya Rais inahitaji matengenezo makubwa ili ilingane na hadhi yake hasa ikizingatiwa hivi sasa ujenzi wa majengo mbali mbali umeimarika Tanzania kwani kuna majengo ya watu binafsi yanakua na ubora zaidi ya makaazi ya Rais jambo ambalo halipendezi. Mhe. Spika, Kamati yetu pia inashauri kwamba nyumba ile iwekewe huduma zote za kisasa za mawasiliano ikiwemo *internet* pamoja na maktaba ndogo ili kiongozi apate kujisomea vitabu na kupata mawasiliano wakati wote, pamoja na sehemu ya ofisi ya ulinzi wa Rais. Hali ya bustani hairidhishi, hivyo kamati inaomba ishughulikiwe ilingane na jina la Ikulu.

Mhe. Spika, Kamati yangu ilipata nafasi ya kutembelea makaazi ya Rais Dar-es-Salaam. Hali ya majengo sio mbaya ingawa kunahitajika matengenezo madogo kwenye paa na ufinyu wa majengo ya makaazi kwa wahudumu na walinzi tunashukuru kuona Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuliona hilo na wameanza kulishughulikia. Pia kamati yetu inasisitiza kuwekwa kwa maktaba pamoja na kufunga huduma za *Internet* kwa ajili ya Rais na walinzi wake ili waweze kupata taarifa mbali mbali zinazotokea duniani wakati wote.

Mhe. Spika, Kamati yetu inaishauri Idara ya Mawasiliano- Ikulu kujitahidi kufuatilia ahadi za Rais anazozitoa sehemu mbali mbali na kuziwasilisha katika wizara husika kwa utekelezaji. Kamati yangu imegundua waheshimiwa wengi huwa wanawakumbusha Mawaziri ahadi za Rais lakini wanasema hawazijui hii inaonesha Idara hii haiwajibiki vizuri na kuwaandikia Mawaziri ahadi za Rais na hii hupelekea kuonekana kama ahadi zinapuuzwa na wananchi kukosa kuwaamini viongozi wao wanapokwenda majimboni na kutoa ahadi. Kamati

inashauri kitengo hiki kupatiwa vifaa vya kisasa ili kuweza kumudu kazi zao kwa ufanisi mkubwa na kwa wakati.

Mhe. Spika, pamoja na *G.S.O* kutoa maelezo ya kuwafanyia upekuzi watu 99, kamati yangu imebaini bado kuna wizara nyingi hazipeleki maombi ya kazi ya waajiriwa wapya. Watu huajiriwa bila ya kukaguliwa hii hupelekea kuajiriwa watu ambao hawana sifa zinazotakiwa, lakini pia wengine kughushi vyeti bandia au visivyokua vyao ili wapate kuajiriwa na matokeo yake kuajiri watu wasiokua na sifa na uwezo kwa kazi wanazopangiwa na kuwaacha watu wenye sifa kuendelea kusota mitaani bila ya kazi na kuzorotesha utendaji wa kazi serikalini na kudumaza maendeleo kwa nchi yetu. Lakini hii pia haitoshi, kubwa zaidi ni kuwavunja moyo vijana wanaojitahidi kusoma lakini wakati zinapokuja ajira huachwa na kuchukuliwa wasiokuwa na sifa.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaitaka *G.S.O* kufanya ukaguzi sio kwa waajiriwa wapya tu bali hata walioko makazini kuanzia Makatibu Wakuu, Manaibu, Wakurugenzi wa wizara, na wengine wote serikalini ili kuweka usawa katika sheria, kwani sheria haimbagui mtu. Kwani Katiba ya Zanzibar kifungu cha 12(1) kinasema **"watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya Sheria."**

Mhe Spika, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ina kazi kubwa za kuandaa vikao vya Baraza la Mapinduzi pia kuweka kumbukumbu za vikao. Kamati yangu inashauri ofisi hii kuweka kumbukumbu zake ipasavyo kwani baadhi ya maamuzi yanayopitishwa na Baraza la Mapinduzi na kuletwa Barazani kusahauliwa na baadhi ya Mawaziri na baadae huleta utata na mshangao kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao huyakumbuka yale yaliyopitishwa na taasisi hizi.

Mhe. Spika, Kamati yetu inatoa pongezi kwa Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho kwa kazi kubwa, nzuri na yenye ufanisi mkubwa kwa hapa nchini na duniani kote kwani inatoa vitambulisho vyenye ubora wa kimataifa. Idara hii imepata tunzo za kimataifa karibu mara tatu hili ni jambo la kupigiwa mfano na kupongezwa sana kwa utendaji mzuri ndani ya Zanzibar. Ingawa hivi sasa Ofisi hii inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa nafasi, Kamati yangu inaiomba Serikali kuwapatia jengo jengine ili kuweza kukidhi mahitaji ya kazi zao.

Mhe. Spika, pamoja na kazi yote hiyo kamati yetu inasikitika kwamba watumishi wa Idara hii hawapatiwi posho maalumu yaani posho nyeti kwani kutokana na unyeti wa kazi zao wanastahiki kupatiwa haki yao hiyo ya msingi. Mhe. Spika, Kamati yetu inashauri kuviboresha zaidi vitambulisho vya Uzanzibari kwa kuweka kumbukumbu zaidi za muhusika ikiwemo mali anazozimiliki, watoto, ajira, dini na kadhalika, ili mtu hata anapohitaji mkopo kwenye vyombo vya fedha iwe ni rahisi kupata kumbukumbu zake kwenye kitambulisho chake.

Hii pia itasaidia hata kuweza kuwatambua wahalifu pamoja na watu wanaomiliki mali zaidi ya uwezo wao. Lakini pia itasaidia kujua watu wanaofanya biashara haramu ambazo huwapatia kipato kisicho halali. Hii pia itasaidia kupunguza ufisadi kwa mali za Serikali na kusaidia uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba bado kunahitajika elimu ya uraia kwani bado kuna vitambulisho zaidi ya 32,186 bado havijachukuliwa na wenyewe, lakini pia uhaba wa wafanyakazi pamoja na vitendea kazi.

Mhe. Spika, Idara ya Serikali za Mitaa imekua ikifanya kazi nzuri ikiwemo kuandaa Sera na Sheria ya Serikali za Mitaa. Kamati yangu bado hairidhiki na kasi ya utayarishaji wa sera hii kwani imeshachukua muda mrefu hadi leo ni ahadi tu.

Kamati yangu inaitaka Wizara kuikamilisha ili iwe Sheria kwa kuja kutekelezwa. Kuchelewa kwa Sheria hii kunapelekea Zanzibar kukosa fursa nyingi za kiuchumi ikiwemo misaada ambapo hivi sasa Mashirika na taasisi nyingi za misaada hua tayari kuzisaidia zaidi Halmashauri kuliko Serikali kuu. Kuchelewa kwa Sheria hii kunakwenda kinyume na malengo ya Serikali ya Mpango wa Kupunguza Umaskini Zanzibar, kwani majimboni mwetu kuna matatizo mengi ya miundombinu ikiwemo barabara za ndani, maji, umeme, skuli na kadhalika.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaitaka wizara kuhakikisha Sera hii inakamilika na baadae kuleta sheria Barazani. Tunaamini kilio chetu hicho Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imekisikia na itakifanyia kazi. Pia kwa kua hivi sasa tumepitisha Sheria kua Sera zote si lazima kuletwa Barazani lakini kwa umuhimu wa sheria hii ni vyema tukapatiwa japo semina ili na sisi kuweza kuchangia. Lakini kamati yetu imeona cha kushangaza sana katika maandalizi hayo Ofisi imeshindwa kuwashirikisha Madiwani ambao ndio wadau wakubwa katika utekelezaji wa Sheria hii. Kwa hiyo, tunaitaka Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwashirikisha Madiwani katika maandalizi ya Sera hiyo.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, moja kati ya tatizo sugu ni ufinyu wa nafasi katika jengo wanalofanyia kazi, ingawa wanalo jengo lao liliopo hapo Amani bado hawajahamia hapo kutokana na sababu mbali mbali na kusababisha jengo hilo kutumiwa na taasisi nyengine kwa shughuli zao. Lakini pamoja na yote hayo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi haioneshi jitihada zozote za kutaka kuhamia katika jengo lao hilo kwani hakuna hata mipango endelevu ya kuhamia hapo. Cha kushangaza zaidi ni matumizi mabaya ya eneo hilo hivi sasa kwani hivi karibuni tu pale mbele ya jengo pameanzishwa *yard* ya kuuzia magari ya *second hand* kutoka Dubai, kuna wachongaji wa magogo ya kuchongea mbao, gereji ya Vespa na kadhalika. Hii inatusikitisha sana kamati kwa kuliachia eneo hilo kutumika kiholela.

Mhe. Spika, pia Mkoa unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uchimbaji ovyo wa mchanga kinyume cha sheria, utumiaji wa dawa za kulevya, uporaji wa vitu ikiwemo simu za mkononi, kwa hiyo kamati yetu inashauri wananchi wa Mkoa huu kuzidisha kasi ya ulinzi Polisi Jamii ili kuhakikisha kwamba tunaweka ulinzi katika maeneo yetu.

Mhe Spika, Kamati yangu ilipata maelezo kutoka Baraza la Manispaa tulipokea maelezo mengi ya utendaji kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana hasa ya kuuweka mji wetu kuwa safi, ingawa wana upungufu mkubwa wa magari ya kuzolea taka pamoja na makontena ya kuwekea taka. Hata hivyo, maeneo mengine hakuna hata sehemu za kuwekea taka, ingawa tulipata faraja ya kusikia wamo mbioni kuleta gari za kuzolea taka kupitia mradi wa *ZUSK* unaofadhiliwa na *WORLD BANK.* Pamoja na jitihada yote hiyo tatizo kubwa lililokuwepo ni mwamko mdogo wa wakaazi wa Mkoa huu wa Mjini Magharibi, ukosefu wa elimu ya usafi, kwani wananchi ndio wachafuzi wakubwa wa mji, wanatupa taka ovyo, wenye maduka pia wakishafagia taka zao huzitupa ovyo hii hupelekea kuwapa kazi kubwa wafanyakazi wa Manispaa ya kufagia wakati kazi yao ni kuzoa taka.

Mhe. Spika, pia kamati yangu inalipongeza Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na *WORLD BANK* kwa mpango wao wa kutaka kujenga mtaro wa maji machafu kutoka Darajabovu hadi Saateni. Mradi huu utawapunguzia wananchi wa maeneo hayo tatizo la maji kufurika na kuingia majumbani mwao wakati wa mvua kubwa inaponyesha. Lakini kamati inatoa wito kwa wananchi wetu wote wa Unguja na Pemba kuacha kutupa taka katika mitaro ya maji kwani husababisha maji kukwama wakati wa mvua na kusababisha mafuriko hata baada ya mitaro kujengwa.

Mhe. Spika, Kamati yangu haikubaliani na utaratibu unaotumiwa na Baraza la Manispaa wa kutoa fedha za maendeleo kwa Madiwani bila ya marejesho ya kazi zilizofanywa na hii hupelekea wananchi kudai kua Baraza la Manispaa halisaidii jamii wakati sio kweli kwani pesa zinatoka lakini hazina maelezo. Kwa hiyo, ni lazima kuweka utaratibu mzuri wa matumizi ya pesa hizo ili ziweze kukaguliwa mahesabu yake. Mhe. Spika, kamati yangu inaishauri Serikali kuwarejeshea asilimia ya mapato yaliyochukuliwa na Serikali kupitia baadhi ya leseni ambayo yalikuwa yanasaidia kuendesha shughuli zao za kazi za kila siku. Kamati yangu pia inalitaka Baraza la Manispaa pamoja na baadhi ya Halmashauri kuepukana na migogoro iliyojitokeza kuhusu makampuni yanayoweka mabango ya matangazo kwenye maeneo yao na ni vizuri kukawa na mikataba maalumu na ya wazi iliyopitishwa na Kamati za Madiwani ili kuondoa dhana mbaya ya rushwa au upendeleo kwa baadhi ya makampuni, kwani hivi sasa kumejitokeza malalamiko katika baadhi ya sehemu kuhusu kutokutendewa haki.

Mhe. Spika, Kamati ilipata nafasi ya kuzungumza na Mkuu wa Wilaya ya Mjini ambaye Ofisi yake ilikua na changamoto ya uchakavu lakini tunashukuru kua hivi sasa imo katika matengenezo, tunaamini ikimalizika tatizo la usalama wa watumiaji wa jengo hilo litaimarika. Changamoto iliopo ni kuongezeka kwa mabaa ya mitaani kamati yangu inamtaka Mkuu wa Wilaya ya Mjini kuidhibiti hali hii hasa kupitia vikao vyao vya Kamati za Ulinzi na Usalama. Pia kamati yangu inamtaka Mkuu wa Wilaya kufuatilia wafanyabiashara ndogo ndogo hasa wanaouza visu na miwani ambao sio wakaazi wa Zanzibar kuwaondoa mara moja kwani wengine hua ni vibaka na hiyo hua ni sababu tu ya kujificha ili kufanya uhalifu huo.

Mhe. Spika, Wilaya ya Magharibi ni eneo ambalo tatizo la uchimbaji mchanga ovyo limekithiri na wakati mwengine linachangia kuhatarisha usalama wa miundombinu ikiwemo kuchimba pembezoni mwa nguzo za umeme mkubwa unaotoka Tanzania Bara. Pia kuna tatizo kubwa la ukataji ovyo miti kwa kutumia misumeno ya umeme. Pia kuna uvamizi wa maeneo ya kilimo ikiwemo mabonde ya mpunga kwa kujenga nyumba za kuishi ambapo hupelekea kuongeza umaskini kwa wanaotumia maeneo hayo kwa kilimo. Pia kamati yangu inalitaka Baraza la Manispaa kama tulivyowashauri kwenye ziara za kamati kulifukia shimo la nyuma ya Uwanja wa Amaan ili kuuhami Uwanja wa Amaan lile jengo lisije likaanguka.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa kazi nzuri hasa kusaidia miradi mbali mbali ya maendeleo majimboni, pia kuimarisha mradi wa uzoaji taka lakini bado kuna changamoto kubwa ya ukusanyaji wa kodi za leseni pamoja na vibali vya ujenzi kwani inaonekana bado kuna baadhi ya mapato aidha hayakusanywi au yanavuja. Kamati inaitaka Halmashauri kujitahidi kubuni vianzio vipya vya mapato pamoja na kuangalia upya mikataba ya uwekaji mabango ya matangazo ambapo ni vyema kufanya utafiti kwa ada wanayolipwa kama inastahili, lakini pia kuangalia na muda wa kumaliza muda wa mikataba hiyo.

Mhe. Spika, Kamati inampongeza Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa jitihada zake na kufanikiwa kujenga jengo lao hapo Tunguu, ingawa halijamalizika lakini kazi zimeanza kutekelezwa ndani ya jengo hilo. Kamati inaiomba Serikali kulimaliza jengo hilo ili liwe na hadhi ya kuwa la Mkuu wa Mkoa. Tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuwapatia fedha katika bajeti ya mwaka unaokuja ili kuhakikisha jengo lile linakamilika.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa kuweza kusaidia miradi ya jamii ikiwemo umeme, maji, skuli na kadhalika. Tunaipongeza kwa ukusanyaji mapato lakini bado tunaitaka kuongeza mapato kwani eneo hilo lina miradi mingi ya uwekezaji ambapo wanawajibika kukatisha vibali vya ujenzi kwa miradi hiyo. Kamati yangu inazitaka Halmashauri zote kusimamia na kutoa maelekezo ya ujenzi hasa katika miradi ya uwekezaji ya kitalii ambapo kamati yangu imeona inaongoza katika ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira.

Mhe. Spika, Kamati pia inaipongeza Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa kusaidia miradi ya jamii lakini bado kamati inaitaka Halmashauri kujitahidi kuongeza vianzio vya mapato kwani bado kuna maeneo wakijitahidi yataweza kuongeza mapato ikwemo ada ya ujenzi hasa kwenye miradi ya uwekezaji ya utalii.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuanzisha ujenzi wa Ofisi yake kwani kwa muda mrefu wamekua wakifanya kazi zao katika mazingira magumu na ufinyu wa nafasi katika jengo hilo na tunaiomba Ofisi hiyo kuharakisha kuhamia katika jengo hilo. Mhe. Spika, hapa pia tunaomba tena Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na kwamba anazungumza pale naamini ananisikia kutenga fedha katika bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kukamilisha jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, katika Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na Mkoa wa Kusini hasa katika maeneo ya ukanda wa uwekezaji katika fukwe zote kumevamiwa na mapapasi wengi bila ya utaratibu kwani limekua kama eneo la maficho kwa wageni ambao huingia Zanzibar na kwenda kufanya kazi katika fukwe zetu na mara nyingine hujiingiza katika kufanya vitendo vya uhalifu na itakapotokea hivyo hakuna pa kuweza kuwapata kwani hata Masheha hawawatambui pa kuwapata.

Mhe. Spika, hivi sasa kumekuwa na malalamiko mengi ya wawekezaji kutokana na uhalifu unaotokea katika hoteli mbali mbali ambapo ndio nguzo kuu ya uchumi wa nchi yetu. Hii ni hatari kwa uchumi na nchi yetu kwa jumla. Kwa hiyo, kamati yangu inaitaka Serikali kuvitumia vikosi vyetu vya SMZ kwa kuwaweka walinzi katika hoteli zilioko karibu na fukwe ili kusaidia kuondoa kabisa vitendo vya uhalifu katika hoteli zetu. Pia kamati yangu iligundua katika ufukwe wa Nungwi kumekua na Bandari bubu ambayo hutumika kwa kusafirishia watu kutokea na kwenda Tanga bila ya utaratibu wa kisheria na kusababisha kuingia wageni kinyume na sheria. Kamati inamuagiza Mkuu wa Mkoa kulifanyia kazi suala hilo.

Mhe. Spika, Kamati yangu ilipokea taarifa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini ‘A’ ambayo inajitahidi kupambana na uharibifu wa mazingira na upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuviondosha vibanda vya biashara za utalii vilivyojengwa kiholela katika maeneo ya fukwe hasa katika maeneo ya Pwani Mchangani. Hata hivyo, wamiliki wa hoteli walivirudisha tena vibanda hivyo kwa maslahi yao ambapo baadae vibanda hivyo huviimarisha kwa kujenga majengo ya kudumu na kupelekea uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, kamati yangu inasisitiza kutoruhusu ujenzi huo wa vibanda hivyo ili kuepusha ukiukwaji wa sheria na uchafuzi wa mazingira.

Aidha, Halmashauri kwa ujumla zinatakiwa zitafute wataalamu wa kuhakikisha kwamba maeneo ya biashara yanajengwa kwa ramani za kuvutia ili kuimarisha mazingira na mandhari ya maeneo husika na kuwavutia watu wote hata wageni wanaokuja nchini kwetu.

Mhe. Spika, Kamati yangu ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini ‘B’ Unguja na kugundua kua kuna uharibifu wa mazingira hasa katika maeneo yaliyokua yakichimbwa mchanga na kufungwa lakini hivi sasa kuna

baadhi ya watu wabaya kwa tamaa zao wamekua wakirejea tena kuendelea kuchimba mchanga. Kamati yangu inaishauri Halmashauri kuzidisha ulinzi katika maeneo hayo ili kuhami hali hii.

Mhe. Spika, Kamati pia ilipata nafasi ya kutembelea Halmashauri zote za Pemba na kimsingi matatizo yanalingana. Kwa mfano, takriban kuna baadhi ya Halmashauri hazina wanasheria wao, jambo ambalo ni tatizo hasa katika kazi zao za kila siku ikiwemo kuwadhibiti wale wanaokiuka taratibu na sheria zilizowekwa na Halmashauri hizo.

Kwa upande wa Baraza la Mji Chake Chake kamati inaitaka Baraza hilo kuuweka katika hali ya usafi mtaro mpya uliojengwa wa kupelekea maji machafu baharini. Pia kutokana na uhaba wa wafanyakazi wa Baraza la Mji la Chake Chake Pemba, baadhi ya kazi tunazishauri baraza hilo kuzitoa kwa watu binafsi, ili kuhakikisha kwamba kazi hiyo ya kuweka mitaro usafi inafanikiwa.

Mhe Spika, kamati yangu inaitaka Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kushirikiana na Shirika la Bandari Zanzibar kusimamia ufukiaji wa mashimo yaliyochimbwa na Kampuni ya *Cogefer*, ambayo yanasababisha kuingia maji ya bahari kwenye mabonde ya mpunga yaliopo hapo shehia ya Mbuyuni. Pia kuweka utaratibu mzuri wa utupaji wa taka kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira.

Mhe Spika, kamati pia inaipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kazi nzuri na tunawataka kuhakikisha kwamba wanafikia malengo ya ukusanyaji wa kodi walizojiwekea.

Mhe Spika, Kamati yangu pia imepata malalamiko mengi kutokea Mikoa mbali mbali kuhusu migogoro ya ardhi ikiwemo za watu binafsi na hata za Serikali. Cha kusikitisha mingi ya migogoro hiyo ya ardhi kuna baadhi ya viongozi wamehusika, cha kusikitisha hata viongozi wetu wakuu wa kitaifa na wao wanajua hilo na wametoa maagizo mara nyingi kumaliza migogoro hiyo ya ardhi, lakini hadi leo hakuna mgogoro wowote ambao umetatuliwa.

Mhe Spika, inaonesha kuwa suala hili serikali imeshindwa kulitatua, nadhani hivi sasa uliruhusu Baraza lako tukufu kuunda Tume Maalum ya kufuatilia migogoro hii ya ardhi na kukuletea ripoti ambayo tunaamini itakuwa suluhisho ya migogoro hiyo katika Mikoa yetu mbali mbali. Mhe. Spika, hali ya majengo ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya huko Bemba sio nzuri, tunaiomba serikali kuliangalia hili kwa hatua ya dharura, angalau nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni kuihami kwa kuiezeka.

Hili suala la nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Mhe. Spika, tunamuomba sana Mhe. Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuangalia uwezekano. Kwa sababu mvua hizi za masika, Mhe. Mkuu wa Wilaya ule wakati wa kulala yeye huwa anatoka nje, anatoka ndani ya nyumba anakaa nje ili asivujiwe. Mhe. Spika, hili nilikuwa naomba kwa mashirikiano makubwa ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo walichukulie hatua ya dharura.

Mhe. Spika, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Bemba, tumepiga kelele sana nyumba yake mbovu. Sasa hivi tunashukuru angalau amehamishwa hapo alipo na amepatiwa makazi ya muda. Hapa tunaiomba sana serikali Mhe. Spika, kama tulivyosema kuwe na mradi maalum wa nyumba za viongozi, ili kuwaondolea kadhia ya kuhama hama kila wakati.

Mhe Spika, Kamati inakipongeza kikosi cha KMKM kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwa kulinda bahari yetu na wanachi wetu. Kamati pia inapongeza kwa kuuetekeleza ushauri wa kamati wa kuongeza boti za uokozi, ambapo husaidia sio tu kwa ulinzi lakini pia inasaidia kwa kuokolea watu pale wanapopata matatizo baharini.

Mhe Spika, KMKM kwa kushirikiana na vikosi vingine, wamefanya kazi kubwa ya kulinda na kuzuia magendo ya karafuu na kuokoa zao la Taifa, Lakini pamoja na kazi yote hiyo kikosi kinakabiliwa na matatizo mengi ya ukosefu wa vitendea kazi, kwa mfano kunahitajika chombo cha kumuandaa askari wakati anajitayarisha kwenda kuzamia chini ya bahari kwa muda mrefu, ili kuweza kumudu ile hali ya hewa ya kule baharini. Mhe. Spika, lakini chombo hicho hawana kwa hivi sasa. Kwa hivyo, inapotokezea maafa makubwa kuwapeleka askari wetu kwenye kina kikubwa cha maji, kwa kweli tunawahatarishia afya zao.

Kutokana na uwezo mdogo wa serikali, kamati inaomba kuwashirikisha makamanda wetu wa vikosi katika safari hizo za sasa hivi zilizoandaliwa na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, safari za China, ili na wao wakajenge urafiki na vikosi vya Jeshi la China, tunaamini wakikaa pamoja wataweza kutusaidia mambo mengi. Pia kikosi hiki kinaupungufu mkubwa wa nguo pamoja na chupa za gesi za kuzamia.

Mhe Spika, kikosi kinamiliki chelezo kilichopo Kibweni ambacho kimeharibika. Kamati inaomba aidha serikali ikishughulikie au kitafutiwe mbia wa kukiendesha, Ambato huyu mbia tayari ameshajitokeza, lakini wanasubiri ruhusa ya serikali, ili kiweze kufanya kazi na kuleta tija kwani kitaingiza fedha na kukarabati vyombo vyake. Pia kikosi kinazo Rada zake ambazo pia zinahitaji kushughulikiwa kwa karibu zaidi.

Mhe Spika, kwa upande wa Pemba hatuna kikosi cha uzamiaji hivi sasa tunavyozungumza. Hili ni tatizo Kubra, tunaiomba serikali kupitia kikosi cha KMKM, kupeleka kikosi maalum cha wazamiaji kule Pemba, ili kusaidia pale inapohitajika kufanya kazi hiyo ya uokozi kwa wananchi wetu kwa haraka. Pia kamati inakitaka kikosi kutafuta hati miliki za maeneo yake kwani kuchelewa kutafuta hati miliki hizo, kunaweza kuleta mgogoro na wananchi katika maeneo zilizo kambi zao. Mhe Spika, lakini hili sio tatizo la kikosi hichi tu, lakini tunamuomba sana Mhe. Waziri hapa kujaribu kuangalia maeneo yote ya idara maalum kuyatafutia hati miliki, kwa sababu hili limekuwa kama ni donda ndugu.

Mhe Spika, kamati yangu haikubaliani na utaratibu unaotumika kwa hivi sasa, kuhusu mgawanyo unaofanywa kwa fedha zinazopatikana za magendo ya karafuu, kwani fedha hizo hugawiwa sawa sawa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na KMKM, kwani KMKM hutumia gharama kubwa kuwatafuta watu wa magendo huhangaika siku nyingi hadi kuwagundua na kuwakamata. Lakini Ofisi za Wakuu wa Mikoa wao hawagharimiki kitu chochote labda kuziuza hizo karafuu zilizopatikana. Ukiangalia KMKM wanakabiliwa na hali ngumu ya utendaji wa kazi ikiwemo uhaba wa mafuta, boti na mashine zake, uchakavu wa majengo yake na hata Magali. Kwa maana hiyo kamati yangu inapendekeza asilimia 10 ya fedha zitakazopatikana katika magendo ya karafuu, basi hizo ndio wapewe Ofisi za Wakuu wa Mikoa na asilimia 20 ziende kwa mtoa taarifa na iliyobaki 70 iende kwa kikosi maalum cha kuzuia magendo, yaani KMKM, ili na wao kuweza kuwajengea uwezo wa kuongeza jitihada katika kazi zao.

Mhe Spika, kuhusu JKU. Serikali tunaiomba ifanye tathmini ya madhumuni ya kuundwa kwa JKU na tija inayopatikana, kwani sisi tunaamini kuwa kikosi hiki kimeanzishwa kwa nia njema na viongozi wetu waasisi, lakini bado huduma inayotolewa hairidhishi kabisa, kwani kikosi kinatengewa fesha chache, hakina vitendea kazi vya kutosha, vijana wanaoamua kwenda JKU kujitolea, wanashindwa hata kupewa posho la sabuni, ukilinganisha na wenzetu JKT Tanzania Bara angalau hupewa posho la sabuni.

Mhe Spika, kamati yangu inaishauri serikali kujipanga upya kuifanya JKU kuwa ndio kimbilio la vijana wetu, kwa maandalizi ya maisha yao ya badea, ili baada ya kumaliza masomo yao wakapate mafunzo ya ujasiria mali, kupata utaalam mbali mbali wa Ufundi ili baadae wakitoka wakajitegemee. Mhe. Spika, kamati yangu inapendekeza kuwa ile bajeti yote ya Wizara ya Kazi, Uwekezaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, basi ingepelekwa kule JKU ili ikawajenge vijana kiuwezo wa kujiajiri.

Pia kamati inashauri zile kazi za vibarua kutoka kwenye makampuni yanayokuja kufanya kazi hapa Zanzibar kungeliwekwa utaratibu wa kupewa vijana wa kujitolea wa JKU. Kama hivi sasa mahoteli mengi hapa Zanzibar yanaajiri walinzi kupitia makampuni yasio ya Zanzíbar, pamoja na wamasai ambao hawajui hata taaluma ya ulinzi. Kwa hivyo, kazi hizi zote kama tungelikuwa na utaratibu mzuri wa kuwapa vijana wetu wa JKU ulinzi, basi vijana wote wangelivutiwa kujiunga na JKU na kusingelikuwa na kelele nyingi kwa vijana wetu, hasa hapa Zanzíbar kukosa ajira. Halikadhalika hata wangelitumika katika kulinda fukwe zetu kwenye mahoteli ya kitalii kusingelikuwa na vitendo vya uhalifu. Kwa sababu hii, ndio maana kamati yangu ikashauri kikosi hiki kama kitafanyiwa tathmini ya kutosha kitawezeshwa basi kitaweza kuleta tija kubwa kama waanzilishi waasisi wa kikosi hichi walivyokusudia.

Mhe Spika, tunaomba sana serikali, kwa kuwa hivi sasa tumeunda idara za mipango, sera na utafiti basi kamati yangu inashauri wafanyiwe utafiti wa kutosha, tunaamini tutakuwa tumeisaidia sana serikali.

Mhe Spika, kamati yangu bado haijaridhika kwa kusuasua mradi wa mboga mboga unaoendeshwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Misri, kwani fedha nyingi sana zimeshatumika, lakini bado tija inayopatikana hairidhishi hadi sasa. Hivyo, kamati yangu inashauri ile kamati ya pamoja ya miradi ifanye tathmini, ya kuona kuna tatizo gani ili kuweza kurekebisha. Ingawa kamati yangu inajuwa kwamba mradi wa mboga mboga wa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar na Serikali ya Misri kupitia kikosi cha JKU unasuasua, kusuasua kwake umechangiwa na machafuko ya kisiasa yaliyokuweko huko nchini Misri. Kwa hivyo, tunaiomba serikali iweze kuchukua hatua za dharura ili kuokoa mradi ule ambao umeshatumia fedha nyingi.

Mhe. Spika, kamati yangu hairidhiki na utaratibu unaofanywa hivi sasa, wa kuwachukua vijana waliokwisha kutumikia JKU zaidi ya mwaka mmoja hapa Zanzibar, na baadae kwenda tena kutumikia JKT huko Bara kwa miaka mingine miwili, ili waajiriwe katika ajira ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mhe. Spika, sisi tunaamini kwamba JKU na JKT ni sawa sawa, kwa hiyo kijana akitokea JKU ni sawa na yule aliyetokea JKT. Kwa hivyo, moja kwa moja wakishapimwa hapa waingie katika ajira ya jeshi, sio kuondoka hapa baadae wakenda tena kutumikia miaka miwili kule JKT.
Mhe. Spika, kwa upande wa upande wa Pemba, JKU wanajitahidi kufanya kazi zao, lakini bado kuna changamoto nyingi zinawarudisha nyuma, ikiwemo uhaba wa fedha, vitendea kazi, usafiri pamoja na madeni. Kamati yangu inaishauri serikali kuanzisha mafunzo ya ufundi kule Pemba kama ilivyo hapa Uguja, ili na vijana walioko kule Pemba na wao waweze kupata mafunzo ya maarifa ya kujitegemea kwa kupitia JKU.

Mhe Spika, kamati yangu inakipongeza kikosi cha Mafunzo, kwa jitihada zao hasa katika ubunifu wa kujitafutia miradi ya kujiendesha wenyewe. Pia kujenga jengo lao la Makao Makuu ya Chuo cha Mafunzo hapa Unguja. Pamoja na pongezi hizo, kamati yangu imegundua kuwa kikosi kinachangamoto nyingi, ikiwemo uhaba wa vitendea kazi kama vile magari, majengo ya askari yamechakaa na kadhalika. Pia tumegundua kuwa makaazi ya wanafunzi (wafungwa) hayaridhishi hata kidogo, kwani yamepitwa na wakati.

Kwa hivyo, tunaiomba serikali kujenga upya magereza au vyuo vya mafunzo, na yatiwe vyoo vya ndani na tena viwe vya *flash,* ili kuondoa harufu mbaya kwa wanafunzi ambao wanaopelekwa katika vyuo vya mafunzo.

Mhe. Spika, pia kamati tunaomba serikali wayatenganishe makaazi ya wale wanaosubiri kuhukumiwa yaani rumande na wanaotumikia vifungo yaani wafungwa. Vile vile Mhe. Spika, tunaomba pia yatenganishwe magereza ya watoto na ya watu wazima. Pia askari wanaowahudumia watoto wavae kiraia na watoto hao pia wapatiwe elimu wakiwa wako gerezani, ili wanapotoka gerezani basi waweze kujiendeleza na elimu huku uraiani.

Mhe Spika, kamati yangu inashauri kuwepo askari wanasheria katika vyuo vya mafunzo, ili kuwasaidia wale wanaohitaji kukata rufaa. Pia kamati yangu, inaziomba Mahkama zetu kuharakisha kesi, kwani kuna baadhi ya watuhumiwa hukaa rumande hadi miaka miwili, bila ya kuhukumiwa na wao bado wakisota rumande na pengine mwisho wa kesi huambiwa hana hatia. Hii inamfanya yule aliewekwa rumande kwa muda mrefu kuwa kama na yeye amefungwa.

Mhe Spika, kamati yangu inakitaka kikosi hicho kuingiza katika bajeti ya mwaka 2012/2013 nyumba ya Mkuu wa Kikosi hicho huko Pemba, kwani wamejitahidi kujenga kwa nguvu zao, lakini kwa hatua waliyofika wanahitaji msukumo mkubwa wa serikali kupitia kwenye bajeti.

Mhe. Spika, kamati yangu imesikitishwa sana, kuonahali ya nyumba za askari wa mafunzo katika kambi ya Kangagani kule Pemba kuwa ni mbovu zinavuja kama chungio. Kwa hivyo, kamati yangu inaitaka serikali kuziezeka haraka nyumba zile, kwani mvua hizi za masika vitu vyao vinaharibika kwa kuroana na mvua. Usiku mzima wakati wa mvua wao hukesha na kuroana kwa mvua. Hali hii inawafanya kujihisi kama na wao wako chuo cha mafunzo. Kitu cha kuchekesha Mhe. Spika, wanafunzi katika magereza ya Kangagani wanalala usingizi kwa sababu hawavujiwi, lakini askari wanaokaa nao wao ndio wanaovujiwa. Mhe. Spika, hili jambo kwa kweli sio zuri sana.

Mhe Spika, kamati inakipongeza Kikosi cha Valantia kwa kuweza kujenga Jengo lao la Makao Makuu hapo Mtoni, kuondokana na tatizo la ufinyu wa nafasi waliokuwepo hapo katika Makao Makuu ya zamani Maisara. Hata hivyo, kikosi hiki kinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uchache wa askari, ukosefu mkubwa wa majengo yaliobora katika makambi yao mengine ukiacha ya Makao Makuu.

Kamati inaitaka wizara kwa makusudi kutafuta hati miliki ya makambi yake yote ya huko Pemba, lakini pia kujenga Makao Makuu ya kikosi hiki cha KVZ kule Pemba, kwani Makao Makuu waliyokuwanayo sasa hivi hayana hata hadhi ya kuitwa makao makuu. Kamati yangu imegundua kuwa kuna uhaba mkubwa wa upatikanaji wa fedha za kufanyia kazi, kitu ambacho kinazorotesha ufanisi katika kazi huko Pemba. Kamati inaagiza utaratibu wa uingizwaji wa fedha ufuatwe, kama ulivyopitishwa kwenye MTEF kwa Unguja na Pemba. Kwa upande wa Pemba kamati imekuta kuna madeni mengi, ambapo madeni hayo huendelea kulimbikizwa kwa sababu vikosi vya Pemba haviingiziwi fedha katika utaratibu uliopitishwa na MTEF.

Mhe Spika, kamati yangu inakipongeza Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa usikivu wao kwa maoni ya kamati yetu, kwani mambo mengi tunayowashauri na tunaporudi tena huwa tayari wameshayafanyia kazi. Kwa hivyo

tunawataka kuendeleza mashirikiano na kamati yetu, ili kuleta ufanisi kwa kazi zao, lakini vile vile kwa nchi yetu. Tunawapongeza kwa kukubali ushauri wa kamati, kwa kuongeza Kituo cha Zimamoto katika wilaya ya mjini, ili kusogeza karibu huduma kwa jamii, hasa ikizingatiwa kuongezeka kwa makaazi ya watu hapa Mkoa wa Mjini na Magharibi. Kamati imeridhika na jitihada za kikosi hichi kwa kuongeza magari ya kuzimia moto, pia kuimarisha majengo yake ikiwemo makao makuu.

Mhe. Spika, kamati yangu inaishauri Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kupitia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, kutiliana mikataba na Idara ya Zimamoto ili kuimarisha huduma za Zimamoto za uwanja wa ndege, kwani hivi sasa kwa uwanja wetu wa ndege unaendelea kuimarika siku hadi siku, basi ni vyema kuhakikisha kwanza tunaimarisha huduma za usalama ikiwemo huduma ya Zimamoto, ili kisijekikawa kikwazo kwa ndege kubwa zinazoongezeka kuja Zanzibar. Suala hili Mhe. Spika, ni muhimu sana kwa uchumi wetu.

Pia tunaitaka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kupitia Shirika lake la Bandari kufungua kituo japo kidogo hapo bandarini, kwani pale ndio lango letu kuu la uchumi na kuna mali na bidhaa nyingi za wafanyabiashara zinazotoka nje ya nchi hupitia pale bandarini. Kwa hivyo, tunashauri kamati tusisubiri litokee tatizo, ndio baadae tutafute ufumbuzi, kwani pale kunakuwa na mali nyingi na zenye thamani kubwa. Pia kamati yangu inaitaka wizara inayoshughulikia mipango miji kuhakikisha kwamba wanapata ushauri kutoka Idara ya Zimamoto, pale wanapotayarisha ujenzi katika mji wetu.

Mhe. Spika, kamati yangu hairidhishwi hata kidogo na utaratibu unaotumiwa wa uingizwaji wa fedha kwa vikosi kwa upande wa Pemba, kwani unasababisha kudhoofisha maendeleo ya vikosi vyetu kwa upande wa Pemba. Kamati inaitaka wizara ya Fedha kuweka *SUB-VOTE* yao maalum kwa vikosi vya SMZ kule Pemba, kwani hushirikishwa katika kuandaa *MTEF*, lakini wakati wa uingizwaji fedha utaratibu wa *MTEF* haufuatwi, na hupelekewa fedha utadhani sio taasisi ya serikali bila ya kufuata bajeti invyoelekeza. Sisi wajumbe wako wa Baraza lako hili tukufu, tunafuatilia namna wizara zinavyotekeleza utekeklezaji wa *MTEF*. Mhe. Spika, hili halina mjadala wala mbadala, kwani ni lazima litekelezwe na utaratibu wa matumizi ya fedha unatakiaw ufuatwe kama ulivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kamati ilikaa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Uongozi wa Wizara ya Fedha, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, na ndugu Ali Salum (mkandarasi) siku ya tarehe 23/12/2011 kujadili kadhia ya madai ya ujenzi wa nyumba ya mapumziko ya *(Rest House)* ya Micheweni kule Pemba. Mkandarasi alikatishwa mkataba wa ujenzi wa *Rest House* hiyo, kwa maelezo kwamba mkandarasi huyo alilipwa fedha zote za ujenzi, lakini hakukamilisha kazi. Kwa maana hiyo, jengo halikuwa na dari, sakafu na milango huku plasta ilipasuka. Hali hii ilipelekea mkandarasi huyo kusitishwa kuendelea na mkataba mwengine wa ujenzi wa uzio, nyumba ya walinzi pamoja na jiko na nyumba ya mapumziko ya Micheweni. Suala la kusitishwa lilimfanya mkandarasi huyo kuishtaki serikali kwa kufungua kesi ya madai Mahamani. Mahkama iliamua mdai na mdaiwa wakubaliane nje ya Mahkama, lakini kwa masharti kwamba mdaiwa amlipe mdai fedha anazodai milioni 104,300,000/=. Makubaliano hayo yahesabike kuwa ni maamuzi ya Mahkama, na mdai asipolipwa anachokidai anaweza kurudi tena Mahkamani.

Mhe. Spika, kamati kwa ujumla haikufurahishwa na kasoro zilizojitokeza katika mchakato mzima wa ujenzi wa *Rest House* ya Micheweni kule Pemba, pamoja na utaratibu wa malipo ya suala hilo. Hivyo, imeona iko haja ya suala hilo kushughulikiwa na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali yaani (PAC).

Mhe. Spika, naomba suala hili serikali itumie busara ya kulimaliza kwa haraka. Hayo yalikuwa ni maoni yangu binafsi. Mhe. Spika, hili tatizo sasa hivi limekuwa kubwa, linaweza likatuletea athari kubwa.

Mhe. Spika, sasa hivi naingia katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kamati katika kazi zake ilitembelea Dar es Salaam, Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufahamishwa kuwa bado Muungano unakabiliwa na changamoto kadhaa kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Spika, kwanza kuna uelewa mdogo kwa wananchi kuhusiana na Katiba za Muungano na Zanzibar. Kwa hivyo, hapa tunaiomba serikali kupitia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, sasa hivi wakati umefika kuwaelimisha wananchi hasa katiba ya Muungano na katiba ya Zanzibar, hasa ukiangalia hapo mbele tutakuwa tuna mchakato mkubwa wa katiba mpya.

2. Kamati imegundua kuwepo kwa migogoro ya kisheria, kwa kanuni na miongozo ya kufanyia kazi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Hali hiyo imepelekea kuwepo kwa vikwazo katika utekelezaji wa baadhi ya mambo.

Mfano gari zenye usaji wa Zanzibar, bado zinaendelea kuzuiliwa kutumika Tanzania Bara mpaka kwanza zisajiliwe upya, wakati gari zinazotoka Tanzania Bara, huwa hazina kikwazo chochote kutembea hapa Zanzibar, hili bado ni tatizo.

3. Mhe. Spika, vile vile hakuna sheria na kanuni zinazowabana wale wanaoshindwa kutekeleza makubaliano ya kuondosha kero za Muungano na kutowekwa muda maalum wa kuzimaliza kero hizo. Kamati imeona hili bado ni tatizo.

4. Tume ya fedha ya pamoja, imeanza kuyachambua mapato na matumizi ya Muungano. Hata hivyo, bado kuna vikwazo kadhaa vya kuliendeleza suala hilo. Tume hiyo haijapata fursa ya kuonana na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano, kumshauri ipasavyo.

   Mhe. Spika, mawaziri wa fedha wa Zanzibar na wa Bara, inaonekana bado kuna ugumu wa kukaa pamoja katika kutatua kero hii. Lakini Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo mapema, mimi nadhani sasa suala hili bora Mhe. Waziri wetu wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atulie apumzike roho yake. Nafikiri sasa hivi tunahitaji kufanya maamuzi yaliyokuwa magumu. Tunahitaji mheshimiwa sasa hivi masuala yako yote ya uchumi kwa Zanzibar, tukukabidhi mwenyewe ushughulikie bila ya kuingiliwa na mtu yeyote.
5. Mhe. Spika, kukosekana kwa ushirika wa Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hili bado ni tatizo.

6. Suala la Nishati na Uchimbaji wa Mafuta. Mhe. Spika, hili bado ni tatizo. Hapa Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo ya mshauri mwelekezi, alipokuja kuzishauri serikali mbili hapa Barazani, suala zima la utafiti na uchimbaji wa mafuta, Zanzibar hatuna chombo ambacho kitakachoweza kusimamia pale mafuta yatakapochimbwa Zanzibar. Kwa hivyo, hili bado ni tatizo na Baraza lako tukufu lilitoa maazimio kwamba itakapoundwa Serikali ya Awamu ya Saba, chombo hiki kitaundwa, lakini mpaka leo bado hakijaundwa.

7. Suala la Uvuvi wa Bahari Kuu na ajira za Wazanzibari katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bado ni tatizo ile *ratio* ya Zanzibar mpaka sasa hivi hatujaipata. Mhe. Spika, haya ni mambo ya sehemu ya kero za Muungano.

8. Vile vile Mhe. Spika, mashirikiano baina ya Serikali ya Zanzibar na taasisi za nje, bado hili limekuwa ni mgogoro.

9. Pia suala la wafanyakazi Serikali ya Muungano wanaoishi Zanzibar, kutumia huduma za Zanzibar lakini bado mapato yake hayaji Zanzibar. Mhe. Spika, hili lilielezwa vya kutosha katika kikao hiki hiki. Kwa hivyo, naomba lishughulikiwe. Lakini Mhe. Spika, kama halikushughulikiwa mimi nafikiri mwaka 2014 hauko mbali, tutaweza kufanya maamuzi ambayo hayatoleta utata katika mambo haya.

10. Mhe. Spika, marekebisho ya sheria ili kodi ya VAT ibaki Zanzibar. Bado inahitajika. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba Mhe. Waziri amesema kwamba sasa hivi anajaribu kuangalia na zaidi baada ya kufanya utafiti dunia nzima, hakuna nchi yoyote ambayo inavyombo viwili vya kodi. Tunaamini Mhe. Waziri atakapokuja katika bajeti basi utafiti wake atakuwa ameshautosheleza, na kuja kutupa maelekezo kwamba chombo cha ZRB, ndio chombo pekee ambacho kitakachoweza kukusanya mapato kwa hapa Zanzibar.

OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS - ZANZIBAR

Mhe. Spika, kamati yangu inaitaka Idara ya Utumishi Serikalini kuiruhusu Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais Pemba, kuajiri dereva na mtumishi kwa ajili ya kumhudumia Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais anapokuwepo kule Pemba, kwani watumishi hao mara zote, huazimwa katika Ofisi ya Makamo wa pili wa Rais au katika Ofisi ya Rais. Tatizo linakuja inapotokezea kuwepo viongozi hao wote kule Pemba, inammbidi Ofisa Mdhamini.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hapa anisikilize vizuri. Inapelekea Ofisa Mdhamini wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kule Pemba, wakati viongozi wote watatu wanapokuwepo kule Pemba aingie jikoni kumpikia Makamo wa Kwanza wa Rais, hili ni tatizo, nakuomba sana Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, uhakikishe kwamba unatoa kibali cha kuajiri mtumishi pamoja na dereva kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kule Pemba.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma amenisikia kwa msisitizo wangu. Mhe. Spika, kwa hivyo tunaomba suala hili lishughulikiwe kwa haraka sana. Pia tunaiomba serikali kuipatia Ofisi ya Makamu wa Kwanza gari kule Pemba, kwani pia huazima gari la Makamu wa Pili, wakati Mhe. Makamu wetu wa Kwanza wa Rais anapokuwa kule Pemba.

Vile vile tunaitaka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa masuala yote yanayohusu Pemba, basi ni lazima yapitie kwa Ofisa Mdhanmini, kwani kuna utaratibu wa baadhi ya maagizo hutoka moja kwa moja Makao Makuu Zanzibar na kwenda kwa Wakuu wa Idara, bila ya kupitia kwa Ofisa Mdhamini. Kwa hivyo, wakati mwengine Ofisa Mdhamini anapohitajiwa maelezo na kamati huwa hana majibu ya kutosha.

Mhe. Spika, kamati yangu ilipata maelezo kutoka Idara ya Mipango, Sera na Utafi. Kamati inaishauri idara kuangalia upya sheria zote zilizo chini ya Ofisi hiyo na kuangalia mapungufu yake, hasa katika masuala ya mazingira ili kuzuia uharibifu wa mazingira, ambao kwa hivi sasa umekuwa mkubwa hapa Zanzibar. Pia ni vyema kukaa pamoja na Ofisi za Halmashauri za Wilaya ili kuweka utaratibu wa ulipaji kodi ya maliasili na ile ya uhifadhi wa mazingira hasa katika yale maeneo yanayovunwa maliasili hiyo, ikiwemo mchanga, mawe, matofali ya kukata miamba, chokaa na kadhalika.

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ukiukwaji mkubwa na wa makusudi wa Sheria za mazingira. Ipo miradi mingi ya uwekezaji haifanyiwi tathmini ya mazingira ambapo hapo baadae husababisha athari kubwa za mazingira, kwani inavyotakiwa miradi yote kwanza kabla ya kupitishwa ni lazima ifanyiwe tathmini ya mazingira. Pia kuna kodi nyingi za mazingira ambazo huwa hazilipwi na hii husababisha kuwa vigumu kuweza kurekebisha kasoro hizo pale zinapotokea matatizo.

Mhe. Spika, katika wizara inayoongoza kwa kuharibu mazingira ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwani miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara huacha mashimo makubwa, ambapo ardhi hiyo huwa haiwezi kutumika tena. Pia ujenzi wa Bandari ya Mkoani uliacha mashimo makubwa ambayo hivi sasa maji ya bahari yanaingia mpaka kwenye mabonde ya mpunga. Lakini miradi yote hiyo haikulipiwa ile kodi inayohitajika ya mazingira. Pia kamati imegundua kuwa bado mifuko ya plastiki inatumika na zaidi katika masoko ya Unguja na Pemba. Kamati inaiagiza Ofisi Makamo wa Kwanza wa Rais kushirikiana na Jeshi la Polisi, kuhakikisha kwamba mifuko hiyo ya plastiki hivi sasa haitumiki tena.

Mhe. Spika, tunaipongeza Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kufanya siku maalum ya kuweza kuichoma moto misumeno ya umeme. Mhe. Spika, hii inaonesha sasa serikali imekusudia kupambana na wahalifu wanaokata miti yetu kwa kutumia misumeno ya moto na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Kamati yangu bado inashauri Idara ya Mazingira kwa kushirikiana na kamati za Mazingira kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi Mazingira sambamba na kufufua klabu za mazingira katika Skuli zote, ambapo kama mfano skuli ya Benbella ilichaguliwa kuwa ”*pilot school*” katika masuala hayo ya uhifadhi wa mazingira. Vile vile tunaomba suala la mazingira liingizwe katika Mtaala wa Masomo hapa Zanzibar, kwani imeonekana uhifadhi wa mazingira ni tatizo sugu kwetu hapa Zanzibar. Kwa hivyo, wanafunzi wakiingiziwa katika mitaala itasaidia kuweza kuepusha tatizo la uharibifu wa mazingira huko baadae.

Mhe. Spika, kamati iliingiwa na shaka kuelezwa kwamba, ni miradi 10 tu kati ya 110 ndiyo iliyopata vyeti au kibali ambayo iliyofanyiwa tathmini ya mazingira, ukitilia maanani kwamba miradi mingi inayoekezwa hapa Zanzibar, inaekezwa kwa kuharibu mazingira na mbaya zaidi inaekezwa bila ya kufanyiwa tathmini ya mazingira. Kutofuatwa kwa sheria na kutotolewa maamuzi kwa wanaoharibu mazingira ni sababu ya msingi inayokwamisha jitihada za utunzaji mazingira hapa Zanzibar. Kamati yangu inaitaka Idara ya Mazingira kuifanyia tathmini ya athari ya mazingira miradi iliyokiuka sheria za mazingira, pamoja na kuweza kutoa adhabu kwa ile miradi ambayo ilikiuka Sheria hizo za Mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira muda mwingi au kwa muda mrefu sasa imekuwa ikitoa *Stop Order* na hakuna hatua nyengine inayochukuliwa, ambayo hivi sasa hata wale wanaopewa *Stop Order* wameshazoea, kwa sababu wanajua wakiekewa *Stop Order* siku ya pili wanaendelea na kazi. Aidha, sheria hiyo haimlazimisha muwekezaji kufanya *Internal Environmental Auditing*. Hali hii humpelekea zaidi kufanya *External Environmental Auditing*. Kamati iliona kwamba kuna haja kwa sheria hiyo kufanyiwa marekebisho, ili kuiwezesha idara kuwa na nguvu zaidi za kisheria, vile vile kuhakikisha muwekezaji anatekeleza *Internal and External Environmental Auditings*.

Mhe. Spika, Kamati ilishuhudia uharibifu wa mazingira uliofanywa na Kampuni ya *MECCO* iliyokuwa ikichimba kifusi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bumbwini. Uchimbaji huo umepelekea kuwepo kwa shimo kubwa lililokuwa likihatarisha mazingira ya eneo hilo.

Kamati inaitaka Idara ya Mazingira kufuatilia uharibifu huo kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ili kuchukua 10% ya uharibifu wa mazingira, kulirejesha shimo hilo katika hali yake ya kawaida, na wananchi waweze kuitumia tena ardhi hiyo. Kamati pia inaagiza shimo hilo lifukiwe kwa kufuata taratibu za kimazingira.

Kamati vile vile ilitembelea Mkoa wa Mjini Magharibi, Kaskazini, na Kusini na kuzishuhudia hoteli nyingi na wala sitaki kuendelea kuzitaja tena ambazo zimefanya uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mhe. Spika, Kamati ilipata kutembelea katika Hoteli moja kubwa Mkoa wa Kusini Unguja Hoteli ya *Palumbo*, kwamba Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwa kweli hoteli ile aifutie kibali cha kuweza kufanya kazi ya *Restaurant* pale walipoharibu mazingira.

Mhe. Spika, hoteli hii imefanya uharibifu mkubwa wa mazingira, yaani wamejenga ukuta ndani ya bahari, wakachukua mchanga mwingi na kufukia na hivi sasa wamegeuza ndio *Restaurant*. Mhe. Spika, narejea tena tunamuomba sana Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwamba aifutie kibali hoteli ile kile cha kufanya kazi katika eneo la baharini, ambalo waliloharibu mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Kamati yangu inatoa tahadhari kwa Idara ya Mazingira kwa tangazo lililotolewa na Wizara ya Mawasiliano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumalizika muda wa bidhaa zinazotumia *Analogue* kuwa zinamaliza muda wake mwishoni mwa mwaka huu, na baadae kuanza kutumika kwa bidhaa za *Digital*. Kamati yangu inaiuliza wizara kwamba je bidhaa hizo za *Analogue* ambazo haziwezi tena kwenda kwenye *Digital* wataweza kuziangamiza kwa utaratibu gani? Kwa sababu bidhaa hizi tunaamini zipo nyingi.

Mhe. Spika, Kamati pia ilishuhudia Hoteli ya *Blue Bay* ya Kiwengwa, na *Season* ya Bwejuu zikiharibu mazingira ya fukwe kwa kuchukua mchanga ufukweni na kutengeneza fukwe za juu, na kuweka kuta kwa ajili ya kuzuia maji ya bahari yasipande juu. Kwa upande wa Hoteli ya *Season* ambayo ilijitetea kwamba mchanga huo eti wameuziwa na muwekezaji mmoja kutoka Afrika Kusini ambapo sisi Kamati tulipokwenda hatukuweza kumuona.

Mhe. Spika, tunaiomba Idara ya Mazingira ihakikishe kuwa taratibu na Sheria za Mazingira zinafuatwa.

Mhe. Spika, Kamati yangu imegundua kuna wenyeji wanaojenga nyumba karibu na fukwe na kuzikodisha kinyemela kwa wageni, ambao wengine wanaishi kinyume na sheria hapa nchini. Hali hii hupelekea kuikosesha serikali mapato na kuhatarisha usalama wa watalii pamoja na nchi. Ilielezwa kwamba *ZIPA* na Idara ya Uhamiaji wanalielewa suala hilo, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.

Kamati inaiagiza Wizara ya Fedha kupitia *ZIPA* na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Uhamiaji, kuhakikisha kwamba nyumba zote ambazo walizokodishwa wageni lazima zifuate utaratibu wa serikali, na kuweza kulipa kodi serikalini pamoja na kuhakikisha usalama wa wageni hao.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Vile vile Kamati inaipongeza Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa kazi kubwa ya kutoa elimu ya kuwatambua na kutowanyanyapaa watu wenye ulemavu, ili waweze kupata haki za msingi katika jamii.

Kamati inaisisitiza idara hii kukamilisha kazi ya kukusanya taarifa *(Database)*, ili kujua idadi kamili ya watu wenye ulemavu na serikali iweze kutoa huduma zinazohitajika kwao. Kwa upande wa Pemba; Idara bado inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi kitu ambacho kinarejesha nyuma juhudi za kuwahudumia walemavu.

Pia Kamati yangu inaitaka Bodi ya Wakandarasi kuhakikisha majengo yote wanayoyapitisha hasa ya huduma za jamii ikiwemo ya serikali, kuhakikisha kwamba yanazingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, Kamati yangu inawalaani wale wote wanaowabaka watu wenye ulemavu hasa wa akili, kwani huwaachia mateso makubwa ikiwemo mimba na maradhi bila ya kuwahudumia. Kutokana na hali hiyo, tunavitaka vyombo vya sheria kuwachukulia hatua kali wote watakaogundulikana na vitendo hivyo. Pia kamati yangu inaitaka serikali kutekeleza ahadi ya kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kwenye masuala ya ajira.

Vile vile Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora suala hili la Haki za Walemavu katika suala la ajira, basi Idara ya Utumishi Serikalini iweze kulizingatia kwa ukamilifu, kwa sababu tumegundua wakati tulipofanya utafiti Mhe. Spika, katika ajira hizi mpya zilizofanyika haikuzingatiwa hasa haki ya watu wenye ulemavu na bado wapo watu wenye ulemavu wamesoma na wanao uwezo wa kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana rafiki yangu ambaye ni swahibu wangu Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia kwako Mhe. Spika, kwa ajira zote zitakazofanyika hivi sasa kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanazingatiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ina kazi kubwa sana ya kudhibiti uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Lakini bado kuna changamoto iliopo kwa jamii nzima, kuwapa msaada wa kupambana na waingizaji na wasambazaji wa dawa za kulevya, lakini kazi hii ni kubwa sana.

Tunawashukuru Polisi Jamii wote walioamua kujitolea kuisaidia kazi hii ngumu hapa nchini kwetu. Tunaziomba taasisi nyengine zinazoshirikiana na idara hii kujitahidi, kwani tatizo hili bado ni kubwa na linaharibu vijana wetu wengi. Kamati yangu inaiomba serikali kuimarisha ulinzi bandarini na kwenye viwanja vya ndege na pia kwenye bandari bubu, ili kuzuia kuingizwa dawa za kulevya. *(Makofi)*

Tunaiomba Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kusimamia vizuri kesi zote za dawa za kulevya hapa Zanzibar na kuhakikisha zinatolewa hukumu kwa haraka. Halikadhalika Mahakama zetu kuwa waadilifu katika kuhukumu hasa kesi za dawa za kulevya pamoja na bangi. Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na vijana wenye kuanzisha *Sobber Houses*, ili kuwanusuru wale vijana waliokwisha kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya na kuwarejesha katika hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Tume ya UKIMWI inajitahidi kufanya kazi zake kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu maambukizi mapya na namna ya kujiepusha, ndio maana kasi ya maambukizi imepungua kwa kiasi fulani. Lakini kazi hiyo kubwa inafanywa kutokana na misaada ya wahisani kutoka nje. Kwa kweli hivi sasa kuna baadhi ya wahisani wameanza kupunguza misaada hiyo, hii ni hatari kubwa kwa nchi yetu, kwani dawa kubwa ya kuzuia maambukizi ni elimu kwa jamii peke yake.

Kwa hiyo, hivi sasa iko haja kwa serikali kutafuta njia mbadala ya kupatikana fedha, kwa ajili ya kuziba hilo pengo la wafadhili lililoanza kujitokeza. Mhe. Spika, kamati inazipongeza Jumuia za *ZAPHA PLUS* Unguja na Pemba kwa kazi kubwa wanazozifanya, kwani bila wao taifa lingelikuwa katika janga kubwa la maambukizi mapya ya UKIMWI. *(Makofi)*

Tunaiomba serikali kupitia Ofisi ya Rais, Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili kuisaidia *ZAPHA PLUS* Pemba, kwani wamefanikiwa kupata mashine ya kutengenezea sabuni yenye thamani karibu ya shilingi 30,000,000/= lakini imeshindwa kufanya kazi hadi leo, kwa sababu haijakamilika na zinahitajika karibu shilingi milioni 11. Mhe. Spika, mashine hii ndio inaweza kuwasaidia wananchi wale kuweza kupata ajira pamoja na fedha kwa ajili ya kuwafikia wale watu waliopata maambukizi ambao wameathirika, pia na kutoa elimu kwa ajili ya kuzuia maambukizi mapya.

Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Spika, na tumeziomba wizara zote hizi tatu ikiwemo Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Ofisi ya Rais kuangalia kuweza kuipatia *ZAPHA PLUS* kule Pemba shilingi milioni 11 na laki 9, ili ile mashine waliyoipata waweze kuitumia kwa ajili ya kupunguza kasi ya maambukizi ya maradhi ya UKIMWI.

OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS- ZANZIBAR

Mhe. Spika, Kamati ilipokea taarifa za vikao vya kero za Muungano, hii kama nilivyoeleza pale mwanzo. Mhe. Spika, Kamati inaitaka serikali kushughulikia ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Makamo wa Pili wa Rais huko Dar-es-Salaam, pia kufanya ukarabati wa nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais huko Dodoma.

Mhe. Spika, hivi sasa kwa upande wa Dar-es-Salaam Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anakaa katika nyumba ambayo si mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na nyumba ile kila siku imekuwa katika midomo. Kwa hivyo, tunaiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwa kuwa kipo kiwanja ambacho tayari kimeshapatikana, basi serikali iandae fedha kwa ajili ya kujenga nyumba hiyo.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Idara kushughulikia kumbukumbu za kuwaenzi viongozi wa Kitaifa hapa Zanzibar, kushughulikia ujenzi wa kumbukumbu ya Muasisi wetu Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume huko kijijini kwao Mwera, kwani kuendelea kuchelewa kujenga jengo hilo itakuja kusababisha kupotea baadhi ya vitu alivyokuwa akivitumia wakati wa uhai wake pamoja na kumbukumbu nyengine za historia za waasisi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na kumbukumbu za viongozi wengine waasisi wa taifa hili la Zanzibar, ambapo katika nyumba hiyo kunatakiwa kuwekwe na mambo mengine kama vile vitabu vilivyoandikwa na viongozi wetu waasisi wa taifa hili.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza *TASAF* kwa kuweza kusaidia sana wananchi kupitia Miradi ya *TASAF*. Lakini bado kuna changamoto ya kuangalia faida inayopatikana hasa katika miradi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, kwani inaonekana fedha nyingi zinatumika, lakini bado kasi ya umasikini kupungua kwake hailingani na fedha ambazo tayari zimeshatumika. Kwa hivyo, tunaiomba *TASAF* kupitia kwako Mhe. Spika, kuisaidia baadhi ya miradi ambayo imekwama majimboni.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kazi nzuri, ingawa hadi leo hawajakuwa na jengo lao. Kwa hivyo, tunawataka kuharakisha taratibu za kuweza kutafuta fedha kwa Unguja na Pemba, ili kuweza kujenga jengo na kuepukana na kukaa katika majengo ya kukodi. *(Makofi)*

Mhe Spika, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ni lazima watendaji wa Tume ya Uchaguzi hivi sasa, wapatiwe nafasi za masomo pamoja na ziara za kushiriki katika chaguzi za nchi mbali mbali, ili kujifunza kuona wenzetu wanavyo endesha chaguzi zao. *(Makofi)*

Kwa upande wa usafiri, kamati inaitaka Tume kuzikatia bima gari zake walizopatiwa na wafadhili, kwani ni gari zenye thamani kubwa. Lakini kamati ilipotembelea iligundua kwamba hazijakatiwa bima. Vile vile Kamati inashauri Tume ya Uchaguzi wakati huu wa amani na utulivu ndio wakati mzuri wa kuweza kutoa elimu hasa katika Elimu ya Uraia pamoja na Upigaji Kura kabla ya kufika wakati wa uchaguzi.

Mhe. Spika, Idara ya Maafa inafanya kazi kubwa ya kukabiliana na maafa pamoja na kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kupitia Kamati za Maafa za Wilaya. Kamati inaitaka Idara kuikamilisha Sera ya Maafa, ili kuweza kuibadilisha sheria iliyopo ambayo ina matatizo mengi kutokana na kukosekana kwa muongozo, kwa kuwa Sera bado haijakamilika na hivyo kutowezesha kuanzishwa kwa Mfuko wa Maafa, ambao utakuwa ndio kianzio cha fedha ili kuweza kusaidia wakati maafa yanapotokea.

Mhe Spika, kamati inaihimiza idara kuharakisha ujenzi wa jengo lake la Tunguu kwa Unguja na kule Pemba, ili kuweza kufanya kazi zao katika eneo hilo. Kwa kweli hapa nilikuwa nikimuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, namuomba anisikilize vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi pamoja na Kamati yangu tunasikitika sana, kwa sababu fedha zilizotoka kwa ajili ya Maafa ya Meli ya *Mv. Spice Islander I*. Kwa kweli ipo orodha ndefu mpaka hivi sasa na watu majina yao hayakutajwa, miongoni mwa majina hayo Mhe. Spika nasikitika sana kwamba wengi wa watu hao wanatoka katika Jimbo la Kwamtipura. *(Makofi)*

Kwa kweli kitu ambacho ninachosikitishwa zaidi kwamba, Tume ya Rais iliyoundwa kwa ajili ya kuchunguza tukio hili la Meli, tume hii ndiyo iliyotoa majina kwa ajili ya kulipwa mafao haya. Mhe. Spika, tume hii kazi waliyoifanya ilikuwa sio yao, kwa sababu hazi hii ilikuwa ni ya Idara ya Maafa, kwa sababu kama wangechukua orodha ya Idara ya Maafa, basi mimi naamini kwamba watu wote wangelikuwa wameshapatiwa fedha hizo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wakati atakapokuja hapa, basi anieleze kwa kina, kwa nini kuna watu wengi ambao wamekumbwa na maafa ambao orodha yao ipo kwa masheha na wala hawakupatiwa fedha hizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, aje na jawabu ya kutosha vyenginevyo nisije nikaanza utaratibu wa kuiundia Tume, Tume ya Rais ambapo orodha yao ndiyo iliyokuwa na majina, ambayo majina hayo mengine tuna wasiwasi sijui kama walikuwemo katika hiyo Tume ya Maafa. *(Makofi)*

Sasa hili Mhe. Spika, nilikuwa nikilizungumza kwa uchungu, kwa sababu humu kuna orodha ndefu ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura ambao hawakuweza kupata fedha hizo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha zaidi kuna mwananchi wangu ambaye katika familia yake kuna watu 9 wote wamefariki katika nyumba yake. Kwa kweli katika orodha ni watu wawili tu ndio waliojitokeza katika orodha ya kulipwa mafao hayo. Vile vile kuna mwengine yeye katika familia yake kuna watu 6 ambao wamefariki na majina yao mawili tu ndio yamejitokeza, tena yamejitokeza wakalipwe fedha zile Pemba wakati mzee wao yupo Unguja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala hili namuomba Mhe. Waziri alichukulie hatua za haraka tena za dharura, kwa sababu isijekuwa haya maafa yakaja kusababisha na maafa mengine pia ya watu kukosa haki zao.

Mhe. Spika, namalizia Idara ya Uchapaji, Kamati yangu inaitaka serikali kuitekeleza ile ahadi yake ya kukihamisha Kiwanda cha Upigaji Chapa, kilichopo Kwa Abass Hussein, kwani kuendelea kuwepo pale ni kuwasumbua wafanyakazi, kwa sababu kinaendelea kuingia maji hasa wakati wa mvua kubwa zinaponyesha.

Vile vile kuharibika kwa nyaraka pamoja na mitambo iliyopo pale. Mhe. Spika, tunaiomba sana serikali kuharakisha taratibu za kuhamisha kiwanda kile pale.

Mwisho kabisa namalizia Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora anisikilize kwa makini. Mhe. Spika, kamati yangu hairidhiki na utaratibu wa mfumo unaotumika hivi sasa wa Baraza kuendeshwa kama Idara ya Serikali, wakati umefika Katiba ya Zanzibar ifuatwe kama inavyoagiza kifungu 5A. (1) kinavyoitaka nchi yetu kuendeshwa kwa mfumo wa mgawanyo wa Madaraka ikiwa ni Serikali, Baraza la Wawakilishi pamoja na Mahakama. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naamini Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria wananisikiliza na naamini wanafahamu ninachokikusudia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza ni chombo kilichopo kikatiba na ndio Ngome ya Wananchi, ambapo matakwa ya wananchi huwakilishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, ni lazima Waheshimiwa wapatiwe huduma bora ikiwemo, mafunzo, ofisi za kufanyia kazi Majimboni mwao, ili wananchi wapate pahala pa kupeleka mahitaji kupitia Wawakilishi wao. Pia wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi na wao wanahitaji maslahi maalum, hasa kutokana na mazingira magumu wanayofanyia kazi kwa kutoa huduma zote zinazohitajika kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, ikiwemo kuwasaidia masuala ya kisheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ofisi yako au sisi Waheshimiwa hivi sasa inabidi tutunge Sheria ya Uendeshaji wa Baraza kama Katiba ya Zanzibar kifungu 77 (2) kinavyoelekeza, ili kuweza kuwa na fursa ya kujipangia mipango yetu kama serikali wanavyojipangia mipango yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wajumbe wako ni vizuri wakapata nafasi za kujifunza uendeshaji wa shughuli za Mabunge katika nchi za Jumuia ya Madola, ili kuwajengea uwezo wa kuisimamia serikali kikamilifu na kupambana na vitendo vya rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na utumiaji mbaya wa madaraka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Kamati yangu haijaridhika kabisa na kitendo cha kuwanyima haki yao ya msingi ya nyongeza za mishahara watumishi wa Baraza la Wawakilishi, kwani mishahara wanayoipata imeamuliwa na chombo kilichokuwepo kisheria, Tume ya Utumishi ya Baraza kutokana na mazingira maalum ya kazi zao.

Kwa hiyo kamati inaiomba serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambao watumishi hawa wa Baraza wako chini yako, kuzingatiwa na tunamshukuru Mhe. Rais wetu ametamka kwamba wale wote ambao waliokuwa na matatizo katika nyongeza za mishahara basi serikali itawashughulikia. Mhe. Spika, ninamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuwa ana-*smiling face* pale, basi naamini kwa sababu yupo karibu na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais watalishughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa sasa nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini na utulivu. Vile vile napenda kukushukuru wewe mwenyewe binafsi Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuwasilisha huu muhtasari mfupi wa maelezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kwa kuwasilisha muhtasari huo. Kwa kweli urefu na ufupi inategemea na namna ya kamati yenyewe ilivyo. Sasa kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ufupi wake ni urefu kwa kamati nyengine. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Mwenyekiti ametumia muda wa saa moja na dakika tano hivi kuwasilisha muhtasari huo. Ninao Waheshimiwa Wajumbe saba, nadhani wanatosha kabisa, ili kuweza kutoa mchango na hatimae tuwaite Waheshimiwa Mawaziri na hatimae tuweze.

Kwa ujumla Mhe. Mwanasheria Mkuu baada ya kutoa hoja tumekubaliana kwamba tunaendelea mpaka shughuli hii imalizike. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kama ilivyo kawaida nafasi ya kwanza inakwenda kwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadaye Mhe. Ismail Jussa Ladhu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuchangia nikiwa mtu wa mwanzo. Kwanza nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kutupa taarifa hii, ambayo ni fupi sana na imeiwasilisha kwa utaalamu, nampa pongezi sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niende mbio na wewe utashangaa kwa jinsi nitakavyochangia kwa *style* ya aina yake. Kwanza Mhe.Mwenyekiti alisema kumtetea mwananchi ambaye ni mkandarasi ambaye alikuwa akijenga ukuta ambao uko Micheweni, kwa kweli na mimi namuunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala hili ni la kusikitisha kwa sababu ndugu yetu huyo alifika pahala mpaka kwenda kuvunja kioo cha gari ya Katibu kwa ajili ya kutafuta haki yake. Mkandarasi huyo alikwenda Mahakamani na kushinda, lakini serikali bado haikumtendea haki, basi na yeye kuamua kufanya hivyo. Mhe. Spika, anaona sasa njia ambayo ni madhubuti ya kuweza kutetea haki yake afanye vitu kama hivyo ambavyo havistahiki.
Lakini Mhe. Spika, inakuwaje serikali kuwa mpaka leo mkandarasi huyo kupewa haki yake ambaye anaitwa *Alhajj Construction* kwa nini asipewe Mhe. Spika. Kwa kweli ni vitu ambavyo tunawajibika sisi kama ni Wawakilishi wa *backbenchers* kuweza kumtetea kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunavyo vielelezo na kama ukiviangalia na kama itaundwa Tume ya Kamati Teule kwa kutumia kifungu cha 117 ukurasa wa 88, basi Mhe. Spika utaona mambo ambayo ni utumbo mtupu uliofanywa, kwa sababu zimelipwa fedha lakini mkandarasi huyo fedha zile hazikumfika, yaani anafanyiwa *fake*, mhuri uliotumika pia ni *fake* kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Kutokana na hali hiyo, kwa nini tunyamaze kimya, kwa nini tusimsaidie, kwa sababu anafika pahala kuleta barua kumtishia Mhe. Waziri wetu, kwa nini tusimlinde.

Lakini itafika pahala Mhe. Spika si vizuri, tumlipe haki yake, kwa sababu huyu mtu amefanya kazi na anadaiwa kwenye maduka, kwa hiyo tumlinde na tumpe haki yake na mimi najua kwamba Wizara ya Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wanasema wameshalipa. Kwa kweli fedha zilizolipwa na Wizara ya Fedha hazikumfika yeye, sasa kazi yenu kuzifuatilia hizi fedha za serikali zimekwenda wapi, huyu mtu tumlipe haki yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sana hilo gazeti la Zanzibar Leo liandike mambo kama haya ya kumtetea mwananchi, yaani tunaomba wapewe kipaumbele kabisa, kwa sababu tunatetea wananchi na sio waandikwe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amechelewa kufika Barazani kwa ajili ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika Baraza letu hili, kwa sababu tayari Mhe. Mwenyekiti amelizungumzia hapa, nadhani ni vyema Mhe. Spika tuwatendee haki wafanyakazi wetu, tuwapatie kama tunavyosema kwamba na wao wanastahiki nyongeza waweze kupewa.

Vile vile nisifu kuhusu hizi Halmashauri zetu na hasa katika Baraza la Manispaa. Mhe. Spika, *Round about* nzuri imetengenezwa, lakini fedha zake hatujui zimepatikana wapi. Kwa hivyo, tunaomba majibu mazuri fedha zile zimepatikana wapi, kwa sababu watu wanauliza tu fedha zile zimepatikana wapi, kwa sababu hakuna sehemu inayoonesha kuwa fedha zile zilikopatikana.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 178 kuhusu makusanyo ya mapato ya bustani ile ya Mji Mkongwe na nilisema Manispaa. Kwa kweli fedha hizi mpaka leo hii hazitambulikani ziko wapi, na imeamuriwa na Mhe. Rais aliyefungua bustani ile kwamba kupatikane *Account* ambayo iwe *separate* kabisa, ambayo isijumuishe masuala ya Mji Mkongwe wala Manispaa. Lakini hatimae tumeambiwa imekwenda katika upande mmoja.
Kwa hivyo, Mhe. Spika tunaomba mpaka leo hii ni kiasi gani ambacho kimekusanywa pale, na fedha hizo zilizokusanywa zimepelekwa wapi na kwa nini ikafanya hivyo? Kwa maana hiyo, ile kauli ya Mhe. Rais haikuwa sahihi na imefanyika mtu anavyotaka mwenyewe. Sasa hayo ni mambo ambayo Mhe. Spika tunawajibika kuweza kuisaidia.

Vile vile niisifu Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kaskazini 'B', hususan Katibu wangu wa Halmashauri amefanya kazi vizuri sana, na hivi sasa pale anatuletea jengo la kisasa ambalo litakuwa na ghorofa. Kwa kweli Mhe. Spika huyo ni mtu mzuri sana, anajitahidi sana katika mambo ya kudhibiti fedha za umma za wavuja jasho, yaani anaonesha vile vitu vya kusaidia kwenye majimbo na kadhalika. *(Makofi)*

Sasa nizungumzie kuhusu Vikosi vyetu vya SMZ. Mhe. Spika, mpaka leo vikosi vyengine vinakatwa mambo ya *football* imehusu nini Mhe. Spika, wapewe haki zao na wala wasikate. Kwa kweli mshahara wenyewe mdogo na halafu leo wanakatwa, kwa nini tuwaonee kama hivyo kuhusu mambo ya timu, masuala ya timu yanajitegemea wenyewe, na tofauti na mtu na mshahara wake, kwa sababu wengine hawana *interest* za mambo ya *football*, lakini wanakatwa mshahara. Mhe. Spika, naomba kabisa hawa watu wapewe haki zao, ili waweze kujikimu mambo yao, kwa sababu mshahara wenyewe mdogo na halafu unakwenda kuukata. Kwa maana hiyo, tunaomba sana Mhe. Spika, fedha hizo hazistahiki kukatwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na kwamba Mhe. Mwenyekiti wangu ameisifu Idara ya Msajili wa Kadi za Utambulisho, lakini mimi simpingi isipokuwa sikubaliani nacho. Mhe. Spika, vitambulisho leo anakwenda kupewa Mkenya, Mburundi pamoja na wengine kwa kweli udhibiti hakuna, ina maana tuko *open* kabisa, nadhani ni vyema tukalifikiria suala hili. Mhe. Spika nawaomba sana waandishi wa habari wajue hilo suala mimi tokea nilivyosema sijawahi kulisikia kwenye magazeti hata siku moja na mwenyewe waziri yupo hawaandiki mambo haya, mtu wa Kitope anakosa kitambulisho anakwenda kupata Mkenya kwa sababu gani ni mambo ya kusikitisha na mpaka leo hakuna sheria iliyochukuliwa na wala hawajakamatwa tunafanya kazi gani, tunamnyima haki yake Mzanzibari mambo mengine yanaudhi hebu tuanalieni jamanai, haki yake kitambulisho lakini anakwenda kupewa Mkenye mpaka leo wapo kibao wana vitambulisho.

Lakini kwa bahati mbaya hawajakamatwa wako hivi hivi mitaani wanatembea na wameshanunua ardhi kesho nakwenda kuonyeshwa ardhi ambayo amenunua Mkenya na kitambulisho chake hichi hapa, kesho tayari nakwenda kuonyeshwa mimi nasema hili suala, nyinyi mawaziri na msifanye kazi mimi nitapambambana nao na wapo *back bencher* watanisaidia hiyo nasema wazi Mheshimiwa *(Makofi).*

Mhe. Spika, kama ulivyosema kuwa unataka letu tuipitishe hii kwa hivyo mimi nakwenda haraka haraka Mhe. Spike, nistahamilie lakini ndio kama unavyojua sisi tunataka tukusaidie ripoti hii ipite kwa utaalam kabisa.

Mhe. Spika, sasa nakwenda kwenye Halmashauri zetu hivi karibuni halmashauri zile za Pemba kuna miradi hii, unajua Mheshimiwa Spika, tumeziruhusu Halmashauri hizi kuwa na *by law* sheria ndogo ndogo sasa zimepita pale tukaziruhusu basi tusizitie mikono tuwaachia wao wenyewe wawe na mbinu za kutafuta *project* za kuweza kujiendesha na wananchi wao, lakini tunawaingiza tunawaambia hao wanaokuja ni matapeli. Matapeli nani jamani tusitumie lugha hizi mtu ambae ameshakubaliana nae kwa misingi ambayo watawekeyana wao wenyewe kwa sheria basi tusiingie pale kutia midomo wakati serikali yenyewe haitoi pesa wala halmashauri hazitoi, sasa hiyo ni moja tunaomba kama tunawakubalia *by law* zitungwe basi naomba kabisa *by law* tuwaachie wenyewe watunge sheria zao ambazo hazikiuki wala hazivunji katiba.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba tena huyu kijana *AL-HAL CONTRACTOR* alipwe haki yake tusimdhalilishe kijana mdogo masikini, dhaifu masikini ukimuona anakwenda njiani anasema kwa nini serikali isimjali kumpa pesa zake, nilisema neno kama hili leo wakati wa afya mtu ambae vile vile na yeye amefukuzwa kazi sasa hivi mahakamani kashinda haki yake tunampiga mpira anaambiwa aende kwa Mwanasheria, mara nenda kwa Haji Omar Kheri tunakwenda wapi nimesahamu Mhe. Waziri naomba radhi Mheshimiwa.

Mhe. Spika, ninaomba radhi kwa kumtaja Mheshimiwa wangu kwa jina lake lakini ni Mhe. Waziri sasa nimesema hilo nitaelekea kwa mwanasheria wangu kwa kuwa ni mwalimu wangu nitakwenda ananijua Mheshimiwa wangu nae anaelekea kwenda hija hatoniangusha, na Mheshimiwa waziri niliyemuita waziri ameshakwenda hija sasa nione huyu kijana wampige mpira wasimlipe pesa zake.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono asilimia mia kwa mia ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa mara nyengine tena leo kupata nafasi ya kuchangia kamati hii nzito kamati ya kusimamiza Ofisi za Viongozi wa Kitaifa, nitajitahidi nizungumze kwa ufupi sana ili na wenzangu wapate nafasi.

Mhe. Spika, mimi moja kwa moja naomba niende katika ukurasa wa 190 wa ripoti katika eneo lililozungumziwa mambo yanayoitwa kero za Muungano ambayo yanashughulikiwa na Ofisi za Makamo wa pili wa Rais hapa

langu mimi dogo tu, katika orodha ya mambo yaliyotajwa hapa pametajwa suala la Nishati na uchimbaji wa mafuta. Niliwahi kutahadharisha kwamba serikali hili suala haijatuwekea wazi kwamba Makamo wa Pili katika hotuba yake mwaka jana alitwambia kwamba suala hili haliingizwi katika kero za Muungano badala yake litashughulikiwa na viongozi wa juu ili kulipatia ufumbuzi.

Lakini baadae kuna majibu yaliyowahi kutolewa na Mhe. Waziri wa Nchi na Makamo wa Pili wa Rais ambayo inalingana na haya yaliyoelezwa hapa sasa, kwamba suala hili limeingizwa katika orodha ya kero za muungano sasa sijui utatuzi wake utakwenda kwa utaratibu upi, lakini nilichotaka kukisema mimi hapo kwa kifupi tu katika kujadili ripoti hii ni kuikumbusha serikali kwamba kikao cha bajeti kinakuja mwaka jana baada ya kujadili kwa urefu sana suala hilo wakati wa bajeti , serikali ilituomba tuwape muda tukawauliza wao tuwape muda gani ili kupata majibu kwa serikali ya muungano na kwamba baada ya hapo kama majibu hatukuridhika tuchukue hatua ya kutekeleza yale maadhimio ya baraza tuliyopitisha mwezi April, mwaka 2009.

Serikali ikaomba mwaka mmoja kwa hivyo nakumbusha tu Mhe. Spika, kwamba mwaka mmoja tokea kipindi cha bajeti unamalizika bajeti inayokuja, kwa hivyo kipindi cha bajeti inayokuja katika suala hili tunahitaji majibu tena sio kwamba inaendelea kushughulikiwa kwamba serikali ya muungano imechukua hatua gani, kama haichukui hatua sasa ndio yale tuliyopendekeza mwaka jana katika bajeti serikali ianze kuchukua hatua za kuyatekeleza ikiwemo kuunda mamlaka ya Zanzibar kusimamia kutoa leseni kwa makampuni na hatimae kutunga sheria yetu ya utungaji wa mafuta Zanzibar ambayo rasimu yake ipo tayari zamani sana. Kwa hivyo nilitaka kulikumbusha tu hilo Mhe. Spika, kwamba ofisi ya makamo wa pili itambue na serikali kwa ujumla kwamba ina deni hilo, iliomba mwaka mmoja na mwaka mmoja sio mwingi tuliutoa kwa muda mrefu sasa hivi unamalizika ikifika bajeti tupate jibu la utekelezaji wa suala hili.

La pili Mhe. Spika, niende hapo hapo kwenye ukurasa wa 192 katika Ofisi ya makamo wa Kwanza wa Rais hapa ripoti ya kamati imeelezea na sina haja ya kunukuu chochote, orodha ya hoteli mbali mbali ambazo zimekiuka sheria ya mazingira. Mimi hapo langu moja tu Mhe. Spika, naiomba serikali ichukue hatua kama sheria inakataza kujenga katika maeneo ya fukwe na mwenye hoteli kajenga katika fukwe au mtu mwengine yoyote dawa ni kuvunja pale palipojengwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama sheria zinatungwa na tukaweka adhabu kwa makosa Fulani lakini halafu baadae adhabu hazitolewi hakuna *tension* kwa uvunjaji wa sheria hakuna mtu yoyote atakayeona umuhimu wa kufuata sheria hiyo katika nchi, kwa hivyo nadhani Mhe. Spika, umuhimu wa kuvitunza visiwa vyetu ni mkubwa zaidi kuliko kutunza hoteli. Sasa kama masuala hayo yanapelekea mmong'onyoko wa ardhi na mambo mengine yanayohusiana na uharibifu wa mazingira, mimi nadhani kama kuna hotali ambazo zimekiuka kauli ya serikali basi serikali ichukue hatua na kuonyesha kwamba serikali ina meno. Ikionekana serikali haina meno Mhe. Spika, hakuna mtu atakayefuata sheria. Kwa hivyo nilikuwa naomba hili tusije tukafika pahali kama alivyosema Mhe. Mshimba mara nyingi ikaambiwa serikali imetiwa mfukoni haya hayakubaliki.

Mhe. Spika, la tatu kwa haraka haraka niende katika hili lililozungumzwa katika hotuba ya Mwenyekiti wa kamati ambayo bahati mbaya katika ripoti halimo, sula la wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi nao kupewa nyongeza yao ya mishahara. Mhe. Spika, tunakubaliana sote kwamba vyombo vitatu hivi kila kimoja kina mamlaka yake na katiba yetu inatambua katika ibara ya 5a mgawanyo wa madaraka, lakini pia katiba ikaweka Tume za utumishi mbali mbali kila mmoja kwa maeneo yake ambayo ndio yanayosimamiwa na ile kamisheni ya utumishi wa umma.

Mhe. Spika, sasa kama tumeamua kuongeza mishahara basi inawahusu wote na kwa chombo kama hiki kwasababu ni muhimili mmoja katika mihimili mitatu basi kina maamuzi yake, sasa kama ilipitishwa na tume ya utumishi ya baraza la Wawakilishi kama kumekuja nyongeza baso inastahiki nyongeza hiyo. Namuomba Mhe. Spika, hili liheshimiwa na lifuatwe.

La mwisho Mhe. Spika, naomba kwenda katika ukurasa wa 181 wa ripoti ya kamati, nimeshtushwa mno lakini kwanza nataka niipongeze kamati kwa sababu imetoa maelezo kwa urefu katika suala hili la *rest house* ya Micheweni, nimeshtusha na maelezo yaliyokuwepo hapa Mhe. Spika, na kuna baadhi ya maeneo mengine hata nimeshindwa kufahamu juu ya kipimo halisi cha fedha kilichotolewa.

Kwa sababu kuna *paragraph* ya pili hapa kutoka chini imejumuisha malipo yote na tarehe zake mbali mbali ilizokuwa zimetolewa yanajumuisha 135,094,750/= lakini na huku juu katika *paragraph* ya 4 kutoka juu ya ukurasa huu pametajwa vile vile pana malipo ya milioni 60, sasa hizi tarehe za malipo huku chini hazionekani ni kama vile malipo ya ziada haya zaidi ya ile 135 milioni na haya ni milioni sitini, kuna milioni arubaini, milioni kumi na milioni kumi sasa nilikuwa naomba mwenyekiti wa kamati akija atupe maelezo kusudi kwamba je haya

ni malipo ya ziada kwa hivyo ukijumlisha na huku chini itakuwa ni 195 milioni au ile 135 milioni zinajumuisha na milioni 60 za juu,

Lakini Mhe. Spika, nimestushwa na maelezo haya ambayo yapo kwenye *paragraph* hii na kwa uzito wake naomba niisome. Inasema *" Ndugu Ali Salim aliyejieleza kwamba yeye ndio Mkurugenzi muendeshaji wa kampuni ya Al-hal Constraction* kampuni ya Zanzibar iliyohusika na ujenzi wa *rest house* ya Micheweni alisema hayatambui malipo yote yaliyofanywa na Wizara ya Fedha kwa kampuni hiyo na kufahamisha kwamba malipo hayo yalifanywa kama ni njama za kumfaidisha Katibu Mkuu Wizara ya Fedha".

Narudia tena Mhe. Spika njama za kumfaidisha katibu Mkuu Wizara ya Fedha na marehemu Ali Hamad Ali Kimti aliyekuwa akitambuliwa na Wizara ya Fedha kwamba yeye ndiye mkandarasi wa kulipwa fedha za ujenzi wa *rest house* kwa niaba ya kampuni hiyo, alibainisha kuwa wakati hayo yakitokea yeye alikuwa nje ya nchi. Sasa katika maelezo ya utetezi humu yeye ameonyesha kwamba huyu sio mtu aliyepaswa kulipwa lakini baadae kamati imebaini katika ukurasa wa 132.

Kwamba huyu ndugu Ali Hamad Ali kama Mkurugenzi mtendaji wa kampuni ya Al-hal alihusika kuweka saini katika mikataba yote miwili na ndiye anayetambuliwa na Wizara ya Fedha katika suala la malipo. Kwa hivyo kuna mkanganyiko mkubwa Mhe. Spika, katika suala hili na hili linaashiria nafasi nyengine Mhe. Spika, ambayo inaonyesha matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mara nyingi tunaonekana wabaya lakini kusema kweli haya mambo yanachosha tunagemewa wawakilishi wa wananchi tunapokuja hapa tukasema basi watendaji wakuu wa mawizara basi wajifunze kutokana na haya, yasijirejee lakini kila siku tunavumbuliwa mapya mapya hizi fedha zinatoka kwa wavuja jasho wa nchi hii. Kwa hivyo Mhe. Spika, hapa katika hotuba yake Mhe. Mwenyekiti kapendekeza kwamba huyu mtu kwanza alipe kwa sababu fedha alizolipwa hazikumfikia yeye, lakini pia pamezungumzwa kukiukwa taratibu kwa sababu watu wawili tofauti au afisi mbili tofauti zinalipa kuwa ni mmoja, Wizara ya Fedha na huku Ofisi ya Mkuu inalipa kwa wakati wake nani walihusika kula fedha hizi. Tuambiwe kama kuna wakubwa tuambiwe hapa kama ni Katibu Mkuu kama hawa hapa tuambiwa ili tuchukue hatua, na kama ulivyosema sipendekezi kuundwa kamati teule maana zitakuwa nyingi na mwisho tutachoka na kamati teule.

Lakini kamati imependekeza kwamba kamati ya *PAC* ikachunguze suala hili kwa undani hili mimi Mhe. Spika, naliunga mkono na nasema hii itakuwa ndio dawa, ikiwa mawaziri ikiwa Makatibu Wakuu, ikiwa Manaibu Makatibu Wakuu, ikiwa Wakuu wa Mikoa yoyote yule hata ikiwa sisi wawakilishi yoyote atakayekula fedha za walipa kodi, maskini wa nchi hii hatua zifuate mkondo wake. Naliunga mkono pendekezo hili Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nasema naunga mkono ripoti ya kamati mia kwa mia kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Mji Mkongwe. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii niweze kuzungumza machache kwa kutoa mchango wangu katika kamati hii, mimi naomba nianze kuchangia katika ukurasa wa 172 ambao unaelezea ofisi ya faragha ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, katika Ofisi hii ya Mhe. Rais naomba ninukuu kidogo. "*Iliendelea na kuimarisha shughuli za Mhe. Rais kama kuratibu safari za nje na ndani ya nchi za Mhe. Rais kufuatilia maagizo na ahadi za Mhe. Rais".*

Mhe. Spika, mimi nilitaka nianzie hapa maagizo na ahadi za Mhe. Rais mimi nina masikitiko makubwa kwa kumuona Mhe. Rais anakuagiza na yeye ni kiongozi wa nchi ndio mkuu kabisa ambae tunamtegemea katika nchi hii, halafu tukaona agizo alilolitoa halifuatwi, alitoa agizo la kusema ng'ombe wasionekane wanadhurura katika mji kwa sababu wanahatarisha mambo mbali mbali, hivyo agizo hilo tunaona halijachukuliwa hatua badi ng'ombe wanaendelea kuzurura mpaka hivi sasa. Kwa hivyo hili linatukatisha tamaa hata sisi wajumbe wa Baraza la wawakilishi kuona pengine haya na sisi tunayoyazungumza humu ndani yanaweza yasichukuliwe hatua kwa sababu sisi ni wadogo kuliko Mhe. Rais, sasa iwapo Mhe. Rais katoa agizo halijafuatwa je sisi waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tunaomba hili liweze kuchukuliwa hatua ili liweze kumpa hadhi rais wetu na kumjenga mapenzi makubwa kwa wananchi wake.

Mhe. Spika, sambamba na hilo pia na ahadi anazotoa Mhe. Rais hili nalo pia lingefuatiliwa kwa umakini zinazopotolewa ahadi na rais zikaweza kutekelezwa ahadi zile kwa wakati muafaka, ili ziweze kumjengea sifa na mapenzi mazuri kwa wananchi wake ukiangalia viongozi waliopita wapo ambao wamestaafu na bado ahadi zipo pale pale hazijalipwa hili ni la masikitiko makubwa. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri hili la ahadi za rais kuweza kulifuatilia kwa makini ili viongozi wetu wanapotoa ahadi basi liweze kufuatiliwa.

Mhe. Spika, niende katika tawala za mikoa hapa naipongeza sana serikali kwanza kwa kuifanyia matengenezo nyumba ya Mkuu wa Mkoa, lakini pia kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Kaskazini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa niende katika vikosi vyetu Mhe. Spika, vikosi vyetu vina hali ngumu na matatizo mengi kweli hatuwezi kutatua matatizo yote kwa wakati mmoja lakini tuangalie vikosi hivi ni vyetu na ndio vya ndani ya nchi yetu, vina hadhi kubwa kwa hivyo lazima tuweze kuonyesha hadhi ile katika vikosi vyetu hivi.

Mhe. Spika, nianze na kikosi cha Chuo cha Mafunzo ambacho tulikitembelea na tukafika mpaka kisiwani Pemba tulikuta hali ngumu sana ya askari wetu hawa, ukiangalia makazi hata Ofisi wanazofanyiwa kazi, tulipowauliza wale wanafunzi ambao wamefungwa basi wao wenyewe walithibitisha wakasema sisi hatuwezi kusema sana kwa sababu ni wafungwa pengine hatuna haki ya kupata mahitaji muhimu. Lakini tunahisi na hawa askari wanaotulinda na wao ni wafungwa wenzetu hili lilituskitisha sana Mhe. Spika, kwa hivyo nimuombe Mhe. Rais kuweza kuvipa hadhi vikiso vyetu ili viendane na wakati.

Mhe. Spika, sambamba na hilo Kikosi cha KMKM ni kikosi ambacho nacho kinafanya kazi kubwa ngumu na muhimu, lakini kinakosa vitendea kazi hivyo hatuwezi kukamata wahalifu wa baharini wakati hakuna vyombo kama bodi za kuweza kufanya kazi vizuri. Lazima tuwapatie vitendea kazi ili na wao waweze kufanya kazi vizuri lakini pia makazi yao, Ofisi zao walizonazo na wao mbovu ushahidi ninao maana jirani zangu Mkokotoni ni KMKM ambapo ofisi yao inavuja, sisi tunaomba mvua ije ili tuneemeke lakini wao wanaomba mvua isije ili wasivujiwe.

Mhe. Spika, kwa hakika vikosi vyote vinahitaji matunzo na jicho la huruma hasa ukizingatia bajeti wanayopewa inakuwa ni ndogo kuliko watu wote na wao ni vikosi vyengine ambavyo vinaweza kujitegemea kama JKU wanajitahidi kulima, magereza wanajitahidi kulima basi tuweze kuvionea imani na kuvipatia nyongeza ya bajeti.

Mhe. Spika, niende katika Baraza la Manispaa hapa kidogo nilita kidogo tu nizungumzie kuhusu usafi wa mji wetu, baraza hili bado lina jukumu kubwa la kusimamia usafi wa mji hakuna lisilowezekana na wenzetu wanafikia mafanikio makubwa si kwa miujiza, lakini wanaweza kuzisimamia sheria zao ambazo wamezitunga na zikaweza kufanya kazi na hatimae wakaweza kufanikiwa.

Hivyo utaikuta miji yao mizuri inapendeza na sisi hili tukilisimamia vizuri na tukisimamia sheria zetu vizuri tunaweza kufikia mafanikio mazuri, kwa sababu hivi sasa tu ukiangalia serikali imejitahidi kusema sema juu ya mfuko basi tunaona hata ile idadi ya mifuko mabarabarani imepungua. Hivyo Mhe. Waziri ajitahidi na kutafuta vitendea kazi ili basi tunapopita katika mitaa tuweze kuona *dustbin* zipo na mwenyewe mtu aone aibu kutupa takataka ovyo na aweze kudhidhibiti mahala pazuri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi pamoja na wananchi pamoja na wanawake wa Mkoa wa Kaskazini, naunga mkono hoja ripoti hii ya kamati naomba radi kidogo Mhe. Spika, sijamalizia.

Jengine ni Wizara hii pamoja na kazi nyengine walizokuwa nazo lakini ni pamoja na kuwaenzi viongozi wetu wakuu, hili mimi nilitaka nimuombe Mhe. Waziri kuwaenzi viongozi wetu wakuu wapo ambao tayari wameshastaafu, lakini wapo wengine ambao wameshafika mbele ya haki lakini kuna hotuba zao nzuri mwanana ambazo zinaweza kutuendesha katika siku hizi na siku za baadae, bado zinaenda na wakati tulipenda kuzisikia hotuba hizo za viongozi wetu hasa za Mhe. Abeid Amani Karume ambae hotuba zake zilikuwa zinakwenda kwa mtazamo wa mbele zaidi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono ripoti ya kamati hii ya viongozi wakuu wa kitaifa kwa asilimia mia moja. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi naomba nichukue nafasi hii nitoe mchango wangu mfupi juu ya kamati hii ambayo Mhe. Hamza Hassan Juma ameitoa hivi punde, mimi nianze moja kwa moja kwenye ukurasa wa 172 kwenye kitengo cha usalama wa Serikali *GSO*. Kwa hakika wananchi wengi hawajui malengo hasa ya kitengo hiki na hata mimi mwenyewe nahitaji kuelimishwa juu ya malengo, madhumuni na kazi za kitengo hiki, Mhe. Mwenyekiti wa kamati amesema hapa kuna baadhi ya wafanyakazi hawafanyi ukaguzi na akapendekeza kwamba kuna baadhi ya hata makatibu Makuu na watu wengine wanahitaji kufanyiwa ukaguzi.

Sasa mimi nahitaji taaluma pengine Mwenyekiti anaweza kunielimisha au pengine hata Waziri anaweza kunielimisha, nimekuta sehemu mbili za waajiri wetu hapa Zanzibar, moja inasema kwamba huyu ni mwana CUF kindaki ndaki aajiriwe na aliajiriwa, na moja ikasema huyu ni Mwana CCM aajiriwe kwa hivyo nahitaji

nielimishwe hii ndio *verting* hasa au nini. Kuambiwa huyu ni CUF aajiriwa au huyu ni CCM *brass band* aajiriwe ndio *verting* hasa iliyokusudiwa na kama hiyo ndio basi kitengo kinafanya kazi vizuri na kiendelee kufanya kazi, na kama hiyo sio basi tuaambiwe nini hasa kazi ya *GSO* kwa madhumuni ya serikali yetu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 188 una madeni ya JKU hawa wanadaiwa Pemba Shs. 25,229,000/= lakini wanadai Sh. 78, 000,000/= ndani ya serikali hii ikiongozwa na Wizara ya Fedha wanadaiwa na JKU, kama watalipwa JKU maana yake watalipa deni baadae watabakia na bakaa Shs. 52.8 milioni. Mhe. Spika, na Mhe. Hamza Hassan Juma waombe mawaziri wako walipe deni hili, haiwezekani kwamba JKU mnawatuma na mnawatumia na kuwahangaisha halafu hamuwalipi. Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, wa kamati hii awaambie Waziri wa Fedha na Mawaziri wengine walipe deni ili kesho kutwa tuwapitishie bajeti yao hatuwezi kuwapitisha fedha wakati mnawanyonya watoto wetu JKU.

Jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti, amenishawishi kwamba tuongeze ule mradi wa mboga mboga kule kwa Pweza Pemba, mimi suingi mkono na siungi mkono kwa sababu gani tumewekeza zaidi ya bilioni 1.2 Bambi, leo Zanzibar tumeshindwa hatuwezi kufanya masihara kwenye serikali, 1.2 Bilioni Bambi hakuna uwezo wa kupata mchicha wa kutumia nyumbani kwangu. Mhe. Spika, huu ni mzaha na namuomba Mhe. Mwenyekiti wazo hili aliwache tusiwapelekee watu fedha wakavuruga haiwezekani.

Mhe. Spika, imefanywa utafiti hapa kwamba Bambi wanazalisha mchicha kidogo sana na wameuza wamepata shilingi laki saba Mmisiri kazichukua Misiri kaona hii ndio nauli yangu kaondoka nazo, hatuwezi kutoa fedha za umma baadae tukafanya masihara lakin saba ndio faida jamaa kaona Misri mbali kachukua nauli twambieni mnafanya nini jamani. Mhe. Hamza Hassan Juma hili nakuomba radhi sana usishawishi mchicha hamuna uwezo nao utaalam labda haupo wa kuzalisha mchika.

Jengine ambalo ningelizungumza mimi niseme chonde Mhe. Spika, suala la ujenzi wa *rest house* Pemba jamani lipeni msipomlipa Mhe. Spika, mtatufanya tuseme mengi na tukisema mengi humu ndani wengine watatoka, huyu hajaibiwa na shetani wala jinni ametumwa na aliyemtuma yumo ndani ya Baraza hili hili mlipeni msipomlipa maana yake tutasema mengi, tukisema mengi wengine mtatoka nje humu. Mhe. Spika, mlipeni serikali wamlipe na hili wala asiambiwe Waziri wa fedha alipe waliomtuma wanajijua wamlipe msimwambie waziri wa fedha tusaidie hajatumwa na Waziri wa Fedha. Waliomtuma jamaa huyu *engineer* wa Pemba wamlipe wanajijua ni aibu gari ya Katibu Mkuu kuipiga mawe Mahakamani kashinda tena mnaogopa nini kumlipa mlipeni, midam mmemnyang'anya na fedha mnazo mumlipe hamna fedha uzeni nyumba mlipe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, huo ndio uwazi wenyewe ndio demokrasia yenyewe lazima tuseme ukweli, jamaa huyu wanamuadhibisha anasikitisha hii serikali ina watu makini msituaibishe unakopa lipa, umehadaa lipa, umenyang'anya lipa. Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Hamza amfahamishe waziri wake aliyehusika na uvamizi wa ofisi hii afanye mpango awalipe watu, vyenginevyo yakitokezea mengine itakuwa nyie serikali ndio wakosa. Mlipeni.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa sababu ya muda Mhe. Mwenyekiti naomba unisaidie ikiwa safari za viongozi wakuu ambao humu hukueleza Zanzibar bahati mbaya hatuna ndege ya serikali, tumekuwa tukipata ndege kutoka Tanzania Bara naomba kujua ndege ile inakodiwa au tunaazimwa, na kama inakodiwa kwa nini SMZ haifanyi utaratibu wa kutafuta ndege yake kwa ajili ya viongozi wakuu wa nchi hii. Taarifa ambazo tunazo ni kwamba kili trip moja kwa safari ya ndege tunatumia zaidi ya milioni nane, ikiwa hivyo ndivyo Rais, Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili safari hizo zikiwa kwa wingi ni pesa ngapi za nchi hii, kwa nini wataalam wa Wizara ya fedha hamtafuti namna ya kununua ndege.

Mhe. Spika, na Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana kabla ya bajeti *rest house*
Engineer alipwe. Naunga mkono hoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutia nyalio kidogo katika hii hoja iliyokuwepo mbele yetu. Hii sitochangia sana kwa sababu nahofia wajumbe wakaja wakakiuka kanuni ya 60(k) nahofia sana kuja wakakiuka kutokana na moda wakaja wakalala au kusinzia na ikabidi uwachukulie hatua. Kwa hivyop nigatia nyalio tu.

Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe, pili niishukuru hii Kamati ya Viongozi Wakuu kwa kutayarisha ripoti nzuri, yenye mantiki kabisa na sio katika kutayarisha tu lakini hata katika kuiwasilisha kwetu. Kwa hiyo nachukua fursa hii kuwapongeza sana.

Mhe. Spika, moja kwa moja sasa niende katika ukurasa wa 173 ambao inazungumzia ile dhana ya serikali ya kutangaza *Diaspora* kwa maana ya wale Wazanzibari wanaoidhi nje ya nchi. Kwa kweli napenda sana niipongeze serikali yetu kwa hili. Kuna Wazanzibari wengi ambao hawapo nchini ambao wanaweza wakatusaidia sana katika maendeleo ya nchi yetu. Napenda kuipongeza serikali kwa kuweza kuweka kitengo hichi. Naamini kwamba sio tu kwamba serikali iwahamasishe katika masuala ya kuinua uchumi wa nchi.

Vile vile wana haki zao nyengine za msingi. Nchi zote zilizokuwepo Kusini mwa jangwa la Sahara kama sisi wanawatumia vyema hawa *Diaspora* kwa ajili ya maendeleo ya nchi yao, sio tu kwa kupeleka fedha au mali. Lakini hata kwa kupata taaluma kupata ushauri wa kitaaluma. Kwa mfano hivi sasa sisi tunapoteza sana kwa sababu tuno watu madhubuti tu katika nchi za nje ambao wana taaluma nzuri, tukiwatumia hawa naamini maendeleo yatapatikana.

Vile vile pia wana haki na wao katika nchi yetu, tuwaandalie utaratibu wa kuweza kuwapa na wao katika haki zao katika nchi. Kwa mfano wana biashara zao kule, wangehitaji pengine kusaidiwa mikopo katika nchi yetu. Nadhani tungeandaa utaratibu huo na wao kuwapa mikopo kama ambavyo waliopo ndani ya nchi wanapata.

Pia hawa wana haki ya kuchagua. Wenzetu wengina mfano kutoka Msumbiji tu hapo, wamekuja juzi juzi walikuwa na uchaguzi hapa wamekuja kuwapigisha kura wa Msumbuji waliyokuwepo hapa nchini, hata waliokuwepo kule Makaani Vitongoji kule, wamepita kura kumchagua Rais wao wa Msumbiji. Mimi nadhani hatutokuwa na dhambi kwa sababu jambo jema huigwa na sisi tukaandaa utaratibu hawa Wazanzibari baada ya kuwa *excess* vizuri nakujua nchi walizo, basi ikifika katika vipindi vya chaguzi wakaundiwa utarabu na wao wa kuchagua Raisi wao. Kwa sababu na wao wale ni raia wetu wanaishi kule kutokana na maisha tu. Kwa hivyo nadhani kwa sababu wenzetu wana utaratu huu na sisi sio mbaya tukaweza kuona ili na wao wanapatiwa haki hii yakuchagua na kuchaguliwa.

Mhe. Spika, mimi niishauri serikali kwamba iko haja na hii Kamati sio tu kwamba Rais akenda kule peke yake au achukue wajumbe wa Serikali tu kwenda kuona na kufanya vikao na hawa *Diaspora* wangechukua hata ujumbe mdogo wa hii kamati ya viongozi wakuu wakaweza kuwashirikisha ili kuona hawa *Diaspora* wako wapi na vipi wanaishi ili wakaweza kushauriana nao vizuri katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Kisha niende katika Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais, ukurasa wa 172. Katika mtu mwenye kazi kubwa katika nchi yetu ni Rais wetu, kama kuna mtu anahitaji mapumziko kutokana na kazi anayoifanya basi ni Mhe. Rais. Kama kuna mtu ambaye anahitaji awe *comfortable* ni Raisi, kwa sababu anaongoza watu katika milioni moja na kidogo katika Zanzibar hii.

Sisi kwenye majimbo yetu tuna watu karibu 7000, au 5000 na tunapata shida sana. Niipongeze serikali kwa kuweza kumjengea ule uzio pale. Vile vile huyu Rais wetu ikiwa mawimbi ni makubwa kule kama jengo limevunjika kutokana mawimbi basi mimi nadhani kuna haja ya haraka sana ikaandaliwa bajeti ya dharura kujengwa *retaining wall* pale, ili asikerwe na mawimbi Raisi wetu anahitaji mapumziko.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba Rais kumuweka barabara ni tatizo, naungana na Mhe. Mwenyekiti. Raisi wetu anatakiwa akae pembezoni mwa mji, sio kumuweka pale ile miembe iliyomzunguka Raisi wetu imeshakuwa mikongwe sana. Mimi nadhani wataalamu waiangalie ikiwa ile miembe haifai basi tutafute miti mengine mizuri tumpandie, tutie ma-*hormones*, ikuwe haraka haraka lakini ile mikongwe pale yasije yakakwanyuka matawi ikawa tatizo. Maana mara moja tawi linaweza likakatika likaja ikawa mtihani kwa Rais watu.

Mimi nadhani miembe gogo yana tatizo ya kukatika matawi, miembe imeshakuwa mikongwe ile, tuandae utaratibu wa kumpatia miti mengine mizuri Raisi wetu, kumuwekea pale na kama tuna utafiti wa kutosha kama ile hoja iliyopita ya kilimo unaweza ukaukata mti leo kama tutafanya utafiti wa kina tunaweza tukaukata mti leo baada ya mwaka mmoja ukawa ni mti mkubwa sana baada ya kuutia makemikali mengi.
Mimi nadhani tufanyeni utaratibu mzuri miti ni mikongwe ile ifanyiwe maarifa, serikali iangalie itaweza vipi. Mimi nikipita huwa nina wasi wasi sana pale, miembe inakatika kienyeji, miti ile tangu miaka ya nyuma tumeirithi. Tumuekeeni miti mzuri ya kisasa kabisa na ile tuangalie utaratibu wa kuweza kuiondosha miti ile.

Mhe. Spika, nende katika Chuo cha Mafunzo katika ukurasa wa 186 ripoti ya Kamati inasema chuo kiliendelea na kazi zake zikiwemo katika kurekebisha tabia ya wanafunzi na kuwa raia wena na kuwapatia wanafunzi mafunzo kupitia kada mbali mbali. Yaani kazi ya chuo kile ni ku- *turn mind set* za wale wana chuo katika kuwaondosha katika tabia mbaya na kuwapeleka katika tabia nzuri. Mimi nilizani Vyuo vile vingekuwa na maadili mazuri lakini leo hii ikiwa ni mtu humiwa kupelekwa pale Chuo ni mtihani. Mimi ni mzoefu sana katika mambo ya kupelekwa Chuo cha Mafunzo hususan katika kipindi cha chaguzi, mimi nimeshakaa jela vipindi

vine. Haki ya faragha katika vyuo vile haipo. Kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binaadamu katika vyuo vyetu vya mafunzo. Unaingia pale kama mtu humiwa lakini unapekuliwe umevuliwa nguo zote. Huu ni ukiukwaji wa haki za binaadamu.

Mhe. Spika, hetu tuwe wataalamu kidogo sisi Zanzibar tumepata uhuru kwa shida na sisi humu ndio wajukuu zetu. Leo mjukuu wa muasisi anakwenda kuvuliwa nguo kwa kupekuliwa, hilo ni tatizo. Ile thamani ya damu zetu sisi tuliyopoteza wajukuu zetu wanaipataje, huku wakinyanyaswa kuvuliwa nguo, kufanywa nini. Mimi nadhani ishafika wakati wa kuweka jela za kisasa, kuwe na *detector*.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya kuna kipindi nilikwenda pale nikapekuliwa kumbe kuna shemeji yangu mle katika watuhumiwa kutayarisha maandamano na mkutano wa hadhara mimi na shemeji yangu tulikamatwa na sote tukavuliwa nguo tunatizama hivi jamani si aibu hiyo. Mimi nadhani iko haja sasa ya kuweka mazingira mazuri ya haki za binaadamu katika magereza yetu. Kinasikitisha zaidi Mheshimiwa mtu anapita pale gerezani keshapekuliwa mpaka mwisho, akiwa kama alivyozaliwa lakini mkija mkenda huko ndani vijana wanavuta bangi mule na huku wameshapekuliwa. Mimi niliumwa na kichwa sana na ndio tatizo la kuwa kila siku nanyoa nywele kwa sababau ya ugonjwa wa kinywa kutokana na bangi iliyokuwa ikivutwa mle jela, mimi sivuti lakini lile moshi lote linaniingia miye, siku zote naanguka napata kizunguzungu.

Nadhani muwe na *detectors* kusudi hayo mambo ya bangi yasipenye katika selo. Halafu la kusikitisha zaidi ni kwamba selo hiyo hiyo ina mwanafunzi na mtu humiwa anakaa humo humo. Tofauti baina ya mfungwa na rumande nyote mnakaa mule mule, mnasagwa tu. Mimi nadhani magereza zetu hazifai kwa sababu ukiingia mle ndani si umeshapekuliwa, umeshavuliwa nguo, njoo sasa katika haki hako ya faragha unavyoikosa katika selo.

Mhe. Spika, kuna kitu kinaitwa mtondoo mle ndani, ni ndoo ambayo unakwendea haja ndani ya selo kuna watu 12 na mle kuna ndoo tu pale. Haya utakaa vipi uende haja mja weye Yailahi, Yarabi, Toba Mungu wangu. Huku unakwenda haja huku unaangaliwa, haiwezi kutoka ndio unapata matatizo ya kongosho dume au kongosho jike, kama tulivyoambiwa juzi na Mhe. Juma Duni pale. Ni tatizo ni ukiukwaji wa haki za binaadamu Mheshimiwa.

Mhe. Spika, kwa nini msitoe choo mle ndani ikawa wafungwa wanakwenda kujisaidia mle mle ndani. Leo tuekewe ndoo, unakenda chooni huku wenzio wanakuangalia nyuma si vizuri kabisa ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binaadamu katika magereza yetu.

Mhe. Spika, katika magereza ya wenzetu mfungwa, mtuhumiwa wana haki hata ya kupata habari unaletewa magazeti, mnawekewa televishen, sisi hatutaki tufike huko kwa sababu pengine nchi yetu haina uwezo. Lakini huu uwezo wa kupekuliwa pale, kuwekewa choo cha shilingi lakini mbili, ikiwa serikali haina uwezo na inahitaji vyoo itwambie sisi tutajenga vyoo mule, kabisa kabisa katika kila selo, tutajenga sisi. Hili linawezekana kabisa. Leo mnaweka vyoo kule kwa kupekuwa madawa ya kulevya huku mtu akienda hakuna choo, ni tatizo.

Naomba Mheshimiwa aone kwamba sisi binaadamu, watoto wetu ni binaadamu na wengine wanaoingia mule sio wafungwa wengine ni watuhumiwa tu msiwapelekeshe haja katika mitondoo yaani ndoo waawekewe vyoo. Hilo moja.

Jengine katika ukuraswa wa 183 nataka nizungumzie hizi halmashauri za Wilaya hii ninayotoka miye Chake-Chake. Mheshimiwa Halmashuri zetu za Wilaya zinakusanya kodi katika sekta mbali mbali na katika nyanja mbali mbali. Nimeona huku wanasema Wilaya ya Chake-Chake imekusanya 9.4 milions sijui kwa kipindi cha mwaka mzima hichi au ni kipindi gani. Unatakiwa unapokusanya kodi kwa wananchi uirushe ili wapate thamani ya jasho lao wale wananchi. Leo hatuoni Halmashauri yetu ya Wilaya ya Chake-Chake inaturudishia nini kodi pale. Ukiangalia 9% ya ile kodi inatoka katika Kware ya kuchimba mawe kule Vitongoji/ Makaani lakini ukenda kule makaani ukishakuchimba mawe kila tripu ile gari inalipa karibu sh. 3,000/- ya jiwe, ikiingia ya kokoto inalipa katika sh. 5,000/- tripu moja ya kokoto na kwa siku moja yanaweza yakaingia hata magari 50 kuchukua kokoto na mawe na kifusi. Niiyombe kamati mkenda mara hii katika mambo haya mkenda hetu ulizieni vizuri kuhusu ukusanyaji wao wa mapato, hususan katika Kware.

Mhe. Spika, nende katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, suala la kupambana na madawa ya kulevya. Kwanza nachukua fursa hii kuipongeza serikali yetu kwa kiasi kikubwa sana kwa jitihada zake katika suala zima la kupambana na haya madawa ya kulevya. Kwa kweli Wazanzibari tunapoteza rasilimali kubwa ya vijana kwa ajili ya kujiingiza katika mambo haya (Mateja).
Mhe. Spika, kuna jambo zuri tu limeanzishwa na raia wetu kuanzisha nyumba za kubadili tabia. La kusikitisha sana Mhe. Spika, kwamba hizi nyumba zimeanzishwa na raia wetu kwa lengo la kuwabadili vijana na

kupunguza idadi ya mateja katika nchi. La kusikitisha inaonekana mkono wa serikali ni mfupi katika kunyooshea misaada majumba yale.

Naiyomba serikali iweze kuandaa hasa *program* na ikiwezekana walete bajeti ya kuweza kusaidia zile nyumba kwa sababu ni muhimu sana katika suala zima la kuwasaidia vijana wetu walioingia katika balaa hili na kuweza kuwatoa. Nadhani wakileta bajeti ya mambo haya basi naamini Baraza lako halitokuwa na kigugumizi katika kupitisha bajeti hiyo.

Mhe. Spika, kuna hili suala la kutekelezewa sheria ya Mazingira ambayo ni changamoto katika hii Wizara ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kama walivyose naomba nifanye *reference* katika ukurasa wa 19.

> "Kuna changamoto zinazoikabili Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kutotekelezwa kwa Sheria za udhibiti wa mazingira ya mwaka 1996 kwa wale wote wanaoharibu mazingira wakiwemo wawekezaji ambao wangi wao huwekeza miradi inayongangia kuharibu mazingira. Mbaya zaidi huekeza miradi bila ya kufanyiwa tathimini ya mazingira"

Mimi bado nasema kama kuna watu wanaoharibu mazingira katika nchi hii basi ni hizi Idara za Serikali hasa Mawasiliano wanaharibu sana mazingira. Sisi wananchi wa Vitongoji kule kazi yetu kubwa ni kulima tungule, katika ardhi ya makaani. Makaa yote hayopo tena wanachimba mashimo mawasiliano kuchimbua vifusi mpaka wanazua maji chumvi. Sasa naona Mawasiliano hawasemwi wanasemwa wawekezaji tu.

Mhe. Spika, mimi nadhani sasa kuna haja ya hawa mawasiliano na wao sasa baada ya kuharibu mazingira wakayafukia mashimo yale, hivi sasa kuna mashimo kule makaani watu hawapati hata kuchunga ng'ombe zao, hawapati kulima. Leo wanawakazimisha watu wanaochimba matofali eti uwandani wafukie mashimo, wakao wao wenyewe mawasiliano ndio wanaoharibu mazingira kule liko la Vumba, liko la Mjini, Vitongoji kule.

Mimi nadhani wale watu wa Uwandani wanaochimba matofali matofali wanatengeneza mazingira, nawapongeza. Kwa sababu watu wa Uwandani ingelikuwa si matofali ya Uwanda ingelikuwa si matofali ya Uwandani basi nakuhakikishi mazingira yangeharibika zaidi. Mhe. Spika, kuchimba kwa matofali ya uwandani kwa kiasi kikubwa ndiko kulikokufanya Wapemba waweze kujenga majumba ya kisasa ya matofali. Ingelikuwa hakuna matofali yale watu wangepata miti sana.

Mimi nakwambia wale wamesaidia sana wanaochimba matofali na wala wasigughudhiwe wale, wamesaidia sana katika kutengeneza mazingira kwa sababu asilimia kubwa ya miti ingejengwa pangekatwa kwa ajili ya kujengea. Tangu yaanze matofali yale hivi sasa miti inapatikana.

Mhe. Spika, ukiangalia bayo anuwai kule Vitongoji sasa hivi unaona ni rangi ya kijani tu kwa sababu sasa watu baada ya kukata miti kujengea wanakwena kununua matofali kule. Mimi nadhani wale wasibughudhiwe, watukubughudhiwa ni hawa watu wa mawasiliano ambao wao wanajenga barabara hatunufaidi siye wa Vitongoji, waharibu tu kule, hatupati hata kulima. Nadhani hili ndio la msingi, Mhe. Mwenyekiti, wale waachiwe wachimba matofali isipokuwa waruhusiwe baadaye waambiwe tu wafukiwe yale mashimo lakini wasibughudhiwe, wale wanatengeneza mazingira wanaochimba matofali. Tena la kufurahisha zaidi ni kwamba asilimia 40 wanaochimba matofali yale ni kutoka Ole katika jimbo la Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mimi nadhani waboreshwe wale kwamba wakishakuchimba mashimo yale wafukie lakini wasibughudhiwe, wabughudhiwe hawa mawasiliano wakisha kuchimba mashimo yao huwa hawayafukii.

Mhe. Spika, wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi ni sawa na wafanyakazi wa tasisi nyengine katika nchi hii. Wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi ni Wazanzibari sawa na Wazanzibari wengine katika nchi hii. Mheshimiwa inasikitisha sana kuona kwamba wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi wametengwa, Serikali imekuwa *buyers*, kwa nini nyongeza iliyofanywa hawa wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi hawakuongezewa mishahara.

Naomba Mhe. Spika, katika hili Mhe. Waziri anaehusika na mambo ya mishahara awaongezee mishahara hawa wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi kama walivyoongezewa mawizara mengine.

Kinyume na hivyo bajeti ya Wizara yake hapa tutakuja kuondoka nayo mbele kwa mbele. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Nataka nizungumze jambo moja tu kwa kuokoa muda.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie Idara ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Hii ipo ukurasa wa 173 katika ripoti hii ya Kamati ya Kushughulikia Viongozi Wakuu. Serikali ilifanya jambo jema sana kuanzisha utaratibu huu wa Wazanzibari kuwapatia Vitambulisho. Nakumbuka miye mara baada ya mapinduzi Januari 1964 na Muungano April 1964 palianzishwa kadi za uraia. Zile kadi lakini zilikuwa za miaka 10. Kwahiyo toka 1964 mpaka 1974 zikawa zimemaliza muda. Tokea wakati ule Wazanzibari hatukuwa tena na utambulisho. Miaka hii ya karibuni serikali wameliona hilo ni jambo zuri na wakalianzisha. Mimi naipongeza sana serikali kwa juhudi hizi, hakuna nchi yeyote katika dunia hii ambayo haiweki utambulisho wa raia zake.

Mhe. Spika, hapa kuna changamoto kidogo katika mambo haya. Kuna haja mimi nashauri sana serikali iangalie sheria ya vitambulisho ili na wale Wazanzibari wasiokuwa ndani ya hivi visiwa hii sheria iwatambue na wao na wapewe vitambulisho vya Uzanzibari. Kwa sababu kuwa kwao nje ya Zanzibar, hakujawaondolewa Uzanzibari wao.

Kasoro kubwa iliyokuwemo katika Idara hii ni kuwanyima Wazanzibari waliokuwepo nje ya Zanzibar Vitambulisho. Nilikuwa nashauri sana serikali iangalie uwezekano wa kufanya marekebisho ya sheria na wale nao wapewe. Nataka nimpongeze sana Mkurugenzi wa Vitambulisho ni mtu mmoja makini sana. Anafanya kazi kwa uangalifu mkubwa. Ukenda pale Ofisini pake unaweza ukapekuliwa kasoro kidogo iwe sawa sawa na kule jela aliposema mwana mapinduzi. Hiyo ni kuonesha kwamba hawataki taarifa zao pale zivuje ovyo ovyo. Hawataki watu waingie pale na mambo ambayo wanaweza kurikodi mazingira ya pale. Ni jambo moja muhimu sana.

Mhe. Spika, lakini nataka niseme kitambulisho ni haki ya kila Mzanzibari na ni haki muhimu sana. Kwa sababu kupitia kitambulisho Mzanzibari ndipo anaweza kupata huduma nyingi katika nchi yetu. Nataka niwalaumu pia wale Wazanzibari ambao tayari wamefanikiwa kusajiliwa na kufanyiwa vitambulisho lakini bado wakawa wanadharau hawendi kuvichukua. Nataka niwalaumu sana ni watu ambao hawapo makini wala hawajui thamani ya hivi vitambulisho. Nawaomba sana kila aliyekuwa ana hakika tayari kitambulisho chake kipo basi akifuate popote kilipo lakini awe nacho mkononi mwenyewe kitamsaidia sana.

Mhe. Spika, nasikitika kidogo kuna Wazanzibari wengi ambao wananyimwa na wanaendelea kunyimwa kupata haki yao hii muhimu sana ya vitambulishi. Mimi nilipata kesi wakati mmoja na ikatangazwa na waandishi wa habari kweli kweli kwamba nimegombana na Sheha kwa kumnyima Mzanzibari kitambulisho.

Mhe. Spika, si jambo jema kabisa kwamba sheria ipo imetunga, kila Mzanzibari ni haki yake kupewa kitambulisho halafu atokee mtu kwa kisingizio, mimi nasema kisichokuwa cha maana halafu ukamnyima mtu haki yake ya kupata kitambulisho. Mhe. Spika, ukiwa na cheti cha kuzaliwa ndicho kile ambacho cha msingi cha kupatia kitambulisho.

Mhe. Spika, mdnao mimi nikishakumzaa mwanangu kama ni hospitali wale madaktari pale ndio wanaoandika zile *particulars*, nadhani wanaweza wakaniuliza tu jina lake nani, nikimwambia lile jina basi. Kile kipande cha hospitali ndicho ninachokipeleka kwenye Idara ya Usajili wa Vizazi na Vifo kwa Mrajisi. Wao ndio wanachapisha cheti. Kama mwanangu namwita Muhammed mrajis akimuandika Muhammad hilo ni kosa na ukenda kule akitafuta kitambulisho hupati. Kosa ambalo sikulifanya miye, limefanywa na Idara ya Serikali lakini ukiangalia upande wa pili hivyo mtu anayeitwa Khalifa ukamwita khalife lakini baba yake ndiye weye weye, na mama yake ndiye yule yule aliyemzaa na kazaliwa na hapa Zanzibar ndio kweli hiyo imnyime mtu kupata haki yake kama kwamba si Mzanzibari tena kwa sababu ya kubadilisha herufi moja.

Mhe. Spika, hili si jambo zuri na nadhani miye tubadilike, tusiwanyime watu haki zao. Kwa utaratibu huu nilifanya utafiti mdogo sana nikagundua kila jimbo la uchaguzi lina watu walionyimwa vitambulisho kwa msingi huu hawapungui 1000 mapaka 1500, tuna majimbo 50 katika Zanzibar hii, hetu tuangalie ni watu wangapi hao. Kwa kweli tunafanya jambo moja bay asana. Mimi nadhani wakati sasa umeshafika wa kuacha, kama ilikuwa ni siasa na mikakati ya siasa chafu. Mhe. Spika, wakati wa siasa chafu umepita sasa Wazanzibari tuko kitu kimoja na kupitia vitambulisho hivi tunaweza tukafanya maamuzi muhimu sana ya nchi yetu, kwani ukishakumnyima mtu unamnyima haki yake muhimu ya kufanya maamuzi. Mhe. Spika, nilidhani Mkurugenzi yupo hapa hili alione akishirikiana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi awaagize Masheha wao wasiwanyime watu hizi haki zao, ni kosa kubwa sana.

Mhe. Spika, jambo baya zaidi ambalo mimi kama nitaendelea kulisikia kuna siku nitapeleka hoja binafsi ya kutaka Idara ya Usajili na Vitambulisho ifanyiwe ukaguzi. Mhe. Itafika siku nitakuomba sana uunde Kamati Teule tukaifanyie ukaguzi.

Mhe. Spika, ikiwa Mzanzibari anaitwa Khalifa lakini cheti chake kimeandikwa Khalife kweli ndio anyimwe kitambulisho cha Uzanzibari mkaazi, lakini leo anakuja Mburundi hapa anapewa kitambulisho, anakuja Mkenya anapewa kitambulisho. Mhe. Spika, wale wanaotembeza korosho ndani ya ungo, wale wakija hapa wanasajili hapa hapa wale wote wanaonesha vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi ili wajisajili mitandao ya simu. Mhe. Spika, hii ni aibu tunamnyima Mzanzibari mwenzetu tunakwenda kumpa mtu yule.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba amesema hapa kwamba ana mfano hai wa Mkenya ana kitambulisho cha Mzanzibari. Kwa kweli haya ni mambo hayavumiliki, na mimi nafanya utafiti lakini kama nitaendelea siku moja nilikwenda pahala katika jimbo langu *wallahi* kuna wale Wanyamwezi wanaolima wanatoka kwao Shinyanga wanakuja hapa wakiomba kazi kwa watu wapewe nafasi ya kulimia mikarafuu. Mhe. Spika, kwa kweli anatoa kitambulisho cha Uzanzibari Mkaazi anakuonesha hiki nimekipata jana, hii ni aibu sana. Mhe. Spika, hii sifa yote niliyompa Mkurugenzi mimi kwa umakini hapa itafutika kabisa. Kwa hivyo, naomba sana idara hii ijirekebishe kama sio hivyo *wallahi* nitapeleka hoja binafsi hapa iundwe kamati teule tukaichunguze idara hii.

Mhe. Spika, sasa hivi keshokutwa sio siri tutafanya mabadiliko ya katiba, wallahi asilimia 30 nina hakika watapiga kura na sio Wazanzibari kwa sababu ya vitambulisho hivi. Mhe. Spika, iko siku tutakua tuko sawa sawa hapa tutauza nchi yetu kwa vitambulisho hivi tusipokua makini, naomba sana tuwe makini kwani hii ni haki ya Wazanzibari jamani nchi ina utambulisho wake. Mhe. Spika, tukifanya mchezo utambulisho wetu tukawapa watu wengine tutakuja kugeuka Wapalestina tutafukuzwa ndani ya nchi yetu sisi hapa. Nasema kwa uchungu mkubwa sana Mhe. Spika, wala mimi siko ndani ya siasa, hili jambo la siasa litapita tu kulikua na vyama vingapi huko mbona havipo. Kwa hivyo, naomba sana Mkurugenzi wa Vitambulisho awe makini zaidi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja hii ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia kidogo katika ripoti iliyotangulia ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayoshughulikia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Mhe. Spika, kwa ufupi kwanza nampongeza Alhaj Shekhe Abdalla Juma kwa namna alivyozungumza kuhusu vitambulisho, lakini kwa sababu ana pahala padogo tu amesahau kupamaliza na mimi naomba nimalize sirejei.

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi na wananchi wake ni Wazanzibari na aliyekua si Mzanzibari maana yake sio mwananchi na utambulisho wa Mzanzibari ni kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi na ikiwa mtu hana kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi hana haki ya Mzanzibari zote zinazohusika ambapo kitambulisho kile kinatumika. Mhe. Spika, hakuna sababu yoyote iliyokua sio ya msingi yakumfanya Mzanzibari akose haki hiyo.

Mhe. Spika, mimi tokea juzi nimesikitika sana kwa maelezo ya uhakika aliyotoa Mhe. Mshimba kua pana wageni hapa wamepewa vitambulisho na wameajiriwa, lakini Wazanzibari wenyewe wanasumbuliwa. Kwa hivyo, lakusikitisha ingalikua kuna tamko rasmi la kiserikali la kukamata kuwa wanafanya kwa sababu hii ingelikua haijambo. Lakini serikali ikitoa maelekezo yake ni safi kabisa na katiba inaeleza vizuri na huyu Sheha hasa ana mamlaka gani anafanya anavyotaka halafu akaachiwa tu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mahala ambapo haki haitendeki siku zote kunakua na matatizo. Mhe. Spika, kwa heshima zote namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa sababu aliahidi katika hotuba zilizotangulia nyuma kua hili suala atalifanyia kazi na kwa sababu ameshasikia mambo ambayo yameshajitokeza kuhusu vitambulisho hivi na umuhimu wake. Kwa hivyo, namuomba afanye kama inavyowezekana yeye ni muungwana, ni mtaalamu na haya mambo anayajua kwa sababu tumemueleza hili suala likae sawa.

Mhe. Spika, pia na sisi wenyewe tusifanye mambo mengine ikawa hatuna sababu ni watu wazima, kuna watu walipiga kura miaka mingi umri wao wengine ni mkubwa hata kuliko mimi. Lakini kuanzia kipindi kilichopita kwa sababu ya kutokua na kitambulisho cha Mzanzibari yule mtu akakoseshwa haki zake zote. Mhe. Spika, huko nyuma amepiga kura sasa hivi hapigi tena, vijana wengine hawapewi, wanaopewa ni wageni na nchi imeingiliwa sote tunajua. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atuvue katika mashaka haya yoyote atakayepiga kura ana kitambulisho hatuwezi kumzuia, lakini wetu tunamzuia hebu tuulizane hivi sasa tuko katika GNU tunafanyiana mashaka kwa nini.

Mhe. Spika, ni kwamba sote tumeungana, serikali yetu ni moja tunakwenda vizuri, tunasikilizana na mataifa yanatutambua kwa sababu wanashangaa tulivyokua na tulipo hivi sasa. Kwa hivyo, kuna sababu gani yakumruhusu Sheha afanye anavyotaka isipokua ni kuwakosesha haki wananchi wanaohusika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili hatuwezi kulistahamilia aone kua hili suala limetatuka kwa sababu amelichukulia ahadi.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kwamba serikali ni chombo cha kuheshimika na kutokea aibu ambazo sio za msingi katika serikali ni jambo la kushangaza. Mhe. Spika, tumemsikia huyu mjenzi ana zile fedha kwa mujibu wa taarifa ilivyo milioni 104 za ujenzi wa *Rest House* iliyoko Micheweni pamoja na *fence* yake. Mhe. Spika, huyu mtu mimi sisemi kwamba ameshachanganyikiwa lakini hizi pesa ni nyingi na katika kufuatilia alikua akifanya kazi kwa kuamini kwamba fedha hizi atalipwa. Lakini yamekua mashaka makubwa na juzi tumesikia aliyoyafanya kuna gari ya Katibu Mkuu aliipiga mawe akaivunja vioo, akatiwa ndani ametolewa kwa sababu za msingi, na leo hii ameshaweka ahadi mbaya sana.

Mhe. Spika, kama haki yake iko kweli basi hakuna sababu yakushindana na masikini ya Mungu ambaye ameshatumia nguvu zake, hii ni serikali. Mhe. Spika, aliyoyaeleza Mwenyekiti wa Kamati zile ni *circumstance evidence* za kutosha kua huyu mtu anadai haki yake. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ulimwengu mzima unasikia kua mtu amedhulumiwa na serikali ina uwezo kwa namna itakavyoona inafaa kumlipa haki zake hasa kwa sababu Mahakama ambayo ndio wenye uamuzi wa mwisho walisema hii haki yake apewe. Kwa hivyo, naomba hili lisije likazungumzwa tena kwa sababu limeshamaliza.

Mhe. Spika, jengine kwanza nitoe shukurani sana kwa kamati kazi kubwa waliyoifanya na katika ripoti zao kuna suala la magendo ya karafuu. Mhe. Spika, wanaohusika na magendo ya karafuu ni KMKM na wenzetu walitembelea mbali sana na ukamataji wa magendo ya karafuu ni KMKM. Mhe. Spika, walipotembea kama kule Sengenya Mtambwe waliona rada hii kua ipo wanajenga vijumba lakini hiyo rada ni mbovu haifanyi kazi.

Mhe. Spika, ile rada ilikua ikisaidia sana pamoja na ushauri wao kua watafutwe Wachina watengeneze, lakini ningeliiomba serikali kwa makusudi kwa ulinzi wa nchi yetu pamoja na kudhibiti karafuu zetu zisitoke nje, basi hii rada ifanyiwe kila inavyowezekana itengenezwe na ifanye kazi. Sio KMKM wakae pale tu kwenye nyumba nzuri, lakini kumbe ile rada ni mbovu na pale wanapokaa pana misitu hua hawajui chochote kinachotokea.

Mhe. Spika, jengine tumeona katika ripoti aliyoeleza Mwenyekiti wa Kamati kua kumekamatwa karafuu na fedha za kuuzia karafuu zimegaiwa katika hali ambyo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa husika ilikua ikichukua asilimia 50 na wale wakamataji yaani KMKM wakipewa asilimia 50. Mhe. Spika, pamoja na kua kamati imependekeza kua Ofisi ya Mkoa ipewe asilimia 10 halafu wakamuingiza mtoa taarifa hapa anapata asilimia 20 na asilimia 70 zipelekwe KMKM. Mhe. Spika, mimi ningeshauri kwamba hizi karafuu ni mali ya serikali na hao wanaolinda na kukamata wanalipwa na serikali kwa hivyo kwa vyovyote ilivyo watoa taarifa, wakamataji KMKM mimi naona hawa ndio wanaohusika na kupata chochote, lakini sio chote chengine kirudi serikalini.

Mhe. Spika, sioni kwa sababu gani Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inapewa asilimia hii kubwa wakati wao sio waajiri wa hawa askari wa KMKM wanaokamata haya magendo ya karafuu. Kwa hivyo, naomba wale wanaohusika na kutoa taarifa pamoja na wakamataji wapewe chochote lakini na vile vile serikali kwa sababu hii ni mali ya serikali asilimia fulani irejeshwe kwenye serikali.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ni uharibifu wa mazingira na wizara inayohusika ni Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mhe. Spika, uharibifu wa mazingira unatokea kutokana na kazi za binadamu kwa njia tofauti. Kuna wengine kwa kujitafutia maisha na kuna wengine kwa shughuli za maendeleo. Lakini kwa vile kila wizara ina taasisi ya utafiti ilikua kwanza pafanywe utafiti kabla ya shughuli yoyote haijaanza.

Mhe. Spika, matokeo yake Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano anaweza akajisifu sana kama amejenga barabara nyingi sana. Lakini kumbe kifusi na mawe amekwenda kuichukua ardhi ya kisiwa hiki kidogo ameifanya mashimo maji yameshaingia, hii ni hatari.

Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri aliliona zamani na hili na Mhe. Spika, naamini una kumbukumbu kwamba Mhe. Waziri alisema ili barabara ziwe za kitaalamu kabisa hizi kokote tunazotumia zinatokana na mawe yaliyopo katika nchi hii hazifai. Kwa vile kwa ukakamavu wake na naamini mengi atayafanya na tunaona ishahara zake hapa Unguja ilivyo na Pemba huko ule wakati wa kutafuta kokoto kutoka nchi nyengine umefika ili waviache visiwa vyetu kwa sababu hii kauli aliitoa yeye mwenyewe kwa kiutalamu kua kokoto hizi hazifai itabidi ziagizishiwe kutoka sehemu yoyote.

Mhe. Spika, la pili hii ripoti imependekeza kua wizara inayohusika na uhifadhi wa mazingira ione kua hali ya mazingira imerejeshwa kama ilivyo, lakini haya sio masuala ya kutoa mapendekezo tu, ni kwamba hapa fedha nyingi zinahitajika. Mhe. Spika, kama wizara haikuwezeshwa kifedha na kiutaalamu na pakafanywa *feasibility study* ya kutosha kwa hivyo haiwezi kabisa ikaweza kumudu kuyarejesha mazingira katika hali iliyo.

Mhe. Spika, kwa hivyo kwa sababu visiwa hivi ni vidogo na kila siku ndio vinapungua, wanaokata matufali wanaviua hawana kazi nyengine yakufanya, wanaokata misitu ndio tena wanaleta ukame na kadhalika. Kwa hivyo, ningeliomba kama tunavyofanya katika mambo makubwa na huku tunakoendelea tunaendelea na shughuli hii, hivyo wakati umefika kwa sababu ya mazingira yalivyoharibiwa tuwaite washauri waelekezi waje waione hali hii *population density* ilivyo, wengine sijui wapangwe vipi na halafu zitafutwe fedha kwa namna yoyote ya kutosha na kwa njia ya kitaalamu na hali hii angalau kurejeshwa hatua kwa hatua tusiende kama tunavyokwenda ni hatari kubwa sana. Mhe. Spika, ningelisema mengi lakini kwa sababu ya muda nashukuru kwa hilo.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipatia nafasi ya kuchangia ripoti ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwanza sina budi kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa kuchangia vizuri kamati yake na kufanya kazi safi hasa kwa kuwasifu viongozi wetu wa kitaifa. Kwa hivyo, mimi nachangia kwa kiongozi mkuu wa kitaifa mwaka 2012 kiongozi wetu lazima apate mambo mapya. Mhe. Spika, kwanza nachangia kwamba kuweza kupata jengo la Ikulu katika Mkoa wa Kusini Unguja. Mhe. Spika, kwa vile miaka mingi katika Mikoa kulikua na majengo ya Ikulu lakini Mkoa wa Kusini ilisahaulika kabisa, kwa hivyo naomba mwaka huu Mhe. Waziri ahakikishe kwamba ameweza kujenga jengo jipya la Ikulu katika Mkoa wa Kusini. Mhe. Spika, ni vigumu kuona Mhe. Rais anataka kupumzika katika Mkoa wa Kusini na kuweza kukodiwa hoteli ambayo itagharimu pesa nyingi sana.

Mhe. Spika, ni kwamba hakuna sababu ya Mhe. Rais hapa hapa nchini kuweza kukaa kwenye hoteli, hiyo ni aibu kitaifa kwa sababu uwezo tunao na sababu tunazo za kuweza kukaa katika Ikulu yetu wenyewe. Mhe. Spika, vile vile nachangia kwa Wakuu wa Wilaya ni aibu kuna Mkuu wa Wilaya ya Kusini na Mkuu wa Wilaya ya Kati anachangiwa Ofisi ya kuazimwa katika majumba ya majenzi. Hiyo ni aibu sana kwamba Mkuu wa Wilaya hana ofisi maalum kama walivyokua na ofisi ya Wakuu wa Mkoa. Mhe. Spika, utakuta Mkuu wa Wilaya ya Kati anachangiwa ofisi wafanyakazi wake wanakaa katika uwa ndio wanafanya kazi. Mhe. Spika, utakuta wafanyakazi wengi wao saa za kazi wako nje kwa sababu hawana ofisi maalum, hiyo ni aibu sana kwani sasa hivi tuna miaka 47 bado tunaazima ofisi za Wakuu wa Wilaya.

Mhe. Spika, vile vile kuhusu vijana wetu wa JKU utakuta vijana hawa Mhe. Mwenyekiti alisema alipokwenda Chokocho alifika katika kambi yao na aliomba waweze kuombewa nafasi za kazi zinapotokea ajira kama vile polisi, jeshi au vikosi vya SMZ. Mhe. Spika, ni kwamba hakuna sababu ya kuombewa nafasi hizo kwa jamaa hawa wa JKU, kwani hizo nafasi ni zao kwa sababu dunia nzima Jeshi la Kujenga Taifa ni lazima kijana yoyote apite katika Jeshi la Kujenga Taifa. Mhe. Spika, kijana akipita katika Jeshi la Kujenga Taifa kwa hapa kwetu Zanzibar ni kupitia JKU, hakuna sababu ya kijana wa JKU kwamba ameshamaliza mkataba wa JKU halafu pale pale anaomba tena nafasi ya kuajiriwa kwenda JKT ndio aweze kupata ajira. Haina sababu yoyote kwa kijana huyo kufanyiwa usajili mara mbili, kijana akishapita katika JKU ni kwamba tayari ameshapita Jeshi la Kujenga Taifa anayo haki ya kuajiriwa katika sehemu yoyote ya serikali.

Mhe. Spika, kwa leo kutokana na muda wenyewe ulivyo na muda umeshakua ni mwingi, hivyo hakuna sababu ya kutetea sehemu nyengine isipokua ni kuwatetea vijana waweze kuajiriwa kwa sababu nafasi ni zao na lazima wapite katika Jeshi la Kujenga Taifa kwa miaka miwili na wakimaliza ni lazima wapate ajira katika serikali yetu. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Kamati ya Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, mimi nataka nimpongeze Mhe. Mwenyekiti na kamati kwa ujumla. Mhe. Spika, kutokana na muda mimi naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kupata wasaa huu mdogo kuchangia michango ya Waheshimiwa mbali mbali waliochangia ripoti hii ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Naomba kwanza nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti pamoja na kamati yetu hii kwa kazi kubwa ambayo tumekua tukifanya pamoja siku zote, mimi nawashukuru sana kwa mawazo yao, michango yao na changamoto nyingi wanazotupa hili lazima niseme wazi kwamba wizara hili ni kubwa kwani mambo yake ni mengi, na yanahitaji ufuatiliaji wa karibu sana. Kwa hivyo, mimi nawashukuru sana kamati kwani wamefanya kazi vizuri sana hata kama mimi sipo lakini watendaji wananisaidia kwenda nao kila mahala na upungufu wote wanatwambia na kubwa zaidi ninalompenda

Mwenyekiti na kamati yake pale wanaposhauri mwelekeo na hili ndio suala la msingi, kwamba usibaini upungufu lakini unashauri nini kiwepo. Kwa hivyo, mimi namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa hilo pamoja na wajumbe wake.

Mhe. Spika, kama nikienda hoja kwa hoja nafikiri mimi ndio nilikua na mengi sana kuliko hata wenzangu. Kwa hivyo, kwa muhtasari tu mimi nimepata kama dondoo kama nane hivi, kwanza ilikua ni *Rest House* ya Micheweni, makaazi ya viongozi hasa ya Mhe. Rais, maakazi ya askari pamoja na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo, vitambulisho, GSO na hasa haki za Mzanzibari kwenye vitambulisho, suala la Manispaa, JKU. Haya ndio niseme waheshimiwa wengi wameyachangia.

Mhe. Spika, lakini kulikua kuna masuala *very specific* yanaulizwa labda kwa mfano Manispaa na kwengineko. Hapa ndio niliposema Mhe. Spika, kama nitajaribu kuyajibu haya nafikiri nitataka saa yako moja nyengine kwa hiyo hapa leo mpaka riamba, lakini sitokwenda huko na nitajitahidi tutawasiliana baadae lakini na bajeti inakuja na hii imetupa changamoto. Kwa hivyo, Mhe. Spika, haya tutayafanyia kazi ili tuone katika bajeti yetu basi huu upungufu ambao mmetwambia basi Mhe. Spika, usiletwe.

Mhe. Spika, kulikua na masuala ambayo ni *specific* kama Mhe. Mshimba yeye aliulizia lile suala la pale *Round About* ya Michenzani kwamba panajengwa pesa zile wanapata wapi. Mhe. Spika, kwa kweli yale maslabi ni ya mradi ya michirizi iliyopita, yale ni mabaki yanayotumika hapa na pesa kidogo tu zinatumika kununulia saruji na mchanga. Kwa kweli hilo sio pesa za bajeti na sio pesa nyingi ni kama milioni moja laki tano basi.

Mhe. Spika, pia aliuliza suala la bustani ya Forodhani pesa zile zinakwenda wapi. Ni kwamba pesa zile makusanyo yake wastani kwa mwaka ni shilingi 33 milioni mpaka 36 milioni au kwa wastani kama wa milioni 2.5 mpaka milioni 3 kwa mwezi. Na pesa hizi zinawekwa kwenye *account* maalumu mpaka nambari ninayo hapa AC021103000615. Kwa hivyo, hizo pesa zinawekwa kwenye *account* hiyo kwa makubaliano ya bodi maalumu ya kuendesha bustani ile.

Mhe. Spika, kuhusu suala la *Rest House* ya Micheweni hili suala ni kwamba waheshimiwa wengi wamelizungumza, hili suala mara nyingi tumeulizwa maswali tumelijibu. Ni kwamba tatizo kubwa sana na imesemwa kwenye ripoti ni kwamba bahati mbaya sana yule mkandarasi aliyekua na huu mradi amefariki, Mungu amrehemu. Kwa hivyo, baada ya kufariki akatokea huyu bwana mwengine aliyetajwa humu bwana Ali Salim na hapa imesemwa kwamba alibainisha kua wakati hayo yakitokea yeye alikua nje ya nchi. Kwa hivyo, haya mambo yote ya malipo, uendeshaji wa kampeni wakati wa ujenzi yote huyu bwana wakati yanafanywa hayo yeye alikua Uingereza. Hii ripoti ndio naisoma ripoti ya Mwenyekiti. Sasa huyu bwana kaja baada ya yule bwana kufariki ajaribu kuendeleza yale mambo. Sasa hapo kutaka kuingia sasa sijui sasa niseme kwamba labda hakuingia kitaratibu.

Naomba ninukuu hapa kwamba, Ndugu Ali Salum aliyejieleza kuwa yeye ndiye Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya *Ah-li Construction Company* ya Zanzibar ilihusika na ujenzi wa *Restaurant* ya Micheweni alisema, “Hayatambui malipo yote yaliyofanywa na Wizara ya Fedha kwa kampuni hiyo na kufahamisha kwamba malipo hayo yalifanywa kama ni njama za kumfaidisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Marehemu Ali Hamad Ali” (Kimti). Sasa kweli Katibu Mkuu Wizara ya Fedha yeye analipa tena zitamfaidisha vipi? Na huyu ndiye marehemu aliyekufa. Sasa tatizo lote Mhe. Spika, liko hapa, hizo kumbukumbu sisi tunazo kumbukumbu zetu za malipo na zimetengwa vizuri sana malipo yote yamefanywa, *main fact* imesemwa humu namshukuru sana mwenyekiti kaeleza vizuri sana. Tumefanya *evaluation* ya ile kazi, tumebaini kwamba kazi iliyofanywa showding, *is not worth while money*, yaani karipua tu, ripoti imesema hapa.

Pesa zilizolipwa ukitizama ni nyingi hiyo ndio tathmini yetu. Sasa tukakubaliana tumlipe kiasi gani mambo yaishe, lakini bado hatujakubaliana alitupeleka korti. Korti aka-*with draw case* yazungumzwe, kuzungumzwa bado ana hasira anafika kuipiga mawe gari ya Katibu Mkuu, sasa *what is that*, maana yake hata hio stahamala hana, unapiga mawe gari ya Katibu Mkuu!
Jana nimeiona barua, na mimi maisha yangu yanahatarishwa amemuandikia Mkuu wa Polisi, na mimi pia sasa hivi jamani maisha yangu yanahatarishwa na bwana huyu, kaandika barua polisi Spika unayo barua hiyo. Sasa mimi ninahusika na nini na hilo suala, sijampa pesa, sishughuliki na pesa sishughuliki na chochote.

Sasa Mhe. Spika, kama humu Barazani unataka tutoe maoni yetu tueleze tufanye kazi tutaeleza, sasa kama mtu anataka kutuhatarishia maisha yetu kwa kufuata njia za pesa namna hiyo aa, nasema *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatulinda bwana, na kama kufa huko *Inshaallah* na tufe, lakini mpaka kuandika barua polisi! Nilitaka kuja nayo nikusomeeni Waheshimiwa hapa, kaandika barua polisi kama sikulipwa mimi Mwinyihaji Makame

ataniua kesho au keshokutwa halafu na yeye atajinyonga, ndio kuna barua kamili hapa. Sasa tunafanya kazi au tunafanya nini.

Kwa hivyo, Wajumbe wako Mhe. Spika, ikiwa tunatishiwa maisha yetu kwa hayo ya kuitetea serikali hii, basi na tutishiwe maisha bwana na hiyo ndio hali. Kwa hivyo, mimi ushauri wangu Mhe. Spika, hili suala mimi nakubali Kamati ya *PAC* na Kamati yetu hii waendelee kulifanyia kazi tupate ukweli wa mambo uko wapi, kama huyu bwana kuna haki yake alipwe, kama kweli iko haki yake hii kampuni kairithi na kuna ushahidi kweli yeye kairithi basi alipwe serikali haimnyang'anyi mtu, serikali inadaiwa mpaka miaka 10 au 20 lakini italipa, lakini isiwe unaifanyia hadaa serikali sivyo.

Vielelezo vimeelezwa hapa malipo uliyolipwa, japo kuna matatizo ya kiutendaji maana yake mengine alikuwa analipa Katibu Mkuu mengine analipa Mkuu wa Mkoa, lakini yote yanatoka Wizara ya Fedha na mtiririko wa fedha zote zimeoneshwa zipo. Kwa hivyo kumu-*implicate* Katibu Mkuu kama nilivyosema hapa kwamba yeye kunamfaidisha, kunamfaidisha nini Katibu Mkuu ni kumuonea masikini wa Mungu bure. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi ninakubaliana kabisa *PAC* na Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa walifanye kazi hili suala liende ndani kabisa, waende ndani *alifu kwa ujiti* tuone nani mkweli na penye mapungufu lisawazishwe, wengine tusihatarishiwe maisha yetu kwa jambo ambalo wala halituhusu.

Mimi nilipokwenda kutembea pale nikaona ni *Rest House* ya Ikulu, nikashauri tu, kama *rest house* jamani ni vyema pakajengwa ukuta kwa nia safi kabisa kama Ikulu yoyote ni vyema pakajengwa ukuta, sasa kusema hivyo ni vyema kujengwa ukuta si uchukue tofali tena unaanza kupanga unajenga ukuta, ufuate taratibu. Sasa mimi anani-*quote* kwamba mimi nimetoa amri, sasa ndio nimetoa amri lakini wewe ufuate taratibu na kama *contractor* utiliane mkataba na nini, sio siku ya pili unachukua tofali unajenga hatwendi hivyo kienyeji.

Mhe. Spika, nimeona hili Waheshimiwa wengi nasema labda walikuwa hawajalifahamu, lakini *there is more than that* ningeomba sana Mhe. Hamza Hassan yeye katoa *summary* tu hapa, bora akae na serikali tumpe yote ya ndani na bahati nzuri tulifanya vikao viwili, tumpe yote tuko tayari na mimi niko tayari kama alivyosema Mhe. Spika, kamati ya *PAC* nao wachunguze kwa undani, kama huyu bwana ana haki yake basi hiyo haki yake alipwe mimi niko radhi kabisa simzuilii pesa ya serikali.

Mhe. Spika, kulikuwa na mengine kama nilivyosema mengi ya ushauri, na mengi ya ushauri tumeyapokea hasa ya kuboresha Vyuo vyetu vya Mafunzo, vyoo vile. Mhe. Saleh Nassor Juma tunakushukuru sana, suala la vitambulisho nalo limechukua sura yake.

Mheshimiwa ni haki ya Mzanzibari kama alivyoeleza Mhe. Abdalla na wengineo, ni haki ya Mzanzibari yeyote apewe kitambulisho kwa mujibu wa sheria ya ukaazi, miezi 36 umetimiza hakuna tatizo tushasema mara nyingi sana, lakini kama hujatimiza yale masharti usi-*force*. Sasa kuna wenzetu wengine bahati mbaya sana wana-*force* na wengine hivyo vitambulisho viko tayari wakavichukue havijachukuliwa, ripoti hii hapa kaandika hapa, Mheshimiwa vitambulisho Pemba viko, vitambulisho vingi havijachukuliwa ukurasa wa 182. Anasema:

"Ofisi ya Msajili na Kadi za Utambulisho Pemba. Imeelezwa kwamba ofisi inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi, ufinyu wa bajeti na wananchi kutokwenda kuvichukua vitambulisho vipya katika ofisi za usajili", anaendelea zaidi Mwenyekiti wa Kamati, "Kamati ilishauri elimu zaidi itolewe kuhusu umuhimu wa kitambulisho cha Mzanzibari kwa wananchi, lakini pia ofisi hiyo iendelee kuvisambaza vitambulisho hivyo vituoni kwa lengo la kuwapatia wahusika". Bado vitambulisho Mheshimiwa watu wamekwenda kujiandikisha vimerundikana kwenye ofisi, sasa kama watu hawapewi hivi vimetokea wapi?

Mimi nakubaliana kabisa kwamba kweli si *fair* kuwapa watu wasiohusika tukawanyima Wazanzibari wenye haki yao, lakini ninachoshauri kama mtu kanyimwa tufuate utaratibu jamani, sasa sisi waheshimiwa tuwashauri watu wetu kwamba kuna fomu inajazwa, uende kwa Mkuu wa Wilaya hanyimwi mtu, aje kwa waziri, kwa Mkuu wa Mkoa haki yake atapewa, hiyo tunazidi kuisema hanyimwi haki ya kitambulisho mtu yeyote Mzanzibari, lakini tufuateni taratibu. Sasa hivi vitambulisho viliopo haviendi kuchukuliwa, watu wanashindwa kwenda kuchukua kwa sababu pale utakuwa *scanned*, utaonekana na pengine kajiandikisha pale na kwengine ndio vimebakia hivyo, lazima tuwe wakweli kwa nini hawaendi kuvichukua hivi.

Hapo Mwera tu Wilaya ya Magharibi nenda utashangaa vitambulisho viliopo, kwa nini sasa mtu haendi kuchukua, anaogopa atakamatwa na kweli tukimkamata anayetudanganya tutamfunga hiyo ndo sheria inavyosema kabisa.

Mhe. Spika, niliona haya mawili niyatilie mkazo sana. Suala la JKU Bambi, kweli ule mradi ni wa mashirikiano na ni mradi wa kutusaidia wa mbogamboga kwa ushirikiano na Misri kidogo ulisuasua kutokana na mikataba, lakini pesa nao Wamisri wanatia, mbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini na Wamisri nao wanatia, sina *figure* kiasi gani. Lakini nakubaliana na ushauri kwamba tungoje tufanye *review* tuone matatizo yake halafu tupate *the way forward* kurekebisha ili mambo yaende vizuri.

Kuhusu makaazi ya askari nimeshazungumza, makaazi ya viongozi wetu ni kweli Viongozi Wakuu lazima wapate makaazi mazuri na lile wazo ambalo Mhe. Hamza Hassan anatupa sana Mhe. Rais kuhama pale, lakini kwanza kupaweka sawa, kupaboresha pale, unafikiri ukuta ule tofauti na zamani umekuja juu na pana *maximum security* pale. Lakini hilo suala la kuondoka pale, basi kama serikali tumelizingatia tutatizama vipi tunaweza tukalitekeleza.

Mhe. Spika, mimi sina zaidi lakini ninachosema kwamba mengi mmetupa, na mmetupa changamoto tutayafanyia kazi tuone yanakwenda vipi. Wizara yetu kubwa lakini haina maana kwamba tusi-*perform* tutajitahidi tutajipanga vizuri tu-*perform* na tuone tunafanikisha. Mhe. Spika, na mimi naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais): Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii kwa idhini yako ili kufanya majumuisho kwa yale ambayo yamejitokeza kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mengi yamejitokeza kama ni ushauri, mapendekezo, kupongeza kwa mfano suala la mazingira kwamba liingizwe katika mitaala. Natumai hilo si tatizo kwa sababu nchi nyingi suala la mazingira limo ndani ya mitaala yao pamoja na mazingira mengine. Masuala ya vifaa vya *analogy* tuviangamize ni namna gani ya kuviangamiza, nina imani wizara itachukua hatua nzuri tu ya kuhakikisha kwamba mabaki hayo ya *analogy* basi yanaangamizwa bila ya kuleta madhara mengine katika jamii. Vile vile wachimba michanga katika fukwe, juu nafikiri ni masuala ya sheria hizi na imependekezwa kwamba basi sheria ichukue mkondo wake. Natumai wizara imesikia hilo na italitizama ikishirikiana na wizara nyengine husika. Kwa sababu haya ni masuala ambayo yanaingiliana na utalii, masuala ya *ZIPA* ya uwekezaji, kwa hivyo naamini kwamba taasisi hizo tatu zitakaa pamoja ili kutizama namna gani ya kuchukua hatua ya kuvunja hoteli hizo zilizojengwa ndani ya fukwe.

Mhe. Spika, vile vile wana mawasiliano ndio ambao wanaharibu mazingira, nao wenyewe watu wa mawasiliano wamesikia na naamini kwamba wizara itakaa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili kutizama namna gani ya kuhakikisha kwamba baada ya ujenzi, au wafanye utafiti wa mazingira kwanza kabla ya kutengeneza barabara zao. Kwa hivyo, naamini kwamba watakaa na watalifanyia kazi suala hilo la kuhakikisha kwamba mle ambamo wanachimba baadae wahakikishe kuwa wanafukia mashimo yale. Na vile vile wachimba matofali nao wasibughudhiwe madhali tu wao baada ya kuchimba wanafukia mashimo, kwa hivyo, mawasiliano nao wafuate nyayo kama hizo wahakikishe kwamba wanajaribu kutengeneza mazingira vizuri.

Kwa kweli Mhe. Spika, mambo yaliyojitokeza takriban sio mengi sana kwa upande wa taasisi hii, isipokuwa ilibidi kwamba mengi yaliyojitokeza hapa ni masuala ya dawa za kulevya kwamba ni tatizo. Hilo ni kweli lakini vile vile wakasifu kwamba elimu inahitajika zaidi na naamini kwamba wizara kila kukicha inaendelea kutoa elimu juu ya dawa za kulevya, na sio dawa za kulevya tu, lakini hata juu ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI, na hiyo vilevile Wajumbe baadhi wamesifu wamesema kwamba hatua inakwenda vizuri hata maambukizi kidogo idadi yake imepungua ukilinganisha na hapo awali.

Vile vile kwamba taasisi iwe na *data base* ya kujua idadi ya walemavu. Naamini wizara hilo watalifanyia kazi kwa sababu ni jambo zuri, ili kujua ni walemavu wangapi kuhakikisha kwamba kila mlemavu basi anapata haki yake na anaingizwa katika orodha.

Mhe. Spika, kwa upande wa taasisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais vile vile ilipendekezwa kwamba lazima viongozi watatu hao basi wawe na nyumba zao maalum kule Dar es Salaam. Nafikiri hilo si suala baya ni suala zuri tu, na naamini basi wizara zote tatu zitakaa pamoja ili kutizama namna gani ya kujenga nyumba za viongozi watatu hao.

Mhe. Spika, sikuwa na mengi isipokuwa nawaahidi wajumbe kwamba, Wizara ya Makamo wa Kwanza wa Rais yale yote ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi basi naamini watayafanyia kazi na nashukuru sana ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendelea na shughuli zetu mpaka wakati huu tukiwa katika hali ya salama na uzima. Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi, lakini nitumie fursa hii pia nimshukuru Mwenyekiti

na Kamati nzima ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa namna ambavyo wamewasilisha vizuri taarifa yao. Ukweli Mhe. Spika, taarifa hii ina maelezo ya kutosha kwetu sisi itasaidia sana katika utendaji wa shughuli zetu.

Mhe. Spika, mengi ya ripoti hii ni ushauri na maelekezo kwa nia ya kutimiza wajibu wetu vizuri zaidi katika kuwatumikia wananchi. Nataka nilihakikishie Baraza lako hili tukufu na kamati kwa jumla kwamba, tutafanya yale ambayo mmetuelekeza kwa ufasaha kabisa ili tutekeleze wajibu wetu.

Mhe. Spika, jambo moja ambalo limejitokeza sana ni suala la maamuzi yanayofikiwa katika vikao vyetu vya pamoja vya mambo ya Muungano, ambapo jambo la msingi ni utekelezaji. Mimi naunga mkono kabisa kamati kwamba, ni kweli mambo haya baada ya kuyafanyia kazi sana basi hapana budi lazima utekelezaji uchukue nafasi yake ili tuweze kuondoa hizi kero ambazo zimekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu. Nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba kwa upande wetu tutaendelea na jitihada ili tuhakikishe kuwa hizi kero zinamalizika. Lakini jambo kubwa ni lile ambalo Mhe. Mwenyekiti amelielekeza hapa kwamba, mchakato wa katiba utatusaidia sana katika kutatua mambo mengi ambayo yako mbele yetu.

Kuhusiana na mambo ya majengo ya Mhe. Makamo wa Rais, tayari Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi ameeleza, na mimi naunga mkono na utaratibu umeshatoka serikalini kwamba kila wizara husika iweze kutenga katika fungu lake la bajeti kwa ajili ya kushughulikia viongozi wetu hawa, ili wapate nyumba zao za makaazi na wasipate bughudha ya aina yoyote pamoja na gari na kadhalika.

Kuhusu majengo ya kumbukumbu ya Mzee Karume tumo tunajitayarisha, ili kuhakikisha kwamba tuwe na majengo hayo na katika kipindi hicho cha bajeti tunategemea kuanza kwa hatua hizo kadiri ya hali ya uwezo wa fedha wa serikali utavyowezekana ili shughuli hiyo iweze kuendelea.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya *TASAF*, ni kweli ushauri tuliopewa tunaupokea tutaufanyia kazi na hivi sasa tumefanya tathmini ya kuweza kujua miradi hii kwa undani zaidi, ili iweze kuwasaidia wananchi vizuri sana kuliko ambavyo hivi inavyofanyika sasa. Kwa hivyo, tunaupokea ushauri na kuufanyia kazi.

Kuhusu masuala ya Tume ya Uchaguzi Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, tunapenda tuupokee ushauri huu na tutahakikisha kwamba suala zima la majengo kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi tunalifanyia kazi, na pia nalo tumejipanga katika bajeti ya mwaka huu tuweke fungu kwa ajili ya kuendeleza suala zima la ofisi hizi za Tume ya Uchaguzi. Tunaamini ni jambo muhimu na tutachukua kila hatua kama serikali, kuhakikisha mambo haya yanakwenda vizuri, licha ya kutegemea serikalini pia tunajaribu kuzungumza na wenzetu wahisani mbali mbali tuone namna gani jambo hili tunaweza kulitekeleza vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu ziara za mafunzo kwa wajumbe wetu wa Tume hii na wafanyakazi hilo ni jambo la msingi, kwa hivyo tutashirikiana na wenzetu kuhakikisha kwamba jambo hili linapata nafasi nzuri. Pia kwa hao wafanyakazi wa tume na makamishna waweze kuona chaguzi za nchi nyengine,hilo ni jambo zuri na kadiri ya hali itavyoruhusu basi sisi hatuna pingamizi naona ni jambo jema na litachukuliwa hatua.

Kuhusu kukatia bima gari za tume hatua zitachukuliwa, kuhusu kutoa elimu ya uraia hatua zitachukuliwa na ndio lengo la Tume yetu ya Uchaguzi. Kuhusu Idara ya maafa ni kweli yako mambo ya msingi ambayo tunatakiwa sasa tuyatekeleze moja likiwa ni suala la sera, takriban tumeshafikia hatua za mwisho na wakati wowote sera hii itakuwa iko tayari. Kwa hivyo, kutokana na sera vile vile tunategemea katika kikao cha Oktoba kuleta sheria ili kufanya marekebisho ya sheria katika suala zima la utaratibu wa kuimarisha Idara hii ya Maafa. Kwa mfumo huo basi, tutakuwa pia tuna Mfuko wa maafa, ijapokuwa hivi sasa Mfuko umeanza kazi lakini utakuwa ule Mfuko kuwepo rasmi kisheria, ni pale ambapo sheria hii tutakayoifanyia marekebisho.

Juu ya hivyo, hatua zinachukuliwa kwa ajili ya kuweka vifaa vya uokoaji, tumezungumza na wenzetu kutoka China pamoja na hivi karibuni Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atafanya ziara kwenda nchini Israel kwa nia hiyo hiyo ya vifaa kwa ajili ya uokoaji.

Mhe. Mwenyekiti alizungumzia jambo moja kubwa sana kuhusu hizi fedha zinazotoka za ubani ama zilizotolewa na wahisani na wananchi mbali mbali kwa ajili ya kuwasaidia wananchi waliopata janga lile la kuzama kwa Meli ya *Spice Islander I*. Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna majina ambayo tuliyapata kutoka kwenye tume ile iliyoundwa ya uchunguzi na ndiyo ambayo kwa sasa hivi tunayafanyia kazi.

Lakini kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan kwamba, wapo wananchi imeonekana katika utekelezaji wa zoezi hili majina yao hayamo kwenye orodha ile ya majina ya vyombo katika Tume ya Uchunguzi. Hivyo hatua

zitachukuliwa kuhakikisha kwamba haki ya kila mmoja wetu inapatikana kwenye jambo lile, na zoezi limeanza kwa hapa Unguja na tayari wilaya zote za Unguja tumeshaanza kutekeleza zoezi hilo. Lakini kutokana na tatizo lililojitokeza ni kwamba, baadhi ya watu ambao inaonekana walikumbwa na janga lile bado hawamo katika orodha ile, kwa hivyo tutachukua hatua kuhakikisha kwamba na wao wanakuwemo ili kila mmoja apate haki yake.

Mhe. Spika, kuhusu Kiwanda cha Uchapishaji, nia na lengo ni hilo hilo kuhamia na serikali ishafanya uamuzi huo na tumo katika matayarisho ya kuhama kutoka kule kwenye kiwanda cha zamani Saateni kuelekea Maruhubi, na tayari serikali imetenga fungu la fedha kwa ajili ya kazi hiyo kwa hivyo harakati zinaendelea.

Mhe. Spika, kuhusu Baraza la Wawakilishi sote tunakubali kwamba ni kweli ngome ya wananchi na kwa msingi huo basi, wizara yangu kwa kushirikiana na kamati hii tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba ile Sheria ya Utawala na Uendeshaji wa Baraza linachukua nafasi yake ili Baraza letu liwe na uhuru zaidi, lifanye kazi kwa ufanisi zaidi na yale yote ya msingi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wangependa kuyaona yaweze kufanyika kwa vizuri na kila mmoja tuweze kutekeleza wajibu wetu vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya migogoro ya ardhi, wizara inayohusika imetakiwa kushughulikia jambo hili na naamini chini ya uongozi wa waziri mpya basi mambo mengi yatatokea ya mafanikio ili tuondoe tatizo lililo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda umekuwa mkubwa, naamini hata wajumbe wenyewe sasa hivi wangehitaji kupumzika kwa sababu ni muda mrefu sana, kitako kimekuwa kirefu kwa kweli kila mmoja ananiandikia vi-*note* vingi kwa hali halisi ilivyo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii, na kuipongeza sana kamati hii na kuwaambia tuko pamoja ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza kutoa majumuisho. Mhe. Spika, nadhani yametosha, isipokuwa moja tu, Mhe. Spika, naomba kwa busara zako, kwa kiti chako, suala la mjenzi wa *Rest House*. Waswahili wanasema, "*Funika Kombe Mwanaharamu Apite*". Sikatai ushauri wa Mhe. Waziri kwamba Kamati ya *PAC*, na Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa turudi tena tukalijadili suala lile. Tutaendelea kupoteza fedha za umma lakini vile vile *final* yanaweza yakaja yakarudi yale yale yule mjenzi alipwe.

Mimi nadhani Mhe. Spika, suala limeshachukua muda mrefu, tutumie busara serikali tuangalie hili suala tulimalize katika utaratibu si wa kugharamika tena, vyenginevyo Mhe. Spika, hofu yangu kwa sababu hili suala lina mikono mingi tusije tukawataja watu hapa ambao wana heshima kubwa katika nchi hii. Kwa sababu kamati ndio kamati, kamati itakapokwenda kila *single cent* ilipokwenda itabidi sasa ije itajwe hii alichukua nani, hii alichukua nani, Mhe. Spika, fedha tunaweza kuja kulipa, lakini vile vile na fedheha nyengine ikaja ikatokea.

Sasa mimi ushauri wangu Mhe. Spika, lakini muongozo utakuwa nao, kwa sababu Mhe. Waziri nafikiri makatibu mezani wameandika kwamba twende tukachunguze. Lakini bado mimi sishawishiki sana, pamoja na kwamba kwenye ripoti ya kamati nilishauri Kamati ya *PAC* iende, lakini naona hili suala sasa hivi haliko katika hatua nzuri.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru, nawashukuru wajumbe wote samahani sikuwataja mliochangia lakini *hansard* itawakumbuka. Nakushukuru sana Mhe. Spika ahsante sana.

Mhe. Spika: Nawashukuru, nakushukuru Mhe. Mwenyekiti sasa Wajumbe niwahoji wale wanaopokea ripoti hii wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana, nakushukuruni kwa kunisaidia pamoja na wenzangu ripoti tatu leo kuzimaliza, ningekuwa nina posho ya nyongeza leo ningetoa. Kwa sababu leo tumefanya kazi kubwa tena kwa mashirikiano makubwa. Nichukue nafasi hii kuwapongeza wote wenyeviti, wajumbe waliochangia, Waheshimiwa Mawaziri, na wote Waheshimiwa Wajumbe ambao mmevumulia kukaa

hapa mpaka muda huu tukaendesha shughuli zetu hizi kwa mafanikio makubwa. Na basi kwa kazi nzuri hiyo sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 18/04/2012 saa tatu asubuhi.

(Saa 4:15 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe
18/04/2012 saa 3:00 asubuhi)